MATUKIO YALIYOCHOCHEA MABADILIKO YA KIMAUDHUI YA USHAIRI NCHINI TANGANYIKA KATI YA MWAKA 1930 HADI 1960

HELINA WANJIKU NJUGUNA

TASNIFU HII IMEWASILISHWA ILI KUTOSHELEZA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMIFU KATIKA SHULE YA SHERIA, FANI NA SAYANSI ZA KIJAMII, CHUO KIKUU CHA KENYATTA

NOVEMBA 2024

UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika chuo kikuu kingine.

5-11-2024

HELINA WANJIKU NJUGUNA **Tarehe**

Tasnifu hii imetolewa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii ya Chuo Kikuu cha Kenyatta.

5/11/2024

PROF.GEOFFREY KITULA KING'EI **Tarehe**

5-11-2024

DKT. RICHARD MAKHANU WAFULA **Tarehe**

TABARUKU

Kazi hii naitabarukia watoto wangu: Angela Wanjiku na Allan Kinyanjui kwa kunivumilia nilipokuwa masomoni hadi nikamaliza. Wanangu nawaachia mwenge huu wa elimu**.**

SHUKRANI

Kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na uwezo wa kuendelea katika safari hii ya kitaaluma. Hakuna jambo lolote ambalo ningeweza kulifanya kama si kwa mapenzi yake Mungu. Pili, shukrani zangu za dhati ziwaendee wasimamizi wangu Prof. Kitula King'ei na Dkt. Richard Makhanu Wafula kwa kuniongoza, kunishauri na kunitia moyo katika kila hatua ya utafiti huu. Niwashukuru kwa maoni na maarifa walionipa ili kuituja tasnifu hadi kufikia kiwango hiki.

Pia, ningependa kutoa shukrani zangu kwa wahadhiri wote wa idara ya Kiswahili kwa kunishauri na kunielekeza kila nilipohitaji msaada wao. Kadhalika, nawashukuru sana wanataaluma na wafanyakazi wote pamoja na wanafunzi wa uzamili na uzamifu wa Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa ushirikiano wao walionionyesha katika kipindi chote cha masomo yangu. Hawakusita kunisaidia pale nilipohitaji msaada wao.

Nawashukuru wasomi wengine Dkt. Ruth Kamunyu wa Pan Africa Christian University na Dkt Maria Ng'ang'a wa shule ya upili ya Mutunguru, Gatundu kwa kunishajiisha kila nilipokaribia kufa moyo. Nawaombea kila la heri.

Shukrani za kipekee zimwendee Bi. Jane Gitau wa shule ya upili ya St. Augustine Gikure, Gatundu aliyenipigia chapa sehemu ya kazi hii. Mola akubariki. Pia, namshukuru mwalimu Juddy Wanjiku Joseph wa shule ya St. Dominic Ikuma, Gatundu kwa kunitia moyo wa kuendelea na masomo.

Mwisho, ningependa kuishukuru sana familia yangu nikianza na watoto wangu, Angela Wanjiku na Allan Kinyanjui. Nawashukuru kwa uvumilivu wenu nilipokuwa masomoni. Usomi wa mama yenu na uamshe ari na msukumo kwenu wa kuthamini masomo.

Aidha, namshukuru kakangu Joram Mwaniki na dada zangu: Margaret Wambui, Mary Nyawira na Miriam Wangui kwa kunitia moyo nilipokuwa masomoni.

Kwa wengine wengi ambao sikuweza kuwataja, wote nawashehenezea shukrani za dhati kutoka kina cha moyo wangu kwa mchango wenu. Mungu awabariki.

YALIYOMO

UNGAMO ..... **ii**

TABARUKU ..... **iii**

SHUKRANI ..... **iv**

YALIYOMO ..... **v**

VIFUPISHO ..... **x**

FASILI YA ISTILAHI ..... **xi**

ABSTRACT ..... **xii**

IKISIRI ..... **xiii**

SURA YA KWANZA **1**

MSINGI WA UTAFITI **1**

1.0 Utangulizi 1

1.1 Usuli wa Utafiti 1

1.2 Suala la Utafiti 5

1.3 Maswali ya utafiti 6

1.4 Malengo ya Utafiti 6

1.5 Sababu za Kuchagua Mada 7

1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti 10

1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ya Utafiti 12

1.7.1 Tafiti Kuhusu Ushairi wa Kiswahili 12

1.7.2 Tafiti Kuhusu Sera ya Lugha 19

1.8 Misingi ya Nadharia 29

1.8.1 Nadharia ya Utegemezi 29

1.8.2 Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha 33

1.9 Mbinu za Utafiti 36

1.9.1 Sampuli 37
1.9.2 Ukusanyaji wa Data 38
1.9.3 Uchanganuzi wa Data 39
1.9.4 Matokeo 39
1.10 Hitimisho 39
SURA YA PILI 41
SERA YA LUGHA NA MAUDHUI YA USHAIRI 41
2.0 Utangulizi 41
2.1 Dhana ya Sera ya Lugha 41
2.1.1 Upangaji wa Lugha 43
2.1.2 Hatua za Upangaji Lugha 44
2.2 Sera ya Lugha ya Kipindi cha Wajerumani (1895-1918) 45
2.2.1 Sera ya Lugha ya Wajerumani katika Utawala 48
2.2.2 Sera ya Lugha ya Wajerumani katika Elimu 49
2.3 Sera ya Lugha ya Kipindi cha Waingereza (1918-1961) 53
2.4 Maudhui katika Ushairi 58
2.5 Ushairi na Hadhi ya Lugha 60
2.5.1 Shairi “Lugha Yetu Kiswahili” 60
2.5.2 Shairi “Kimefuzu Kiswahili” 65
2.5.3 Shairi “Kiswahili” 68
2.5.4 Shairi “Kiswahili” 70
2.5.5 Shairi “Kitumike Kiswahili” 74
2.6 Ushairi na Sauti ya Watu 76
2.6.1 Maudhui ya Amani 77
2.6.2 Maudhui ya Heshima 79
2.6.4 Maudhui ya Utetezi wa Haki 83

2.6.5 Maudhui ya Uhuru 88
2.7 Hitimisho 91
SURA YA TATU 93
KAMATI YA LUGHA YA AFRIKA MASHARIKI NA MAUDHUI YA USHAIRI 93
3.0 Utangulizi 93
3.1 Shughuli za Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki 93
3.1.1 Usanifishaji wa Kiswahili 97
3.1.2 Mashindano ya Uandishi 99
3.1.3 Kuundwa kwa Shirika la Uchapishaji wa Vitabu 101
3.2 Utunzi wa Mashairi 103
3.3 Ushauri kwa Watunzi wa Mashairi 114
3.4 Umuhimu wa Mashairi 122
3.5 Mchango wa Shaaban Robert katika Kueneza Kiswahili 126
3.6 Hitimisho 130
SURA YA NNE 132
KANUNI ZA UTUNZI WA MASHAIRI NA MAUDHUI YA USHAIRI 132
4.0 Utangulizi 132
4.1 Maana ya Ushairi 133
4.2 Kanuni za Utunzi wa Mashairi: Mtazamo wa Amri Abedi 137
4.2.1 Vina 146
4.2.2 Mizani 147
4.2.3 Kituo 148
4.2.4 Muwala 148
4.2.5 Urari 149
4.2.6 Utoshelezaji 149

4.2.7 Kiini 150
4.2.8 Lugha Mwafaka 151
4.3 Utunzi wa Mashairi ya Arudhi 152
4.4 Hitimisho 162
SURA YA TANO 163
HARAKATI ZA UPIGANIAJI UHURU NA MAUDHUI YA USHAIRI 163
5.0 Utangulizi 163
5.1 Vyama vya Kisiasa 163
5.1.1 Matumizi ya Kiswahili Katika Vyama vya Kisiasa 164
5.2 Ushairi kama Chombo cha Kisiasa 166
5.3.1 Dhuluma za Kikoloni 168
5.3.2 Utetezi wa Haki 176
5.3.3 Umoja na Ushirikiano wa Waafrika 181
5.3.4 Kupigania Utamaduni wa Waafrika 185
5.3.5 Sifa za Viongozi Bora 188
5.3.6 Uzalendo 192
5.3.7 Mchango wa Chama cha TANU katika Kuunganisha Wananchi 198
5.3.8 Madaraka ya Kujitawala 201
5.3.9 Sifa kwa Kiongozi Nyerere 203
5.3.10 Hamu ya Kupata Uhuru 206
5.4 Hitimisho 209
SURA YA SITA 211
MUHTASARI, MATOKEO, MCHANGO NA MAPENDEKEZO 211
6.0 Utangulizi 211
6.1 Muhtasari wa Tasnifu 211
6.2 Matokeo ya Utafiti 214

6.3 Mchango wa Utafiti 218
6.4 Changamoto za Utafiti 219
6.5 Mapendekezo ya Utafiti 220
MAREJELEO 222
Viambatisho 234
KIAMBATISHO A: Kibali cha Utafiti Chuo Kikuu cha Kenyatta 347
KIAMBATISHO B:Kibali cha Utafiti Taasisi ya Taaluma za Kiswahili 348
KIAMBATISHO C: Kibali cha Utafiti Chuo Kikuu cha Dar es Salaam 349
KIAMBATISHO D: Kibali cha Utafiti Chuo Kikuu Huria cha Tanzania 350

VIFUPISHO

U.M.C.A	Universities Mission to Central Africa
E.A.L.B	East African Literature Bureau
I.L.C	Inter-territorial Language Committee
E.A.I.L.C Bulletin	East African Inter- territorial Language Committee Bulletin
ILC Bulletin	Inter-territorial Language Committee Bulletin
C.M.S	Church Missionary Society
BM	Bethel Missionaries
G.P.S	German Protestant Society
G.P.M	German Protestant Missionaries
K.A.R	Kings African Riffles
T.A.N.U	Tanganyika African National Union
T.A.A	Tanganyika African Association
TTACSA	Tanganyika Territory African Civil Servants Association
KNPA	Kilimanjaro Native Planters Association
UTP	United Tanganyika Party
TUKI	Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili
TATAKI	Taasisi ya Taaluma ya Kiswahili
Juz	Juzuu
Na	Nambari
Mhr	Mhariri
Whr	Wahariri
uk	Ukurasa
kur	Kurasa

FASILI YA ISTILAHI

Matukio	Mambo yanayoathiri utunzi wa shairi kimaudhui.
Maudhui	Ni jumla ya masuala yanayozungumziwa katika shairi.
Ushairi wa Kiswahili	Ni aina ya ushairi unaotolewa kwa Kiswahili na unaozingatia kanuni za utunzi wa mashairi.
Sera	Ni utaratibu wa kuendesha jambo ili kukidhi haja za serikali, chama au dini.
Sera ya Lugha	Ni maamuzi yanayohusu matumizi ya lugha yanayofanywa na serikali yanayoathiri shughuli za kitaifa. Pia, maamuzi yanayohusu uteuzi wa lugha za taifa na rasmi na namna ya kuziendeleza.
Usanifishaji	Ni uamuzi wa kuchagua lugha moja au mojawapo ya lahaja za lugha na kuifanyia marekebisho ya kimatamshi, kisarufi, kimaana na kimaandishi ili iweze kutumika katika shughuli rasmi kwa mfano, katika elimu, fasihi, sayansi, utawala na mawasiliano rasmi.
Lugha ya taifa	Ni lugha iliyoteuliwa kutumika katika taifa zima na inayoweza kutekeleza wajibu wa taifa. Huwa kitambulisho cha utamaduni na ustaarabu wa taifa zima. Hunuiwa kuwa lugha itakayodumisha umoja kwa kuwaunganisha wananchi.
Kanuni	Kaida za utunzi wa mashairi ya arudhi.
Utegemezi	Ni dhana inayoeleza jinsi Waafrika wanavyotukuza lugha na utamaduni wa kigeni.
Ubidhaaishaji	Ni dhana inayotumiwa kueleza lugha kama bidhaa yenye umuhimu na thamani kutokana na majukumu inayotimiza katika jamii.
Urasimi mkongwe	Kipindi cha kabla ya majilio ya wakoloni waliotawala nchi za Afrika kati ya mwaka 1728 hadi 1885.
Urasimi mpya	Kipindi cha kupigania uhuru wa Waafrika waliotawaliwa na wakoloni kati ya mwaka 1945 hadi 1960.
Kipindi cha utasa	Kipindi kilichokuwa na tungo chache za fasihi kati ya mwaka 1885 hadi 1945

ABSTRACT

This study investigated the events that contributed to the change of themes in Kiswahili poetry in Tanganyika from the year 1930 to 1960. The poems were selected from the following texts: *Koja la Lugha* (1969), *Kielezo cha Fasili* (1968), *Masomo Yenye Adili* (1967), *Pambo la Lugha* (1966), *Mashairi ya Saadan* (1966), *Diwani ya Mnyampala* (1965), *Diwani ya Akilimali* (1963) and *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri* (1954). The study was guided by four objectives: to explain how the language policy of Tanganyika before independence contributed to the change of themes in Kiswahili poetry, to explain how the roles of The Inter Territorial Language Committee contributed to the change of themes in Kiswahili poetry, to explain how the conventional rules of Kiswahili poetry composition contributed to the change of themes in Kiswahili poetry and to explain how the events during the struggle for independence in Tanganyika from the year 1950 to 1960, contributed to the change of themes in Kiswahili poetry. The research method used was discourse analysis of the selected texts. The study was guided by two theories: Dependency Theory and Commodification of Language Theory. The tenets of Dependency Theory were used to investigate how the Africans decolonized themselves by promoting and spreading Kiswahili. Also, they were used to investigate how the poets defended the African culture, language, political structures and praised the African writers. The tenets of Commodification of Language Theory were used to investigate the main themes present in poems during the colonial period. Also, the tenets were used to investigate the poets' contribution to the spread of Kiswahili through political themes. The meaning of a poem was explained according to language use and context in relation to the whole poem. The research findings indicated that the poets chose their themes based on the events and the community life during the colonial period. The language policy during the German and British rule allowed the use of Kiswahili in governance and education though Kiswahili was a language of lower status compared to English. The poets promoted Kiswahili by praising the language and stating its importance to the people of Tanganyika in their poems. The roles of Inter Territorial Language Committee influenced the poets to choose themes that encouraged and guided the African writers, explained the importance of poetry together with the role of poets in promoting Kiswahili. The conventional rules in Kiswahili poetry influenced the poets to encourage composition of poems guided by those rules. The events during the struggle for independence in Tanganyika from the year 1950 to 1960, influenced the poets to compose poems with the following themes: resistance to colonialism, fight for African rights and culture, praise to the TANU party and its leader Julius Nyerere, desire for freedom, good leadership qualities and patriotism. This study has contributed to knowledge in the area of development and change of Kiswahili poetry. This study recommended that more research, be done on other poems of the same writers and others. Also, research to be done on development of themes in Kiswahili poetry; composed after Tanzania gained its independence up to date.

IKISIRI

Utafiti huu ulishughulikia matukio yaliyochochea mabadiliko ya kimaudhui ya ushairi nchini Tanganyika kati ya mwaka 1930 hadi 1960. Utafiti ulizingatia mashairi kutoka diwani zifuatazo: *Koja la Lugha* (1969), *Kielezo cha Fasili* (1968), *Masomo Yenye Adili* (1967), *Pambo la Lugha* (1966), *Mashairi ya Saadan* (1966), *Diwani ya Mnyampala* (1965), *Diwani ya Akilimali* (1963) na *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri* (1954). Utafiti huu uliongozwa na malengo manne: kueleza jinsi sera ya lugha ya kipindi cha ukoloni ilivyochochea mabadiliko ya kimaudhui katika ushairi, kubainisha jinsi shughuli za Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki zilivyochochea mabadiliko ya kimaudhui katika ushairi, kudhihirisha jinsi kanuni za utunzi wa mashairi zilivyochochea mabadiliko ya kimaudhui katika ushairi na kuelezea jinsi harakati za upiganiaji uhuru zilivyochochea mabadiliko ya kimaudhui. Mbinu za utafiti zilizotumika ni uchanganuzi wa matini katika diwani teule. Utafiti uliongozwa na Nadharia ya Utegemezi na Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha. Mihimili ya Nadharia ya Utegemezi ilitumika kubainisha jinsi ya kusitisha utegemezi wa lugha za kikoloni kwa kutetea na kuitukuza lugha ya Kiswahili. Pia, mihimili ilitumika kuchunguza jinsi washairi walivyotetea utamaduni, lugha, siasa na kutukuza waandishi wa Afrika katika mashairi yao. Mihimili ya Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha ilitumika kuchunguza maudhui ya mashairi ili kubainisha masuala muhimu yaliyoshughulikiwa katika kipindi cha ukoloni nchini Tanganyika. Maana ya shairi ilipatikana kwa kuzingatia muktadha wa kilugha na kuuhusisha na shairi zima. Matokeo ya utafiti yalidhihirisha kwamba, watunzi wa mashairi wa kipindi cha ukoloni nchini Tanganyika waliteua maudhui kutokana na hali ya jamii na mazingira ilivyokuwa wakati huo. Sera ya lugha ya kipindi cha utawala wa Wajerumani na cha Waingereza iliunga mkono matumizi ya Kiswahili katika utawala na elimu ingawa kilichukuliwa kuwa lugha ya hadhi ya chini ikilinganishwa na Kiingereza. Washairi walikitetea na kukitukuza kupitia maudhui ya mashairi yaliyohusu sifa na umuhimu wa Kiswahili kwa Watanganyika. Shughuli za Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki zilichochea uteuzi wa maudhui ya kuhimiza utunzi, kutoa ushauri kwa watunzi, kueleza umuhimu wa mashairi pamoja na kueleza mchango wa washairi katika kueneza Kiswahili. Kanuni za utunzi wa mashairi zilichochea utunzi wa mashairi yenye maudhui ya kuhimiza utunzi wa mashairi ya arudhi. Harakati za upiganiaji uhuru wa Tanganyika kati ya mwaka wa 1950 hadi 1960, zilichochea utunzi wa mashairi yenye maudhui yafuatayo: kupinga dhuluma, kutetea haki, kupigania utamaduni wa Waafrika, kusifu chama cha TANU na kiongozi Nyerere, kuwa na hamu ya kupata uhuru, sifa za viongozi bora na uzalendo. Utafiti huu umechangia kwa kuongeza maarifa katika maendeleo na mabadiliko ya ushairi wa Kiswahili. Utafiti huu unapendekeza utafiti zaidi ufanywe katika diwani nyingine za washairi husika na za watunzi wengine wa mashairi ya arudhi. Pia, utafiti zaidi ufanywe kwa kuzingatia mabadiliko ya kimaudhui ya ushairi wa Kiswahili katika kipindi cha baada ya uhuru wa Tanzania hadi sasa.

SURA YA KWANZA

MSINGI WA UTAFITI

1.0 Utangulizi

Katika sura hii vipengele vilivyowekea msingi utafiti huu vimejadiliwa. Vipengele hivyo vinahusu usuli wa mada, suala la utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada pamoja na upeo na mipaka ya utafiti. Aidha, utafiti ulishughulikia yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi ya nadharia na mbinu za utafiti.

1.1 Usuli wa Utafiti

Ushairi wa Kiswahili una historia ndefu na umekuwa ukitumiwa kama chombo cha kuwasilishia ujumbe kwa jamii katika vipindi tofauti vya kihistoria. Kulingana na Kezilahabi (1983: 148), ushairi wa Kiswahili umekuwa ukikua katika vipindi vifuatavyo: kipindi cha urasimi mkongwe, kipindi cha utasa, kipindi cha urasimi mpya na kipindi cha sasa. Baadhi ya ushairi wa kipindi cha urasimi mkongwe (1728-1885) ni *Utenzi wa Al-Inkishafi* (1810-1820), *Utenzi wa Fumo Liyongo* (1913), *Utenzi wa Mwana Kupona* (1858) na *Mashairi ya Muyaka* (1776-1840). Ingawa tarehe za kuandikwa kwa tenzi hizi ni za kukisia, ziliandikwa katika karne ya kumi na nane na nusu ya kwanza ya karne ya kumi na tisa (Mulokozi, 1999: viii).

Ushairi wa Kiswahili umepitia mabadiliko mengi yanayoonekana katika mikondo ya kimaudhui na fani mbalimbali (Mohamed, 1990: 67). Maudhui ya ushairi wa kipindi cha urasimi mkongwe yanahusu mafunzo ya kidini, wosia, siasa na uongozi miongoni mwa mengine. Kwa kuwa maudhui ya fasihi yoyote huzalika kutokana na hali ya jamii ilivyo kwa wakati wake, mshairi huzingatia historia ya jamii yake, hali ya jamii kwa wakati uliopo na mahitaji au matarajio ya siku zake za mbeleni (King'ei na Kemoli,

2001: 4). Kwa hivyo, maudhui ya ushairi yamekuwa yakibadilika katika vipindi tofauti vilivyofuatia urasimi mkongwe.

Kati ya mwaka 1885 na 1945, mataifa ya Ulaya yalikuwa yakigawana bara la Afrika na kulikuwepo na vita vya dunia mara mbili. Hali hizi zilisimamisha uandishi. Huu ndio muhula wa utasa katika fasihi ya Kiswahili kwa sababu ya uhaba wa utunzi (Shitemi, 2010: 5). Hata hivyo, maandishi machache yaliandikwa yakiwemo *Utenzi wa Vita vya Majimaji* ulioandikwa na Abdul Karim bin Jamaliddini (1957) na *Utenzi wa Vita vya Uhuru* ulioandikwa na Shaaban Robert (1967) (Kezilahabi, 1983: 149). Ushairi wa muhula wa utasa ulikuwa na maudhui ya vita, unyanyasaji na ukatili tofauti na maudhui ya ushairi yaliyowasilishwa katika kipindi cha urasimi mkongwe. Katika kipindi hiki kanuni za uandishi wa mashairi hazikuzingatiwa sana. Michafuko ya kisiasa miongoni mwa jamii za Waswahili ilitatanisha usalama wao na kuathiri harakati zao za kitamaduni ikiwemo utunzi. Hata hivyo, hali ilibadilika wakati wa kipindi cha maajilio ya wakoloni walioitawala nchi ya Tanganyika.

Katika kipindi cha ukoloni, Tanganyika ilitawaliwa na Wajerumani kati ya mwaka 1896 hadi 1918 na Waingereza kati ya mwaka 1918 hadi 1961. Kulingana na Kiango (2004: 67), sera ya lugha ya kipindi cha utawala wa Wajerumani ilikiunga mkono Kiswahili. Kiswahili kilitumika kama chombo cha mawasiliano katika shughuli za kibiashara, kiutawala na kielimu. Kadhalika, Waingereza walipoanza kutawala waliendeleza na kuieneza lugha ya Kiswahili. Kiswahili kiliteuliwa kuwa lugha ya kufundishia shule za msingi. Kutokana na wingi wa lahaja za Kiswahili, shughuli za kidini na kielimu zilitatizika na ikabidi lahaja moja isanifishwe kama lahaja rasmi. Kutokana na haja ya

usanifishaji na ukuzaji wa Kiswahili, Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki iliundwa rasmi mwaka wa 1930.

Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki ilichangia katika kuendeleza uandishi wa Kiswahili. Baadhi ya shughuli zake zilikuwa ni kuwashauri waandishi kuhusu vitabu walivyokusudia kuandika. Pia, kamati ililenga kuvitafsiri au kuviandika upya kwa Kiswahili vitabu vilivyopendekezwa. Kamati iliandaa mashindano ya kuandika insha na vitabu ili kuwatia ari waandishi wa Kiswahili. Shaaban Robert alikuwa miongoni mwa waandishi waliowahi kushinda katika mashindano hayo. Vilevile, kamati ilivitafsiri vitabu vya sayansi kwa Kiswahili na ilizingatia uchapishaji wa vitabu vya Kiswahili sanifu ili kuwashawishi waandishi wapya (Mbaabu, 2007: 31). Gorman (1974: 425) anaeleza kuwa, vitabu vingi vilichapishwa mwaka wa 1948 wakati shirika la uchapishaji la East African Literature Bureau lilipoanzishwa. Shirika hili lilipitia miswada yote ya Kiswahili na kuthibitisha ubora wa lugha yake. Kutokana na maelezo hayo, Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki ilichangia kuendeleza uandishi wa fasihi ushairi ukiwemo.

Katika kipindi cha urasimi mpya kuanzia mwaka wa 1945 hadi 1960, watunzi wa mashairi walianza kuchimbua miundo ya mashairi ya akina Ali Koti na Muyaka na kuitumia kutunga mashairi yao wenyewe (Wafula na Njogu, 2007: 49). Kwa hivyo, walizivumbua upya kunga za utunzi na kuzitumia katika utunzi wao. Huu ndio wakati wa washairi kama Amri Abedi, Shaaban Robert, Mathias Mnyampala, Akilimali Snow-White, Khamis Amani na Saadani Kandoro waliosifika nchini Tanganyika.

Upeo wa juu wa kipindi cha urasimi mpya wa fasihi ya Kiswahili ulitokea kilichochapishwa kitabu chake Amri Abedi: *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri* (1954). Kulingana na maoni ya Kezilahabi (1983:150), kitabu hiki kilihitajika ili kuweka kiungo kizuri cha wakati uliopita na urasimi mpya. Kwa hivyo, kulitokea msisimko wa utunzi wa mashairi yaliyozingatia kanuni za utunzi au arudhi.

Kipindi cha urasimi mpya kinaenda sambamba na wakati wa mwamko wa Mwafrika dhidi ya mkoloni. Washairi walitunga mashairi ya kisiasa na wengine wakaoongoza vyama vya kisiasa kama vile Saadan Kandoro (Mulokozi na Sengo, 1995). Hiki ni kipindi ambacho maudhui ya ushairi wa Kiswahili yalibadilika. Mashairi mengi yalichapishwa magazetini (Mbaabu, 1985: 61). Kutokana na ubaguzi na unyanyasaji wa Waafrika katika ngazi zote serikalini, Shaaban Robert alipata msukumo na ilhamu ya kutunga mashairi ya kisiasa ndiposa alitunga shairi "Chama cha Waafrika" katika *Pambo la Lugha* (1966: 9) ili kuonyesha msukumo wa kisiasa (Masinde, 2003). Kulingana na Chiraghdin na Mnyampala (1977: 70), chama cha kisiasa cha TANU kilibuniwa mwaka wa 1954 na kuanzisha ofisi zake takribani katika kila kijiji. Wafuasi wake waliongozwa na msemo "Uhuru na Kazi" (Clarke, 1960: 137). Pia, chama kiliendeleza siasa ya kutumia Kiswahili katika juhudi zake za ukombozi. Hatua hii ilileta mwamko katika kuiendeleza lugha ya Kiswahili katika pembe zote za nchi. Maelezo haya yanabainisha kuwa ushairi ulitumika kuleta mwamko wa kisiasa.

Kulingana na Syambo na Mazrui (1992: vii), msanii hupata tajriba na mawazo ya utungo wake kutokana na mazingira anayokumbana nayo. Kwa hivyo, watunzi wa mashairi

katika kipindi cha kabla ya uhuru wa Tanganyika waliteua maudhui yao kutokana na uhalisi wa maisha ya wakati ule jambo linalodhihirika katika utafiti huu.

Ushairi wa Kiswahili umekuwa ukitumiwa kuyaelezea maisha ya binadamu na mambo yanayomzingira. Mazingira ya mwandishi huathiri uteuzi wake wa lugha na maudhui anayowasilisha katika tungo lake. Matukio makuu ya kipindi fulani cha historia ya jamii yanadhihirika kupitia fasihi ya kipindi hicho. Kwa hivyo, uteuzi wa maudhui huathiriwa na matukio katika jamii. Kwa msingi huo, utafiti huu ulilenga kuchunguza matukio yaliyochochea mabadiliko ya kimaudhui ya ushairi wa Kiswahili nchini Tanganyika kati ya mwaka 1930 hadi 1960.

1.2 Suala la Utafiti

Kihistoria, ushairi wa Kiswahili umefanyiwa tafiti mbalimbali. Watafiti waliotangulia kama vile Momanyi (1991), Chacha (1987) na Masinde (2003) walishughulikia ushairi wa kabla ya karne ya ishirini. Pia, walizingatia masuala ya kimtindo kama matumizi ya taswira na jazanda katika ushairi. Tofauti na tafiti hizo, utafiti huu ulizingatia ushairi wa kipindi cha urasimi mpya katika kipengele cha maudhui. Utafiti wa awali umebainisha kuwa, ushairi wa Kiswahili umebadilika kadri jamii inavyobadilika kwa mujibu wa wakati. Utunzi wa mashairi unasawiri maendeleo na mabadiliko ya jamii. Mshairi huweza kutunga kazi yake kutokana na matukio ya kihistoria. Kwa hivyo, katika kipindi cha urasmi mpya, kuna matukio yaliyoathiri ubunifu wa maudhui. Kwa misingi huo, palikuwa na haja ya kuchunguza matukio yaliyochochea mabadiliko ya maudhui ya ushairi wa Kiswahili kati ya mwaka 1930 hadi 1960 nchini Tanganyika. Matukio hayo ni pamoja na sera ya lugha ya kipindi cha ukoloni, shughuli za Kamati ya Lugha (ya

Kiswahili) ya Afrika Mashariki, kanuni za utunzi wa mashairi na harakati za upiganiaji uhuru wa Tanganyika.

1.3 Maswali ya utafiti

Utafiti huu ulidhamiria kuyajibu maswali yafuatayo:

1. Je, sera ya lugha ya kipindi cha ukoloni ilichangia vipi mabadiliko ya kimaudhui ya ushairi nchini Tanganyika?
2. Ni uhusiano upi uliopo kati ya shughuli za Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki na mabadiliko ya kimaudhui ya ushairi nchini Tanganyika?
3. Kanuni za utunzi wa mashairi zilichangia vipi mabadiliko ya kimaudhui ya ushairi nchini Tanganyika?
4. Harakati za upiganiaji uhuru zina mchango gani katika mabadiliko ya kimaudhui ya ushairi nchini Tanganyika?

1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti uliongozwa na malengo yafuatayo:

1. Kueleza jinsi sera ya lugha ya kipindi cha ukoloni ilivyochochea mabadiliko ya kimaudhui ya ushairi wa Kiswahili nchini Tanganyika.
2. Kubainisha jinsi shughuli za Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki zilivyochochea mabadiliko ya kimaudhui ya ushairi wa Kiswahili nchini Tanganyika.
3. Kufafanua jinsi kanuni za utunzi wa mashairi zilivyochochea mabadiliko ya kimaudhui ya ushairi wa Kiswahili nchini Tanganyika.
4. Kueleza jinsi harakati za upiganiaji uhuru zilivyochochea mabadiliko ya kimaudhui ya ushairi wa Kiswahili nchini Tanganyika.

1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Mada hii imechaguliwa kwa kuzingatia kwamba ushairi wa Kiswahili una historia ndefu. Ushairi umekuwapo katika vipindi tofauti vya kihistoria. Katika kipindi cha urasimi mkongwe, ushairi uliotungwa ulibeba maudhui yanayohusu wosia, mafunzo ya kidini, siasa na uongozi. Ushairi wa kipindi cha utasa ulibeba maudhui ya vita, unyanyasaji na ukatili. Nchini Tanzania ushairi umekuwepo katika kipindi cha utawala wa Waarabu, Wajerumani na Waingereza. Pia, watunzi wa mashairi wanaathiriwa na nguvu za mabadiliko ndani na nje ya mazingira yao (Masinde, 2003). Hivyo, uteuzi wa maudhui unaathiriwa na mahitaji ya jamii katika nyakati tofauti. Aidha, fasihi ni kielelezo cha jamii; haina budi ieleze hali halisi ya maisha ya jamii inayohusika. Ni sharti fasihi ibebe ujumbe maalum kwa hadhira ya jamii inayokusudiwa (Gibbe na Mvungi, 1987: 1). Kwa kuwa uteuzi wa maudhui huathiriwa na mahitaji ya jamii, utafiti huu ulilenga kuchunguza matukio yaliyochochea mabadiliko ya kimaudhui ya ushairi wa kipindi cha urasimi mpya (kipindi cha ukoloni) nchini Tanganyika. Matokeo ya utafiti huu yanatazamiwa kuwanufaisha wakuza mitaala kwa sababu yataongeza maarifa kuhusu uhakiki wa mashairi ya Kiswahili hasa katika suala la maudhui.

Matokeo ya utafiti yanatazamiwa kubainisha masuala muhimu yaliyozingatiwa na washairi wa kipindi cha ukoloni ili kudhihirisha mabadiliko ya kimaudhui kwa kuyalinganisha na ya ushairi wa kabla ya ukoloni. Hivyo, utafiti huu unatoa mchango katika maendeleo na mabadiliko ya kimaudhui katika ushairi wa Kiswahili.

Watunzi wa mashairi walioteuliwa, Mathias Mnyampala, Akilimali Snow-White, Amri Abedi, Shaaban Robert na Saadani Kandoro walikulia nchini Tanganyika na walitunga

mashairi katika kipindi cha ukoloni. Kwa hivyo, utunzi wao umeathiriwa na maisha na mazingira ya jamii, jambo linalodhihirika katika uteuzi wao wa maudhui ya ushairi.

Shaaban Robert alikuwa mshairi maarufu wa wakati wa ukoloni na kila aliyewahi kusoma tungo zake hakukosa kupata fundisho fulani kwa tungo hizo (Eliufoo, 1967: ix). Kushadidia kauli hii Abedi, 1968: xiii) anaeleza kwamba Robert alishughulikia kila uwanja wa ushairi kwa uzani na umbo. Shaaban Robert alitunga Diwani za mashairi zifuatazo: *Tenzi za Marudi Mama na Omar Khayyam* (1973), *Almasi za Afrika* (1972), *Sanaa ya Ushairi* (1972), *Almasi za Afrika na Tafsiri ya Kiingereza* (1972), *Mashairi ya Shaaban Robert* (1971), *Koja la Lugha* (1969), *Mapenzi Bora* (1969), *Mwafrika Aimba* (1969), *Kielezo cha Fasili* (1968), *Ashiki Kitabu Hiki* (1968), *Masomo Yenye adili* (1967), *Insha na Mashairi* (1967), *Pambo la Lugha (1966)* na *Utenzi wa Vita vya Uhuru* (1961). Hivyo, ni miongoni mwa watunzi waliosifika Tanganyika. Diwani zake nne ziliteuliwa kwa sababu zina maudhui ya sifa na umuhimu wa Kiswahili, kanuni za utunzi na masuala ya uongozi. Pia, Robert alikuwa mmojawapo wa Waafrika wa kwanza waliojiunga na Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki mwaka wa 1939 (Mbaabu 2007: 62). Kwa hivyo, alishiriki katika uundaji wa sera ya lugha ya wakati wa ukoloni kwa sababu alitunga mashairi kwa Kiswahili sanifu.

Akilimali (1963) ametunga mashairi mia moja na kumi na tano. Katika dibaji, Abedi ameyasifu mashairi yake kwa kudokeza kuwa “mashairi yake ni matamu sana mara tu utakapoyangalia ikiwa na mwelewa wa mashairi utashitukia umenaswa ndani ya ladha kama anasavyo mlamba asali” . Pia, anaeleza kuwa “amejitahidi sana kupanga vina vizuri kuvidumisha na kadhalika mizani. Hivyo, mashairi yake hayana taabu na mazuri

kuimbika” (Akilimali, 1963: vii-viii). Mashairi haya yameteuliwa kwa kuwa na maudhui ya sifa na umuhimu wa Kiswahili, siasa na uongozi.

Mnyampala (1965) ameandika mashairi mia moja sabini na nane. Mashairi hayo yana maudhui yaliyozingatiwa katika utafiti huu. Baadhi ya mashairi yana maudhui yafuatayo: sifa na umuhimu wa Kiswahili, umuhimu wa utunzi, kanuni za utunzi wa mashairi, siasa na uongozi.

Kandoro (1966) ni mmoja kati ya watu kumi na saba walionzisha chama cha TANU mwaka wa 1954. Pia, ni mmoja wa watu waliopigania uhuru wa Tanganyika. Kwa kuwa alipigania uhuru kimatendo na kimaandishi mashairi yake yameteuliwa kwa kuwa yana maudhui ya kisiasa.

Abedi (1954) aliorodhesha kanuni au arudhi zinazopaswa kufuatwa katika utunzi wa mashairi ingawa siye mwanzilishi wa mashairi ya arudhi. Mashairi yake yameteuliwa kwa kuwa ni mashairi ya arudhi. Pia, mashairi hayo yana maudhui ya umuhimu wa umoja na utetezi wa utamaduni wa Mwafrika.

S. Robert, M. Mnyampala, K. Akilimali, S. Kandoro na A. Abedi walitunga mashairi kwa Kiswahili sanifu tofauti na washairi wa kipindi cha urasimi mkongwe waliotumia lahaja za Kiswahili. Vilevile, washairi hawa walitunga kazi zao wakati sera ya lugha ya kipindi cha ukoloni ilipokiunga mkono Kiswahili. Pia, mashairi yao yana mwelekeo wa kudhihirisha uzingatiaji wa arudhi katika uwasilishaji wa ushairi wa Kiswahili. Aidha, katika kipindi cha ukoloni ushairi wa Kiswahili ulitumika kama chombo cha

kuwahamasisha Watanganyika kutetea huru wao. Isitoshe, washairi waliathiriwa na shughuli za Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki zilizowahimiza kutunga mashairi kwa Kiswahili sanifu na kutoa ushauri kuhusu utunzi. Kwa hivyo, utafiti huu ulichunguza jinsi matukio yafuatayo yalivyochochea mabadiliko ya kimaudhui ya ushairi nchini Tanganyika kati ya mwaka 1930 hadi 1960: sera ya lugha ya kipindi cha ukoloni, shughuli za Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki, uandishi wa kanuni za utunzi wa mashairi na harakati za upiganiaji wa uhuru kati ya mwaka 1950 hadi 1960.

1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti ulishughulikia matukio yaliyochochea mabadiliko ya kimaudhui ya ushairi wa Kiswahili nchini Tanganyika kati ya mwaka 1930 hadi 1960. Mashairi yaliteuliwa kutoka diwani zifuatazo*:* *Koja la Lugha* (1969), *Kielezo cha Fasili* (1968), *Masomo Yenye Adili* (1967), *Pambo la Lugha* (1966), *Mashairi ya Saadan* (1966), *Diwani ya Mnyampala* (1965), *Diwani ya Akilimali* (1963) and *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri* (1954). Diwani hizo ziliteuliwa kwa sababu zina mashairi ya arudhi yaliyotungwa kwa Kiswahili sanifu. Vilevile, zilitungwa na watunzi wa mashairi kutoka Tanganyika katika kipindi cha ukoloni kinachozingatiwa katika utafiti huu. Aidha, diwani hizo zilibainisha maudhui tofauti na yale ya ushairi wa vipindi vya urasimi mkongwe na utasa yaliyohusu dini, wosia uongozi, vita na unyanyasaji. Kwa hivyo, zilidhihirisha mabadiliko ya kimaudhui kati ya ushairi wa kipindi cha urasimi mpya na vipindi vilivyotangulia. Diwani nne za S. Robert ziliteuliwa kwa sababu zilibainisha maudhui mbalimbali yaliyozingatiwa katika utafiti huu zikilinganishwa na diwani zake nyingine. S. Robert alikuwa mshairi maarufu nchini Tanganyika katika kipindi cha ukoloni kutokana na mchango wake katika utunzi wa fasihi (Chuachua, 2011:41).

Utafiti huu ulishughulikia watunzi kutoka Tanganyika kwa sababu utunzi wa mashairi ulikuwa umeenea katika kipindi cha ukoloni nchini Tanganyika tofauti na sehemu nyingine za Afrika Mashariki. Vilevile, watunzi wa mashairi walikuwa wengi wakiwemo: K. Amani, S. Robert, M. Mnyampala, S. Kandoro, A. Abedi na A. Snow-White.

Kipindi cha mwaka wa 1930 hadi 1960 kiliteuliwa kwa sababu Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki iliundwa rasmi katika mwaka wa 1930. Matukio yaliyotokana na shughuli za kamati hiyo yalishughulikiwa katika utafiti huu. Pia, nchi ya Tanganyika ilipata uhuru katika mwaka wa 1961. Kwa hivyo, utafiti huu ulijikita katika kipindi cha kabla ya ukoloni kufikia mwaka wa 1960.

Utafiti ulizingatia jinsi washairi husika walivyoteua maudhui na kana kwamba waliathiriwa na matukio mahsusi yaliyotokana na sera ya lugha ya kabla ya uhuru, shughuli za Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki, kanuni za utunzi wa mashairi na harakati za upiganiaji uhuru wa Tanganyika.

Watunzi wa mashairi A. Abedi, M. Mnyampala, S. Robert, A. Snow White na S. Kandoro waliteuliwa kwa sababu tungo zao zina mashairi ya arudhi. Pia, tungo hizo zina maudhui yaliyozingatiwa katika utafiti huu tofauti na diwani za watunzi wengine. Utafiti huu ulizingatia mashairi ya watunzi husika yanayobeba maudhui yenye sifa na umuhimu wa Kiswahili, umuhimu wa utunzi, kanuni za utunzi wa mashairi na siasa na

uongozi. Utafiti haukushughulikia tanzu zingine za fasihi andishi kama vile riwaya zilizoandikwa na watunzi wa mashairi husika.

1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ya Utafiti

Sehemu hii imeshughulikia yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti. Katika sehemu ya kwanza kuna baadhi ya kazi zinazohusu ushairi wa Kiswahili na sehemu ya pili inahusu kazi zinazoshughulikia sera ya lugha. Sehemu hizi mbili zinabainisha pengo lililotokana na tafiti za awali. Baadhi ya kazi zinazohusu ushairi wa Kiswahili ni pamoja na Kyamba (2018), Kyamba (2016), Nyongesa (2015), Mogeni (2015), Ndwiga (2013), Yunus (2013), Masinde (2003), Momanyi (1991) na Chacha (1987). Baadhi ya kazi zilizoshughulikia sera ya lugha ni pamoja na Marshall (2015), Eleuthera (2007), Brock-utne na Holmarsdottir (2004), Mkude (1999), Moyd (1996), Mbaabu (1991), Mkude (1999), Rubagumya na Lwaitama (1990), Mwansoko (1990), Rugemalira, Rubagumya, Kapinga na wengine (1990). Kwa hivyo, ushairi wa Kiswahili umefanyiwa tafiti mbalimbali. Hata hivyo, hakuna utafiti uliochunguza matukio yaliyochochea mabadiliko ya kimaudhui ya ushairi nchini Tanganyika kati ya mwaka 1930 hadi 1960. Pia, hakuna utafiti ulioongozwa na Nadharia ya Utegemezi na Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha.

1.7.1 Tafiti Kuhusu Ushairi wa Kiswahili

Mwingilianomatini katika ushairi wa Mathias Mnyampala umeshughulikiwa na Kyamba (2018). Azma kuu ya utafiti huo ni kuchunguza na kuchambua ushairi wa Mnyampala kimwingilianomatini. Data ilikusanywa kutoka kazi teule zilizochapishwa ambazo ni: *Diwani ya Mnyampala* (1965), *Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi* (1965) na *Ngonjera za UKUTA* Na. 1 (1970). Pia, data ilikusanywa kutoka

miswada ya Mnyampala isiyochapishwa ifuatayo: Hazina ya Washairi, Mahadhi ya Kiswahili na Mashairi ya Vidato. Utafiti ulilenga kupambanua muktadha wa utunzi uliomsukuma mwandishi kutunga kazi teule za ushairi wa Kiswahili. Pia, utafiti ulihakiki mbinu za kifani zinavyotumika kuibua maudhui ya ushairi pamoja na kutathmini mchango wa kazi za ushairi za Mnyampala katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili. Utafiti huo uliongozwa na Nadharia ya Mwingilianomatini. Matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha kuwa Mnyampala amechangia pakubwa katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili. Mojawapo ya mchango wake ni kuongozwa na Nadharia ya Kimapokeo katika utunzi wa mashairi yake inayosisitiza upekee wa shairi la Kiswahili kimuundo hasa urari wa vina na mizani. Kwa kutumia nadharia hii, Mnyampala ameibua mbinu mpya za utunzi kama vile mbinu ya mtiririko na msisitizo. Pia, utafiti umevumbua miswada, barua na nyaraka mbalimbali za kifasihi zenye mchango mkubwa katika ushairi na fasihi ya Kiswahili. Utafiti ulibainisha kuwa kazi za Mnyampala zinaingiliana, zinakamilishana na kutegemeana na matini nyingine tangulizi. Utafiti huo uliufaa utafiti huu kwani umedhihirisha kuwepo kwa uhusiano mkubwa kati ya muktadha wa utunzi, mbinu za kifani na uibuaji wa maudhui ya kazi teule za Mnyampala. Kinyume na utafiti huo ulioangazia athari za muktadha wa kijamii, kisiasa na kiuchumi wa uandishi wa kazi teule za Mnyampala, utafiti huu ulishughulikia matukio yaliyoathiri uteuzi wa maudhui ya mashairi yake katika *Diwani ya Mnyampala* (1965).

Kyamba (2016) ametafiti muundo wa mashairi katika *Diwani ya Mnyampala* (1965) na nafasi yake katika kuibua maudhui. Utafiti ulilenga kuangalia vipengele vya muundo kama mishororo, beti, mizani, vina, kituo au kibwagizo na mkarara. Mtafiti alichunguza

jinsi muundo ulivyotumika kuibua dhamira mbalimbali za kisiasa, kijamii na kiuchumi. Pia, alidadisi namna mbinu za kimuundo zilivyofanikisha usawiri na ubainishaji wa falsafa ya utunzi kuhusu ushairi wa Kiswahili na nafasi yake katika jamii. Utafiti umedhihirisha kuwa Mnyampala amesawiri vyema Nadharia ya Kimapokeo kwa kuzingatia kanuni za ushairi zinazosisitiza urari wa vina na mizani na utoshelevu. Aidha, ametumia lugha isiyo na matusi yaani lugha ya hekima ambayo ni falsafa yake ya kuzingatia lugha fasaha isiyo na matusi. Utunzi wa *Diwani ya Mnyampala* unaonyesha kiwango cha kupevuka kwa msanii kifikra na kiutendaji. Utafiti huo una manufaa kwa utafiti huu kwa kubainisha kwamba Mnyampala ameweza kuihuisha na kuweka misingi ya Nadharia ya Kijadi ya ushairi. Kwa hivyo, amechangia katika sanaa na maendeleo ya ushairi wa Kiswahili. Utafiti huo ni tofauti na utafiti huu kwa sababu ulichunguza mbinu za kimuundo katika ushairi wa Mnyampala ilhali utafiti huu ulichunguza maudhui ya ushairi, mashairi ya Mnyampala yakiwemo.

Suala la mtindo na dhamira katika ushairi wa Kiswahili limeshughulikiwa. Nyongesa (2015) amechunguza mtindo na dhamira ya mashairi ya washairi chipukizi kutoka Kaunti ya Bungoma. Amechanganua tamathali za usemi kama mtindo wa kuwasilisha ujumbe. Pia, amedhamiria kuonyesha jinsi mtindo wa kutumia tamathali za usemi ulivyofanikisha usawiri wa dhamira na maadili yaliyofumbikwa katika mashairi. Utafiti huo uliufaa utafiti huu kwa kubainisha kuwa watunzi hutunga kutokana na yanayojiri katika mazingira yao, hutumia lugha kiubunifu ili kuwasilisha ujumbe na dhamira lengwa kwa jamii. Kinyume na utafiti huo uliozingatia mtindo na dhamira ya mashairi ya washairi kutoka Bungoma, utafiti huu unazingatia mashairi ya watunzi kutoka nchi

ya Tanganyika ili kuchunguza matukio yaliyochochea uteuzi wa maudhui katika mashairi yao.

Utafiti wa fani na maudhui katika mashairi ya magazeti ya Taifa Leo umefanywa na Mogeni (2015). Utafiti umezingatia maudhui katika mashairi ya magazeti ya Taifa Leo. Utafiti umebainisha kwamba fani na maudhui ni mambo mawili yanayochangia ufanisi wa dhamira ya mtunzi wa ushairi wa Kiswahili. Utafiti huo uliufaa utafiti huu kwa kudokeza kuwa watunzi wa mashairi hujikita katika kila nyanja ya maisha ya binadamu. Falsafa zao zimedhihirisha mtazamo pamoja na msimamo wao kuhusu maswala tofauti ya kijamii, kisiasa na kiuchumi. Hata hivyo, utafiti huo ulijikita katika suala la fani na maudhui, kinyume na utafiti huu ulioshughulikia matukio yaliyochochea uteuzi wa maudhui husika. Utafiti huu sawa na wa Mogeni utachangia katika suala la maudhui ya ushairi wa Kiswahili.

Mtindo katika ushairi wa Kiswahili umefanyiwa uchunguzi. Ndwiga (2013) ameshughulikia mtindo katika mashairi ya *Diwani ya Karne Mpya*. Alilenga kuchunguza mitindo mahsusi iliyotumiwa na watunzi, kuchunguza jinsi mitindo hiyo ilivyofanikisha usawiri wa dhamira na maudhui na kuainisha sifa za matumizi ya lugha ya watunzi. Utafiti huo una manufaa kwa utafiti huu kwani ulidhihirisha kwamba, mtindo ni muhimu katika uwasilishaji wa maudhui. Mtindo hueleza jinsi msanii alivyoteua maneno yake na namna alivyoyapanga katika ujumbe wake na kuuwasilisha katika umbo. Hivyo, mtindo na maudhui ni vipengele vinavyojengana. Kinyume na utafiti huo uliojikita katika suala la mtindo uliofanikisha maudhui, utafiti huu ulishughulikia matukio yaliyoathiri ubunifu wa maudhui ya mashairi.

Yunus (2013) alishughulikia masuala ya kisiasa katika ushairi wa Saadan Kandoro kwa kutoa mifano katika mashairi yake. Utafiti ulilenga kuainisha dhamira za kisiasa zinazojitokeza katika mashairi yake. Pia, utafiti ulieleza mbinu za kisanaa zinazotumiwa katika kuibua masuala ya kisiasa pamoja na falsafa yake katika ushairi wake. Nadharia zilizoongoza utafiti ni Semiotiki, Umaksi na Ufeministi. Utafiti huu unabainisha kuwa Kandoro anaeleza dhamira za kisiasa zinazohusiana na ukombozi wa Mwafrika kutoka mikononi mwa wakoloni na kuweza kujitawala wenyewe. Ili kufanikiwa katika jambo hili, Kandoro anawataka wananchi kuungana pamoja na kudai uhuru kwa kujiunga na chama cha TANU. Anatumia mbinu za kisanaa kama vile lugha ya kitamathali, wahusika na mitindo mbalimbali ili kueleza dhamira za kisiasa. Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa Kandoro ana falsafa ya kimapinduzi, utu, ujamaa na kujitegemea. Masuala ya kisiasa yalishughulikiwa katika utafiti huu. Utafiti huo una manufaa kwa utafiti huu kwa sababu umedhihirisha mchango wa Kandoro katika harakati za kupigania uhuru wa Tanganyika kwa kuangazia masuala ya kisiasa katika mashairi. Hata hivyo, utafiti huo ni tofauti na utafiti huu ulioshughulikia matukio yaliyochochea maudhui ya kisiasa katika ushairi wa Kandoro.

Uchanganuzi wa maendeleo na mabadiliko ya maudhui katika ushairi wa Kiswahili umechunguzwa na Masinde (2003). Utafiti huo umechunguza maudhui ya kisiasa, kiuchumi na kijamii na jinsi yalivyosawiriwa katika vipindi tofauti vya kihistoria. Vilevile, utafiti huo umetathmini iwapo uchambuzi wa kihistoria unaweza kusaidia kufafanua uelewaji wa ushairi wa Kiswahili. Utafiti huo umeongozwa na Nadharia ya Uhistoria Mpya. Utafiti umehusisha maendeleo ya jamii katika vipindi vya urasimi,

urasimi mpya na kipindi cha sasa na mabadiliko ya maudhui ili kudhihirisha kwamba, mazingira ya kihistoria na kijamii huathiri utunzi wa kifani na kimaudhui. Utafiti huo una manufaa kwa utafiti huu katika kubainisha kwamba, misingi na mikondo ya historia ya jamii huipa fasihi umbo lake kifani na kimaudhui pamoja na mwelekeo. Hivyo, ushairi wa Kiswahili unaweza kueleweka na kutathminiwa vyema kwa kuwekwa katika muktadha maalum kihistoria. Utafiti huu unashughulikia matukio ya kihistoria ya kipindi cha ukoloni ili kuchunguza athari zake katika uteuzi wa maudhui ya ushairi. Tofauti na utafiti huo uliojikita katika vipindi tofauti vya kihistoria, utafiti huu ulizingatia kipindi cha urasimi mpya. Utafiti huo, ulishughulikia masuala ya kidini na ya kijamii tofauti na utafiti huu ulishughulikia matukio yaliyoathiri ubunifu wa maudhui ya ushairi. Kinyume na utafiti huo ulioongozwa na Nadharia ya Uhistoria mpya, utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Utegemezi na Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha.

Momanyi (1991) amechunguza matumizi ya taswira kama kielelezo cha uhalisi katika Utenzi wa Al Inkishafi. Utafiti huo ulilenga kuhakiki matumizi ya taswira katika Utenzi wa Al Inkishafi na jinsi taswira hizi zinzvyoibushwa na Sayyid Abdalla kama vielelezo vya uhalisi. Pia, Kuchunguza iwapo ufanifu na uvunjifu wa mji wa Pate una uhusiano katika uteuzi wa taswira na ujenzi wa maudhui katika kazi hii. Vilevile, kustawisha hoja na kutoa ithibati zozote ikiwa kuna uhusiano wowote kati ya mazingira ya mshairi na usanii wa kazi yake hasa taswira alizoteua. Aidha kuchunguza iwapo muundo wa kazi za fasihi uliokuwepo na lugha iliyotumiwa wakati wa mwandishi vina uhusiano wowote na uteuzi huu. Matokeo ya utafiti yalibainisha kwamba, mazingira yalichangia pakubwa katika uandishi wa Utenzi wa Al Inkishafi. Pia, Maudhui ya Sayyid Abdalla yana uhusiano na mazingira halisi yaliyomzaa na kumlea. Fasihi ni sanaa inayotumia maneno

katika kuyaeleza na kuyahakiki maisha na mazingira ya jamii. Fasihi ni zao la jamii ambalo huchota maudhui yake katika harakati za maisha ya kila siku. Utafiti huo una manufaa kwa utafiti huu kwa sababu umebainisha kuwa, mwandishi wa kifasihi huweza kuandika kazi yake kutokana na matukio fulani ya historia. Tukio fulani huweza kumwathiri mwandishi kiasi cha kumpa ilhamu ya kuandika kuhusu tukio hilo au kuchota taswira zake kuzungukia tukio hilo kwa madhumuni ya kuelimisha au kuutahadharisha umma. Hata hivyo, utafiti huo ni tofauti na utafiti huu kwa sababu utafiti huo umeshughulikia ushairi wa kipindi cha urasimi mkongwe. Utafiti huu umejikita katika ushairi wa kipindi cha urasimi mpya. Pia, utafiti huo umejikita katika suala la kimtindo hasa matumizi ya taswira ilhali utafiti huu unashughulikia matukio yaliyochochea mabadiliko ya maudhui katika ushairi.

Chacha (1987) amechunguza maana na ufasiri wa ushairi wa Kiswahili kama unavyosawiri mabadiliko ya jamii ya Waswahili. Utafiti huo ulilenga kuchunguza maana za kijamii zinazopatikana katika ushairi wa Kiswahili. Utafiti ulitathmini uhusiano uliopo kati ya jamii ya Waswahili na ushairi wa Kiswahili. Ufasiri wa maana umeshughulikiwa kupitia matumizi ya jazanda katika ushairi. Pia, utafiti umetambua muktadha ambapo jazanda zimetumika katika shairi. Uchunguzi wa hali ya diglosia kati ya lahaja ya Kimvita na Kiswahili sanifu imejadiliwa ili kubainisha jinsi tofauti za kilahaja huathiri ufasiri wa jazanda na maana ya shairi. Utafiti umebainisha kuwa, utunzi wa mashairi unasawiri maendeleo na mabadiliko ya kijamii katika jamii ya Waswahili kupitia mahusiano yao na watu wa bara la Asia na tamaduni za kigeni. Kwa kutumia mtazamo wa Ethnografia katika uchunguzi wa matumizi ya lugha, jazanda zinazotumika katika ushairi wa Kiswahili zinajadiliwa. Jazanda hizo zinahusishwa na

uhalisi wa kijamii na kihistoria katika jamii ya Waswahili. Utafiti unadhihirisha kuwa, maana ya ushairi wa Kiswahili inaongozwa na muktadha. Ni katika mipaka ya muktadha ambapo watu wa jamii lugha moja huafikiana vile watafasiri shairi na jazanda zilizotumika. Watunzi wa mashairi huteua maudhui kutokana na shughuli za jamii kama vile mikutano ya kisiasa na sherehe za arusi. Utafiti unahusisha ushairi na shughuli za jamii pamoja na mabadiliko ya kijamii katika jamii ya Waswahili. Jinsi ushairi unavyobadilika kiumbo na kimaudhui, jamii nayo inaendelea kubadilika ili kuangaza mabadiliko hayo. Mabadiliko hayo yanaeleweka vyema kupitia matumizi ya jazanda. Utafiti huo una manufaa kwa utafiti huu kwa sababu unadhihirisha kuwa, mshairi hutunga shairi kuhusu mambo yanayohusiana na shughuli za kila siku za jamii yake. Hata hivyo, utafiti huo ni tofauti na utafiti huu kwa sababu utafiti huo unashughulikia ufasiri wa shairi na matumizi ya jazanda jinsi yanavyosawiri mabadiliko ya kijamii ilhali utafiti huu unazingatia matukio yanayochochea mabadiliko ya kimaudhui ya ushairi.

1.7.2 Tafiti Kuhusu Sera ya Lugha

Marshall (2015) amechunguza jinsi Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki na Taasisi zilizofuatia kuanzia mwaka wa 1930 hadi 1970 zilivyotumika kuondoa ukoloni wa lugha ya Kiswahili. Utafiti huo umeeleza kuwa serikali za kikoloni za Waingereza zilizotawala nchi za Kenya, Uganda, Tanganyika na Zanzibar zilikuza lugha ya Kiswahili kama *Lingua Franca* katika nchi hizo. Sera ya lugha ya kukuza Kiswahili iliungwa mkono na Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki. Kufikia miaka ya 1920, Waingereza waliamua kukuza na kusanifisha Kiswahili ili kurahisisha mipango ya utawala wa koloni zao. Hata hivyo, katika miaka ya 1940, waligundua kuwa Lugha ya Kiswahili ilitumika kama chombo cha kuunganisha wananchi kupigania uhuru wao. Kwa hivyo, Waingereza waliamua kubadilisha sera ya lugha ya kueneza Kiswahili.

Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki iliyojihusisha na masuala ya kijamii iligeuzwa ikawa inashughulikia utafiti wa kiisimu na fasihi ya Kiswahili. Watanganyika wazalendo walijitolea kukuza Kiswahili kama ishara ya utaifa. Waliruhusu kamati iendelee na kazi yake kama taasisi ya utafiti. Taasisi hii ilitafiti na kukuza Kiswahili hata baada ya Tanganyika kupata uhuru. Matokeo ya utafiti huo yanabainisha kuwa ukoloni ulirahisishwa kwa kudhibiti lugha ya Waafrika. Vilevile, utafiti huo unadhihirisha kuwa ikiwa Waafrika wanataka kuzuia uharibifu wa kiutamaduni, wanapaswa kudumisha lugha za Kiafrika. Utafiti huo unaelezea shughuli za Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki zilizolenga kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili jambo linalofaa utafiti huu. Hata hivyo, utafiti huu ni tofauti kwa sababu ulichunguza jinsi shughuli za Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki zilivyochochea mabadiliko ya maudhui ya ushairi nchini Tanganyika.

Sera ya lugha katika elimu na maendeleo nchini Tanzania imefanyiwa utafiti na Eleuthera (2007). Ameangazia sera ya lugha kuanzia kipindi cha ukoloni hadi sasa kwa kuzingatia lugha ya Kiingereza na Kiswahili katika elimu. Ameshughulikia matumizi ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia katika shule za msingi na jinsi Kiingereza kinavyotumika katika shule za sekondari. Matokeo ya utafiti huo yanaonyesha kuwa, kuna matatizo ya sera ya lugha inayodidimiza viwango vya elimu, kwani wanafunzi wengi wanaacha masomo na wengine kuanguka mitihani kwa kutofahamu lugha ya Kiingereza katika shule za sekondari. Utafiti huo unadhihirisha kuwa viwango vya elimu vinaweza kuwa bora, lugha ya kufundishia ikiwa Kiswahili. Kwa hivyo, sera ya lugha inafaa kubadilishwa. Utafiti huo unabainisha athari ya utegemezi wa lugha za kigeni jambo linalofaa utafiti huu. Hata hivyo, utafiti huo unahusu sera ya lugha katika

elimu na maendeleo nchini Tanzania, tofauti na utafiti huu uliochunguza sera ya lugha kama mojawapo ya matukio yaliyochochea mabadiliko ya maudhui ya ushairi nchini Tanganyika.

Matatizo na changamoto zinazotokana na sera ya lugha na matumizi yake nchini Tanzania na Afrika Kusini yameshughulikiwa na Brock-Utne na Holmarsdottir (2004). Walichunguza athari ya sera za lugha katika ufundishaji wa wanafunzi darasani. Wameeleza kuwa sera ya lugha nchini Tanzania inatatiza kwa sababu Kiswahili ni lugha ya taifa na rasmi ingawa lugha ya Kiingereza ni rasmi pia. Suala la lugha halijashughulikiwa katika Katiba ya Tanzania. Katika Katiba ya Afrika Kusini, lugha rasmi ni kumi na moja kwa hivyo, sera ya lugha inabainika. Katika mataifa yote mawili, wanafunzi wengi wanatatizika kimasomo kwa sababu lugha za kufundishia ni za kigeni. Utafiti huo unaonyesha kuwa, ingawa kuna sera rasmi zilizotolewa, walimu wanatumia lugha yoyote ile wanayoweza kutumia vyema pamoja na wanafunzi wao. Baadhi ya mbinu ambazo walimu wanatumia ili kufanikisha ufundishaji ni tafsiri, kubadilisha msimbo na kuchanganya ndimi. Kwa hivyo, wanafunzi wanatatizika kwa sababu mitihani inachapishwa kwa Kiingereza. Jambo hili linachangia matokeo mabaya katika mitihani. Utafiti huo umebainisha kuwa sera ya lugha huathiri namna lugha inavyotumiwa kwa sababu husaidia jamii kujieleza, jambo linalofaa utafiti huu.Tofauti na utafiti huo, utafiti huu unazingatia athari ya sera ya lugha katika ubunifu wa maudhui ya ushairi wa Kiswahili.

Mkude (1999) amechunguza ujenzi wa demokrasia na sera ya lugha nchini Tanzania kwa kuzingatia Kiswahili /Kiingereza dhidi ya lugha za jumuiya ndogondogo. Lugha

za jumuiya ndogo ndogo ni lugha ambazo hazitumiki kwa ajili ya matumizi katika shughuli kuu za serikali. Ujenzi wa demokrasia ni utaratibu unaopania kufika na kutekeleza mpango wa kisiasa unaowapa wananchi mamlaka ya kufanya maamuzi kila wakati. Ushiriki mzuri wa wananchi wote unachukuliwa kufanyika palipo na ujuzi na mazoea ya lugha inayotumika kufanya maamuzi. Katika jamii yenye wasemaji wa lugha za jumuiya ndogo ndogo, inaweza kuhisi kuwa imetengwa na kuwekwa pembezoni kwa sababu ya kutojua lugha rasmi. Kwa hivyo, ni wajibu wa serikali kuchagua kwa ajili ya matumizi rasmi lugha inayofaa na madhubuti na kuwasaidia wananchi wote kuwa mahiri katika lugha hiyo. Lugha za kigeni hazifai kufikiriwa kupewa hadhi ya lugha rasmi kwa muda mrefu kwa sababu ya vipingamizi kadhaa. Kuzing'ang'ania ni kuendelea kuwaondoa watu wa kawaida kutoka katika mkondo unaowapa uwezo wa kisiasa na ukombozi wa kiuchumi. Hata hivyo, uwezo wa kutumia lugha hupaswa kuandamana na elimu ya jumla katika kanuni na amali za demokrasia kwa kutumia miundo rasmi na ile isiyokuwa rasmi. Utafiti unabainisha kuwa, lugha za kigeni hazifai jamii hasa watu wa kawaida. Pia, kutozimudu lugha za kigeni kunawazuia kushiriki vyema kisiasa na kiuchumi. Kwa hivyo, utafiti unagusia suala la kusitisha utegemezi wa lugha za kikoloni, jambo linalofaa utafiti huu. Tofauti kati ya utafiti huu na utafiti huo inaipa kazi hii nguvu kwamba, haja ipo ya utafiti zaidi kuhusu athari ya sera ya lugha katika ubunifu wa maudhui ya ushairi.

Moyd (1996) ametafiti uhusiano wa lugha na mamlaka kwa kuangazia Waafrika na Wazungu pamoja na sera ya lugha ya kipindi cha utawala wa Wajerumani nchini Tanganyika. Utafiti huo unatilia mkazo mtazamo wa Waafrika kuhusu sera ya lugha ya Wajerumani nchini Tanganyika. Pia, utafiti huo unaangazia jinsi Wajerumani na

Waafrika walivyotumia Kiswahili kwa njia tofauti. Utafiti huo unachunguza uchangamano wa sera ya lugha ya Wajerumani nchini Tanganyika kuanzia kipindi cha utawala wa Wajerumani katika mwaka wa 1890 hadi wakati wa Vita vya Majimaji vya mwaka wa 1905. Sera ya lugha ya Wajerumani ilitofautiana kutegemea makundi yaliyohusika katika ukoloni nchini Tanganyika. Makundi haya ni watawala wa Kijerumani, Wamishenari, maofisa wa serikali wa Wajerumani pamoja na Watanganyika. Ubaguzi wa rangi ulidhihirika katika utekelezaji wa sera ya lugha. Watawala wa kikoloni na Wamishenari wakati mwingine walizuia kupatikana kwa elimu isipokuwa kwa kutumia lugha zao. Utafiti huo unaelezea matumizi ya lugha ya Kiswahili kabla na baada ya ukoloni. Watanganyika kutoka sehemu mbalimbali wenye asili tofauti walitumia Kiswahili kwa mujibu wa matakwa yao. Matokeo ya utafiti yanabainisha kuwa, lugha hiyo ilikuwa chombo cha mawasiliano kwa walioelimika waliotumika kama wapatanishi kati ya watawala wa kikoloni na Waafrika waliotawaliwa. Ukinzani wa matakwa ya Waafrika na Wazungu, Wamishenari, watawala wa Kijerumani na Waafrika pamoja na wafanyakazi, ulizua mitazamo tofauti kuhusu sera ya lugha ya Wajerumani. Utafiti huo unaelezea sera ya lugha ya kipindi cha utawala wa Wajerumani nchini Tanganyika na jinsi ilivyotekelezwa na Wajerumani na Waafrika jambo linalofaa utafiti huu. Tofauti na utafiti huo, utafiti huu ulichunguza jinsi sera ya lugha ya kipindi cha utawala wa Wajeumani na Waingereza ilivyochochea ubunifu wa maudhui ya ushairi nchini Tanganyika.

Kuna tafiti zinazoshughulikia sera ya lugha nchini Kenya na Tanzania. Mbaabu (1991) amechunguza athari za sera ya lugha na maendeleo ya Kiswahili nchini Kenya kati ya mwaka 1930 hadi 1990. Katika utafiti wake, amechunguza sera ya lugha kama

inavyoelezwa katika makala za serikali na ripoti za tume mbalimbali za elimu. Alilenga kuelezea sababu ya kutoendelezwa kwa lugha ya Kiswahili licha ya kutangazwa kama lugha ya taifa nchini Kenya. Aidha, alilenga kueleza athari za sera ya lugha katika maendeleo ya Kiswahili nchini Kenya kwa kulinganisha na maendeleo yake nchini Tanzania. Utafiti huu uliongozwa na nadharia changamano: Nadharia ya Utegemezi na Nadharia za Sera za Umma na za Mpango wa Lugha. Utafiti huo uliufaa utafiti huu kwa kuelezea sera ya lugha katika elimu nchini Tanganyika. Kinyume na utafiti huo, utafiti huu ulichunguza uhusiano kati ya sera ya lugha na uteuzi wa maudhui ya ushairi nchini Tanganyika.

Rubagumya na Lwaitama (1990) wameshugulikia sera ya lugha katika suala la kisiasa na kiuchumi nchini Tanzania. Wameangazia matatizo yanayotokana na sera ya lugha na kupendekeza suluhisho. Sera ya lugha inaonyesha kuwa, Kiswahili hufundishwa kama somo katika shule za msingi na sekondari. Pia, Kiswahili ni lugha ya kufundishia katika shule za msingi lakini Kiingereza hutumiwa katika shule za sekondari na vyuoni. Matatizo yanayotokana na sera hii ni kwamba, hakuna walimu wa kutosha wa kufundisha kwa lugha ya Kiingereza. Pia, uchapishaji wa vitabu vya Kiingereza unagharimu fedha nyingi hivyo, hutegemea misaada ya kigeni. Aidha, wanafunzi wengi wana matatizo ya lugha ya Kiingereza. Kwa hivyo, ufundishaji huwa mgumu. Isitoshe, masuala ya kiteknolojia hayafundishwi vyema kwa sababu ya shida ya mawasiliano kati ya walimu na wanafunzi yanayotokana na matumizi ya Kiingereza. Wanapendekeza kuwa, shule chache za sekondari zitumie Kiingereza kama lugha ya kufundishia na zingine zote Kiswahili ili mwanafunzi achague shule aitakayo kutegemea uwezo wake wa lugha. Vilevile, Kiingereza kifundishwe kama somo katika shule zote. Kadhalika,

Kiswahili kitumike kama lugha ya kufundishia shule za msingi, sekondari na vyuo lakini Kiingereza kifundishwe kama lugha ya kigeni sawa na Kifaransa, Kichina, Kirusi na Kijapani. Matokeo ya utafiti yanabainisha kuwa, sera ya lugha ya sasa iliteuliwa kwa madai kuwa nchi za Afrika haziwezi kuendelea kijamii na kiuchumi bila usaidizi wa nchi za Ulaya zilizozitawala. Kwa hivyo, nchi za Afrika zinaendeleza utegemezi kwa kutumia lugha za kikoloni katika mawasiliano na elimu ya sayansi na kiteknolojia. Kwa sasa, katika masuala ya kisiasa na kiuchumi duniani, kuna haja ya kubadilisha sera za lugha zinazopendelea lugha ya kikoloni ili kuwasiliana na mataifa mengine duniani na kukuza lugha za kiafrika. Mataifa ya Afrika yanapaswa kuanza kufundisha Kijerumani, Kikolea, Kichina, na kadhalika. Pia, yanafaa kuteua lugha za Afrika kama lugha za kufundishia badala ya lugha ya Kiingereza, Kireno, na Kifaransa. Isitoshe, yanapaswa kufundisha masuala ya kisayansi na kiteknolojia kwa raia wake kwa lugha wanaoifahamu na rahisi kueleweka. Utafiti huo unagusia suala la utegemezi wa lugha za kikoloni na athari zake katika jamii, jambo linalofaa utafiti huu. Utafiti huo ulishughulika sera ya lugha katika suala la kisiasa na kiuchumi ilhali utafiti huu ulizingatia athari ya sera ya lugha katika ubunifu wa maudhui ya ushairi.

Mwansoko (1990) anachunguza dhima ya waundaji istilahi za Kiswahili katika kutekeleza sera ya lugha ya sasa nchini Tanzania. Anaeleza kuwa uteuzi wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya taifa na rasmi katika Tanzania huru iliongeza dhima na hadhi ya Kiswahili. Kiswahili kilianza kutumiwa katika shughuli nyingi za ndani za serikali pamoja na Bunge, kufundishia shule za msingi na uwezekano wa kufundishia shule za sekondari na mahakama za kiwango cha chini (Morrison, 1976). Jambo hili lilimaanisha kuwa kulikuwa na haja ya kuunda istlahi mpya. Sera ya lugha mwanzoni mwa mwaka

wa sabini, ilipendekeza matumizi ya lugha ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia katika shule za sekondari na vyuo ingawa ilibadilishwa katika mwaka wa 1984. Waundaji istilahi waliokuwa na motisha walisitisha kazi kutokana na mabadiliko hayo ya sera ya lugha. Utafiti huo unaonyesha haja ya kuendelea kuunda istilahi ili kukidhi mahitaji ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia na lugha ya kimataifa. Utafiti huo unabainisha kuwa, sera ya lugha huathiri ukuzaji na maendeleo ya lugha jambo linalofaa utafiti huu. Hata hivyo, utafiti huu ni tofauti kwa kuwa ulishughulikia sera ya lugha kama mojawapo ya matukio yaliyoathiri ubunifu wa maudhui katika kipindi cha ukoloni.

Isitoshe, sera ya lugha katika elimu nchini Tanzania imefanyiwa utafiti na Rugemalira, Rubagumya, Kapinga na wengine (1990). Walitoa maoni ya wanaisimu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika warsha iliyofanyika Disemba 1986. Walizingatia sera rasmi ya lugha ya kufundishia katika elimu. Walikiri kwamba, ijapokuwa Kiingereza ndio lugha rasmi ya kufundishia shule za sekondari, Kiswahili ndicho kinachotumika na kwamba lugha hii ndiyo ya pekee inayowafaa wanafunzi wa Tanzania kujifunzia masomo ya sekondari. Kuendelea kung'ang'ania Kiingereza kama lugha yenye hadhi katika elimu ya sekondari, kutaathiri maendeleo ya Kiswahili katika nyanja za taaluma. Pia, operesheni ya kuendeleza na kudumisha matumizi ya Kiingereza kama ile ya mradi wa miaka minne inayofadhiliwa na Shirika la Maendeleo ya Wingereza kwa Nchi za Nje (Britain Overseas Development Administration) haifai. Mradi huu hautakifanya Kiingereza kupata hadhi ya kuwa lugha ya elimu nchini Tanzania. Aidha, kuendelea kutumia lugha mbili kufundishia elimu kama ilivyo sasa itazifanya lugha zote kukwama na kuvia zisifae kufundishia wala kujifunzia. Wanaeleza kuwa mfumo wa elimu katika

jamii yoyote unafaa kutekelezwa kwa lugha inayotumiwa vyema na walimu na wanafunzi. Kwa upande wa Tanzania, Kiswahili ndiyo lugha inayofaa. Utafiti wao unaoanisha sera ya lugha na lugha za kufundishia nchini Tanzania. Utafiti huo una manufaa kwa utafiti huu kwa kudokeza kuwa, matumizi ya lugha ya Kiingereza kama lugha ya kufundishia unaendeleza hali ya utegemezi jambo ambalo halifaidi jamii. Tofauti na utafiti huo uliochunguza sera ya lugha katika elimu, utafiti huu unachunguza sera ya lugha ya kipindi cha ukoloni na athari zake katika ubunifu wa maudhui ya ushairi nchini Tanganyika.

Aidha, utafiti umefanywa na Mwanzi (1986) kuhusu sera ya lugha katika shule za msingi nchini Kenya. Utafiti huo, uliangazia athari za lugha ya Kiingereza kama lugha ya kufundishia katika shule za msingi. Matokeo ya utafiti yanabainisha kuwa, umilisi wa lugha ya Kiingereza unachukuliwa kuwa kigezo cha kuwa na elimu bora katika mazingira ya watoto. Pia, matumizi ya Kiingereza yanasaidia watoto kuwasiliana na wenzao wa jamii tofauti wanaotoka katika mazingira tofauti. Hivyo, ujifunzaji wa Kiingereza unatiliwa maanani na watoto na walimu. Kutokana na muktadha wa kihistoria, kisiasa na kiuchumi, Kiingereza kinachukuliwa kama lugha ya kimataifa inayowezesha wanajamii kushiriki katika shughuli za kimataifa. Kwa hivyo, matumizi yake kuanzia viwango vya chini vya elimu ni muhimu ili kuboresha matumizi ya baadaye. Ufanisi wowote wa shughuli za kielimu hutegemea lugha ya kufundishia. Uteuzi wa lugha hutegemea mtazamo wa wanafunzi na jamii kuhusu lugha husika. Vilevile, mtazamo wa watu wazima huwaathiri watoto. Ikiwa mtazamo wa watu wazima ni chanya, watoto watakuwa tayari kufunzwa kwa lugha husika. Pia, ikiwa watoto wenye mtazamo chanya masomo yao yatafanikiwa na kuboreshwa kutokana na

uwezo wao wa kuzingatia masomo darasani yanayotolewa kwa lugha ya Kiingereza. Utafiti huo unaonyesha uhusiano uliopo kati ya sera ya lugha na uteuzi wa lugha ya kufundishia. Utafiti huo una manufaa kwa utafiti huu kwani unabainisha kuwa, sera ya lugha huathiri matumizi ya lugha na mtazamo wa wanajamii kuhusu lugha fulani. Kadhalika, lugha hutumiwa na kuendelezwa ikiwa wanajamii wana mtazamo chanya kuihusu. Hata hivyo, utafiti huo umezingatia sera ya lugha katika shule za msingi ilhali utafiti huu ulilenga kuchunguza athari ya sera ya lugha katika ubunifu wa maudhui ya ushairi.

Kutokana na udurusu na tafiti za awali kuhusu mada, imebainika kwamba kuna tafiti nyingi zilizofanywa kuhusu ushairi wa Kiswahili. Tafiti zimeshughulikia muundo, mtindo, dhamira, fani na maudhui katika ushairi. Kinyume na tafiti hizo, utafiti huu ulizingatia matukio yaliyoathiri ubunifu wa maudhui ya ushairi katika kipindi cha urasimi mpya. Tafiti zingine zimezingatia sera ya lugha kwa kuihusisha na mamlaka, maendeleo ya Kiswahili, elimu, demokrasia na uundaji wa istilahi. Tofauti na tafiti hizo, utafiti huu ulizingatia sera ya lugha ya kipindi cha ukoloni nchini Tanganyika kama mojawapo ya matukio yaliyoathiri ubunifu wa maudhui. Aidha, utafiti unaohusu Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki umezingatia jinsi kamati hiyo ilivyotumika kueneza Kiswahili. Kinyume na utafiti huo, utafiti huu ulishughulikia athari za shughuli za Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki katika ubunifu wa maudhui. Utafiti huu umehitajika kufanywa ili kuziba pengo hilo.

1.8 Misingi ya Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia mbili ili ziweze kukamilishana katika kutimiza malengo ya utafiti. Nadhiria hizo ni: Nadharia ya Utegemezi na Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha.

1.8.1 Nadharia ya Utegemezi

Ukuaji wa Nadharia ya Utegemezi iliasisiwa mwaka wa 1948 kulipoundwa Tume ya Kiuchumi ya Umoja wa Mataifa ya Marekani Kusini yaani "United Nations Economic Commission for Latin America" (ECLA) chini ya mkurugenzi wake Raoul Prebisch. Tume hiyo iliundwa ili kutoa misaada ya kiteknolojia kwa mataifa ya Marekani Kusini. Baadhi ya waasisi wengine ni Paul Baran (1957) na Andre Gunder (1969). Prebisch na wenzake walikuwa wamegundua kuwa ukuaji na maendeleo ya kiuchumi katika mataifa tajiri ulisababisha shida nyingi za kiuchumi katika mataifa yanayoendelea. Sababu zilizotolewa ni kwamba, mataifa yanayoendelea huuza bidhaa nyingi kwa mataifa tajiri yanayotengeneza bidhaa tofauti na kisha kuyauzia mataifa yanayoendelea. Hivyo, nchi zinazoendelea hazipati faida yoyote. Jambo hili liliwafanya waangazie uhusiano uliopo kati ya mataifa yanayoendelea na mataifa tajiri.

Nadharia ya Utegemezi ilitumiwa kuelezea hali hii ya tofauti za kiuchumi za kimataifa. Wana Umaksi Mpya walikuwa wamechukulia tofauti hizi kama tokeo la unyanyasaji wa kibepari. Katika mfumo wa ubepari, mali inamilikiwa na idadi ndogo ya watu. Watu hao wanaipata mali yao kutokana na unyonyaji wa umma na hasa wafanyakazi. Sunkel (1969) anaeleza, utegemezi kama maendeleo ya kiuchumi ya nchi kwa kuzingatia athari za nje za kisiasa, kiuchumi na kitamaduni katika sera za maendeleo ya kitaifa.

Dos Santos (1971) anasisitiza kipengele cha historia katika mahusiano ya utegemezi. Anaeleza kwamba "kihistoria miundo ya uchumi wa dunia unapendelea nchi fulani huku ukiathiri zingine na kudidimiza uwezekano wa kuendelea kiuchumi. Hali hii inasababisha uchumi wa mataifa fulani kutegemea kukua na kuendelea kwa mataifa mengine."

Kutokana na maelezo ya Sunkel na Dos Santos kwamba utegemezi unabainisha mifumo ya kimataifa inayogawika katika matapo mawili: tapo kitovu na tapo pembezoni. Tapo kitovu ni tapo linalohusisha mataifa yaliyoendelea kiuchumi. Mataifa haya ni yale ambayo yana maendeleo ya kiviwanda yaliyo katika Shirika la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo yaani *Organisation of Economic Cooperation and Development* (OECD). Tapo pembezoni ni tapo la mataifa yanayoendelea hasa Marekani Kusini, nchi za Asia na Afrika. Nchi hizi hutegemea uuzaji wa bidhaa chache ili kupata fedha za kigeni. Masuala ya kiuchumi yanapata athari za nje katika mataifa yanayoendelea. Athari hizi ni pamoja na mashirika ya kimataifa, ufadhili wa kigeni, mawasiliano na njia zingine zozote ambazo mataifa yaliyoendelea hutumia ili kujiwakilisha kiuchumi katika mataifa ya kigeni.

Uhusiano wa nchi zilizoendelea na zinazozoendelea unabadilika kwa sababu nchi hizo huinuana na kuongeza ruwaza zisizo sawa. Isitoshe, utegemezi hutokana na mifumo ya kihistoria inayotokana na ubepari wa kimataifa. Kwa mujibu wa Gunder Frank (1972), utafiti wa kihistoria unaonyesha kuwa ukosefu wa maendeleo katika nchi zinazoendelea ulitokana na matukio ya kihistoria ya kiuchumi ya zamani ya nchi zinazoendelea. Pia,

ulitokana na mahusiano ya kibiashara kati ya nchi hizo. Mahusiano hayo ndiyo sehemu muhimu ya mifumo ya kibepari duniani.

Nadharia ya Utegemezi imetumiwa na waandishi wengi kama Walter Rodney (1972), Frantz Fanon (1952), Mohamed Babu (1994), Ibrahim Hussein (1971), Ali Mazrui na Alamin Mazrui (1995). Rodney katika kitabu chake *How Europe Underdeveloped Africa* (1972), anaeleza kuwa ukosefu wa maendeleo katika nchi za Afrika ulitokana na unyanyasaji wa nchi za Ulaya. Mataifa ya Afrika yalikuwa na maendeleo yake kabla ya ukoloni lakini walipoteza nguvu za kisiasa na kiuchumi kutokana na biashara ya watumwa na ukoloni. Ukoloni ulisambaratisha uchumi wa Afrika na kuboresha maendeleo ya kiteknolojia katika mataifa ya Ulaya kwa maana hii, mifumo ya ubepari na unyanyasaji imeathiri Afrika pakubwa. Wakoloni waliathiri utamaduni, sanaa, fasihi na miundo ya kifamilia ya Waafrika. Kwa kuwa Waafrika walipoteza nguvu zao za kisiasa na kiuchumi, hawangeweza kutetea utamaduni, siasa au uchumi wao.

Frantz Fanon kwa upande mwingine ametumia Nadharia ya Utegemezi katika vitabu vyake: *Black Skins, White Masks* (1952), *The Wretched of the Earth* (1961) na *Toward the African Revolution* (1964). Maandishi yake, ameonyesha jinsi Waafrika walivyopoteza utu na utamaduni wao kutokana na ukoloni. Anapendekeza walionyanyaswa watetee uhuru hata kama wangetumia vita. Fanon (1952: 25) anasema kuwa watu weusi wanapotumia lugha ya mkoloni wanapoteza utamaduni wao na kumiliki ule wa mkoloni. Ujuzi wa lugha ya mkoloni unaotambuliwa na mkoloni unaakisi utegemezi unaoshusha hadhi ya watu weusi.

Mataifa mengi ya Afrika yanategemea lugha za kikoloni jambo linalosababisha utegemezi wa kiutamaduni. Mtu anapojifunza lugha ya kigeni anaanza kuonea fahari mitindo ya mavazi, chakula, nyimbo, sinema, mfumo wa elimu, dini na mambo mengine yanayoweza kuwa na athari hata za kiuchumi (Mbaabu, 1996: 8).

Matumizi ya lugha za kikoloni katika elimu barani Afrika kumeathiri ukuaji wa lugha za kiafrika. Pia, utamaduni na fasihi simulizi za Waafrika zinapotea kwa kutegemea lugha za kikoloni. Nchi za Afrika zenye lugha asilia iliyoenea ni kama Kenya na Tanzania zinazotumia Kiswahili kama lugha ya taifa. Hata hivyo, ni nchi ya Tanzania pekee inayotumia lugha ya kiafrika hasa Kiswahili kama lugha ya kufundishia katika shule za msingi kote nchini (Abdulaziz, 1971: 160-178). Hivyo, lugha nyingi za Kiafrika zinakabiliwa na hatari ya kutoweka kwa kuwa hazitumiki katika kutolea elimu. Ingawa lugha za kikoloni haziwezi kutupiliwa mbali, athari zake zinaweza kupunguzwa kwa kukuza lugha za kiafrika zitumike kutolea elimu ya msingi pamoja na matumizi mengine ya kitaifa (Mbaabu, 1996: 13).

Utafiti huu uliongozwa na mihimili ya Nadharia ya Utegemezi inayohusu jinsi ya kusitisha hali ya utegemezi wa lugha za kigeni. Ngugi wa Thiong'o katika kitabu chake *Decolonosing the Mind: The Politics of Language in African Literature* (1986), ameeleza jinsi ya kusitisha utegemezi wa lugha za kigeni. Anasema kuwa ikiwa mataifa ya Afrika yatasitisha utegemezi wa lugha za kikoloni, yanapaswa kupandisha vyeo lugha za Kiafrika zenye hadhi ya chini ili zitumike katika nyanja tofauti. Hivyo, mihimili iliyotumika ni hii ifuatayo:

(i) Ukoloni unahusu kusambaratisha ama kutothamini kimakusudi utamaduni wa jamii (Ngugi, 1986: 16). Mhimili huu ulitusaidia kuchunguza jinsi hali ya utegemezi wa lugha za kigeni iliweza kuondolewa kwa kutetea na kuitukuza lugha ya Kiswahili nchini Tanzania katika kipindi cha ukoloni. Utafiti huu ulichunguza jinsi washairi walivyotukuza Kiswahili katika tungo zao.

(ii) Ili kuondoa utegemezi wa lugha za kigeni, Waafrika wanapaswa kutetea na kudumisha uchumi, siasa, utamaduni, lugha na waandishi wazalendo wa Afrika (Ngugi, 1986: xii). Mhimili huu ulitusaidia kuchunguza jinsi washairi walivyotetea utamaduni, lugha, siasa na kutukuza waandishi wa Afrika katika mashairi yao.

(iii) Jamii inayonuia kujikomboa kutokana na ukoloni haina budi kutumia lugha yao ya kienyeji kuwaunganisha watu ili kuwa na umoja kwa lengo la kuleta ukombozi (Ngugi, 1986: 3). Mhimili huu ulitumiwa kubainisha mchango wa washairi katika kutetea na kukuza lugha ya Kiswahili Tanzania huku baadhi yao wakiwa wanachama wa Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki kama vile Shaaban Robert.

iv) Uteuzi na matumizi ya lugha katika jamii ndio unaotambulisha jamii kwa kuihusisha na mazingira na ulimwengu kwa jumla (Ngugi, 1986: 13). Mhimili huu ulitumiwa kubainisha kanuni za utunzi wa mashairi zilizotumika katika utunzi wa mashairi.

1.8.2 Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha

Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha ina misingi yake katika kazi za Pierre Bourdieu na kuendelezwa na Monica Heller (2010), David Block (2010), Deborah Cameron

(2012) na Alexandre Duchene (2012). Dhana ya ubidhaaishaji imeweza kutumika katika Isimujamii. Dhana hii ni ya kisasa inayohusu mabadiliko ya lugha na utambulisho wake katika sehemu mbalimbali duniani inayotokana na sera za kiuchumi na utekelezaji wake katika kipindi hiki. Wanaisimu wameelezea vile lugha inaweza kubadilishwa kuwa bidhaa muhimu katika soko kwa kutumia miktadha ya mahali pa kazi, biashara, utalii na elimu (Cameron, 2012: 352).

Lugha inapochukuliwa kuwa bidhaa inamaanisha kuwa kuna soko ambalo lugha hiyo huweza kuuzwa kwa vile ina thamani. Dhana ya soko la lugha ina misingi yake katika maandishi ya Pierre Bourdieu. Bourdieu katika kitabu chake *Language and Symbolic Power* (1991) anaeleza uhusiano wa lugha, utawala na siasa. Anachukulia lugha sio tu kama chombo cha mawasiliano lakini kama uwezo fulani unaomfanya mtu kufuata mambo anayoyapenda ama kuonesha umilisi alionao. Anashikilia kuwa usemi fulani unaweza kueleweka kama zao la uhusiano kati ya "soko la lugha" na "mazoea ya lugha" (Bourdieu, 1991: 38). Watu hutumia maneno kulingana na mahitaji ya kijamii au ya soko yaani hadhira inayokusudiwa. Kwa hivyo, kila mahusiano ya kilugha hata kama ni ya kibinafsi huashiria muundo wa jamii inayoelezewa. Mawazo yake yanaeleza upya njia ambazo matumizi ya lugha yanatofautiana kutegemea hadhi na jinsia. Pia, mawazo yake yanatoa mtazamo mpya wa vile lugha hutumika katika siasa kwani maneno huashiria matendo na sifa za utawala.

Kulingana na Block (2010: 294), ubidhaaishaji wa lugha ni njia ya kuondoa thamani ya lugha fulani kutokana na matumizi yake ya kimsingi ya mawasiliano na utambulisho wa kitaifa na kiutamaduni na kuipa thamani kwa kuwa na matumizi mengine duniani.

Park na Wee (2012: 125) wanasema kuwa kuna uwezekano wa kuchukulia lugha kama rasilmali ya kiuchumi inayoweza kukuzwa iwe na faida ili ipate kuuzwa. Ufafanuzi huu unatokana na mawazo ya Monica Heller. Kulingana na Heller, ubidhaaishaji wa lugha unaweza kuelezwa kwa njia mbili. Kwanza, lugha ambayo ilikuwa inahusishwa na kazi, umilisi wa kimasomo, elimu na mawazo ya kiakili inabadilishwa na kuwa bidhaa kama pesa. Pili, lugha inayobadilishwa na kutumika kama bidhaa hutegemea uwezo wake wa kutumika kwa mfano, mtu anapotafuta kazi.

Ubidhaaishaji ni dhana inayoeleza michakato mbalimbali inayobadilisha uwezo wa lugha na kuwa faida. Mabadiliko haya yachukua miundo tofauti kama ujuzi wa lugha fulani kuwa rasilmali katika mfumo wa uzalishaji ama kuinua biashara, uwezo wa kuajiriwa ama matumizi katika eneo fulani. Katika mfumo huu, lugha fulani zinaeleweka kuwa na thamani maalum inayoziongoza kuwa na faida inayozifanya kuenea. Isitoshe, michakato ya ubidhaaishaji imeweza kuchanganuliwa katika muktadha wa kutolea elimu ya juu, utalii, lugha ya kimaeneo ama katika uzalishaji wa bidhaa za kuuzwa kama kadi, vikombe au shati zenye maandishi au maneno ya lugha asilia.

Kulingana na Shitemi (2011: 4) lugha ni bidhaa yenye umuhimu na thamani ya kisarafu katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kwa hivyo, inahitaji kupangiwa, kuendelezwa, kudumishwa na kuwezekewa. Pia, lugha ni bidhaa na sarafu maalum yenye kuwekewa thamani katika viwango mbalimbali vya mahusiano ya kibinadamu kwa mujibu wa majukumu inayochangia na kutimiza miongoni mwa wanajamii na mikakati yao ya kuendeleza maisha (Shitemi, 2011: 5).

Mihimili ya Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha iliyotumika ni kama ifuatayo:

1. Lugha hutumiwa na watu kulingana na mahitaji ya kijamii au "soko" yaani hadhira inayokusudiwa. Mhimili huu ulitusaidia kuchunguza maudhui ya mashairi ili kudhihirisha masuala muhimu yaliyoshughulikiwa kabla ya uhuru wa Tanganyika.
2. Lugha inayochukuliwa kuwa yenye faida katika jamii huenea. Mhimili huu ulitusaidia kuchunguza mchango wa mashairi katika kuenea kwa Kiswahili kwa kushughulikia masuala ya kisiasa.
3. Lugha hutumika sio tu kama chombo cha mawasiliano lakini hubainisha uwezo fulani unaomfanya mtu aonyeshe umilisi wa lugha alionao. Mhimili huu ulitusaidia kuchunguza jinsi washairi walivyoteua maudhui ili kuwasilisha ujumbe katika mashairi yao.

1.9 Mbinu za Utafiti

Muundo wa utafiti huu ni uchanganuzi wa matini. Data iliyopatikana maktabani ilitosheleza mahitaji ya utafiti huu uliohusisha kipindi cha kabla ya uhuru wa Tanganyika kati ya mwaka wa 1930 hadi 1960. Ingawa utafiti haukuhusisha kitengo cha nyanjani, matokeo ya utafiti huu hayakuathirika kwa kuwa, utafiti huu ni wa kihistoria uliozingatia uchanganuzi wa matini zilitungwa katika kipindi cha ukoloni. Data iliyotumika katika utafiti huu ilikusanywa kutoka kwa diwani nane za mashairi zilizoteuliwa. Diwani hizo ni *Koja la Lugha* (1969), *Kielezo cha Fasili* (1968), *Masomo Yenye Adili* (1967), *Pambo la Lugha* (1966), *Mashairi ya Saadan* (1966), *Diwani ya Mnyampala* (1965), *Diwani ya Akilimali* (1963) and *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri* (1954). Uteuzi wa diwani hizo ulifanywa kwa kutumia mbinu kusudio

kwa kuwa zinadhihirisha mashairi yenye maudhui yaliyozingatiwa katika utafiti huu. Usomaji na uhakiki wa mashairi yaliyoteuliwa ulifanywa. Vilevile, udurusu wa maandishi kuhusu uhakiki wa kazi za fasihi hasa ushairi ulifanywa ili kupata maarifa zaidi. Maoni hayo yalisaidia katika kuupa msingi utafiti kinadharia na katika ukusanyaji wa data.

1.9.1 Sampuli

Uteuzi wa watunzi wa mashairi pamoja na diwani zilizoshughulikiwa ulifanywa kwa kutumia mbinu kusudio. Mbinu ya usampulishaji kusudio ilitumiwa ili kupata data kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Mashairi yaliyoteuliwa ni yale yaliyobeba maudhui yafuatayo: sifa kwa lugha ya Kiswahili, umuhimu wa utunzi wa mashairi, kanuni za utunzi wa mashairi, siasa na uongozi. Mashairi yasiopungua mia moja yalishughulikiwa. Mbinu ya usampulishaji kusudio ilitumiwa kwa sababu inahusu uteuzi wa vitafitiwa kutegemea maamuzi ya mtafiti kutokana na vigezo anavyozingatia (Orodho, 2009: 147). Diwani ziliteuliwa kwa msingi kwamba zilitungwa kwa Kiswahili sanifu katika kipindi cha ukoloni na watunzi wake walikuwa maarufu nchini Tanganyika. Kadhalika, diwani hizi zina mashairi ya arudhi yaliyozingatiwa katika utafiti huu. Isitoshe, mbinu kusudio ilitumika katika kuteua watunzi wa mashairi kutoka nchi ya Tanganyika na waliotunga katika kipindi cha ukoloni. Kwa hivyo, uteuzi wao wa maudhui umeathiriwa na mazingira sawa.

1.9.2 Ukusanyaji wa Data

Data ilikusanywa kwa kusoma mashairi teule kutoka diwani za watunzi wafuatao: Abedi (1954), Mnyampala (1965), Akilimali (1963), Robert (1966, 1967, 1968, 1969) na Kandoro (1966). Diwani nne za Shaaban Robert zilichunguzwa kwa sababu mashairi kutoka diwani moja hayakubeba maudhui yote yaliyozingatiwa katika utafiti huu. Diwani zilizoteuliwa zilikuwa na maudhui yaliyozingatiwa zikilinganishwa na diwani zingine za Shaaban Robert. Mashairi yaliyoteuliwa yalisomwa na kuhakikiwa ili kubainisha maudhui yaliyomo. Maudhui yote yalipangwa katika makundi manne kwa sababu kila kundi liliwakilisha lengo la utafiti wenye malengo manne. Kundi la kwanza lilijumuisha mashairi yenye maudhui ya sifa kwa lugha ya Kiswahili. La pili lilihusu umuhimu wa utunzi wa mashairi. La tatu lilishughulikia kanuni za utunzi wa mashairi na la nne lilizingatia siasa na uongozi.

Maudhui ya sifa kwa lugha ya Kiswahili yalibainika pale mshairi anasifu Kiswahili, anahimiza watu wajifunze Kiswahili na anaonyesha umuhimu wa Kiswahili. Maudhui ya umuhimu wa utunzi wa mashairi yanabainika pale mshairi anasifu magazeti ya Kiswahili, anashauri watunzi wa mashairi, anaeleza umuhimu wa mashairi na kuonyesha ubingwa wa kutumia Kiswahili.

Maudhui ya kanuni za utunzi wa mashairi yanabainika pale mshairi anahimiza utunzi wa mashairi ya arudhi. Maudhui ya siasa na uongozi yanabainika pale mshairi anaeleza sifa za viongozi bora, anaeleza umuhimu wa uzalendo, anatetea uhuru wa Tanganyika , anasifu vyama vya kisiasa, anaonyesha umuhimu wa umoja wa Afrika na anatetea utu na utamaduni wa Mwafrika.

1.9.3 Uchanganuzi wa Data

Data zilizokusanywa ziliwasilishwa kwa njia ya maelezo. Data hizo zilipangwa kwa makundi manne kila kundi likiwakilisha lengo la utafiti. Mashairi yenye maudhui sawa yaliwekwa katika kundi moja na kuchambuliwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti na kuhakikiwa kwa kuongozwa na mihimili ya Nadharia ya Utegemezi na Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha. Data zote zilizokusanywa zilihakikiwa na kupangwa kimantiki ili kubaini kwa urahisi data zinazojibu maswali ya utafiti.

1.9.4 Matokeo

Matokeo ya utafiti huu yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Kuambatana na lengo la kwanza, matokeo yalihusu jinsi sera ya lugha ya kipindi cha ukoloni kati ya mwaka 1930 hadi 1960 ilivyoathiri ubunifu wa maudhui ya ushairi. Kutokana na lengo la pili, maelezo yalihusu jinsi shughuli za Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki zilivyoathiri ubunifu wa maudhui ya ushairi. Kwa kuzingatia lengo la tatu, maelezo yalihusu jinsi kanuni za utunzi wa mashairi zilivyoathiri ubunifu wa maudhui ya ushairi. Kuambatana na lengo la nne, maelezo yalihusu namna harakati za upiganiaji uhuru wa Tanganyika kati ya mwaka 1950 hadi 1960 zilivyoathiri ubunifu wa maudhui ya ushairi.

1.10 Hitimisho

Katika sura hii, msingi wa utafiti umewekwa kwa kuelezea maudhui ya vipindi tofauti vya kihistoria vya ushairi wa Kiswahili. Maudhui ya ushairi yamekuwa yakibadilika kadri jamii inavyobadilika kwa mujibu wa wakati. Maudhui ya ushairi wa kipindi cha

urasimi mkongwe yalihusu mafunzo ya kidini, ushujaa, wosia, siasa na uongozi. Maudhui yalibadilika wakati wa muhula wa utasa, mashairi yalibeba maudhui ya vita, unyanyasaji na ukatili. Maudhui hayo yalibadilika katika kipindi cha ukoloni kutokana na matukio ya kipindi hicho cha urasimi mpya. Utafiti ulilenga kuchunguza matukio yaliyoathiri ubunifu wa maudhui ya kipindi cha ukoloni ili kuendeleza suala la maendeleo na mabadiliko ya ushairi wa Kiswahili. Nadharia zilizotumiwa katika uchanganuzi wa data zimejadiliwa ambapo Nadharia ya Utegemezi na Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha zimejadiliwa. Tafiti zilizofanywa kuhusu ushairi wa Kiswahili zimefafanuliwa. Tafiti kuhusu ushairi wa Kiswahili zimezingatia muundo, mtindo, dhamira na maudhui.Tafiti kuhusu maendeleo na mabadiliko ya ushairi wa Kiswahili zimechunguza ushairi wa kipindi cha urasimi mkongwe kwa kuzingatia masuala ya kisiasa, kijamii na kiuchumi. Tafiti zilizofanywa zimebainisha kuwa, hakuna utafiti uliofanywa kwa kuzingatia matukio yaliyochochea mabadiliko ya kimaudhui ya ushairi wa kipindi cha ukoloni nchini Tanganyika. Pia, hakuna utafiti uliofanywa kwa kutumia nadharia zilizotumiwa katika utafiti huu.

Katika sura ifuatayo, uchunguzi umefanywa wa jinsi ya sera ya lugha ya kipindi cha ukoloni nchini Tanganyika ilivyochochea mabadiliko ya kimaudhui ya ushairi wa Kiswahili.

SURA YA PILI

SERA YA LUGHA NA MAUDHUI YA USHAIRI

2.0 Utangulizi

Sura iliyotangulia iliweka msingi wa jumla wa utafiti. Ilieleza usuli, suala la utafiti, malengo, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada, msingi wa nadharia pamoja na mbinu za utafiti. Ilibainika kuwa maudhui ya ushairi wa Kiswahili yamekuwa yakibadilika katika vipindi tofauti vilivyofuatia urasimi mkongwe. Udurusu wa kazi zinazohusiana na mada hii unadhihirisha kuna haja ya utafiti kuhusu matukio yaliyochochea mabadiliko ya kimaudhui katika ushairi wa Kiswahili.

Sura hii ililenga kuchunguza jinsi sera ya lugha ya kipindi cha ukoloni ilivyochochea mabadiliko ya maudhui ya ushairi nchini Tanganyika kati ya mwaka wa 1930 hadi 1960. Kwa kuwa Tanganyika ilitawaliwa na Wajerumani na Waingereza, sera ya lugha ya vipindi vyao vya utawala ingezingatiwa ili kuchunguza jinsi ilivyoathiri maendeleo ya Kiswahili hasa kipengele cha ushairi. Ili uhusiano huo ufahamike vilivyo ilibidi kufahamu msingi wake.

2.1 Dhana ya Sera ya Lugha

Sera ya lugha ni maamuzi yanayofanywa na watawala na wanasheria wenye majukumu ya kufanya maamuzi yanayoathiri utendaji na taratibu za matumizi ya lugha katika kiwango cha kitaifa (Gorman, 1974: 397). Kwa mujibu wa Fasold (1988: 187), sera ya lugha inahusu matendo rasmi ya serikali yanayoamua hadhi ya lugha na muundo wake. Spolsky (2004: 262) anaongezea kuwa, sera ya lugha inahusu maamuzi ya hadhi, matumizi, mipaka ya lugha pamoja na haki za wazungumzaji wa lugha husika.

Kwa mujibu wa Buliba, Kimani na Mwihaki (2006: 115), sera ya lugha ni maamuzi ya kudhamiria yanayoipa lugha hadhi mahsusi katika jamii. Ni maamuzi yanayofanywa na watu wenye madaraka ya kiutawala na kisheria. Pia, ni maamuzi yanayohusu uchaguzi wa kisheria; uchaguzi wa lugha za kutumiwa katika nyanja mbalimbali zinazodhibitiwa na vyombo vya dola kama vile bunge, shule, mahakama na kadhalika. Kwa kuwa nyanja hizi za mawasiliano ni za kitaifa, basi uchaguzi wa lugha itakayochaguliwa unahusu pia uchaguzi wa lugha za taifa na rasmi na namna zitakavyoendelezwa. Aidha, sera ya lugha ni maamuzi juu ya matumizi ya lugha yanayochukuliwa au yanayofanywa na asasi zenye majukumu ya kimamlaka na kisheria ambazo maamuzi yake yanaathiri taratibu na utekelezaji wa shughuli na mpango wa kitaifa (Mathooko, 2007: 116).

Kutokana na fafanuzi hizo, inadhihirika kuwa, sera ya lugha ni mojawapo ya sera za umma kwa kuwa inahusu maamuzi yanayoathiri raia wa nchi husika. Kwa kuwa sera huundwa kutegemea mahitaji ya jamii, huzingatia amali, imani na malengo ya kitaifa kutegemea rasilmali zilizopo. Hivyo, sera ya lugha ni muhimu katika maendeleo ya kiuchumi, mabadiliko ya kijamii na utimizaji wa malengo ya kitaifa (Dubhashi, 1986: 19). Katika kiwango cha kitaifa, sera ya lugha hujaribu kutambua mahitaji ya kilugha ya taifa kwa kuzingatia jamii na makundi mbalimbali ya kitamaduni. Vilevile, hutambua majukumu ya lugha mbalimbali katika maisha ya wananchi wa taifa linalohusika. Aidha, huunda mikakati inayohitajika katika kusimamia na kukuza au kustawisha nyenzo na rasilmali za lugha.

Sera ya lugha ina vipengele viwili muhimu: sera inayohitaji kufuatwa na lugha inayochaguliwa au zilizochaguliwa ambazo sera hiyo huzingatia au hutilia maanani. Vipengele hivi hufuatwa na utathmini wa sera nzima na uchaguzi wa lugha. Kwa hivyo, sera ya lugha hulenga kutoa mwongozo au uamuzi kuhusu utaratibu wa matumizi ya

lugha, mwelekeo wa matumizi ya lugha katika jamii, kutoa ushauri kwa watawala kuhusu utumiaji wa lugha na kuelezea tabia na mwenendo wa lugha kulingana na namna inavyotumiwa katika jamii.

2.1.1 Upangaji wa Lugha

Lo Bianco (2010: 143-176) anachukulia upangaji wa lugha kama sehemu ya sera za umma inayohusu mabadiliko ya matumizi ya lugha kupitia mitazamo ya wazungumzaji kuhusu lugha katika mawasiliano. Hivyo, anaoanisha maamuzi yanayofanywa na viongozi na matumizi ya lugha katika jamii. Kwa mujibu wa Cooper (1989: 30), upangaji wa lugha ni utaratibu unaoleta mabadiliko ya matumizi ya lugha, ujifunzaji na uzungumzaji pamoja na ukuzaji wa lugha unaotekelezwa na taasisi za kiserikali ama mashirika mengine ya kijamii. Haugen (1966: 50-71) anaeleza kuwa, upangaji wa lugha ni utathmini wa mabadiliko ya lugha. Ni shughuli ya kutayarisha tahajia, sarufi na kamusi sanifu ili kuwaongoza wazungumzaji katika jamii yenye lugha tofauti. Rubin na Jernudd (1971: xiv) wanaonelea kuwa, upangaji lugha ni juhudi za kimakusudi za kuleta mabadiliko katika lugha ya maandishi au ya mazungumzo au zote mbili zinazochukuliwa na taasisi zilizoundwa kutekeleza jambo hili. Upangaji lugha hunuia kumaliza matatizo ya lugha kwa kuchukua uamuzi ulio bora zaidi. Upangaji lugha ni mbinu ya kuchunguza mabadiliko ya lugha ili kuweza kufanya ubashiri kuhusu jinsi ya kutekeleza mabadiliko hayo. Pia, unamaanisha maendeleo, utekelezaji na utathmini wa mbinu maalum za kutatua matatizo mahsusi ya lugha katika kiwango cha kitaifa. Katika nchi zenye lugha nyingi, mpango wa lugha huhitajika ili kupata lugha itakayotumika kwa manufaa ya jamii katika kuendeleza na kudumisha uchumi, biashara, umoja na uelewano wa jamii. Kutokana na fafanuzi hizi inadhihirika kuwa, upangaji wa lugha ni

utaratibu wa kuweka mikakati ya kuendeleza lugha na kugawa majukumu ya lugha katika jamii.

Upangaji wa lugha huwa na viwango viwili muhimu. Katika kiwango cha kwanza, sera kuhusu uteuzi wa lugha ndio jambo la kimsingi. Uteuzi wa lugha hutekelezwa na viongozi wa kisiasa kwani hufuata sana maongozi ya siasa katika taifa linalohusika. Uteuzi wa lugha huzingatia jukumu au hadhi itakayopewa lugha ilioteuliwa kuwa lugha ya taifa au rasmi. Wanasiasa huchunguza lugha ifaayo kuteuliwa kwa kuzingatia baadhi ya masuala kadha kama vile maoni ya wananchi na wataalamu kuhusu uteuzi wa lugha, idadi ya watu wanaotumia lugha husika, matakwa ya taifa kama vile elimu, biashara, mawasiliano ya kimataifa pamoja na umaarufu wa lugha ya kimaandishi na kimazungumzo (King'ei, 2010:11).

Kiwango cha pili ni kile cha kuhakikisha kuwepo kwa mfumo mmoja uliokubalika wa kuizungumza au kuiandika lugha iliyoteuliwa. Utaratibu wa kuhakikisha mfumo sawa wa kuitamka au kuiandika lugha hujulikana kama kusanifisha lugha. Hivyo, lugha sanifu ni ile lahaja au lugha iliyoteuliwa ili kutumika katika shughuli zote za kitaifa hasa katika elimu na sheria pamoja na utawala. Usanifishaji hutekelezwa kwa mwongozo wa wataalamu wa lugha wakishirikiana na serikali kupitia mashirika au taasisi za umma kama vile vyuo vikuu, mashirika ya utafiti au elimu. Upangaji na uendelezaji wa lugha huongozwa na sera thabiti ya lugha inayopangwa na kuandaliwa huku ikijikita katika hatua nne.

2.1.2 Hatua za Upangaji Lugha

Haugen (1983: 269-290) anapendekeza hatua nne zinazohusiana na upangaji lugha kama zifuatazo:

1) Kuchagua lugha au uchaguzi wa msimbo. Huku ni kuamua ni lugha gani itakayotumiwa,

2) Ufafanuzi wa msimbo. Huku ni kule kuamua mitindo au nyanja nyingine za matumizi ya lugha. Ni kutenga mitindo na maeneo ya utumiaji wa lugha hiyo,

3) Utekelezaji wa majukumu. Huku ni kusambaza msimbo wa lugha uliochaguliwa na kufafanuliwa. Ni kueneza muundo wa lugha ambayo imechaguliwa na

4) Usambazaji. Huku ni kuendeleza, kutekeleza au kutumia msimbo kukabiliana na majukumu ya kiisimu na kitamaduni.

Kando na hatua hizi nne, Haugen (1983) anapendekeza mpango wa lugha uzingatie mambo yafuatayo:

1) Hali ya kiuchumi ili kuchunguza kama nchi ina uwezo wa kutekeleza mpango wa lugha,

2) Hali ya kijamii ili kuchunguza kama mpango wa lugha unazingatia idadi ya lugha za kijamii na jinsi zinavyoingiliana na

3) Hali ya kisiasa inachunguza msimamo wa watawala na watawaliwa kuhusu mpango wa lugha.

Ufanisi wa upangaji wa lugha kwa kiasi kikubwa unategemea ukubalifu wa wananchi wanaoongozwa. Hata hivyo, shughuli za upangaji lugha ni za kisiasa kwani zinahusu wanasiasa kuliko wanaisimu. Utekelezaji nao pia uko mikononi mwa serikali. Kwa hivyo, serikali ina jukumu kubwa katika kuandaa sera ya lugha.

2.2 Sera ya Lugha ya Kipindi cha Wajerumani (1895-1918)

Tanganyika ilikuwa ni sehemu ya koloni ya Wadachi iliyokuwa inaitwa “Deutsch Ostafrika” yaani Afrika ya Mashariki ya Wadachi. Eneo hili lilikuwa linajumuisha pia

nchi za Rwanda na Burundi. Nchi ya Tanganyika ilianza kutawaliwa na Wajerumani kuanzia mwaka wa 1885 hadi 1917. Hata hivyo, Wajerumani hawakutawala kwa muda mrefu baada ya kushindwa Vita vya Kwanza vya Dunia (Mbaabu, 1991: 46).

Wajerumani walipoanza kutawala Tanganyika mwaka wa 1885, lugha ya Kiswahili ilikuwa imeenea katika nchi (Petzell, 2012: 1). Kiswahili kilikuwa kimeenezwa na Waarabu na wafanyabiashara Waswahili hadi sehemu za bara katika vituo vya biashara vya Tabora na Ujiji. Pia, wamishenari wa Kikatoliki na Kiprotestanti walikuwa wameanzisha misheni na shule zao katika eneo la pwani. Lugha ya Kiswahili ilitumiwa kufundishia au kama mojawapo ya masomo yaliyofundishwa pamoja na ya kiufundi. Kwa hivyo, Kiswahili kilitumika kama linguafranka katika Tanganyika hata kabla ya kuja kwa Wajerumani.

Badala ya kuchagua Kiswahili kama lugha ya utawala, Wajerumani waliamua kutumia Kijerumani katika utawala na elimu. Walijaribu kufunza masomo yote katika shule walizoanzisha kwa Kijerumani lakini hawakufanikiwa. Walibadili nia na kutumia Kiswahili katika utawala na elimu. Kwa kufanya hivyo, waliinua hadhi ya Kiswahili. Polome na Hill (1980: 181) wanaeleza kwamba, walifanya ujuzi wa lugha ya Kiswahili kuwa muhimu katika maeneo nje ya pwani na vituo vya biashara. Marcia (1965: 40) anaongeza kuwa, Wajerumani walitumia Kiswahili kama lugha ya utawala kwa kuwa ndiyo iliyokuwa mwafaka. Hivyo, walitetea lugha ya Kiswahili iliyopingwa na Wamishenari waliopendelea lugha za kienyeji.

Uteuzi wa Kiswahili kama lugha ya utawala pamoja na Kijerumani ulipingwa na baadhi ya wamishenari wa Kiprotestanti waliokihusisha Kiswahili na maenezi ya dini ya Kiislamu kutoka pwani hadi bara. Wamishenari walisisitiza matumizi ya lugha za

kienyeji. Kwa upande mwingine, wamishenari wa Kikatoliki wa Kiroma walikuwa wanatumia Kiswahili katika umisheni. Wamishenari wa Kikatoliki wa Kiroma na wa Kianglikana walitumia Kiswahili isipokuwa katika Buhaya pale ambapo Waafrika walikipinga (Iliffe, 1979: 210). Hata hivyo, Waprotestanti wa Kijerumani walisisitiza matumizi ya lugha za kienyeji. Utawala wa Wajerumani ulipoanza kuwafadhili wamishenari hao katika shule zao, upinzani uliisha (Malik, 1996: 156). Ufadhili huu ulilenga kupata wafanyakazi wenye ujuzi ambao wangepewa nafasi za kazi zilizokuwa zinaongezeka katika utawala. Kulingana na Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, lugha inaweza kubadilishwa na kuwa bidhaa muhimu katika "soko" au jamii kutokana na matumizi yake katika muktadha wa mahali pa kazi (Cameron, 2012: 352-361). Hivyo, lugha ya Kiswahili ilipewa hadhi ya juu kutokana na mahitaji ya kijamii au "soko" ya kuweza kupata ajira wakati wa utawala wa Wajerumani.

Wajerumani walikuwa na mashamba makubwa ya kahawa katika maeneo ya Bukoba, majani chai katika maeneo ya Kagera na mkonge katika maeneo ya Tanga. Katika mashamba hayo, wafanyakazi walikuwa Waafrika kutoka pwani na bara ambao walitumia Kiswahili kuwasiliana. Hali hii ilisaidia kueneza matumizi ya Kiswahili katika mashamba hayo. Pia, wafanyakazi hao waliporudi makwao waliendelea kutumia Kiswahili na hata wakaingiza katika Kiswahili maneno kutoka lugha zao za kwanza. Hivyo, walichangia upanuzi wa msamiati wa Kiswahili. Maelezo haya yanabainisha kuwa Wajerumani walikieneza Kiswahili kwa sababu kilitumika katika utawala na elimu. Kwa hivyo, waliinua hadhi ya Kiswahili nchini Tanganyika.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, lugha inayochukuliwa kuwa yenye faida katika jamii huenea (Park na Wee, 2012: 26). Hivyo, Waafrika walieneza

lugha ya Kiswahili kwa sababu ilikuwa chombo cha mawasiliano. Aidha, Wajerumani walikienzi Kiswahili kwa sababu kilitumika katika utawala na elimu.

2.2.1 Sera ya Lugha ya Wajerumani katika Utawala

Wajerumani walilazimika kujifunza Kiswahili ili waweze kuhudumu katika utawala wa Kijerumani. Walipotoka Ujerumani walishauriwa kujifunza Kiswahili huko kwao kabla ya kuja Tanganyika na hali hii ilisaidia Kiswahili kuenea. Yeyote ambaye hangekimudu, hakuruhusiwa kuajiriwa katika utawala wa Kijerumani. Hali hii iliwatia ari Waafrika wengi kujifunza Kiswahili ili wapate nafasi ya kuajiriwa. Wajerumani waliwaajiri watu wa pwani walioweza kuzungumza kwa Kiswahili na waliopata elimu kutoka shule za Kurani kulikofunzwa kusoma na kuandika kwa hati za Kiarabu (Kaniki, 1980: 201). Iliffe (1979: 208) anaongeza kuwa, Soden, Gavana wa kwanza wa Tanganyika aliyetawala sehemu ya pwani alitaka kuwa na mahusiano na watu wa bara. Kwa azma hii, aliwatumia watu wa pwani waliozungumza Kiswahili katika mahusiano hayo.

Watawala wa Kijerumani waliteua wawakilishi wao yaani Akida, Jumbe na Liwali katika sehemu mbalimbali za nchi na wawakilishi hao walitakiwa kujifunza Kiswahili. Cheo cha chini kilikuwa ni cha Mwalimu, cha kati ni cha Akida na cha juu kilikuwa cha Liwali. Maliwali walikuwa wenye asili ya Waarabu waliofanya kazi katika makao makuu ya wilaya. Kulingana na Ingham (1962), Maakida walishughulikia masuala ya sheria na uamuzi wa kesi pamoja na kuchukua kodi kwa niaba ya serikali. Pia, walitafuta wafanyakazi wa serikali wa kazi za mikono au wa mashamba ya watu binafsi. Maakida walikuwa wazee wa vijiji au sehemu zilizoitwa jumbe. Maakida wengi walifanya kazi yao bila usimamizi na waliweza kuelewana na watu. Hata hivyo, wengine walikuwa katili (Maxon, 1986: 166). Maakida walipata vyeo vya uongozi kutokana na ujuzi wa lugha ya Kiswahili jambo ambalo lilisababisha watu wengi kutamani ujuzi wa lugha

hiyo hasa katika sehemu za bara. Hivyo, ujuzi wa lugha ya Kiswahili ulionekana kama njia ya kujiendeleza kwani mtu angepata ajira, apandishwe cheo na apate mshahara mkubwa (Iliffe, 1969: 158). Ripoti zote walizozitoa kwa viongozi wao Wajerumani ziliandikwa kwa Kiswahili. Ripoti yoyote isiyokuwa kwa Kiswahili ingepuuzwa. Kwa hivyo, hali hii ilichangia kukua na kuenea kwa Kiswahili. Hata hivyo, baadhi ya Waafrika walikipinga kwa kukinasibisha na hao Maakida na Maliwali ambao walikuwa wakiwakilisha utawala wa dhuluma.

Katika kipindi cha ukoloni, lugha ya Kiswahili ilitumika kama chombo cha mawasiliano miongoni mwa Watanganyika. Tena, ilitumika katika utawala wa mikoa kama lugha rasmi. Kiswahili kilitumika kama njia ya kufikia watu lakini sio ya watu kufikia watawala (Malik, 1996: 155-159). Ujuzi wa lugha ya Kiswahili ulikuwa ni njia moja ya kuweza kushirikishwa katika ajira ya ngazi ya chini. Mtu alihitaji ujuzi wa lugha ya Kiingereza ili kupata ajira ya ngazi ya juu. Kwa sababu hiyo, Watanganyika waliona Kiswahili kama lugha ya kiwango cha chini ndiposa washairi wakakitetea.

Kulingana na Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, maelezo haya yanathibitisha kuwa, lugha hupewa hadhi kutokana na majukumu inayochangia na kutimiza miongoni mwa wanajamii pamoja na mikakati yao ya kuendeleza maisha. Lugha ya Kiswahili ilipewa hadhi ya juu kutokana na matumizi yake katika utawala na ajira.

2.2.2 Sera ya Lugha ya Wajerumani katika Elimu

Katika miaka ya 1890 lugha ya Kiswahili iliteuliwa kama lugha ya utawala wa Wajerumani. Kwa kufanya hivi Wajerumani waliinua hadhi ya lugha ya Kiswahili katika sehemu za bara na sehemu zilizokuwa mbali na vituo vya misafara ya biashara. Wajerumani walianza kutoa elimu kwa Waafrika na lugha ya kufundishia ilikuwa Kiswahili ili Waafrika waweze kuchukua nafasi za kazi za kiutawala. Walihitaji

makarani na mafundi katika utawala, wafanyakazi wa reli na mashamba (Polome na Hill, 1980: 201). Kwa hivyo, shule zilifunguliwa katika sehemu nyingi nchini. Kadri shule za watawala zilivyofunguliwa katika sehemu mbalimbali nchini, ndivyo Kiswahili kilivyoenezwa katika sehemu zingine nje ya vituo vya misafara ya biashara na pwani.

Ingawa lugha zingine hazikupuuzwa, Kiswahili kilipendelewa kwa kuwa kilikuwa kimefanyiwa utafiti na kuandikiwa vitabu. Kwa mfano, J. Krapf wa dhehebu la CMS aliandika kitabu kilichoitwa *Outline of the Elements of the Kiswahili Language with Special Reference to the Kinika Dialect* mnamo mwaka wa 1850. Kitabu hicho alikiandika katika lahaja ya Kimvita. Pia, aliandika Kamusi inayoitwa *Dictionary of the Swahili Language* mnamo mwaka wa 1882 (Whiteley, 1969: 13). Kulikuwa pia na Kitabu cha Askofu Edward Steere wa dhehebu la UMCA: "*A Handbook of the Swahili Language as Spoken in Zanzibar."* Kitabu hicho kilichapishwa mwaka wa 1870 katika lahaja ya Kiunguja. Kulingana na Were na Wilson (1968: 208), wamishenari walihimizwa na watawala kuanzisha shule za Waafrika. Kufikia mwaka wa 1914 Waafrika 155,000 walikuwa shuleni. Pia, watawala walijenga shule za viwango vyote katika vituo vikuu vya biashara. Kufikia mwanzoni mwa Vita vya Kwanza vya Dunia, wanafunzi 6,000 walikuwa katika shule za watawala. Matokeo yake ni kuwa, Wajerumani walipata Waafrika ambao wangefanya kazi za ukarani na wa kuhudumu katika utawala waliozungumza Kiswahili.

Wamishenari walifungua shule nyingi ambazo zilitoa mafunzo katika fani mbalimbali kama vile useremala na uashi ambapo lugha ya kufundishia ilikuwa Kiswahili. Kulingana na Iliffe (1979: 223), mashirika ya Kiprotestanti ya Kijerumani yaani GPS kama vile wamishenari wa Bethel (BM) kufikia mwaka wa 1911 walikuwa na wanafunzi zaidi ya elfu mbili katika shule zao. Wamishenari hawa walipinga sana elimu

lakini walipendekeza ujifunzaji wa kazi za mikono. Walifundisha Kiswahili katika shule moja tu yao.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, maelezo haya yanabainisha kuwa, lugha ya Kiswahili ilikuwa kama bidhaa muhimu kwa sababu ilikuwa inatumiwa kulingana na mahitaji ya kijamii ya kuwatolea elimu. Kupitia njia hii, Kiswahili kilienea.

Wafanyakazi kama vile makarani walikuwa wakihamishwa kila mara kutoka sehemu moja hadi nyingine nchini. Wafanyakazi walipelekwa sehemu yoyote bila kujali kama wangefahamu lugha ya wenyeji au la. Kwa hivyo, walilazimika kutumia lugha ya Kiswahili. Kwa sababu hiyo, Wajerumani walianzisha shule kwa madhumuni ya kuwafunza Waafrika wachache ambao wangehudumu katika utawala kwa kufanya kazi ndogo ndogo kama za ofisini, mahakamani na za ulinzi. Hatua hii ilisaidia Kiswahili kukua na kuenea kwa sababu kilitumiwa kufundishia shuleni. Wanafunzi wengine walitumwa Zanzibar kwa masomo zaidi ya ualimu na ukarani katika Chuo cha Mtakatifu Andrea cha UMCA. Katika chuo hiki wanafunzi wa asili mbalimbali waliwasiliana kwa Kiswahili kama inavyoripotiwa katika sehemu ya barua iliyoandikwa na mwanafunzi mmoja mwezi wa Januari mwaka wa 1894. Wamishenari walianzisha vituo vya kueneza Injili ambapo Kiswahili kilitumiwa katika mahubiri. Whiteley anaeleza kuwa, mara nyingi vituo hivyo vilijengwa kwenye njia za misafara ya biashara ili kurahisisha mawasiliano baina ya wamishenari hao. Kwa mfano, kulikuwa na vituo huko Mombasa, Zanzibar, Tanga, Bagamoyo, Ujiji na Tabora. Pia, wamishenari walitafsiri maandiko ya Biblia kwa Kiswahili (Whiteley 1969: 53-57).

Kulingana na Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, lugha yenye faida katika jamii huenea. Kwa kuwa Waafrika walitumia Kiswahili katika mahubiri pamoja na kusoma Biblia za Kiswahili, lugha ya Kiswahili ilienea nchini Tanganyika.

Wajerumani walianzisha shule mjini Tanga katika mwaka wa 1893 ili kuwafunza Waafrika waweze kuchukua nafasi za maafisa wa ngazi za chini katika utawala. Kufikia mwaka wa 1903, kulikuwa na shule nane za serikali, kumi na mbili za utawala wa mitaa na kumi na tano za wamishenari. Ingawa Kijerumani kilifundishwa kama somo shuleni, Kiswahili kilitumiwa kama lugha ya kufundishia (Rubagumya, 1990: 6). Wasomi kama Velten Seidel, Buttner na wengine walitoa vifaa ambavyo vingetumika kufundishia kozi hiyo kutoka Berlin. Gavana Rechenberg aliyetawala kuanzia mwaka wa 1906 hadi 1912 pamoja na Gavana aliyefuatia H. Schenee, walikuwa wanazungumza Kiswahili kwa kuwa walikuwa wamesoma kozi hiyo. Sio watawala na masetla pekee waliojifunza na kuzungumza Kiswahili lakini pia wamishenari ingawa baadhi walijifunza lugha za kienyeji za sehemu walikoishi na kufanya kazi.

Elimu ilisisitizwa na kufikia mwaka wa 1911 idadi ya wanafunzi ilikuwa 30,000 katika shule za msingi, watawala wakawa 3,500 na wanafunzi 2,500 wakawa wanapata elimu ya juu. Shule nyingi zilikuwa za msingi zilizomilikiwa na wamishenari. Lugha ya kufundishia ilikuwa Kiswahili ingawa kulikuwa na chache zilizofundishwa kwa Kijerumani (Clarke, 1960: 106). Vitabu vilianza kuchapishwa na wamishenari wa UMCA katika misheni ya Magila. Waliandika historia ya Shambala iliyojulikana kama *Habari za Wakilindi* mwaka wa 1905. Pia, waliandika katika magazeti ya kwanza kwa Kiswahili: *Masimulizi* (1888) na *Habari za Mwezi* (1884). Wamishenari wa GPM katika mwaka wa 1910 walitoa magazeti ya *Pwani na Bara* kila mwezi yaliyofikia nakala 2,000 kufikia mwaka wa 1914. Wamishenari wa dhehebu la Wakatoliki walitoa gazeti

la *Rafiki Yangu* kila mwezi lililokuwa na mafunzo ya kidini (Whiteley, 1969: 60). Kufikia mwaka wa 1910 nakala 11,000 za vitabu vidogo vilivyojulikana kama *Barazani* viliuziwa umma. Hivyo, kuna ushahidi wa kutosha unaoonyesha kuwa wananchi waliweza kusoma magazeti na vitabu vya Kiswahili na kupitia njia hii Kiswahili kilienea nchini.

Kulingana na Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, lugha huwa kama bidhaa muhimu inapoeleweka kuwa na thamani maalum inayoiongoza kuwa na faida inapohusishwa na kazi, umilisi wa kimasomo na elimu (Heller, 2010: 101-104). Kwa hivyo, kutokana na majukumu ya Kiswahili kama nyenzo ya kujipatia elimu wakati wa utawala wa Wajerumani, Watanganyika walijifunza na kukieneza Kiswahili.

2.3 Sera ya Lugha ya Kipindi cha Waingereza (1918-1961)

Baada ya Vita vya Kwanza vya Dunia, Waingereza waliitwaa sehemu ya Afrika Mashariki ya Wadachi kwa mkataba maalum wa Umoja wa Mataifa yaani "League of Nations" katika mwaka wa 1919. Tarehe moja, Februari mwaka wa 1920, sehemu ya koloni ya Wadachi bila nchi za Rwanda na Burundi ilipewa jina la Tanganyika (Nsekela, 1965:1). Kwa hivyo, wakoloni waliofuata Wajerumani walikuwa Waingereza. Waingereza walipoanza kutawala waliuona mpango wa Wajerumani wa kutumia Kiswahili kuwa wa manufaa sana katika kujenga utawala wao. Hata hivyo, waliona utawala wao ungekabiliwa na hatari kama lugha ya Kiswahili ingetumiwa peke yake kwa sababu Kiswahili kingepata hadhi ya juu kuliko Kiingereza. Kiingereza kiliteuliwa kama lugha rasmi huku Kiswahili kikitumika katika utawala wa wilaya na mikoa.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Utegemezi, ukoloni unahusu kusambaratisha ama kutothamini kwa makusudi utamaduni wa jamii. Kwa hivyo, ingawa lugha ya Kiswahili

ilikuwa imeenea na kutumika katika utawala na elimu, ilidunishwa na wakoloni kwa kuinua hadhi ya Kiingereza jambo lilioathiri maenezi ya Kiswahili.

Katika mwaka wa 1925, Waingereza walibadilisha mpango wa elimu. Lugha zilizotumiwa kufundishia madarasa ya kwanza zikawa ni lugha za kienyeji. Kiswahili kilitumiwa kufundishia madarasa ya kati na Kiingereza katika madarasa ya juu. Waingereza walifanya kazi kubwa katika kuendeleza na kuieneza lugha ya Kiswahili. Azma yao kubwa ilikuwa ni kupata njia rahisi ya kuwapatia watu elimu ya msingi, elimu ambayo ilihitajika sana kwa ajili ya kuwapata wasaidizi wa watawala wao wa ngazi za chini. Waingereza waliiona lugha ya Kiswahili kuwa duni. Sera zao hazikuruhusu itumiwe kama lugha ya kufundishia katika shule za viwango vilivyokuwa zaidi ya shule za msingi, badala yake Kiingereza ndicho kilichotumiwa katika shule za sekondari na vyuo. Katika viwango vya juu vya elimu, Kiswahili kilifundishwa tu kama somo miongoni mwa masomo mengine. Hata wamishenari waliona umuhimu wa kutumia lugha iliyojulikana na watu wengi hata kama hawakupenda mahusiano yake na Uislamu. Hata hivyo, kutokana na sera hiyo, Kiswahili kilipewa nafasi ya chini ofisini kwa sababu kilitumiwa na watu wa tabaka la chini. Pia, taasisi za elimu ya juu za wanafunzi wa Afrika Mashariki hazikufunza Kiswahili lakini zilitumia Kiingereza ili kuwadhihirishia wanafunzi umuhimu wake.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, lugha inapochukuliwa kama bidhaa hupewa thamani na kuwa na matumizi mengine zaidi ya matumizi yake ya kimsingi ya mawasiliano na utambulishi wa kitaifa na kiutamaduni (Block 2010: 287-304). Hivyo, kwa kuwa ujuzi wa Kiswahili ulihitajika kama chombo cha kutolea elimu na utawala, Waingereza hawakuwa na budi kukitumia katika elimu. Kwa njia hii walikikuza na kukiendeleza Kiswahili kote nchini Tanganyika.

Waingereza walitumia Kiswahili katika jeshi zima lililoitwa Jeshi la Waafrika la Mfalme yaani K.A.R. Jeshi hili lilikuwa likitumika katika nchi zote za Afrika Mashariki. Kwa mujibu wa Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, lugha ni kama bidhaa na sarafu muhimu yenye kuwekewa thamani katika viwango mbalimbali vya mahusiano ya kibinadamu kwa mujibu wa majukumu inayochangia na kutimiza miongoni mwa wanajamii. Kwa kuwa Kiswahili kilikuwa lugha ya mawasiliano katika nchi za Afrika Mashariki, kiliteuliwa kuwa chombo cha mawasiliano jeshini. Kupitia njia hii, Kiswahili kiliweza kuenea.

Pia, Kiswahili kilitumiwa mahakamani katika kushughulikia kesi za Waafrika ingawa ripoti na hukumu za kesi ziliandikwa kwa Kiingereza na baadaye zilitafsiriwa kwa Kiswahili ili kuwawezesha washtakiwa kuzielewa. Whiteley (1969: 62) anaeleza kuwa, lugha ya mahakama za kiwango cha chini ilikuwa ni Kiswahili lakini mahakama za juu zilitumia Kiingereza. Ni dhahiri kuwa Kiswahili kilitumika kama lugha rasmi sawa na Kiingereza.

Watumishi wote wa serikali na wale wa madhehebu ya kidini waliamrishwa kuufanya na kufuzu mtihani mgumu wa Kiswahili kabla ya kuruhusiwa kufanya kazi zilizohusiana moja kwa moja na maisha ya wananchi. Kazi hizo ni pamoja na biashara, kilimo na uinjilisti. Ingawa Waingereza walitumia Kiswahili kueneza siasa zao nchini Tanganyika, lugha iliyotumiwa kutekeleza shughuli muhimu za serikali ni Kiingereza. Watanganyika wangeweza kuajiriwa kazi za ngazi za juu pamoja na kupandishwa cheo kazini kama wangefaulu vyema katika Kiingereza. Roy -Campbell (2001) anaeleza kuwa, Waingereza walikuwa na mpango wa kuwa na kundi ndogo la wasomi nchini Tanzania ambao wangetumiwa katika utawala huku Watanganyika wengi wakiwa na elimu ya kiwango cha chini. Nafasi za utawala na vyeo vya hadhi ya juu vilihusishwa

na ujuzi wa lugha ya Kiingereza (Roy-Campbell, 1995: 27). Maelezo haya yanadhihisha kuwa, Waafrika waliendelea kutegemea lugha ya mkoloni iliyopewa hadhi ya juu ikilinganishwa na Kiswahili ili kupata cheo kazini.

Nadharia ya Utegemezi inasisitiza kwamba, ukoloni unahusu kusambaratisha ama kutothamini kwa makusudi utamaduni wa jamii (Ngugi, 1986: 16). Hivyo, Waingereza waliendeleza utegemezi wa kiutamaduni kupitia utegemezi wa lugha ya kikoloni ya Kiingereza.

Ingawa Kiswahili kilisisitizwa sana shuleni, ofisini na kufanywa katika mitihani kilipewa nafasi ya pili baada ya Kiingereza. Kwa mujibu wa Mazrui na Mazrui (1995:9), Kiswahili kilikuwa lugha ya mawasiliano iliyopewa hadhi ya wastani kati ya lugha ya hadhi ya juu ya Kiingereza na lugha za kienyeji za hadhi ya chini. Sera ya lugha ya Waingereza iliwafanya Watanganyika kukichukulia na kukiona Kiswahili kama lugha duni ambayo haingewafaa isipokuwa katika viwango vya chini. Hata hivyo, ijapo Waingereza walitatiza maenezi ya Kiswahili, walichangia maendeleo yake kwa namna nyingine. Waingereza waliunda Kamati ya Lugha ya Afrika mashariki (I.L.C) mnamo mwaka wa 1930. Kamati hiyo ilikuwa na jukumu la kusanifisha na kukuza Kiswahili (Mbaabu, 2007: 26). Kulingana na Polome (1967: 24), kamati hiyo ya lugha ilichangia pakubwa katika maenezi ya Kiswahili na matumizi yake katika maandishi kwa kufadhili utafiti wa kiisimu, kuhimiza uandishi wa fasihi, kusimamia utoaji wa kamusi na vitabu pamoja na kutoa maamuzi kuhusu miswada iliyoletewa kamati kabla ya uchapishaji. Mbaabu (1985: 206) anaongezea kuwa, kazi ya kamati hii iliweka msingi imara katika maendeleo ya Kiswahili. Vilevile, kamati ilianzisha shirika la uchapishaji wa vitabu (E.A.L.B) mnamo mwaka wa 1948. Shirika hili lilichapisha vitabu vingi kwa lugha ya

Kiswahili (Gorman, 1974: 424). Hii ni ithibati kuwa sera ya lugha ya kipindi cha utawala wa Waingereza iliendeleza lugha ya Kiswahili.

Katika kipindi cha ukoloni Kiswahili kilikuwa maarufu kwa sababu kilikuwa kimekuzwa na kusambazwa kutoka pwani hadi bara kupitia misafara ya biashara ya Waarabu, utawala wa kikoloni na wamishenari. Kwanza, wamishenari walikifanyia Kiswahili utafiti na wakaandika vitabu. Ludwig Krapf wa shirika la C.M.S alichapisha kitabu chake, *Swahili Grammar*, mnamo mwaka wa 1850 naye Askofu Edward Steere wa shirika la U.M.C.A akachapisha kitabu: *A Handbook of the Swahili Language* mnamo mwaka wa 1870 (Mbaabu, 2007: 9). Pia, wamishenari walifungua shule nyingi ambazo zilitoa mafunzo mbalimbali kama vile useremala na uashi, ambapo lugha ya kufundishia ilikuwa Kiswahili. Vilevile, wamishenari walianzisha vituo vya kueneza Injili ambapo Kiswahili kilitumiwa katika mahubiri. Aidha, wamishenari walitafsiri maandiko ya Biblia kwa Kiswahili. Isitoshe, wamishenari walianza kuchapisha magazeti kwa Kiswahili. Maelezo haya yanadhihirisha kuwa, wamishenari walichangia maenezi ya Kiswahili kwa njia tofauti.

Kulingana na Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, watu hutumia lugha yenye thamani na faida kwa wanajamii, jambo linalofanya lugha hiyo kuenea. Hivyo, Kiswahili kiliendelezwa na wamishenari kwa sababu kilikuwa chombo cha kuenezea Injili.

Kutokana na maelezo kuhusu sera ya lugha ya kipindi cha ukoloni, imedhihirika kuwa, Wajerumani na Waingereza waliendeleza na kueneza lugha ya Kiswahili kutokana na umuhimu wake katika utawala. Kulingana na Watanganyika, Kiswahili kilikuwa lugha yenye hadhi kuliko lugha zao za kienyeji (Malik, 1996: 155). Watunzi wa mashairi wa kipindi cha ukoloni walijitahidi kukuza Kiswahili kwa kutunga mashairi kwa Kiswahili

sanifu ili kubainisha hadhi yake. Washairi waliweka kamusi ndogo ya msamiati uliotumika katika diwani zao kwa mfano, Abedi (1954:134-148). Msamiati waliouunda uliendelea kutumiwa na wenyeji na hata ukaingizwa katika kamusi za wakati huo au za baadaye. Kulingana na Shitemi (2010: 7), washairi walishikilia kuzieneza kunga za utunzi na wakaziandikia na kuzihifadhi katika maandishi yao. Tungo nyingi zilitungwa na kuchapishwa ama katika magazeti au katika vitabu. Kwa hivyo, kwa kuwa mashairi haya yaliandikwa kwa Kiswahili sanifu, yalieneza na kukuza Kiswahili.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Utegemezi, Waafrika wanapaswa kutetea na kudumisha lugha na utamaduni wao ili kuondoa utegemezi wa lugha za kikoloni. Hivyo, washairi walisitisha utegemezi wa lugha za kikoloni kwa kueneza na kukuza Kiswahili kupitia utunzi wa mashairi ya Kiswahili. Watunzi wa mashairi waliisifu lugha ya Kiswahili na kuelezea umuhimu wake kwa Watanganyika. Baadhi ya mashairi yao yanabeba maudhui ya Kiswahili.

2.4 Maudhui katika Ushairi

Kwa mujibu wa Msokile (1993: 88), maudhui ni mawazo, fikra na ujumbe uliomo katika kazi ya fasihi. Naye Senkoro (2011: 1) anaeleza kuwa, maudhui ya kazi ya fasihi hujumuisha mawazo na pengine mafunzo mbalimbali yaliyomsukuma mtunzi ama msanii hadi akatunga na kusana kazi fulani ya sanaa. Kulingana na Njogu na Chimerah (1999: 21), maudhui ni ujumbe wa jumla kuhusu matukio, kitu, wahusika au hali ya maisha kama yanavyojitokeza katika kazi ya fasihi, iwe riwaya, tamthilia, ushairi au wimbo. Kutokana na maelezo hayo ni wazi kuwa, kila kazi ya fasihi huwa na maudhui yake.

Maudhui katika ushairi yametolewa fafanuzi mbalimbali. Kwa mujibu wa King’ei na Kemoli (2001: 50), maudhui ni jumla ya mambo, mawazo, mafundisho na ujumbe

unaowasilishwa na mshairi kwa hadhira yake. Kisia na Mwarandani (2007: 8) wanaeleza kuwa, maudhui ni yale masuala yanayozungumziwa na mtunzi wa shairi. Kutokana na fafanuzi hizo inadhihirika kuwa maudhui huwa ni jambo kuu liongelewalo na kushughulikiwa katika shairi. Maudhui ni ujumbe mkuu au muhimu unaojitokeza katika shairi.

Maudhui kila wakati hubadilika kulingana na hali ya mazingira na utamaduni. Utamaduni unapobadilika, mabadiliko hayo hujitokeza katika maudhui ya fasihi ya watu wake (Mazrui, 1988: xiii). Kwa mfano, Muyaka alitunga mashairi ya uzalendo na vita katika enzi za ukoloni wa Waarabu mjini Mombasa. Alitunga mashairi yaliyowatia moyo na ari wenyeji wa pwani kwa kupinga juhudi za kutawaliwa ndiposa akatunga shairi "Mkija Mtaviweza" (Abdulaziz, 1979: 133-134). Kulingana na Wamitila (2002: 96), tungo za ushairi za mwanzo mwanzo zilikuwa na dhamira na maudhui ya kidini lakini tungo za baadaye zilipanuka kidhamira na kujihusisha na masuala ya kijamii, kiuchumi, kisiasa, kisaikolojia na kadhalika. Mulokozi (1999: vi) anashadidia maelezo hayo kuwa, ushairi wa Kiswahili una historia ndefu kwa sababu ulianza kuandikwa kwa hati ya Kiarabu katika karne ya kumi au kabla. Uandishi uliambatana na imani ya dini ya Kiislamu. Hivyo, tenzi nyingi zilizoandikwa wakati huo zilihusu dini. Kwa mfano, dhamira kuu ya *Utendi wa Inkishafi* ni kufafanua maana ya maisha inayohusiana na dini ya Kiislamu. Kwa hivyo, mabadiliko ya usanii wa maudhui ya ushairi wa Kiswahili hufuatia mabadiliko katika sera ya maisha ya jamii kwa ujumla (Masinde, 1992: 19).

Maudhui hupimwa kwa kutegemea wakati wa wale wanaoandikiwa; inafaa zaidi kuandikia jamii mambo ambayo yanawagusa kwa kipindi chao (Kuvuna, Mvati na Maliachi, 1992:21). Kwa hivyo, mshairi huhakikisha kwamba anazungumzia mambo ambayo anafikiri jamii inayahitaji katika wakati huo. Massamba (1983: 80) anaongeza

kuwa, mshairi anapotunga shairi, hutoa hisia au maoni yake juu ya jambo fulani. Maoni hayo hutolewa kufuatana na jinsi anavyoliona jambo lile na anavyoamini kuhusu jambo hilo. Hata hivyo, mshairi hupima na kuona kama hayo anayotaka kusema au kuandika yana uzito wowote katika jamii. Kwa hivyo, mshairi huhakikisha kwamba anazungumzia mambo ambayo anafikiri jamii inayahitaji katika wakati huo.

2.5 Ushairi na Hadhi ya Lugha

Sera ya lugha ya kipindi cha ukoloni iliunga mkono matumizi ya lugha ya Kiswahili. Mashairi yaliyotungwa katika kipindi cha ukoloni yaliinua hadhi ya lugha ya Kiswahili tofauti na lugha za kienyeji. Watunzi wa mashairi walieleza sifa na umuhimu wa Kiswahili nchini Tanganyika katika mashairi yao.

2.5.1 Shairi "Lugha Yetu Kiswahili"

Mnyampala (1965) katika shairi "Lugha Yetu Kiswahili", anasifu lugha ya Kiswahili kwa kutaja sifa zake. Katika ubeti wa kwanza anasema:

> Siachi kuisifia, lugha yetu Kiswahili,
> Wenyewe twajivunia, twaitumia kuwili,
> Kama wali kwa samli;
> Samli wali kitia, utadharau ugali,
> Asokula hujutia, moyoniwe umdhili,
> Lugha yetu Kiswahili, twazama na kuibuka (Mnyampala, 1965: 123).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, hataacha kuisifu lugha ya Kiswahili kwa kuwa ni tamu. Anailinganisha na wali uliotiwa samli kwa kuwa ni mtamu hasa ukilinganishwa na ugali. Kwa hivyo, Kiswahili hakiwezi kulinganishwa na lugha nyingine. Pia, anasema asiyekitumia hujiaibisha mwenyewe kwa kuwa Kiswahili ndio lugha ya watu wote.

Isitoshe, mshairi anabainisha kuwa, Kiswahili hutumiwa kutoa kauli na mafumbo kwa wale wapumbavu. Wanaume wanaposhindwa kufumbua huwanyemelea mashekhe na hata kuwalipa ili wawasaidie.

Katika ubeti wa tatu mshairi anasema:

> Lugha yetu twapatia, utamu kama asali,
> Hakuna wa kuchukia, wenyewe si bahili
> Maneno hayo kubali,
> Uyakubali sawia, kila njia kila hali,
> Kila mtu mahamia, na wenyeji hujadili,
> Lugha yetu Kiswahili, twazama na kuibuka (Mnyampala, 1965: 123).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, Kiswahili ni lugha tamu kama asali. Hakuna mtu anayekichukia na wazungumzaji wake si wachoyo. Wageni na wenyeji hutumia Kiswahili kwa kuwa ni lugha ya watu wote. Mshairi anaendelea kueleza kuwa, Kiswahili kinajulikana na wenye nguvu na wanyonge. Kinatumiwa katika utunzi wa mashairi ya aina tofauti yale yenye ukali na ya upole yanayofunza tabia njema kwa wanadamu ili waache kuwa na utani na kutoheshimu watu.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, lugha inayochukuliwa kuwa yenye faida katika jamii huenea. Kwa hivyo, lugha ya Kiswahili ilikuwa na faida kwa jamii ndiposa ikajulikana na wenye nguvu na wanyonge. Pia, lugha ya Kiswahili ilitumiwa na washairi kuwashauri Watanganyika.

Vilevile, katika ubeti wa tisa mshairi anasema:

> Kiswahili narudia, bora sana Kiswahili,
> Maghani twakiimbia, hadi nyingine shughuli,

Kwa mafumbo na methali,

Methali zenye wasia, nazo ardhilihali,

Mpaka tukajifia, kifo kikitukabili,

Lugha yetu Kiswahili, twazama na kuibuka (Mnyampala, 1965: 124).

Katika ubeti huu, mshairi anasisitiza kuwa, Kiswahili ni lugha bora. Hutumiwa katika methali, mafumbo na maghani. Methali za Kiswahili zina ushauri na zitatumika siku zote. Kwa hivyo, Kiswahili kitatumika siku zote za maisha yao.

Aidha, katika ubeti wa kumi mshairi anasema:

Lugha haina udhia, hutamkwa kwa sahali,

Matajiri huchumia, wanapositahimili,

Kila pembe huwasili,

Huwasili huwajia, nchini wakaitaali,

Hadi wakafurahia, wasichukie muhali

Lugha yetu Kiswahili, twazama na kuibuka (Mnyampala, 1965: 124).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, lugha ya Kiswahili haina taabu kwa kuwa husemeka kwa urahisi. Matajiri wanapofanya biashara huitumia katika kila pembe nchini. Kwa hivyo, hurahisisha mawasiliano kati yao na wenyeji.

Nadharia ya Ubidhaaishaji wa lugha inasisitiza kuwa, lugha hutumiwa na watu kulingana na mahitaji ya kijamii ya hadhira inayokusudiwa. Kwa hivyo, lugha ya Kiswahili ilitumika kama chombo cha mawasiliano ya kibiashara jambo lililoieneza kote nchini Tanganyika.

Mshairi anabainisha umuhimu wa Kiswahili katika ubeti wa sita. Anasema:

Popote twaitumia, Barazani na Sikuli,

Kunena na kubishia, sukari na pilipili,

Na mengine mengi pia,
Pia tunashuhudia, yaletayo mushikeli,
Hata kama twasinzia, daima kila pahali,
Lugha yetu Kiswahili, twazama na kuibuka (Mnyampala, 1965: 124).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza matumizi ya Kiswahili nyumbani na shuleni. Ni lugha inayotumiwa katika mazungumzo na mijadala ya mazuri na mabaya na hata yenye kasoro. Kwa hivyo, Kiswahili kina matumizi mapana.

Pia, katika ubeti wa tano mshairi anasema:

Kiswahili ni Rupia, tukisema kwa akili,
Kiswahili twavukia, tuende ng'ambo ya pili,
Muungwana na Mjoli,
Mjoli huwa huria, akakipata kibali,
Uhuru huufikia, kwa Mola hutawakali,
Lugha yetu Kiswahili, twazama na kuibuka (Mnyampala, 1965: 124).

Katika ubeti huu, mshairi anabainisha umuhimu wa Kiswahili kwa kukilinganisha na rupia yaani pesa kinapotumiwa ipasavyo. Lugha hii itawasaidia kuvuka ng'ambo ya pili yaani kuwaondoa utumwani na kuwa huru huku wakimtegemea Mungu. Mshairi anaeleza kuwa matumizi ya Kiswahili yatawatoa watu katika utumwa wa kutumia lugha za kigeni.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, lugha huwa bidhaa muhimu kutokana na majukumu inayochangia na kutimiza. Lugha ya Kiswahili ilikuwa muhimu kwa sababu ilitumiwa katika shughuli za kijamii na kisiasa. Kupitia matumizi ya Kiswahili, Waafrika wanasitisha utegemezi wa lugha za kikoloni.

Fauka ya hayo, katika ubeti wa saba mshairi anasema:

Ni lugha ya biladia, alotujalia Jalali,

Wahabu katujalia, katupa katusabili,

Kakamilisha kamili,

Kamili katupambia, kumbuka zake fadhili,

Lugha yatusaidia, mara kumi twabadili,

Lugha yetu Kiswahili, twazama na kuibuka (Mnyampala, 1965:124).

Katika ubeti huu, mshairi anamshukuru Mungu kwa kuwajalia lugha ya Kiswahili bila malipo. Mshair anasema ni lugha ya biladia yaani ya mjini inayowasaidia sana kwa kuwa na matumizi mengi. Katika ubeti wa nane, mshairi anaorodhesha umuhimu wa Kiswahili. Anasema:

Ufundi twajifunzia, usonara na vipuli,

Na kuijua dunia, ya haramu na halali,

Ya sadaka na kusali,

Kusali kusujudia, Mungu atupe kubuli,

Hotuba twahutubia, yale maneno ya kweli,

Lugha yetu Kiswahili, twazama na kuibuka (Mnyampala, 1965: 124).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, Kiswahili hutumiwa kutoa mafunzo hasa ya usonara. Pia, Kiswahili hufunza watu mambo ya ulimwengu; mazuri na mabaya. Isitoshe, Kiswahili hutumika katika masuala ya kidini ya kuabudu, kusali na kutoa sadaka. Vilevile, Kiswahili hutumiwa kutoa hotuba za ukweli. Kwa hivyo, lugha ya Kiswahili ni muhimu kwa sababu ina majukumu mengi katika jamii.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, maelezo haya yanabainisha kuwa, lugha ya Kiswahili ilikuwa kama bidhaa muhimu yenye thamani kwa sababu

ilitumiwa na wanajamii kama chombo cha kutolea ushauri, mafunzo ya kiufundi na kidini.

Kulingana na Nadharia ya Utegemezi, Waafrika wanapaswa kutetea na kudumisha lugha yao ili kusitisha utegemezi wa lugha za kikoloni. Hivyo, mshairi anatukuza Kiswahili kwa kubainisha majukumu yake katika jamii.

2.5.2 Shairi "Kimefuzu Kiswahili"

Mnyampala (1965) katika shairi "Kimefuzu Kiswahili", anadhihirisha furaha yake kwa Kiswahili kuteuliwa kuwa lugha ya taifa. Katika ubeti wa kwanza anasema:

> Asante sana waziri mkuu, ombi letu kukubali,
> Kwa Mungu tunarukuu, twamsujudu kuwili,
> Twainua mikono juu, kumshukuru Jalali,
> Kwa kufuzu Kiswahili, wananchi tumefurahi (Mnyampala, 1965: 154).

Katika ubeti huu, mshairi anamshukuru Waziri mkuu kwa kukubali maombi yao ya kukiteua Kiswahili kutumika katika Baraza kuu. Mshairi anamshukuru Mungu kwa mafanikio waliyopata.

Aidha, katika ubeti wa nne anasema:

> Tuvike yake kumbuu, lugha yetu ya halali,
> Ilindwe kama tumbuu, tuseme yenye akili,
> Tuunge na vitunguu, tukaange kwa samli,
> Kwa kufuzu Kiswahili, wananchi tumefurahi (Mnyampala, 1965: 155).

Katika ubeti huu, mshairi anapendekeza watu wote washerehekee kuteuliwa kwa Kiswahili kuwa lugha ya taifa. Pia, anapendekeza Kiswahili kilindwe kama tumbuu kwa kuwa ni lugha ya halali.

Vilevile, katika ubeti wa tano mshairi anasema:

> Tuisomee Juzuu, Sala zote kila hali,
>
> Tumepanda kisuguu, lugha yetu tuijali,
>
> Itembee kwa miguu, toka hapa hadi mbali,
>
> Kwa kufuzu Kiswahili, wananchi tumefurahi (Mnyampala, 1965: 155).

Katika ubeti huu, mshairi anapendekeza Kiswahili kitumike katika majuzuu na katika sala. Aidha, waendeleze na kueneza Kiswahili ili kifike mbali.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Utegemezi, Waafrika wanapaswa kutetea na kudumisha lugha yao kama njia ya kusitisha utegemezi wa lugha za kikoloni. Kwa hivyo, Mshairi analenga kueneza Kiswahili kote nchini kama njia ya kusitisha utegemezi wa lugha za kikoloni.

Pia, katika ubeti wa sita mshairi anasema:

> Lugha nyingine tutuu, Chungu kama pilipili,
>
> Huchoma kama tunuu, lile la moto mkali,
>
> Hutwangusha chini puu, kutoijua kamili,
>
> Kwa kufuzu Kiswahili, wananchi tumefurahi (Mnyampala, 1965: 155).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, lugha nyingine si nzuri kwani ni chungu kama pilipili. Watu wanapojaribu kujifunza lugha nyingine hawafanikiwi kabisa.

Isitoshe, katika ubeti wa saba mshairi anasema:

Tuliivamia vuu, nayo hatujui kweli,

Twajua kijuu-juu, twakwamakwama mahali,

Sasa tuipe Khuluu, lugha yenye mushikeli,

Kwa kufuzu Kiswahili, wananchi tumefurahi (Mnyampala, 1965: 155).

Katika ubeti huu, mshairi anabainisha kuwa, lugha nyingine wanazijua kijuujuu kwa hivyo, wanakwamakwama wanapozitumia. Pia, wanapotosha kauli na kuwafanya waonekane kama hawana akili timamu.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, lugha hutumika sio tu kama chombo cha mawasiliano bali pia hubainisha uwezo fulani unaomfanya mtu aonyeshe umilisi wa lugha alionao. Hivyo, Waafrika waliweza kujieleza vyema kwa Kiswahili kwa kuwa ndio lugha yao ya asili walioielewa vyema tofauti na lugha zingine za kikoloni.

Fauka ya hayo, katika ubeti wa kumi mshairi anasema:

Kaditama tunukuu, zile mbinu za methali,

Sidharau kuu-kuu, simo na vitendawili,

Tuunge kwa karafuu, lugha yetu ya asali,

Kwa kufuzu Kiswahili, wananchi tumefurahi (Mnyampala, 1965: 155).

Katika ubeti huu, mshairi anamalizia shairi lake kwa kueleza kuwa, lugha ya Kiswahili ni tamu kama asali. Anapendekeza watumie methali, simo na vitendawili. Mshairi anadhihirisha kuwa wananchi wanafurahi kwamba Kiswahili kimekubalika nchini.

Kama inavyodhihirika katika Nadharia ya Utegemezi, maelezo haya yanabainisha kuwa hali ya utegemezi wa lugha za kikoloni ilikuwa imeondolewa kwa kuitukuza na kuisifu lugha ya Kiswahili.

2.5.3 Shairi "Kiswahili"

Akilimali (1963) katika shairi lake "Kiswahili", anasifu lugha ya Kiswahili kwa kueleza sifa zake. Katika ubeti wa kwanza anasema:

> Kiswahili sina budi, kukipa sana makamo,
> Ni lugha yangu ya jadi, kwa uzawa nimo humo,
> Yanipatia muradi, na kunikuzia kimo,
> Nitokapo ni jadidi, pia heshimani nimo (Akilimali, 1963: 26).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, Kiswahili ni lugha yake ya jadi iliyomkuza mpaka akawa mtu mzima. Kwa sasa yuko imara na anaheshimika.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, lugha hutumika sio tu kama chombo cha mawasiliano bali pia hubainisha uwezo fulani unaomfanya mtu aonyeshe umilisi wa lugha alionao. Hivyo, mshairi anaheshimika kwa kuwa na umilisi wa Kiswahili.

Aidha, katika ubeti wa pili mshairi anasema:

> Katika yangu fuadi, napenda bila kikomo,
> Kukipenda sina budi, kwa ufasaha na upimo,
> Tamu kama zamaradi, kwa fasaha iliyomo,
> Kwa maneno nafanidi, bila kuwa mtetemo (Akilimali, 1963: 27).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, anapenda Kiswahili kwa moyo wake wote kwa kuwa ana ufasaha. Mshairi analinganisha utamu wa Kiswahili na zamaradi kwa upande wa ufasaha. Pia, anaweza kujieleza vizuri bila hofu. Maelezo haya yanabainisha kuwa, lugha ya Kiswahili ilikuwa yenye hadhi ikilinganishwa na lugha za kienyeji. Kwa hivyo, ujuzi wa Kiswahili ulikuwa jambo la kujivunia.

Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha husisitiza kuwa lugha yenye faida katika jamii huenea. Kwa kuwa lugha ya Kiswahili iliweza kutumika kujieleza vizuri, ilienea kote nchini Tanganyika wakati wa ukoloni.

Pia, katika ubeti wa tatu mshairi anasema:

> Ingawa najitahidi, kujifunza kila somo,
> Lugha za kila biladi, ni kwa kutafuta chumo,
> Bali sipati muradi, ila naambua zumo,
> Ni bure yangu juhudi, kusema sipati kimo! (Akilimali, 1963: 27).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, ingawa amejitahidi kujifunza masomo na lugha za kila nchi hajafanikiwa kwa njia yoyote. Anafanya hivyo tu anapotafuta mapato lakini hapati faida yoyote.

Isitoshe, katika ubeti wa nne mshairi anasema:

> Jama tufanye itikadi, tuyafukie mashimo,
> Ambayo yaloshitandi, kuificha lugha humo,
> Na walio mahasidi, washone yao midomo,
> Lugha nchini izidi, pasipo kuwa ukomo (Akilimali, 1963: 27).

Katika ubeti huu wa mwisho, mshairi anapendekeza waharibu mambo yote yanayozuia kuenea kwa lugha ya Kiswahili ili iweze kusambaa. Wale ambao ni maadui wasiopenda maendeleo ya Kiswahili wanyamaze ili lugha izidi kuendelea. Katika shairi hili Kiswahili kinasifiwa.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Utegemezi, Waafrika wanapaswa kutetea na kudumisha lugha yao ili kuondoa utegemezi wa lugha za kikoloni (Ngugi 1986: xii). Kwa hivyo, mshairi anaieneza lugha ya Kiswahili kwa kuisifu na kuitukuza.

2.5.4 Shairi "Kiswahili"

Robert (1966) ameandika shairi refu lenye beti thelathini na moja liitwalo "Kiswahili." Katika shairi hili, anasifu lugha ya Kiswahili kwa kueleza sifa na uzuri wake pamoja na umuhimu wake kwa jamii. Katika ubeti wa kwanza anasema:

> Titi la mama litamu, hata likiwa la mbwa,
> Kiswahili naazimu, sifayo inayofumbwa,
> Kwa wasiokufahamu, niimbe ilivyo kubwa,
> Toka kwa chemchemu, furika palipozibwa,
> Titi la mama litamu, jingine halishi hamu (Robert, 1966: 27).

Katika ubeti huu, mshairi anatumia sitiari ya titi la mama kurejelea lugha ya Kiswahili. "Mama" ni jazanda inayotumiwa kuwakilisha taifa linalotumia lugha ya Kiswahili. Hata kama Kiswahili kinadharauliwa kama vile 'titi la mbwa', kwa maoni yake ni lugha muhimu. Kiswahili kina sifa nyingi lakini kuna watu wasiofahamu. Hivyo, angependa sifa hizo zijulikane kote hata kule ambako Kiswahili hakijajulikana. Mshairi angependa kiwe na uhai ama kienee hata kama kinazuiwa na wakoloni ndipo akasema 'toka kama chemchemu, furika palipozibwa'. Kwa hivyo, Kiswahili ni lugha tamu hakiwezi kulinganishwa na lugha za kigeni.

Kama Nadharia ya Utegemezi inavyosisitiza kwamba ukoloni unahusu kusambaratisha ama kutothamini kwa makusudi utamaduni wa jamii, wakoloni walizuia maenezi ya Kiswahili. Hata hivyo, mshairi anakitetea na kukitukuza.

Pia, katika ubeti wa tatu mshairi anasema:

> Lugha yangu ya utoto, hata leo nimekua.
> Tangu ulimi mzito, sasa kusema najiua,
> Sawa na manukato, moyoni mwangu na pua,

Pori, bahari na mto, napita nikitumia,

Titi la mama litamu, jingine halishi hamu (Robert, 1966: 27).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, Kiswahili ni lugha yake tangu utotoni. Imekuwa kama manukato puani na moyoni mwake. Anaitumia kila mahali anapokwenda tena humwondoa katika matatizo ya mawasiliano. Mshairi ametumia ishara za pori, bahari na mto ili kuonyesha mambo yanayoweza kuzuia mawasiliano.

Isitoshe, katika ubeti wa nne mshairi anasema:

Sababu ya kupenda, lafidhi yangu natoa,

Natumia toka ganda, na kiini chanelea,

Lugha nyingine nakonda, wakati nikitumia,

Mbele nikitaka kwenda, ulimi wangu hukwaa,

Titi la mama litamu, jingine halishi hamu (Robert, 1966: 27).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza sababu ya kupenda lugha ya Kiswahili. Anajua lafudhi yake na anaitumia kuelezea kila jambo bila shida tofauti na lugha zingine.

Vilevile, katika ubeti wa sita mshairi anasema:

Usemi na akili, ni pambo vikilingana,

Kwa lugha ya Kiswahili, sina cha kunibana,

Kama natoa kauli, na fikira kufanana,

Lugha nyingine bahili, ujima kwangu hazina,

Titi la mama litamu, jingine halishi hamu (Robert, 1966: 27).

Katika ubeti huu, mshairi anasema kwamba, Kiswahili kinaelezea mawazo yake vizuri kwani usemi na akili zake hulingana. Lugha zingine haziwezi kuelezea fikira zake kwa utaratibu. Vilevile, mshairi anasisitiza jambo hili anapoeleza kuwa, Kiswahili kinatumika kuelezea mawazo yake yote na hutumiwa mahali popote. Lugha ya kigeni

haimtoshi kwani anapoitumia hawezi kuelezea mawazo yake. Mshairi anatumia lugha za kigeni ili apate ajira huku akielewa kuwa asiyetumia lugha yake ni maskini. Anaeleza kuwa lugha kama Kiarabu, Kirumi na Kiingereza zinapendeza na amejaribu sana kujifunza lakini anapozungumza hubezwa.

Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha husisitiza kuwa lugha yenye faida katika jamii huenea. Kwa kuwa lugha ya Kiswahili iliweza kutumika kujieleza vizuri, ilienea kote nchini Tanganyika wakati wa ukoloni. Pia, mshairi anaisifu lugha ya Kiswahili kwa kubainisha matumizi yake kama vile kurahisisha mawasiliano kwa kuilinganisha na lugha za kigeni ili kusitisha utegemezi wa lugha za kigeni na kukikuza Kiswahili kote nchini Tanganyika. Mshairi anasema kila mtu ana lugha yake anayoitumia vyema. Kiswahili kinampa hadhi na heshima anapokitumia. Kwa Kiswahili, mshairi anaweza akauliza na akajibu maswali bila shida. Anasema ataacha tamaa ya lugha zingine.

Zaidi ya hayo, katika ubeti wa kumi na nane, mshairi anasema:

> Kiswahili tajiri, kwa fasaha na methali,
> Na mimi nafikiri, wakati hauko mbali,
> Kitaweza kufasiri, elimu mbalimbali,
> Kwa akili na uzuri, kiwape watu fadhili,
> Titi la mama litamu, jingine halishi hamu (Robert, 1966: 29).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, Kiswahili ni lugha tajiri kwa kuwa na ufasaha na methali. Anaona kuwa lugha hii itakuja kutumiwa katika elimu na itawasaidia watu. Mshairi anatarajia kuona matumizi ya Kiswahili katika vitabu na kamusi. Ingawa lugha hii inasifika, bado iko nyuma lakini polepole sifa yake itavuma kwa kuwa ni lugha bora yenye fahari na heshima.

Kama inavyodhihirika katika Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, lugha inayochukuliwa kuwa yenye faida katika jamii huenea. Kwa hivyo, Kiswahili kilienea wakati wa ukoloni kwa kuwa lugha yenye hadhi na iliyosifika kote nchini Tanganyika.

Mshairi anaelezea umuhimu wa lugha ya Kiswahili. Anasema:

> Mfano neno la jambo, mkato wa una jambo,
> Jibu lake ni si jambo, tafsiri sina jambo,
> Tazama hili pambo, lizidishavyo urembo,
> Wa kuulizana mambo, kwa usemi wenye umbo,
> Titi la mama litamu, jingine halishi hamu (Robert, 1966: 28).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, maamkizi kwa Kiswahili ni mepesi sana na mema tofauti na lugha zingine. Kwa mfano, salamu "Una Jambo?" jibu lake ni "Sijambo". Anaeleza jinsi salamu hujitokeza kama pambo. Mshairi anaongeza kuwa, lugha ya kigeni inahitaji mtu kujifunza jambo ambalo halimtishi. Hata hivyo, lugha ya kulelewa ni tamu na huna budi kuitumia wakati wowote. Aidha, mshairi anaeleza kuwa, Kiswahili ni mojawapo ya lugha kuu kumi na mbili duniani. Hivyo, hutumiwa kuwaridhia haja watu wa asili mbalimbali kwa sababu hakina upungufu. Pia, Kiswahili kimekopa maneno kutoka kwa lugha nyingine kama vile lugha zingine zinavyofanya. Kwa hivyo, Kiswahili hakiwezi kupuuzwa kwa kukosa manufaa kwani kina msamiati wa kutosha.

Katika ubeti wa ishirini na tatu mshairi anasema:

> Kiswahili kina sifa, kwa nahau na maana,
> Hufanya na mataifa, mengi kusikilizana,
> Kikitoa taarifa, kwa wengi huwa bayana,

Na iwapo kitakufa, roho nyingi zitanuna

Titi la mama litamu, jingine halishi hamu (Robert, 1966: 30).

Katika ubeti huu, mshairi anabainisha umuhimu wa Kiswahili. Kiswahili hufanya mataifa mengi kusikilizana kinapotumiwa kutoa taarifa waziwazi. Kwa hivyo, ikiwa Kiswahili kingekufa, watu wengi wangeathirika. Mshairi anaendelea kueleza kuwa, Kiswahili hutumika katika ushairi kuelezea mambo mbalimbali. Anakilinganisha na Mto Nili ambao hutoa rutuba kutoka mbali hata Misri. Mto Nili husafiri wakati wa masika na jua kali. Kwa hivyo, Kiswahili kina matumizi mengi na hutumiwa nyakati zote. Shairi hili linatoa sifa tele za lugha ya Kiswahili.

Kulingana na Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, lugha hupewa thamani kwa kuwa na matumizi mengine duniani sio tu matumizi yake ya kimsingi ya mawasiliano na utambulisho wa kitaifa na kiutamaduni (Block 2010: 294). Hivyo, Kiswahili kinasifika kwa sababu ni lugha ya kimataifa yenye majukumu mengi kama vile kuwa ugwe wa kuwaunganisha watu wa mataifa mbalimbali. Mshairi anaisifu lugha ya Kiswahili kwa kuwa kama bidhaa muhimu kutokana na faida zake katika jamii.

2.5.5 Shairi "Kitumike Kiswahili"

Kandoro (1966) katika shairi "Kitumike Kiswahili", anapendekeza Kiswahili kitumike katika Baraza la Tanganyika ambalo lilikuwa la serikali ya kikoloni.

Katika ubeti wa pili mshairi anasema:

Baraza la Tanganyika, ambalo la serikali

Ndilo tunalo litaka, litumike Kiswahili

Tupate Waafrika, kuendesha serikali

Kitumike Kiswahili, Baraza la Tanganyika (Kandoro, 1966:142).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, ikiwa Kiswahili kitatumika katika Baraza la Tanganyika Waafrika watakuwa wanaendesha serikali ama watashirikishwa na wakoloni.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Utegemezi, jamii inayonuia kujikomboa kutokana na ukoloni haina budi kutumia lugha moja ya kuwaunganisha (Ngugi, 1986: 3). Kwa hivyo, mshairi anadhihirisha kuwa, matumizi ya Kiswahili katika utawala yangesitisha utegemezi wa lugha za kikoloni na kukikuza Kiswahili.

Pia, katika ubeti wa tatu mshairi anasema:

> Sheria zinapotoka, tuzisome bila ghali
> Ndipo tujue hakika, za haramu na halali
> Ili tupate zishika, na kuzitii kwa kweli
> Kitumike Kiswahili, Baraza la Tanganyika (Kandoro, 1966:142).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza umuhimu wa Kiswahili kwani sheria zingeandikwa kwa Kiswahili wangeweza kuzisoma na kuzielewa ili wapate kuzitii.

Isitoshe, katika ubeti wa nne mshairi anasema:

> Tanganyika kwa hakika, ni kabila mbalimbali
> Zote zimekutanika, kutumia Kiswahili
> Tukipata Tanganyika, kiwe lugha serikali.
> Kitumike Kiswahili, Baraza la Tanganyika (Kandoro, 1966:143).

Katika ubeti huu, mshairi anabainisha umuhimu wa Kiswahili kama lugha ya jamii mbalimbali. Kwa hivyo, anapendekeza Kiswahili kiteuliwe kama lugha ya mawasiliano serikalini.

Aidha, katika ubeti wa nane mshairi anasema:

Hawale Tanganyika, kwa lugha ya Kiswahili
Tupate kuelimika, ifanyavyo serikali
Nasi sasa tumechoka, kusemwa tungali mbali
Kitumike Kiswahili, Baraza la Tanganyika (Kandoro, 1966: 143).

Katika ubeti huu, mshairi anatoa maoni yake kuwa Kiswahili kingetumika, Watanganyika wangeweza kuelewa shughuli za serikali. Matumizi ya lugha za kigeni yaliwatenga Watanganyika na kuwafanya waishuku serikali ya kikoloni kwani hawakushirikishwa ndiposa mshairi akasema "Watanganyika twataka, kusikose Kiswahili. Ndipo itutoke shaka, kuishuku serikali". Mshairi anabainisha umuhimu wa Kiswahili kama lugha rasmi nchini Tanganyika.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, lugha inayochukuliwa kuwa yenye faida katika jamii huenea. Kwa hivyo, lugha ya Kiswahili ilisifika na kuenea kwa kuwa lugha ya mawasiliano nchini Tanganyika.

2.6 Ushairi na Sauti ya Watu

Sera ya lugha ya kipindi cha ukoloni ilihimiza matumizi ya lugha ya Kiswahili kutokana na majukumu iliyotimiza katika jamii. Mashairi yaliyotungwa katika kipindi cha ukoloni yalitumiwa kama chombo cha kujieleza. Washairi walitumia ushairi kuhimiza Watanganyika waishi kwa amani, udugu na heshima. Pia, ushairi ulitumiwa kupigania haki, usawa na uhuru.

2.6.1 Maudhui ya Amani

Washairi walitunga mashairi yanayohimiza Watanganyika wakae kwa amani. Abedi (1954) katika shairi "Sote Tu wa Nyumba Moja", anawashauri Watanganyika waishi kwa amani. Katika ubeti wa kwanza anasema:

> Japo twakhitilafiana, Dini yetu dini moja,
> Si vibaya kuonyana, kwa kutoleana hoja,
> Lakini tukigombana, tutakizua kiroja
> Sote tu wa nyumba moja, ikifa tutacharara (Abedi, 1954: 102).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, ingawa wanahitilafiana katika jambo, dini yao ni moja kumaanisha kuwa wana imani sawa. Wanaweza kuonyana kwa kutoleana hoja lakini wakigombana wataharibu kwa kuwa wote ni wa nyumba moja na ikiharibika wataumia. Mshairi anawashauri watu waishi kwa amani. Mshairi anaeleza kuwa, katika dini yao wana Mtume Muhammad Seyidina ambaye anapendwa kwa kuwapa faraja. Kwa kuwa imani yao inashabihiana, hawafai kuzozana kwani wote wataumia. Anamalizia shairi kwa kutaja kitabu kitakatifu cha dini yao yaani Kurani. Kitabu hiki ndicho kinachotoa mwongozo na kutosheleza haja za watu wa dini yao. Hivyo, anapendekeza wafuate mafundisho yake ili waishi kwa amani. Mshairi anawaonya Watanganyika dhidi ya ugomvi baina yao.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, lugha hutumiwa na watu kulingana na mahitajii ya kijamii au hadhira inayokusudiwa. Kwa hivyo, mshairi anatumia lugha ya Kiswahili kuwahimiza Watanganyika waishi kwa amani.

Pia, katika shairi "Umoja" Abedi (1954), anahimiza wananchi waishi kwa umoja bila ugomvi. Anatumia sitiari za wadudu wanaoishi pamoja kama vielelezo bora vya umoja. Katika ubeti wa kwanza anasema:

Msituni nikakuta, nyuki wamo mzingani,

Kwa juhudi wanakita, mara nje mara ndani,

Husuda wameikata, hata hawasengenyani,

Nyuki ni wadudu duni, wanashinda kwa umoja (Abedi, 1954: 82).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, alienda msituni akakuta nyuki wamo mzingani wanakita nje na ndani. Hawana wivu wala masengenyo wanaishi kwa umoja. Mshairi anawashauri wananchi waige mfano wa nyuki ili wawe na amani. Mshairi anaendelea kueleza kwamba, aliona mchwa wanafanya kazi pamoja kwa bidii bila udanganyifu. Siafu nao wakiwa na mizigo yao kichwani wanatembea njiani. Wao si wachokozi lakini ukiwahini wanakuwa wakali. Mshairi haelewi sababu ya wanadamu kutoelewana. Anawashauri wananchi wasiwe na hamu sana ya uongozi bali waunge mkono wataalamu wachache wasije wakavunja umoja wao. Katika shairi hili, mshairi anahimiza watu waige mfano wa wadudu ili waishi kwa amani na umoja.

Robert (1968) anahimiza wananchi waishi kwa amani. Katika shairi “Ubora Wetu”, anasema kuwa umaskini na ukosefu wa afya mwilini ni shida kubwa. Lakini kuwa na rafiki katika mahakama ni vyema kuliko kuwa na pesa mfukoni. Tena, ukosefu wa chuki ungewafanya wote waende peponi. Mshairi anasisitiza umuhimu wa kuishi kwa amani.

Katika ubeti wa pili mshairi anasema:

Amani yetu haba moyoni kwa uadui na magombano,

Kama hatuna matumaini na ukunjufu na tangamano,

Tunao ukufi wa imani katika pori la makindano,

Fahari yetu duni thamani kwa kukosa masikilizano,

Ubora wetu ni mapatano, na leo huwaje nuksani? (Robert, 1968: 42).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, watu hawana amani moyoni kwa sababu ya uadui na ugomvi kama watu ambao hawana matumaini, furaha na masikilizano. Wana chembe ndogo tu ya imani na utukufu wao hauna thamani kwa ukosefu wa maridhiano. Ubora wao tu ni kuwa na mapatano lakini leo wana ugomvi. Katika shairi hili mshairi anasisitiza umuhimu wa kuishi kwa amani.

Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha inasisitiza kuwa, watu hutumia lugha kulingana na mahitaji ya kijamii. Kwa hivyo, ushairi wa Kiswahili ulitumiwa kuwahamasisha watu waishi kwa amani. Kiswahili kilitumika kama chombo cha kuwaunganisha Watanganyika.

2.6.2 Maudhui ya Heshima

Sera ya lugha ya kipindi cha ukoloni nchini Tanganyika iliunga mkono matumizi ya lugha ya Kiswahili. Washairi walitunga kazi zao kwa Kiswahili sanifu**.** Ushairi wa Kiswahili uliotungwa wakati wa ukoloni ulikuwa kama sauti ya watu kwani washairi waliutumia kushauri Watanganyika. Baadhi ya maudhui yao yalihusu amani, udugu na heshima. Walitunga mashairi ya kuhimiza watu kujiheshimu au kuheshimu wengine.

Robert (1968) anaonyesha umuhimu wa heshima katika shairi “Heshima”. Mshairi anaeleza kuwa, kama kuhitaji heshima kwa mtu ni uhalifu, heri afilie mbali kuliko kuishi duniani. Maisha ya mtu hayapendezi kama hayana heshima kwani hakuna kitu kingine cha kufurahisha mtu zaidi ya kutukuzwa kwa cheo. Kila mtu anapenda kuwa na heshima. Ni jambo lililo azizi sana kwa mwanamume au mwanamke. Unapompa mtu heshima anakutukuza katika maisha yake na hawezi kukusahau katika moyo wala fadhili yake. Katika shairi hili mshairi anadhihirisha umuhimu wa kuheshimiwa.

Pia, Robert (1967) anaeleza kuwa uzuri wa mtu si umbo wala sura lakini ni tabia. Katika ubeti wa pili wa shairi “Uzuri” anasema:

Uzuri kupita huu,
Katika hii dunia,
Nawapa msisahau
Ni uzuri wa tabia,
Ni johari ya heshima duniani kila mara (Robert, 1967: 96).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, uzuri wa tabia ni zaidi ya uzuri wowote duniani. Hangependa watu wasahau hilo kwani ndio johari ya heshima duniani. Mshairi anabainisha kuwa mtu mwenye tabia njema anaheshimika.

Katika ubeti wa nne mshairi anasema:

Tazama! Dunia nzima,
Huendeshwa na tabia,
Kama tabia si njema,
Si ajabu kupotea,
Kitu kilicho adhama ni tabia ya busara (Robert, 1967: 96).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, dunia nzima huendeshwa na tabia. Kama tabia si njema si ajabu mtu akapotea. Kwa hivyo, kitu kilicho adhama ni tabia ya busara. Katika shairi hili, mshairi anasifu uzuri wa tabia unaovuta heshima.

Suala la heshima linadhihirika tena katika Robert (1969). Katika shairi “Tabia”, mshairi anasisitiza kuwa, tabia njema inamfanya mtu aheshimike. Katika ubeti wa tatu anasema:

Fanya adabu kwa watu, adabu husaidia,
Adabu libasi kwetu, kashifa inazuia,
Kisha hutukuza utu, jambo hili huwaniwa,

Utatukuka jina, kwa uzuri na tabia (Robert, 1969: 43).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, mtu akiwa na adabu kwa watu anazuia kashifa na kutukuza utu. Tena, anatukuka jina kwa kuwa na tabia nzuri. Mshairi anaeleza kuwa, ikiwa mtu ni maskini na ana tabia njema anathaminiwa duniani kwa kuwa mtu wa maana. Kuna matajiri ambao hawapati marafiki kwa sababu ni hatari kuwakaribia kutokana na tabia zao baya. Kadhalika, kuna wanyonge wanaojitafutia tonge kwa njia inayokubalika kisheria wanaosifika kwa uzuri wa tabia. Kisha kuna wenye nguvu wanaotumia nguvu zao vibaya na kujitia hatarini halafu wanalaumu dunia. Mshairi anasisitiza kuwa, mtu husifika kutokana na tabia yake njema.

Robert (1969) anaendelea kuangazia suala la heshima katika shairi "Wema". Katika ubeti wa kwanza anasema:

Panda mbegu ya wema, yaote mapendeleo,
Panda mbegu ya heshima, ili uvune cheo,
Uovu si mbegu njema, zao lake machukio,
Tena hupata lawama, apandaye mbegu hiyo (Robert, 1969: 53).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, mtu akiwa mwema anapendwa na watu. Akiwa mwenye heshima anapewa cheo lakini akiwa mwovu anachukiwa na kulaumiwa. Anaendelea kueleza kuwa, mtu anapotenda wema asiwe na haraka ya kupata mazao kwani haraka huleta hasara. Watu wengi wameumia kwa kupuuza hayo. Mshairi anawashauri watu watende mema na waheshimu wengine.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, watu hutumia lugha kulingana na mahitaji ya jamii inayokusudiwa. Hivyo, ushairi wa Kiswahili ulitumiwa kama chombo cha kujieleza na kushauri Watanganyika wawe na matendo mema na heshima.

2.6.3 Maudhui ya Udugu

Akilimali (1963) anashauri watu kuhusu udugu ili waelewane. Katika shairi “Jirani Yako ni Ndugu”, mshairi anaeleza kuwa, jirani ya mtu ni nduguye na wanapaswa kuelewana. Siri ya moyoni anaweza kuambiwa kwani anaaminika kuwa mfadhili. Anaonya dhidi ya kumfanyia jirani ufidhuli. Ingawa jirani ni dhalili mtu anaweza kula na kucheka pamoja naye kwa sababu ni ndugu yake. Si vizuri kuchunguzana hali na kuwa na utesi msije mkatengana. Mtu anapopewa chakula na jirani apaswa kula na kumshukuru kwani ni ishara ya upendo wa ndugu. Akiwa na shida anastahili kusaidiwa maadamu mtu yu karibu naye. Katika shairi hili mshairi anashauri majirani wapendane na kuchukuliana kama ndugu.

Pia, katika shairi “Udugu” Akilimali (1963) anasema:

> Udugu kweli haiba, pambo zuri la moyoni,
> Ikiwa nyote mwashiba, mtakuwa furahani,
> Mtaishi kwa mahaba, bila kuwa nukusani,
> Udugu bila ya hivyo, asili hampatani (Akilimali, 1963: 63).

Katika shairi hili fupi, mshairi analinganisha udugu na urembo ambao ni pambo la moyo. Ikiwa watu wote wana udugu, wanafurahi kwa sababu wanaishi kwa mapenzi bila fujo yoyote. Anamalizia shairi kwa kueleza kuwa, ndugu hawapatani kama hawapendani.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, lugha ya Kiswahili ilikuwa kama bidhaa yenye thamani kwa sababu ilitumiwa kama chombo cha kujieleza. Washairi walishauri Watanganyika waishi kama ndugu katika mashairi yao.

Shaaban Robert (1966) anaangazia suala la udugu katika shairi "Udugu." Mshairi anaeleza kuwa, amepata barua kutoka kwa mshairi mwingine na kwamba hajabadilisha kauli yake kuwa udugu utaendelea kati yao. Mtunzi anamshauri asiwe na wasiwasi. Katika ubeti wa pili anasema:

> Mkataa wingi mchawi, hili si masihara,
> Wala nyumba haiwi, kwa jingo moja imara,
> Ndugu hakataliwi, kumkataa hasara,
> Wingi ni ustawi, upeke una madhara (Robert, 1966: 2).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, anayekataa kushirikiana na wengine ni mchawi. Nyumba haiwezi kuwa kwa jengo moja imara bali inahitaji majengo mengine. Mtu hawezi kumkataa ndugu kwa sababu ni hasara. Watu wakiwa wengi wanastawi lakini upweke una madhara. Mshairi anabainisha umuhimu wa kuwa na ushirikiano au udugu.

2.6.4 Maudhui ya Utetezi wa Haki

Utetezi wa haki za watoto unadhihirika katika shairi "Tutalea Mwana Gani". Mnyampala (1965) anauliza watalea watoto gani ikiwa wanawake wanaendelea kuavya mimba. Anatetea watoto wapewe haki yao ya uhai. Katika ubeti wa nne anasema:

> Mtu hawezi kulima, pasi kufyeka porini,
> Na kulimia mapema, kupalilia shambani,
> Mambo hayo ni lazima, ndipo ale kivulini,
> Tutalea mwana gani, iwapo wana twanyonga? (Mnyampala, 1965: 19)

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, mkulima huanza kwa kufyeka pori kisha akalima na kupalilia shamba ndiposa apate mavuno. Kwa hivyo, wanawake wanapaswa kutunza mimba hadi wapate watoto kama vile mkulima anavyotunza shamba. Mshairi

anaeleza kuwa, watoto hutoa mtu katika umaskini akaishi kwa furaha. Kuna wanawake wanaoenda kwa mganga wasije wakapata kilema au wakakosa kupata mtoto. Mwanamke hawezi kuwa mama mpaka apate mtoto.

Pia, katika ubeti wa kumi mshairi anasema:

> Asozaa ni nakama, sikitiko duniani,
> Ana huzuni daima, humuomba Rahamani,
> Tuache anojinyima, kwa sheria za kidini,
> Tutalea mwana gani, iwapo wana twanyonga? (Mnyampala, 1965: 19).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kwamba, mwanamke asiyepata mtoto hupata masikitiko daima na humwomba Mungu amjalie mtoto. Hata hivyo, kutokana na sababu za kidini kuna wanawake wasiopata watoto lakini wengine wanasikitika wasipopata. Wanawake wanaopata watoto wanastahili wawatunze. Mshairi anapinga mauaji ya watoto kwa kuavya mimba.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, lugha inayobadilishwa na kutumika kama bidhaa muhimu hutegemea uwezo wake wa kutumika katika jamii. Ushairi wa Kiswahili ulitumika kama sauti ya watu kwani washairi walitumia Kiswahili kutetea watoto wapewe haki ya kuishi.

Kwa upande mwingine, Akilimali (1963) anatetea haki za vilema. Katika shairi “Hujafa Hujaumbika”, anaonya watu dhidi ya majitapo na kuchukia vilema. Katika ubeti wa pili mshairi anasema:

> Si wajibu upasao, vilema kuvikasiri,
> Hujajua maishao, viwaje yatashamiri,
> Anayedharau hao, mwisho wake hula mori,

Hujafa hujaumbika, jilinde na majitapo (Akilimali, 1963: 11).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, si vizuri kuwadharau vilema kwa sababu hatujui vile maisha yao yatashamiri. Anayewadharau mwisho hujiumiza. Kama mtu hajafa anaweza kuwa kilema pia. Kwa hivyo, kila mtu anapaswa aepuke maringo.

Aidha, katika ubeti wa nne mshairi anasema:

Hautakupa salama, usinune na jeuri,
Usinyanyase vilema, vilivyo umba Kahari,
Hujafa huna salama, mtu hakosi dosari,
Hujafa hujaumbika, jilinde na majitapo (Akilimali, 1963: 11).

Katika ubeti huu, mshairi anaonya watu dhidi ya kuwanyanyasa vilema walioumbwa na Mungu. Kila mtu aliye na uhai hakosi dosari. Kwa hivyo, anapendekeza tuache majitapo na tusiwe wajeuri kwa vilema. Mshairi anaeleza kuwa, hata kama mtu anajipamba vyema asije akawaita wenzake wanyama kwa ujeuri. Mshairi anaonya watu wasiwe na kiburi kinachozaa uadui na chuki.

Utetezi wa haki za wanawake unadhihirika katika mashairi ya Shaaban Robert. Katika shairi “Mume na Mke”, Robert (1966) anatetea wanawake. Katika ubeti wa nane anasema:

Mwanamke shetani, watu wengine wanena,
Kuja kwake duniani, kuwa ameleta laana,
Nami kwa yakini, juu ya hili nabishana,
Kuwa ana thamani, na mwanamume walingana (Robert, 1966: 32).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, kuna watu wanaosema mwanamke ni shetani na aliyeleta laana duniani. Mshairi anapinga jambo hilo na kueleza kuwa mwanamke ana thamani sawa na mwanamume. Kumdunisha mwanamke ni ujinga na ni hatia

kumuumbua. Mwanamke ni sehemu ya mwili wa mwanamume ndiposa akasema "mwanamke ni mwili, damu yetu na mfupa". Anapendekeza mume na mke washirikiane kulea watoto na wapewe heshima sawa. Kila mmoja ana jukumu la kumwinua mwenziye ili wapate mapato mengi. Mshairi anaeleza kuwa, ni wajibu wa mwanamume kumshukuru mwanamke kwa kipato anachopata. Mwanamke si kufuru lakini alikuja kusaidia mume. Hivyo, mume asimdhuru na kumsababishia upweke. Anauliza udhuru uko wapi wa kumuumbua. Anaendelea kueleza kuwa, hakuna haja ya kumlaumu kuwa na makeke bali wanaume wanapaswa kuepukana na ugomvi.

Kama Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha inavyoeleza, lugha huwa kama bidhaa muhimu kutokana na majukumu inayochangia na kutimiza katika jamii. Lugha ya Kiswahili ilikuwa kama bidhaa muhimu kwani ushairi wa Kiswahili ulikuwa chombo cha kujieleza kwa kutetea haki za wanawake katika jamii. Jambo hili lilifanya Kiswahili kuenea nchini Tanganyika.

Katika ubeti wa thelathini na mbili mshairi anasema:

> Mwanamke mtukufu, sawa na mwanamume,
> Ulimwengu waarifu, mwenye akili apime,
> Maneno ya uumbufu, watu bure wasiseme,
> Akiwa na udhaifu, bia na mwanamume (Robert, 1966: 34).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, mwanamke atukuzwe sawa na mwanamume. Ulimwengu ukubali hayo na maneno ya uumbufu yasisemwe kwani ana udhaifu sawa na mwanamume. Kumtaja mwanamke kwa ubaya kunamfanya awe nyuma ashindwe kuendelea. Hivyo, wanawake wasitishwe eti hawawezi kitu wala wasidunishwe lakini wakaribishwe washirikiane na wanaume.

Katika ubeti wa thelathini na sita mshairi anasema:

Mke nyumbani faraja, kushinda mtumishi,
Mshahara hana haja, na kazi haimchoshi,
Hutumika bila tija, pato halimshawishi,
Hutimiza na haja, hata mwisho wa kuishi (Robert, 1966:35).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kwamba, mwanamke akiwa nyumbani hufanya kazi kushinda mtumishi na hatarajii mshahara wowote. Mwanamke anafanya kazi inayochosha ingawa hapati mapato ya kumshawishi kuendelea kufanya kazi. Hufanya kazi mradi tu yuko hai. Ijapokuwa umbo la mwanamke ni dhaifu, hana upungufu wa akili na maarifa. Kazi ya mwanamke inastahili sifa sio kashifa. Katika shairi hili, mshairi anabainisha kuwa mwanamke ana haki sawa na mwanamume. Mwanamke anastahili heshima sawa na mwanamume.

Isitoshe, katika shairi "Mwanamke si Kiatu", Robert (1966) anaendelea kutetea wanawake. Katika shairi hili, anamjibu mshairi mwingine aliyewakashifu wanawake. Katika ubeti wa tatu anasema:

Wanawake wana laana, jibu lako ufedhuli,
Tena mimi naona, lawama lastahili,
Kuwa hujui kunena, u mchache wa akili,
Wanawake bora sana, ni hazina ya awali (Robert, 1966: 19).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, ni ufedhuli kusema wanawake wana laana. Anayesema hivyo, ana akili chache kwa sababu wanawake ni hazina ya awali.

Aidha, katika ubeti wa nne anasema:

Laana ni kosa moja, kubwa katika kauli,
Ambalo limefuja, maneno na kubadili,

Mwanamke ana haja, sawa wa hali,

Mke hazai kioja, ila kwa mbegu dhalili (Robert, 1966: 20).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, kumwona mwanamke kama laana ni kosa kubwa linaloharibu kauli yoyote ile. Mwanamke ana haja na hali sawa na mwanamume. Mwanamke hafanyi mambo ya ajabu ila tu pale anapodhalilishwa. Mshairi anaendelea kueleza kuwa, mwanamke ni mtawala kila mahali nyumbani kwake. Hivyo, mwanamke ana umuhimu sana nyumbani ila hakubali kufanywa kiatu ama kugandamizwa. Mshairi anaongeza kuwa, kuna wanaume wanaowavunjia heshima wanawake na wao huvunjiwa pia. Wanaume hukimbilia sheria inayomkandamiza mwanamke. Katika shairi hili mshairi anadhihirisha kuwa, mwanamke anastahili heshima sawa na mwanaume.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, maelezo haya yanadhihirisha kuwa, lugha ya Kiswahili ilikuwa kama bidhaa muhimu katika jamii kwa sababu ilitumika kuwatetea wanawake waheshimike. Kwa kuwa lugha yenye faida kwa jamii hukua, Kiswahili kilienea kote nchini Tanganyika.

2.6.5 Maudhui ya Uhuru

Washairi wa kipindi cha ukoloni walihimiza Watanganyika watetee uhuru wa nchi yao. Kwa mujibu wa Nadharia ya Utegemezi, jamii inayolenga kujikomboa kutokana na ukoloni haina budi kutumia lugha moja ya kuwaunganisha watu ili kuleta ukombozi. Hivyo, washairi walitumia Kiswahili kuwahimiza Watanganyika kutetea uhuru wao kama njia mojawapo ya kusitisha utegemezi wa utawala wa kikoloni.

Kandoro (1966) katika shairi “Siafu Wamekazana”, anaelezea juhudi za wananchi za kupigania uhuru. Ametumia jazanda ya nyoka kurejelea wakoloni na siafu kuashiria wananchi. Mshairi anaeleza kuwa, wananchi wamekasirika na kuanza kumshambulia mkoloni ambaye ana hasira pia. Katika ubeti wa pili anasema:

Shimoni ataondoka, hilo nataja kwa jina,

Nyoka anajua fika, siafu wakiungana,

Nguvu zinaongezeka, shimoni watagombana,

Siafu wamekazana, nyoka amekasirika (Kandoro, 1966: 138).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, anajua mkoloni ataondoka nchini. Hata mkoloni anajua fika kuwa "siafu wakiungana" yaani wananchi wakiungana uwezo wao utaongezeka na kuhakikisha kuwa mkoloni atashambuliwa. Mshairi anabainisha umuhimu wa wananchi kushirikiana katika mapambano. Wananchi wakiungana kupigana na mkoloni, mkoloni hatakuwa na uwezo wa kumfokea mwananchi. Hivyo, mkoloni atalazimika kuondoka nchini. Anawajulisha wananchi kuwa katika mapambano wananchi wataumia lakini mkoloni ataondoka.

Katika ubeti wa sita mshairi anasema:

Nyoka akishaondoka, na siafu hujazana,

Shimoni wakipeleka, vyakula kutiliana,

Ndilo walilolitaka, wale kwa kutulizana,

Siafu wamekazana, nyoka amekasirika (Kandoro, 1966: 138).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, mkoloni atakapoondoka wananchi watasherehekea. Wataishi maisha mazuri ndiposa akasema "shimoni wakipeleka vyakula kutiliana". Shairi hili linalenga kubainisha umuhimu wa wananchi kuungana katika mapambano ya kupigania uhuru.

Pia, katika shairi "Kwetu ni Kwao kwa Nini?", Kandoro (1966) anauliza sababu ya wakoloni kuhamia nchi ya Tanganyika na kuifanya yao. Anaeleza kuwa, haelewi kiini cha mtu kuuliza maswali kuhusu kitu cha mtu na umuhimu wa kitu hicho kisicho chake.

Aidha, haelewi sababu ya mtu kuchukua kitu cha mwingine na kukifanya chake. Katika ubeti wa mwisho mshairi anasema:

> Mtu kwao kuthamini, ijapokuwa jiweni
>
> Pia alale mtini, na baraza liwe chini
>
> Nile matunda porini, kuitwa kwenu kwa nini?
>
> Kwetu ni kwao kwa nini, na kwao kwetu kwa nini? (Kandoro, 1966: 139).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, mtu anafaa athamini kwao hata kama ni jiweni. Ingawa analala mtini na baraza lake liko chini ya mti au anakula matunda ya porini anastahili athamini kwao. Katika shairi hili mshairi anakashifu wakoloni kwa kuhamia nchi ya Tanganyika na kuifanya koloni yao.

Kulingana na Nadharia ya Utegemezi, ukoloni unahusu kusambaratisha ama kutothamini kwa makusudi utamaduni wa jamii. Hivyo, mshairi analenga kusitisha utegemezi kwa kudai uhuru wa Watanganyika. Anawazindua Waafrika wapiganie uhuru wa nchi yao kwa kuwaondoa wakoloni waliohamia na kumiliki nchi ya Tanganyika.

Robert (1968) anahimiza watu waingie vitani wapambane na wakoloni. Katika shairi “Kufua Moyo”, mshairi anaeleza kuwa, siku panga itakapochomolewa mashujaa wataenda vitani na kusababisha machafuko. Ardhi italowa kwa mmiminiko wa damu. Hii ndio siku watu mashuhuri watajipambanua kwa matendo. Watu watajikusanya pamoja na kujiuliza kama ni bora kufa kwa vita au kufa kwa maradhi ya sondo. Mshairi anaendelea kusema:

> Uvundo wa mashujaa,
>
> Ni sawa na manukato,

Marashi katika pua,

Hauna harufu nzito,

Ama rihi ya maua,

Njema isiyo fukuto (Robert, 1968: 49).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, uvundo wa maiti ya mashujaa ni sawasawa na manukato au marashi au harufu nzuri ya maua katika pua za watu. Uvundo wa mashujaa hauna harufu ya karaha wala fukuto. Harufu hii nzuri hujaa tele katika hewa na katika ardhi yenye mimea. Mauti ya mashujaa huacha fahari kubwa kwa watu wote na ni urithi unaopendelewa na watu. Ni urithi wa majohari yaliyo bora katika ulimwengu. Mauti ya vitani hufanana na ndoto katika usingizi. Katika shairi hili, mshairi anawahimiza wananchi wajitolee na wawe tayari kupigana na mkoloni wapate uhuru. Anawasifu mashujaa ili kuwatia moyo wa kwenda vitani.

2.7 Hitimisho

Sura hii imechunguza jinsi hali ya sera ya lugha ya kipindi cha utawala wa Wajerumani na Waingereza ilivyochochea mabadiliko ya maudhui ya ushairi. Uchunguzi umeonyesha kuwa Wajerumani waliendeleza na kukuza lugha ya Kiswahili kama lugha ya utawala. Kwa upande mwingine, Waingereza walikiona Kiswahili kama lugha yenye hadhi kuliko lugha zingine za kienyeji ingawa kilichukua nafasi ya pili baada ya Kiingereza. Kutokana na sera hiyo, watunzi wa mashairi walikitetea na kukisifu katika mashairi yao huku wakieleza umuhimu wake katika jamii. Utunzi wa mashairi uliathiri sera ya lugha kwa sababu ulihimiza matumizi ya Kiswahili sanifu. Washairi waliweka kamusi ndogo ya msamiati uliotumika katika diwani zao jambo lililopanua msamiati wa lugha ya Kiswahili. Washairi walitoka sehemu mbalimbali kote nchini kwa hivyo, walieneza Kiswahili hata sehemu za bara. Ingawa mashairi yaliyotungwa katika kipindi hiki cha ukoloni yalibeba maudhui mbalimbali, baadhi yalitukuza lugha ya Kiswahili

na kuhimiza Watanganyika waikuze na kuieneza kote nchini. Vilevile, utunzi wa mashairi uliinua hadhi ya Kiswahili kutokana na majukumu yake katika jamii. Ushairi ulitumika kama sauti ya watu kwa sababu ulipigania haki, usawa, na uhuru. Aidha, ushairi ulihimiza Watanganyika wajiheshimu na wakae kwa amani na udugu. Kwa mujibu wa Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, maelezo haya yanabainisha kuwa, Kiswahili kilikuwa bidhaa muhimu yenye thamani kubwa kutokana na faida yake katika jamii. Kwa kuwa lugha inayochukuliwa kuwa yenye faida katika jamii huenea, Kiswahili kilipata kutukuzwa na kuenezwa kote nchini Tanganyika. Mihimili ya Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha ilitumiwa kuchunguza jinsi lugha ya Kiswahili ilitumika kama bidhaa yenye thamani ndiposa ikasifika na kutukuzwa katika ushairi. Vilevile, Mihimili ilitumiwa kuchunguza faida ya lugha ya Kiswahili kama chombo cha kujieleza. Mihimili ya Nadharia ya Utegemezi ilitumiwa kuchunguza jinsi Waafrika walivyositisha utegemezi wa lugha za kikoloni kwa kuisifu na kuitukuza lugha ya Kiswahili. Vilevile, mihimili ilitumiwa kuchunguza jinsi Waafrika walivyotumia Kiswahili kama ugwe wa kuwaunganisha na kuwa na umoja ili kuleta ukombozi.

Katika sura ifuatayo, shughuli za Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki zilichunguzwa jinsi zilivyochochea mabadiliko ya maudhui katika ushairi wa Kiswahili.

SURA YA TATU

KAMATI YA LUGHA YA AFRIKA MASHARIKI NA MAUDHUI YA USHAIRI

3.0 Utangulizi

Sura iliyotangulia ilichunguza jinsi sera ya lugha ya kipindi cha ukoloni ilivyochochea mabadiliko ya maudhui ya ushairi katika nchi ya Tanganyika iliyotawaliwa na Wajerumani na Waingereza. Sera ya lugha ya kipindi cha utawala wa Wajerumani ilikiendeleza na kukikuza Kiswahili kama lugha ya utawala na elimu. Waingereza waliteua Kiingereza kama lugha ya elimu. Waliinua hadhi ya Kiswahili kuliko lugha za kienyeji. Kutokana na sera ya lugha ya kipindi cha Waingereza kati ya mwaka 1918 hadi 1961, watunzi wa mashairi walikitukuza na kukisifu Kiswahili huku wakiwahimiza wananchi wakikuze. Mashairi yaliyotungwa katika kipindi cha ukoloni yanabeba maudhui ya sifa na umuhimu wa Kiswahili.

Sura hii ililenga kuchunguza jinsi shughuli za Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki zilivyochochea mabadiliko ya maudhui ya ushairi nchini Tanganyika kati ya mwaka wa 1930 hadi 1960. Baadhi ya shughuli za kamati hiyo zilikuwa ni kusanifisha Kiswahili, kuandaa mashindano ya uandishi wa Kiswahili pamoja na kuunda shirika la uchapishaji wa vitabu.

3.1 Shughuli za Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki

Tume ya Phelps-Stokes iliyodhaminiwa na Wakfu wa Phelps-Stokes wa Marekani ilitembelea nchi ya Tanganyika mwaka wa 1924. Tume hiyo iliilalamikia hali ya kukosa ushirikiano kati ya serikali na misheni katika shughuli za elimu ya Waafrika. Ilionelea kwamba Waafrika walikuwa na haki ya kusomeshwa kwa kutumia lugha zao za kwanza ili kuhifadhi utamaduni wao. Gavana wa Tanganyika, Sir Donald Cameron aliitisha mkutano mwaka wa 1925 ili kujadili sera ya elimu nchini. Ilitambuliwa kuwa kulikuwa

na haja ya kutumia lugha moja ya kufundishia ili kupunguza gharama za elimu. Kiswahili kiliteuliwa kwa kuwa, kilikuwa kikitumika kama lugha ya mawasiliano kati ya watu na ya kibiashara kote nchini. Kutokana na mkutano huo, kamati ya uchapishaji iliundwa ili kuchapisha vitabu vya shule kwa Kiswahili. Ilitarajiwa kuwa kamati hiyo ingehudumia nchi zote za Afrika Mashariki zilizokuwa zikitumia Kiswahili. Pia, kulikuwa na haja ya kuwa na mtindo mmoja wa maandishi ya Kiswahili. Vitabu vya shule na vitabu vya ziada vilitakiwa kuandikwa kwa lahaja moja sanifu kwani kulikuwa na lahaja kumi na tano za Kiswahili. Isitoshe, kulikuwa na mitindo kadha ya Kiswahili cha bara na matumizi ya hati mbili tofauti; Kiarabu na Kirumi. Kwa hivyo, Kiswahili kilihitaji kusanifishwa. Tanganyika na Zanzibar walikubaliana kusanifisha lahaja ya Kiunguja kama ilivyoandikwa na Askofu Edward Steere na wamishenari wa U.M.C.A katika mwaka wa 1925.

Kwa kuwa kusanifisha Kiswahili kulihitaji ushirikiano wa nchi nyingine za Afrika Mashariki, ilikubaliwa mradi huo ufanywe kwa ushirikiano. Mkutano wa nchi zote za Afrika Mashariki uliitishwa Mombasa Juni 5, mwaka wa 1928. Mkutano huo ulihudhuriwa na wawakilishi wa Kenya, Uganda, Tanganyika na Zanzibar pamoja na Mwanaisimu maarufu Carl Meinhof. Uamuzi muhimu katika mkutano huo ulikuwa ni kuchaguliwa kwa Kiunguja kama lahaja ya kusanifisha Kiswahili. Pia, mkutano uliamua kushirikiana kimataifa katika miradi ya uandishi wa kamusi na sarufi ya Kiswahili. Aidha, mkutano uliamua kuunda kamati ambayo ingekuwa na uwezo wa kuchagua, kuandika upya na kutafsiri vitabu vya shule (Mbaabu, 2007: 26).

Katika mkutano wa wakurugenzi wa elimu wa nchi zote za Afrika Mashariki na ya kati uliofanyika Dar es Salaam mwaka wa 1929, iliamuliwa kuundwa kwa Kamati ya Kimataifa ya Lugha ya Kiswahili. Kuanzia tarehe 1, Januari mwaka wa 1930, Kamati

ya Kiswahili ya Afrika Mashariki ilianzishwa ikiwa na jukumu la kusanifisha na kukuza Kiswahili. Kuanzia mwaka wa 1930 hadi mwaka wa 1942, makao makuu ya kamati hiyo yalikuwa mjini Dar es Salaam na baadaye kuanzia mwaka wa 1963 hadi 1964 kamati ilipogeuzwa kuwa Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. Kwa mujibu wa Ratcliffe (1942: 5-6), baadhi ya malengo ya kamati yalikuwa yafuatayo:

(i) Kusanifisha maandishi na kuhakikisha kwamba kuna mtindo mmoja unaotumiwa katika nchi zote zinazohusika.

(ii) Kuhakikisha kwamba kuna aina moja tu ya msamiati wa zamani na ulioazimwa katika makamusi yote, hasa makamusi ya shule.

(iii) Kuhakikisha kwamba sarufi imesanifishwa kwa kuchapisha vitabu vya sarufi.

(iv) Kuwatia moyo na kuwasaidia waandishi ambao lugha yao ya kwanza ni Kiswahili.

(v) Kuwashauri waandishi wote kuhusu vitabu wanavyokusudia kuandika.

(vi) Kusahihisha na kusanifisha lugha ya vitabu vyote vilivyopendekezwa kutumiwa shuleni.

(vii) Kutoa orodha ya vitabu vya lazima na vya ziada vinavyohitajika shuleni.

(viii) Kufanya mpango wa kutafsiri au kuviandika upya kwa Kiswahili, vitabu vilivyopendekezwa.

(ix) Kukagua na kusanifisha Kiswahili cha vitabu hivyo kabla havijachapishwa.

(x) Kusahihisha na kutoa mawaidha (ya kurekebisha) vitabu vyote vinavyoshughulikiwa na kamati.

(xi) Kutoa taarifa kwa waandishi wa habari kuhusu njia tofauti (mitindo) ya kusomesha katika kila nchi.

(xii) Kujibu maswali yote yanayohusu lugha ya Kiswahili na maandishi yake.

(xiii) Kufanya jambo lolote lile ambalo lingesaidia kuyatimiza madhumuni haya (Ratcliffe, 1942: 5-6).

Mkutano wa kwanza wa kamati ulifanyika mjini Nairobi mnamo Aprili 1930. Mwenyekiti alikuwa mkurugenzi wa elimu nchini Kenya. Fredrick Johnson alichaguliwa kuwa katibu wa kwanza wa kamati. Mambo muhimu yaliyojadiliwa yalihusu usanifishaji wa Kiswahili, taratibu za kushughulikia miswada na vitabu vilivyopelekwa kukaguliwa, uandishi wa makamusi, ratiba ya vitabu vitakavyoandikwa mwaka huo pamoja na upeo wa kamati.

Kamati ilitafsiri vitabu vya fasihi na vya sayansi kwa Kiswahili na ilizingatia uchapishaji wa vitabu vya Kiswahili sanifu kwa lengo la kuwashawishi waandishi wapya waendelee kufanya hivyo. Kwa mfano, *Kisiwa Chenye Hazina* (1929), *Safari za Gulliver* (1932) *na Mashimo ya Mfalme Suleimani* (1948). Matbaa ya kuchapisha vitabu yalichapisha baada ya ithibati ya kamati kupatikana kwani vitabu hivyo vingetumiwa katika shule za serikali na zile zenye kupata ruzuku ya serikali. Ithibati hiyo ilidhihirisha kuwa vitabu vya Kiswahili vingepata wanunuzi, jambo ambalo lilisaidia kupunguza gharama ya kuchapisha vitabu vya Kiswahili ambavyo havikuwa na wasomaji wengi nje ya shule. Waandishi walipata moyo wa kuandika walipojua kwamba vitabu vyao vingetumika kote katika Afrika Mashariki.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, lugha huwa kama bidhaa muhimu inapokuwa na faida katika jamii. Kwa hivyo, lugha ya Kiswahili ilitumika

katika uandishi wa vitabu vilivyotumika kote nchini. Matokeo yake ni kuwa Kiswahili kilipata hadhi ndiposa kikaenea kote nchini.

3.1.1 Usanifishaji wa Kiswahili

Kulingana na Ferguson (1968: 3), usanifishaji ni hali ambapo lahaja moja ya lugha inaendelea kukubalika katika jamii lugha kama muundo mwafaka zaidi katika eneo kubwa la jamii. Lahaja hii inachukuliwa kuwa wastani au sanifu. Lahaja wastani au sanifu ni ile inayokubaliwa kama njia kamili ya kuandika lugha (Mbaabu, 1978: 7).Kulingana na King'ei (2010: 112), lugha sanifu ni ile iliyoteuliwa ili kutumika katika shughuli zote za kitaifa hasa katika elimu na sheria pamoja na utawala. Usanifishaji wa lugha ni utaratibu wa kuhakikisha njia au mfumo sawa wa kuitamka na kuiandika lugha au lahaja. Maoni hayo yanashadidiwa na Ipara na Maina (2008: 33) wanapoeleza kuwa, usanifishaji ni uamuzi wa kuchagua lugha moja au mojawapo ya lahaja za lugha na kuifanyia marekebisho ya kimatamshi, kisarufi, kimaana na kimaandishi ili iweze kutumika katika shughuli rasmi.

Kulingana na Mathooko (2007: 111), usanifishaji unanuia kuiendeleza lugha kwa mtindo mmoja, kuwa na ulinganifu wa matumizi ya maneno yaliyokuwepo na yale mapya, kupatikana ulinganifu wa sarufi, kuangalia uwezo wa lugha hiyo, kuandikwa upya na kupambanuliwa. Kwa hivyo, kusanifisha lugha ni ule utaratibu wa kuondoa tofauti zote za kilahaja, kimaeneo na kitabaka katika othografia, msamiati, sarufi na matamshi.

Kwa mujibu wa Mbaabu (1985: 204), othografia inapaswa kusanifishwa ili kupata mtindo mmoja wa kuandika kila neno katika lugha kulingana na matamshi. Hivyo, lugha sanifu ni aina ya usemi unaokubalika katika jamii kama lugha wastani ya mawasiliano inayotumiwa katika maandishi na mazungumzo rasmi.

Utaratibu wa kusanifisha lugha huanzishwa tu iwapo pana haja ya kuwa na lugha sanifu itakayotumika katika kuandikia, kufunzia na kuchapishia sheria pamoja na vitabu vingine rasmi. Utaratibu huu hufuata hatua kadha kama anavyoeleza King'ei (2010: 115). Kwanza, kuna uteuzi wa lahaja au lugha mojawapo ambayo itakuwa msingi wa lugha. Pili, kuna uteuzi wa lahaja mojawapo kuwa lugha rasmi au lugha ya taifa. Tatu, kuna hatua ya uteuzi au uundaji wa asasi au chombo cha kuboresha lugha iliyoteuliwa kama vile baraza, halmashauri au taasisi. Hatua inayofuata ni ya kuunda, kupanua na kupanga matumizi ya msamiati maalum au istilahi zinazohitajika katika nyanja mbalimbali kama vile ufundi, sayansi, kilimo na nyinginezo. Hatua hii pia inashirikisha uundaji wa othografia, utunzi wa vitabu vya sarufi vinavyoelezea matumizi sahihi ya lugha. Hatua ya mwisho ni ya usambazaji wa msamiati maalum au istilahi kupitia vyombo vya habari na hasa majarida, kamusi na vitabu maalum.

Usanifishaji wa Kiswahili ulichochewa na hali ya kuwepo kwa lahaja nyingi za Kiswahili. Kulikuwa na haja ya kuwa na lugha au lahaja moja ambayo ingeeleweka na kila aliyekifahamu Kiswahili. Pia, hati ya Kiarabu na Kirumi zilitumiwa kuandika Kiswahili. Jambo hili lilisababisha tofauti katika namna ya kuendeleza maneno. Kuna sababu mbili za kidini zilizopelekea kusanifishwa kwa Kiswahili. Kwanza, kulikuwa na haja ya kutoa mafunzo ya kidini na mahubiri ya Injili kwa lahaja moja. Wamisheni kama vile Krapf wa dhehebu la C.M.S na Askofu Steere wa dhehebu la U.M.C.A walikuwa na haja ya kutumia lahaja moja ili kuepuka hali ya kutoelewana katika mahubiri, mafundisho na maandishi yao. Krapf na wenzake walitumia lahaja ya Kimvita ilhali Steere alitumia Kiunguja. Pili, kulikuwa na haja ya kutafsiri maandiko ya Biblia kwa lahaja moja ili watu wengi wayasome na kuyaelewa. Aidha, kulikuwa na haja ya kusawazisha maandishi ya kitaalamu. Viongozi wa kidini waliokuwa wataalamu wa

lugha walikuwa wametunga vitabu vya Kiswahili. Krapf alikuwa ametunga kamusi na kuandika kitabu cha sarufi kilichoitwa *Swahili Grammar* (1850) kwa lahaja ya Kimvita. Steere kwa upande mwingine alikuwa amechapisha kitabu kwa jina *A Handbook of the Swahili Language* (1870) kwa lahaja ya Kiunguja. Tofauti zilizojitokeza katika maendelezo ya maneno na msamiati zilizusha ubishi mkali huku kila mmoja akitetea msimamo wake.

Kadhalika, kulikuwa na sababu mbili za kielimu zilizopelekea kusanifishwa kwa Kiswahili. Kwanza, kulikuwa na haja ya kutumia lahaja moja kufundishia shuleni ili kudumisha mawasiliano kati ya walimu na wanafunzi. Pili, kulikuwa na haja ya uandishi wa vitabu vya elimu kwa kutumia lahaja moja. Ili kukabiliana na matatizo hayo ya kidini na kielimu, nchi za Afrika Mashariki ziliungana na kuanzisha Kamati ya Lugha (ya Kiswahili) ya Afrika Mashariki ili kusanifisha na kukuza Kiswahili. Kiunguja kiliteuliwa kama msingi wa kusanifisha Kiswahili kwa sababu kilikuwa kimeenea kama lugha ya biashara kuliko Kimvita na lahaja zingine. Pia, Kiunguja kilitumiwa na watu wengi kwa kuwa na wepesi wa kufahamika. Isitoshe, Kiunguja kilikuwa kimefanyiwa uchunguzi mwingi na wataalamu na kutumiwa katika shughuli za kielimu na kidini.

Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha inasisitiza kuwa lugha inayotimiza mahitaji katika jamii huwa yenye faida na ndio huenea. Kwa hivyo, Kiunguja kiliteuliwa kwa kuwa na manufaa kwa jamii kama lugha ya biashara pamoja na matumizi yake katika utawala na elimu.

3.1.2 Mashindano ya Uandishi

Ili kuwatia moyo Waafrika waweze kuandika na kutosheleza mahitaji ya vitabu vya fasihi, Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki ilianzisha mashindano ya kuandika insha mwaka wa 1935. Katika kuwapa waandishi motisha ya kuendeleza vipawa

vilivyogunduliwa katika mashindano ya insha, mashindano ya uandishi yalianzishwa mwaka wa 1939. Huu ndio mwaka ambao Waafrika wa kwanza akiwemo mwandishi mashuhuri Shaaban Robert na wengine mmoja mmoja kutoka kila koloni walijiunga na kamati. Kutokana na mashindano hayo, miswada mingi ilipelekewa kamati. Shaaban Robert alipata nafasi ya kuchapisha kazi zake na kupanua ushairi. Mashindano hayo yalianza kuwashirikisha washindani wazungu katika mwaka wa 1942 ili kukuza uandishi wa Kiswahili miongoni mwa watawala wa siku za baadaye (Ratcliffe, 1942: 9). Kamati ilikuwa ikichapisha vitabu vya Kiswahili sanifu ili iwashawishi waandishi wapya na kuhakikisha kwamba vitabu vilikuwa vikitafsiriwa kwa Kiswahili.

Mashindano ya uandishi wa Kiswahili yaliendelea wakati wa Vita vya Pili vya Dunia. Zawadi mbili za kwanza za uandishi wa insha zilinyakuliwa na Wakenya wawili kutoka shule za upili za wavulana za Alliance na Mang'u. Zawadi ya tatu ilinyakuliwa na mtu mmoja kutoka Masasi Tanganyika. Mnamo mwaka wa 1943, Waafrika walioshiriki kwenye mashindano ya uandishi wa Kiswahili, ikiwa ni pamoja na askari jeshi walikuwa 215 lakini hakukuwa na yeyote aliyeshiriki kutoka shule za Waingereza. Shaaban Robert aliwahi kushinda katika mashindano hayo. Kitengo cha kamati kilichokagua mashindano ya uandishi kiliridhika kwamba mashindano hayo yalisaidia katika kueneza ujuzi wa kusoma na kuandika Kiswahili.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, lugha hutumika sio tu kama chombo cha mawasiliano lakini hubainisha uwezo fulani unaomfanya mtu aonyeshe umilisi alionao. Hivyo, umilisi wa lugha ya Kiswahili ulidhihirika katika mashindano ya uandishi yalioieneza lugha ya Kiswahili kupitia uandishi wa insha na vitabu vya Kiswahili.

3.1.3 Kuundwa kwa Shirika la Uchapishaji wa Vitabu

Shirika la Uchapishaji wa Vitabu la Afrika Mashariki lililojulikana kama East African Literature Bureau (E.A.L.B) liliundwa mwezi wa Januari, mwaka wa 1948 kama mojawapo ya huduma zilizotolewa na East African High Commission. Shirika liliundwa baada ya kufanywa uchunguzi ulioagizwa na mkutano wa magavana wa Afrika Mashariki. Uchunguzi huo ulifanywa kuanzia Julai, mwaka wa 1945 hadi 1947. Kulingana na Chege (1978: 128), E.A.L.B ilirithi kampuni ya uchapishaji ya C.M.S iliyojulikana kama Ndia Kuu Press (Highway Press). Mkurugenzi wa kwanza wa E.A.L.B alikuwa C.G. Richards. Makao makuu ya shirika hilo yalikuwa mjini Nairobi lakini kulikuwa na matawi madogo mjini Kampala na Dar es Salaam. Tawi la Dar es Salaam lilihudumia Tanganyika na Zanzibar.

Shirika la E.A.L.B lilipewa mamlaka ya utoaji na uchapishaji wa vitabu. Kazi hiyo hapo awali ilikuwa ikifanywa na Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki. Pia, kazi ya upangaji wa mashindano ya uandishi wa Kiswahili ilikabidhiwa E.A.L.B ingawa usomaji na utoaji uamuzi wa maandishi hayo ulikuwa ukifanywa na kamati. Shirika hili lilitoa huduma za maktaba kwa kutumia magari yaliyozitembelea shule za miji ya Afrika Mashariki. Huduma hii ya maktaba pia ilitolewa kupitia njia ya posta.

E.A.L.B ilianzishwa ili kukabiliana na mahitaji ya vitabu yaliyokuwa yakiongezeka kwa haraka kati ya Waafrika walioelimika. Kwa hivyo, ilitarajiwa kuchapisha na kutawanya vitabu vya fasihi kwa watu wa kawaida, vitabu vya lazima vya shule, vitabu vya kilimo na ufundi vya watu wazima, magazeti au majarida, kuwasaidia waandishi wa kiafrika na kutoa huduma za maktaba (E.A.L.B, 1950: 2).

Kamati iliweza kuchapisha jarida la *E.A.I.L.C Bulletin* ambalo lilikuwa jukwaa la kujadili masuala muhimu yanayohusu Kiswahili. Maswali ya umma kuhusu maneno

mapya, asili ya maneno na maneno yaliyoazimwa na kisha maneno yaliyokubaliwa yalichapishwa katika *ILC Bulletin.* Mnamo mwaka wa 1954 jarida lilibadilishwa jina kutoka *Bulletin* hadi *Journal.* Katika mwaka wa 1956, mbali na kuchapisha Jarida, kamati ilianza kutayarisha vitabu vya ziada ambavyo vingechapishwa kama nyongeza kwa Jarida. Karibu vitabu hivyo vyote vilikuwa tenzi. Kulikuwa na *Utenzi wa Vita vya Wadachi* kilichohaririwa na J.W.T Allen na *Utenzi wa Vita vya Majimaji* kilichoandikwa na Abdul Karim bin Jamaliddini na kuhaririwa na W.H Whiteley. Vitabu vingine vya ziada vilivyochapishwa mwaka wa 1958 ni *Maisha ya Siti Binti Saad* cha Shaaban Robert na *Maisha ya Hemed bin Mohammed yaani Tippu Tip kwa Maneno Yake Mwenyewe* kilichoandikiwa utangulizi kihistoria na kufasiriwa na Bi. Alison Smith. Pia, Jarida hilo lilichapisha makala fupi iliyoitwa "Halmashauri ya Kiswahili ya Afrika Mashariki" iliyoandikwa na Shaaban Robert wa Tanganyika. Makao makuu ya E.A.L.B ambayo yalikuwa Nairobi yalichapisha vitabu vya Kiingereza, Kiswahili na lugha za kwanza. Vitabu vyote vilivyochapishwa na tawi la Dar es Salaam vilikuwa vya Kiswahili au Kiingereza. Kiswahili kilikuwa kimeenea kote Zanzibar na Tanganyika kwa hivyo, uchapishaji wa vitabu vya Kiswahili ulieneza Kiswahili kote nchini.

Kutokana na shughuli za Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki, imebainika kuwa, ilifanikisha upatikanaji wa maandishi kwa Kiswahili sanifu baada ya kusanifisha Kiswahili. Kwa kuzingatia uchapishaji wa vitabu kwa Kiswahili sanifu hasa kuanzia mwaka wa 1948 shirika la E.A.L.B lilipoundwa, waandishi wengi walitiwa moyo wa kuandika vitabu. Isitoshe, mashindano ya kuandika insha na vitabu yaliwatia ari waandishi wa Kiswahili. Kwa hivyo, shughuli za Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki zilihimiza utunzi wa kazi za fasihi ushairi ukiwepo. Washairi walitunga mashairi yenye

maudhui ya kuhimiza utunzi wa mashairi, kutoa ushauri kwa watunzi, kuelezea umuhimu wa mashairi pamoja na mchango wa washairi.

3.2 Utunzi wa Mashairi

Mnyampala (1965) ametunga mashairi yanayolenga kuhimiza utunzi wa mashairi. Kwa mfano, shairi "Yaliyopita Yamepita". Katika ubeti wa kwanza anasema:

> Hapana cha upinzani, cha ugomvi na matata,
> Watunzi na ubishani, vile watunzi kuteta,
> Sasa wanayo imani, umoja wamelumbata,
> Ya ugomvi yamepita, na tutunge ya uhuru (Mnyampala, 1965: 120).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, mizozo na ubishani uliokuwepo kati ya washairi umeisha na sasa wana imani kuwa watakuwa na umoja. Anawahimiza watunge mashairi ya uhuru. Pia, katika ubeti wa pili mshairi anasema:

> Ya uhuru yatungeni, ya ugomvi yamepita,
> Tanganyika nchi amani, nchi haina wasalata,
> Washairi unganeni, na utunzi kutakata,
> Ya ugomvi yamepita, na tutunge ya uhuru (Mnyampala, 1965: 120).

Katika ubeti huu, mshairi anaendelea kuwahimiza washairi watunge mashairi ya uhuru. Tanganyika ni nchi ya amani. Kwa hivyo, washairi waungane ili utunzi uwe bora. Mshairi amewataja washairi wa maeneo tofauti kote nchini Tanganyika na kuwashauri waendeleze utunzi wa mashairi. Baadhi ya waliotajwa ni Bwana Gonga, Khamis bin Amani, Damieni na Mandevu.

Kulingana na Nadharia ya Utegemezi, utegemezi wa lugha za kigeni unaweza kuondolewa kwa Waafrika kutetea na kudumisha uchumi, siasa, utamaduni, lugha na

waandishi wazalendo wa Afrika (Ngugi 1986: xii). Hivyo, ili kusitisha utegemezi washairi walihimiza Watanganyika kudumisha lugha ya Kiswahili na kutetea uhuru wa nchi yao.

Pia, katika shairi "Chama na Kibarikiwe", Mnyampala (1965), anasifu chama cha watunzi wa mashairi. Katika ubeti wa nne mshairi anasema:

> Chama shairi kuimba, na wengi yatamaniwe,
> Chama watunzi kuchimba, tungo njema zitakiwe,
> Chama lugha na kilemba, vidarane vyongokewe,
> Chama na kibarikiwe, kisitawi na kupendwa (Mnyampala, 1965: 80).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, chama kinafaa kiwe na mashairi ya kuimbwa yanayopendwa na watu. Watunzi watunge tungo njema zenye lugha inayopendeza. Anakiombea chama kistawi na kupendwa. Katika ubeti wa sita mshairi anasema:

> Chama kipige marimba, milio zifurahiwe,
> Chama kizidishe namba, watunzi wanyanyuliwe,
> Chama kipate wa Pemba, na Unguja kisifiwe,
> Chama na kibarikiwe, kisitawi na kupendwa (Mnyampala, 1965: 80).

Katika ubeti huu, mshairi angependa wanachama wa chama cha washairi wafurahi. Mshairi anaeleza matarajio yake kuwa, wataongezeka na kuwe na wanachama kutoka Pemba na Unguja. Kwa hivyo, watunzi wa mashairi watakuwa wengi. Vilevile, chama kiwe na matawi yake huko Bukwimba, Kigoma na Kiserawe. Mshairi anaendelea kueleza kuwa, chama ndio kimepanda shamba na lazima lilimiwe yaani chama ndio kimeanza kazi na lazima kiendeleze utunzi wa mashairi ili yawe mengi na yasipungue kiweze kusifika.

Mnyampala (1965) ametunga mashairi kadhaa yanayosifu magazeti ya Kiswahili yaliyokuwa yanachapisha mashairi ya watunzi mbalimbali kama vile gazeti la *Mwananchi* na la *Kiongozi*. Katika shairi "Mwananchi Usonge Mbele", Mnyampala (1965) analisifu gazeti la *Mwananchi* na kuliombea lizidi kukua. Katika ubeti wa pili wa shairi anasema:

> Pasiwe mtu kupinga, *Mwananchi* usonge mbele,
>
> Tena usifanywe bunga, na kama juzi na vile,
>
> *Mwananchi* itoe kunga, kwa lafidhi ya upole
>
> *Mwananchi* usonge mbele, songa usirudi nyuma (Mnyampala, 1965: 66).

Katika ubeti huu, mshairi anaomba pasiwe pakatokea mtu akazuia gazeti la *Mwananchi* kuendelea ama kuonesha kuwa halina umuhimu kama zamani. Mshairi anapendekeza gazeti lieleze kunga za utunzi wa mashairi kwa lugha inayoeleweka.

Vilevile, katika ubeti wa tisa anasema:

> *Mwananchi* litoe mwanga, ling'ae na vigelegele,
>
> Ukweli hutauvunga, ufiche ukweli ule,
>
> Uwachongee mizinga, waonje asali wale,
>
> *Mwananchi* usonge mbele, songa usirudi nyuma (Mnyampala, 1965: 67).

Katika ubeti huu, mshairi angetaka gazeti la *Mwananchi* lielimishe na kufurahisha watu. Pia, angependa lisifike kwa kueleza ukweli na kuwaletea tungo tamu kama asali watakazofurahia.

Aidha, gazeti la *Mwananchi* linaendelea kusifiwa katika shairi “Mwananchi Utabalaji”. Mnyampala (1965) anaeleza furaha yake kuwa gazeti la *Mwananchi* limetolewa. Katika ubeti wa kwanza anasema:

Risala imetufika, imenea kila mji,
Mwananchi amezalika, nasi tumlishe uji,
Nasi tumefurahika, tunaipiga buruji,
Mwananchi utabalaji, kiza kuu litoweke (Mnyampala, 1965: 67).

Katika ubeti huu mshairi anasema kuwa, habari imeenea kila mji kuwa kuna gazeti mpya limeanza kutolewa. Washairi ndio “watakaolilisha uji” yaani wataliandikia mashairi lizidi kukua. Mshairi anaeleza kuwa, washairi wamefurahi ndiposa wanapiga tarumbeta. Mshairi anaposema “Mwananchi utabalaji, kiza kuu kitoweke” anamaanisha kuwa, angependa gazeti litoe nuru ama lielimishe watu kwa mambo wasiyoyajua. Mshairi anasema gazeti hili linapendwa na wageni na wenyeji kutoka mijini na vitongojini. Anaendelea kueleza kuwa, analiombea gazeti lipate baraka kwa kushirikisha washairi wote. Gazeti halitakuwa na mchukiaji bali litaneemeka kwa kupata mtaji.

Katika ubeti wa nane mshairi anasema:

Hakuna la kuchujuka, tupo nasi wapambaji,
Daima tutaandika, tupo sisi wandikaji,
Habari ziso na shaka, kwani wapelelezaji,
Mwananchi utabalaji, kiza kuu litoweke (Mnyampala, 1965: 67).

Katika ubeti huu mshairi anaeleza kuwa, watu wa kulipamba gazeti wapo yaani watunzi wa mashairi wanaoandika habari njema zisizo na shaka. Anasema washairi wanafanya upelelezi kabla ya kuandika gazetini.

Vilevile, katika ubeti wa tisa anasema:

> *Mwananchi* umeumbika, nasifu Mtengenezaji,
> U mwepesi kusomeka, na vyepesi kwa mwuzaji,
> Kurasa zimepanuka, kutimiza mahitaji,
> *Mwananchi* utabalaji, kiza kuu litoweke (Mnyampala, 1965: 67).

Katika ubeti huu, mshairi analisifu gazeti la *Mwananchi* kwa sababu linasomeka vizuri na bei yake ni nafuu.Tena, lina kurasa pana zinazotimiza mahitaji ya habari zake. Mshairi ana matumaini kuwa utunzi wa mashairi utaendelea.

Gazeti la *Mwananch*i linaendelea kusifiwa katika shairi "Johari Ninakupamba."Katika shairi hili, Mnyampala (1965) analinganisha *Mwananchi* na johari kwa kuwa na thamani. Katika ubeti wa tatu mshairi anasema:

> Tenzi *Mwananchi* ridhie, ndio johari napamba,
> Kurasani nipambie, kati kati nikiwamba,
> Niwambe kikukalie, kiache kuyumba yumba,
> Johari ninakupamba, pambo la waraka tenzi (Mnyampala, 1965: 69).

Katika ubeti huu mshairi anasema kuwa, atalipamba gazeti la *Mwananchi* kwa mashairi hadi liridhike. Mashairi yake yatakuwa katika kurasa ili gazeti liwe imara. Anasema gazeti hilo linaweza tu kupambwa vizuri kwa tenzi yaani mashairi. Pia, katika ubeti wa nne anasema:

> *Mwananchi* ujivalie, wakusifu hata shamba,
> Na watu washangilie, shangwe iende sambamba,
> Ndipo wakukimbilie, pasi na watu kugomba,
> Johari ninakupamba, pambo la waraka tenzi (Mnyampala, 1965: 69).

Katika ubeti huu, mshairi anasema kuwa, gazeti likipambwa kwa mashairi litasifika hata vijijini na watu watalipenda. Anaendelea kusema kuwa sifa zake zikienea washairi watalitungia mashairi hata wale wa mbali kama Msimba. Hivyo, mshairi anaonyesha umuhimu wa kutunga mashairi na kuyachapisha magazetini.

Isitoshe, katika shairi "Mwananchi Kua Salama", Mnyampala (1965) anasifu gazeti la *Mwananchi* na kuhimiza washairi watunge tungo ili zipambe na kulikuza gazeti. Katika ubeti wa tatu mshairi anasema:

> Wasili hapa jamali, *Mwananchi* mwenye hekima,
> Kurasazo tusabili, tujisomee nudhuma,
> Uwafunze majahili, watokane na zahama,
> *Mwananchi* kua salama, twakuombea salama (Mnyampala, 1965: 68).

Katika ubeti huu, mshairi anatamani gazeti la *Mwananchi* liwafikie kwa sababu lina hekima inayowafunza washairi waache kugombana. Washairi kutoka Dodoma ni kumi na wawili wanaosoma gazeti na wenye uwezo wa kutunga mashairi bora. Amewataja washairi kama Jitukali, Nyamaume, Shabani Musa Bin Omari, Mary Mangwela na wengine. Mshairi anawasifu kwa kuwa wana heshima. Anawasihi watunge mashairi ili gazeti la *Mwananchi* likue vyema.

Kulingana na Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, watu hutumia lugha kulingana na mahitaji ya jamii au hadhira inayokusudiwa. Hivyo, washairi wa Dodoma walitunga mashairi ili yachapishwe katika gazeti la *Mwananchi* kwa lengo la kuwaelimisha wananchi. Kupitia njia hii Kiswahili kilienea kote nchini.

Gazeti lingine linalosifika ni gazeti la *Kiongozi*. Katika ubeti wa tatu wa shairi "Kiongozi Mtukufu", Mnyampala (1965) anasema:

Uzuri wako pekee, hapana ulinganifu,
Kila mara utokee, zidi usiwe pungufu,
Tamaa tukupokee, kila mwezi maradufu
Kwa sifa na utukufu, *Kiongozi* uendelee (Mnyampala, 1965: 27).

Katika ubeti huu mshairi anasema kuwa, uzuri wa gazeti la *Kiongozi* hauwezi kulinganishwa na wa gazeti lingine. Mshairi angependa liwe linatolewa mara mbili kila mwezi. Katika ubeti wa kumi mshairi anasema:

Kaditamati tupambie, ndiwe wetu msanifu,
Kiongozi tupambie, mema yasiyo tukifu,
Mashairi tutilie, yenye heshima hawafu,
Kwa sifa na utukufu, *Kiongozi* wendelee (Mnyampala, 1965: 27).

Katika ubeti huu mshairi anasema kuwa, gazeti la *Kiongozi* ndilo linaweza kuwaletea mashairi mazuri na yenye heshima. Hivyo, analisifu na angependa liendelee kukua.

Mnyampala (1965) anaendelea kusifu gazeti la *Kiongozi* katika shairi "Twongoze kwa Mteremo". Katika ubeti wa kwanza mshairi anasema:

Kiongozi ja murua, Gazeti lenye nderemo,
Ninaliombea dua, lizidishe chake kimo,
Kimo bora cha kukua, kwa kurasa za masomo,
Kila habari zenye simo, tuongoze *Kiongozi (*Mnyampala, 1965: 143).

Katika ubeti huu mshairi kuwa, anasema gazeti la *Kiongozi* ni nzuri na linafurahisha. Angependa lizidi kukua ili lipate kuelimisha watu. Mshairi anaendelea kuonyesha umuhimu wa *Kiongozi.* Katika ubeti wa tano anasema:

Kua nimekuteua, ushike sana milimo
Ya maarifa panua, ya Elimu na Kilimo,
Hali ya nchi pindua, usawazishe vipimo,

> Mashairi ya mzamo, tuongoze *Kiongoz*i (Mnyampala, 1965: 143).

Katika ubeti huu mshairi anasema kuwa, angependa gazeti hili likue na kupanua maarifa yake ya elimu na kilimo. Pia, gazeti lieleze hali ya nchi na kuongoza katika kutoa mashairi. Hivyo, mshairi anabainisha umuhimu wa gazeti hili.

Isitoshe, Mnyampala (1965) analisifu gazeti la *Kiongozi* katika shairi "Kukuzwa Twafurahia". Katika ubeti wa kwanza mshairi anasema:

> Hadi nyoyo zimependa, nafsi kufurahia,
>
> Kiongozi umetanda, tulivyo tukililia,
>
> Ama kweli umeshinda sote tunashangilia,
>
> Kukuzwa twafurahi, *Kiongozi* twakupenda (Mnyampala, 1965: 38).

Katika ubeti huu, mshairi anasema amefurahi sana kwa sababu gazeti la *Kiongoz*i limeenea kama walivyotaka. Kwa hivyo, anashangilia ushindi wa kukua kwa gazeti analolipenda. Mshairi angependa gazeti liwafikie watu wa nchi ya Tunisia na nchi za kusini mwa bara la Afrika bila tatizo lolote. Gazeti lionyeshe ufundi wake katika utunzi wa mashairi huku likieleza matendo ya siku ya uhuru. Mshairi anadhihirisha umuhimu wa mashairi yaliyokuwa katika gazeti la *Kiongozi.*

Kama Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha inavyoeleza, lugha yenye hadhi na faida katika jamii huenea. Kwa hivyo, lugha ya Kiswahili ilienea kwa kutumiwa katika mashairi yaliyoshughulikia masuala muhimu katika jamii.

Kandoro (1966) alitunga shairi "Tukifanye Chama Chetu Watungaji Mashairi" ili kuhimiza washairi kutunga mashairi. Katika shairi hili anawasihi washairi waunde chama chao na wawe na gazeti lao. Mshairi anaeleza kuwa, ni kazi ya washairi kutunga

mashairi kwani wasipofanya hivyo watakuwa wanajihasiri. Katika ubeti wa tatu anasema:

> Wenzangu tujisitiri, tusitiriwe na watu,
> Utungaji mashairi, wahifadhi lugha yetu,
> Tusimame kiamiri, kujenga muruwa wetu,
> Tukifanye chama chetu, watungaji mashairi (Kandoro, 1966: 28).

Katika ubeti huu, mshairi anabainisha kuwa, utungaji wa mashairi ni muhimu kwani unahifadhi lugha ya Kiswahili. Anawaomba washairi wasimame imara na wawe na heshima. Vilevile, katika ubeti wa nne mshairi anasema:

> Tujitoe kwa hiari, tuikuze lugha yetu,
> Mafunzo yenye hiari, yawe gazetini mwetu,
> Na mafunzo ya hatari, tutupe ndani ya mwitu,
> Tukifanye chama chetu, watungaji mashairi (Kandoro, 1966: 28).

Katika ubeti huu mshairi anaeleza kwamba, ikiwa wangependa kuikuza lugha yao hawana budi kutoa mafunzo gazetini kupitia mashairi. Pia, wasitoe mafunzo yasio na maana au hatari. Anawaomba washairi wajitoe kwa hiari na kutoa mali yao ili waanzishe chama cha watungaji mashairi. Mshairi anapendekeza wachague kiongozi ambaye angetangaza wito huo na tena waamue kule ambako wangeanzisha ofisi zao. Shairi hili linabainisha haja ya utunzi wa mashairi ili kukuza na kuendeleza Kiswahili.

Nadharia ya Utegemezi inasisitiza kuwa ili kuondoa utegemezi wa lugha za kikoloni, Waafrika wanapaswa kutetea na kudumisha lugha yao. Hivyo, mshairi alihimiza washairi waikuze lugha ya Kiswahili kama njia ya kusitisha utegemezi wa lugha za kikoloni.

Robert (1969) anahimiza washairi watunge mashairi. Katika shairi "Wafu Wenye Sauti" amewataja washairi kadhaa akiwaomba wajibu swali lake lililokuwa katika gazeti la *Mamboleo.* Washairi wanaoombwa kutunga mashairi ni pamoja na Bwana Mwalimu Kihere, Abushiri wa Mbwana na Haya bin Hanasa. Katika ubeti wa pili mshairi anasema:

> Abushiri wa Mbwana, tunga kwa vituo,
> Mistari pima sana, pasiwe ipitanayo,
> Kisha iwe na maana, ueleze watu hao,
> Popote ulipoona, miujiza kama hiyo (Robert, 1969: 1).

Katika ubeti huu, mshairi anamhimiza Abushiri atunge shairi kwa kuzingatia vituo. Pia, apime mishororo ili itoshane kisha iwe na maana kwa watu. Katika ubeti wa nne mshairi anasema:

> Tena Mzee Waziri, stadi wetu wa leo,
> Simulia kwa shairi, Mombo mji ukaao,
> Namna ya wasafiri, wazikao kama hao,
> Tunga kwa mistari, isiyopitana cheo (Robert, 1969: 1).

Katika ubeti huu, mshairi anamwambia Mzee Waziri asimulie jinsi mji wa Mombo ulivyo kishairi huku akieleza jinsi wasafiri walivyo. Mshairi alimtaka atunge shairi kwa kuzingatia utoshelevu wa mishororo. Mshairi anasema majibu ya swali lake anayangoja katika gazeti la *Mamboleo.* Kupitia njia hii mshairi anahimiza utunzi wa mashairi.

Kama Nadharia ya Utegemezi inavyoeleza kuwa Waafrika wanaweza kuondoa utegemezi kwa kutetea na kudumisha waandishi wa kiafrika, mshairi anawataja na kuwasifu washairi wa Kiswahili. Kupitia utunzi wa mashairi yaliyochapishwa gazetini, lugha ya Kiswahili ilienea.

Aidha, katika shairi “Moyo unapopenda”, Robert (1969) anaeleza jinsi moyo wake unavyopenda kutunga na kusifu mashairi. Katika ubeti wa kwanza mshairi anasema:

> Kutunga na kukusifu, ni alama ya kupenda,
> Wala usitie hofu, jambo hili nikitenda,
> Nalitenda kwa unyofu, wala usidhani inda,
> Na njia japo ndefu, mimi sitachoka kwenda (Robert, 1969: 7).

Katika ubeti huu mshairi anasema kuwa, anapenda kutunga na kusifu mashairi. Kwa hivyo, mtu asiwe na wasiwasi anapomwona akitunga mashairi kwani anafanya hivyo kwa moyo mwema. Ingawa anapata shida hatakufa moyo. Mshairi yuko tayari kukabiliana na matatizo yoyote atakayokubana nayo ili afanikiwe. Kwa kuwa moyo wake unapenda utunzi, hupata nguvu mpya inayomhimiza kuendelea. Isitoshe, mshairi anaendelea kubainisha kuwa yuko tayari kutunga mashairi.

Katika shairi “Gazeti Halina Nafasi”, Robert (1969) anasema kuwa, anajitahidi kutunga mashairi yaani utenzi. Katika ubeti wa kwanza mshairi anasema:

> Ahsante Bwana Edi, salamu nimeziona,
> Nitafanya jitihadi, utenzi uzidi tena,
> Beti elfu idadi, zimekwisha patikana,
> Na nyingine zaidi, kiwandani nazisana (Robert, 1969: 49).

Katika ubeti huu, mshairi anamweleza Bwana Edi yaani mhariri wa gazeti kuwa amepokea salamu zake. Kisha anasema anajitahidi kutunga mashairi. Tayari ameandika beti elfu moja na zingine zinaandaliwa. Aidha, katika ubeti wa pili anasema:

> Nasikitika gazeti, sasa nafasi halina,
> Karatasi hatupati, zimekuwa shida sana,
> Tunazopata katiti, hazitoshi kama jana,

Zikichapwa nyingi beti, habari zitabanana (Robert, 1969: 49).

Katika ubeti huu, mshairi anasikitika kuwa, gazeti halina nafasi kwa hivyo, hata akitunga beti nyingi hazitatoshea gazetini kwani habari zitabanana. Mshairi angependa gazeti likue kwa urefu na upana ili azidishe beti alizotunga. Anamwombea Hitler ashindwe vita ili atunge shairi linaloelezea kuwa vita vimeisha. Katika shairi hili, mshairi anabainisha hamu aliyonayo ya utunzi na utunzi wake unahusu masuala yaliyomo katika jamii.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, lugha yenye faida huenea kutokana na majukumu yake katika jamii. Hivyo, Kiswahili kilienea kwa sababu kilitumika kama chombo cha kujieleza.

3.3 Ushauri kwa Watunzi wa Mashairi

Robert (1969) anawashauri washairi waelewane katika shairi "Kundi". Katika ubeti wa kwanza anasema:

Kundi moja wanakaa, wadudu wadogo sana,
Na ndege wenye manyoya, kundi moja hupatana,
Wanadamu vibaya, kutengana kwa fitina,
Kwani hatuna haya, siku zote kugombana? (Robert, 1969: 76).

Katika ubeti huu mshairi anasema kuwa, wadudu wadogo na ndege hukaa katika kundi moja na hupatana lakini binadamu hutengana kwa fitina na hawaoni haya. Kwa maoni yake, binadamu ameumbwa tofauti na wanyama kama vile, simba, mamba, mbogo, nungu au nyoka lakini anazua zogo kama wanyama. Binadamu anamfanyia mwingine hila na kumsababishia machungu yanayomdhuru. Tofauti na nyoka binadamu hana sumu kinywani lakini maneno yake yanaharibu ushirika. Katika ubeti wa saba anasema:

Wala hatuna mikonga, mfano kama wa tembo,

Hutamanije kutunga, kuburuga kila jambo,

Kwa kusudi la kugonga, wenzetu kwa makumbo,

Na kuwavutia janga, tufananao kwa umbo? (Robert, 1969: 76)

Katika ubeti huu mshairi anasema kuwa, binadamu ameumbwa tofauti na tembo kwani hana mikonga. Anajiuliza kinachosababisha mtunzi kutunga kazi inayovuruga mambo na kuwaumiza wenzake na kuwaletea janga ingawa wote wanafanana yaani ni watunzi. Kwa hivyo, mshairi angependa washairi waishi kwa amani na wajue kuwa binadamu wote ni sawa yaani binadamu wote hufanana kiumbo.

Kama Nadharia ya Utegemezi inavyosisitiza, jamii inayonuia kujikomboa kutokana na ukoloni haina budi kutumia lugha moja ya kuwaunganisha watu ili kuwa na umoja kwa lengo la kujikomboa. Mshairi anatumia lugha ya Kiswahili kuwashauri Watanganyika waungane na waishi kwa amani. Kwa hivyo, lugha ya Kiswahili inatumiwa kuwakomboa Watanganyika kutokana na utegemezi wa lugha za kikoloni.

Kandoro (1966) anawashauri watunzi wa mashairi katika shairi "Haki Huvunja Milima". Katika ubeti wa tatu anasema:

Najua tangu zamani, wajinga watanisema,

Mwakipoteza kiini, cha mambo niliyosema,

Kutukana gazetini, mwajivunjia heshima,

Haki huvunja milima, niliambiwa shuleni (Kandoro, 1966: 67).

Katika ubeti huu mshairi anasema kuwa, alijua tangu zamani kuwa wajinga wangemsema kwa kutoelewa aliyoyasema. Anasisitiza kuwa kwa kutukana gazetini, washairi wanajivunjia heshima. Anaendelea kusema kuwa:

Mjibuo fikirini, mbona mwajibu hasama,

Ninavyotaka yakini, Afrika kusimama,

Mbona meli baharini, mwaiendesha mrama,

Haki huvunja milima, niliambiwa shuleni (Kandoro, 1966: 67).

Katika ubeti huu, mshairi anawashauri watunzi wafikirie majibu wanayoyatoa kwa sababu yanazua uhasama. Yeye angependa kuona bara la Afrika likiwa imara kwa hivyo, anawaombea washairi wasiharibu mambo.

Mnyampala (1965) ametunga mashairi mengi yanayowashauri watunzi wa mashairi wapendane. Katika shairi "Komesheni Magombano", anawakanya kuzozana kwani wanafaa kuwa marafiki. Katika ubeti wa kwanza mshairi anasema:

Mwache mkiki-mkiki, ugomvi na matetano,

Nakanya hamkanyiki, mnazidi mzozano,

Nasema halisimbuki, simbiko kwazo mifano,

Komesheni magombano, watunzi ni marafiki (Mnyampala, 1965: 14).

Katika ubeti huu, mshairi anawashauri washairi waache ugomvi na mzozo ili utunzi usitatizike kwani watunzi ni marafiki. Pia, anawaonya dhidi ya mashindano yasiyofaa lakini angependa waungane. Katika ubeti wa tatu anasema:

Dhihaka huleta chuki, na huvuta utengano,

Shindano halikatiki, kidimbwi ndani ya chano,

Ninyukwe sitetereki, kaja yangu muungano,

Komesheni magombano, watunzi ni marafiki (Mnyampala, 1965: 14).

Katika ubeti huu mshairi anasema kwamba, dhihaka huleta chuki inayosababisha utengano. Utengano nao huleta dhiki kwa hivyo, "ngoma haichezeki" yaani utunzi wa mashairi unaathirika washairi wanapoanza mapambano. Amewataja washairi maarufu

kama vile Jitukali, Nyamaume, Shaaban, Snow-White, Mwinyihatibu na wengine na kuwaomba waache ugomvi. Mshairi anamsifu mshairi maarufu Shaaban Robert anayejulikana kote Afrika Mashariki kama kiongozi wa mikutano ya washairi. Anamwomba atafute suluhisho ili waweze kuvuta washairi wapate kuongezeka na kufikia laki moja. Aidha, anawasihi mashabiki wao waache kuzidisha ugomvi.

Kama Nadharia ya Utegemezi inavyosisitiza, Waafrika wanapaswa kutetea na kudumisha waandishi wazalendo wa Afrika ili kuondoa utegemezi. Mshairi anawataja washairi maarufu na kuwahimiza waendelee kutunga mashairi bila ugomvi ili wawavutie watunzi wengine. Utunzi wa mashairi ukiendelezwa Kiswahili kitaenea na kusitisha utegemezi wa lugha za kikoloni.

Katika ubeti wa kumi na mbili mshairi anasema:

> Tusifanye uzandiki, vijembe mikwaruzano,
>
> Hivyo huleta hamaki, na kutiana mikono,
>
> Nayo siyo itifaki, iletayo husiano,
>
> Komesheni magombano, watunzi ni marafiki (Mnyampala, 1965: 15).

Katika ubeti huu, mshairi anawaomba washairi waache uzandiki na kukwaruzana kwa mafumbo. Jambo hili linaweza kuleta hamaki na kusababisha mapigano yanayoharibu uhusiano wa washairi. Mshairi anamalizia shairi kwa kuwasihi mashabiki wa washairi waache kuzidisha ugomvi badala yake waelewane katika hali yoyote ile.

Katika shairi “Usitunge Uchokozi”, Mnyampala (1965) anawaonya washairi hasa Bwana Mbwana dhidi ya uchokozi. Katika ubeti wa tatu mshairi anasema:

> Wafumba fumbo mchana, lifumbuliwe na njozi?
>
> Kupima refu na pana, ukuta tia timazi,

Kumbuka utaachana, urudi kuwa bomozi,

Usitunge uchokozi, kutaja mtu na jina (Mnyampala, 1965: 60).

Katika ubeti huu mshairi anaeleza kuwa, ingawa mtunzi wa shairi anatoa fumbo asitaje mtu kwa jina kwani huo ni uchokozi. Mshairi anapaswa awe makini anapofumba asije akaharibu uhusiano wa washairi. Anamalizia shairi kwa kusema kuwa:

Halmashauri tuna, Sheikh Kombo mwangalizi,

Watu wanapogusana, kwa matusi na utwezi,

Mwenyewe ndiye supana, kufunga na mfunguzi,

Usitunge uchokozi, kutaja mtu na jina (Mnyampala, 1965: 60).

Katika ubeti huu, mshairi anashukuru kuwepo kwa Sheikh Kumbo anayewaongoza watunzi waache matusi na utwezi. Katika shairi hili, mshairi anawashauri washairi watunge mashairi yasiyozua uchokozi. Mshairi anasema ingawa mshairi anatoa fumbo asitaje mtu kwa jina kwani huo ni uchokozi.

Pia, katika shairi "Washairi Hupendana", Mnyampala (1965) anasisitiza kuwa, washairi wanapaswa kupendana na kwamba kashifa si ushairi. Utunzi wa mashairi ya kashifa unawavunjia heshima na kusababisha matusi, mizozo na utengano. Katika ubeti wa tano mshairi anasema:

Pendana kama Dodoma, sisi tunavyopendana,

Tuwavute wa Mrima, mpate nanyi patina,

Na Unguja waadhama, sote tuje kuungana,

Washairi hupendana, kashifa si ushairi (Mnyampala, 1965: 62).

Katika ubet huu, mshairi anawasifu washairi wa Dodoma kwa kupendana. Wao wana umoja na ushirikiano kwa kila jambo. Mmoja wao akishambuliwa wanaungana kumwokoa. Mshairi angependa waungane na washairi wa Mrima na Unguja waunde chama kimoja. Anasema washairi wanapozozana watu watawachukulia kuwa watu

wasio na akili. Anawaongoza washairi jinsi ya kutunga mashairi yenye maarifa na mafunzo mbalimbali kama ya kilimo, kufuma fulana na kusana. Anamalizia kwa kusema kuwa, ikiwa washairi wangekuwa watu wazima na wasijifanye vijana, chama chao kingefana.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, lugha huwa bidhaa muhimu kutokana na majukumu inayotimiza katika jamii. Ushairi wa Kiswahili ulitumiwa kutoa mafunzo mbalimbali kwa jamii. Kwa hivyo, lugha ya Kiswahili ilienea kwa sababu ilitumiwa na washairi wa maeneo tofauti kama vile Unguja na Tanganyika.

Katika shairi “Mzozo Wangu Patano”, Mnyampala (1965) anaeleza kuwa, siku zote anashangaa kuona vijana wasiopenda ushirikiano wanaotukanana. Anawajulisha kwamba washairi hupendana. Anawaeleza kuwa, washairi hupatana wakaendesha mikutano ya maana na kutunga mashairi mazuri. Hawatengani kwa fitina na minong’ono. Anamwomba Sihiyana awashauri washairi watano wasioelewana kwani aliongea na Adam na wakaelewana. Khalfani na Gonga nao wanaombwa waache mapigano. Makarani na Miraji wanastahili kusameheana ili waache kashifa na matusi. Katika ubeti wa tisa mshairi anasema:

> Ya Illahi ya Rabana, wajalie mapatano,
> Wapeane muawana, yenye upenzi maneno,
> Mawaidha kupeana,wasia na tangamano,
> Mzozo wangu patano, washairi hupendana (Mnyampala, 1965: 108).

Katika ubeti huu, mshairi anamwomba Mungu awajalie washairi mapatano waweze kutumia maneno ya mapenzi. Pia, washairi washauriane na washirikiane. Katika ubeti wa mwisho anasema:

> Namuomba Subuhana, alete afikiano,
> Tuache kununiana, tupatane kama ngano,
> Ndipo utunzi tanona, tuachapo utengano,
> Mzozo wangu patano, washairi hupendana (Mnyampala, 1965: 108).

Katika ubeti huu, mshairi anamwomba Mungu awasaidie waelewane na kuacha kununiana waweze kupatana kama ngano. Wanapoacha utengano utunzi wa mashairi utaendelea.

Fauka ya hayo, katika shairi "Bure Wanajikalifu", Mnyampala (1965) anaendelea kushauri washairi waungane. Anamsifu Miraji Zodo kwa utunzi na vitendo vyake kwa sababu amewaonya wapinzani waache kashifa na wakubali kuungana. Katika ubeti wa tatu mshairi anasema:

> Adam ashike gunzi, apasuguwe pachafu,
> Wawekwe katika konzi, kufanya usuluhifu,
> Umoja huwa ni kanzi, zinapotunzwa sarafu,
> Tujiunge kwa sufufu, tungo njema kuzisana (Mnyampala, 1965: 119).

Katika ubeti huu, mshairi anamwomba Adam atafute suluhisho kwa kuwaleta washairi pamoja. Umoja umefananishwa na hazina kubwa inayohifadhiwa ardhini. Mshairi angependa washairi waungane kwa wingi waweze kutunga mashairi mema. Washairi wengi wangeungana, wachache waliobaki hawangeweza kufanikiwa. Washairi

wanaombwa wasikubali kudhoofika kwa mashairi yanayozua kichefuchefu bali wakubali kuacha ugomvi.

Vilevile, Mnyampala (1965) anawasifu washairi wa Dar es Salaam kwa kuacha ugomvi. Katika shairi “Penda -Chako Nimefurahi” anasema kuwa, hakuwahi kukaa au kudiriki kuwatembelea washairi wa Dar es Salaam lakini alikuwa amefurahia mapenzi yao. Katika ubeti wa nne mshairi anasema:

> Na Mungu awabariki, vita mfanye suluhi,
>
> Mapenzi kwenu yabaki, na itoweke kebehi,
>
> Uhuru tuumiliki, kuchao na asubuhi,
>
> Penda- Chako nafurahi, kwa washairi wa Dar (Mnyampala, 1965: 138).

Katika ubeti huu, mshairi anamwomba Mungu awabariki washairi wanapotafuta suluhisho la vita vyao. Anawaomba washairi wawe na mapenzi na kuacha kudharauliana mpaka wapate uhuru.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Utegemezi, jamii inayonuia kujikomboa kutokana na ukoloni haina budi kutumia lugha moja ya kuwaunganisha watu ili kuwa na umoja kwa lengo la kuleta ukombozi. Washairi walitumia lugha ya Kiswahili kutungia mashairi yaliyoeleza kuwa ikiwa wangeungana na kusuluhisha tofauti zao wangeweza kupigania uhuru wao na kuondoa utawala wa kikoloni.

Katika ubeti wa mwisho anasema:

> Kaditama siandiki, nakuoneni malihi,
>
> Tusi sasa hamtaki, mambo mumetanabahi,
>
> Nawaombea Maliki, naomba kwenu nasahi,

Penda- Chako nafurahi, Kwa washairi wa Dar (Mnyampala, 1965: 138).

Katika ubeti huu, mshairi anawaona washairi wa Dar es Salaam kuwa werevu au wazuri kwa sababu hawataki matusi. Kwa hivyo, anawaombea Mungu awape nasaha. Katika shairi hili, mshairi anawahimiza washairi watunge mashairi yasiyo na matusi.

Kulingana na Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, lugha yenye thamani huenea. Washairi walikuza lugha ya Kiswahili kutokana na thamani yake kama chombo cha kujieleza.

3.4 Umuhimu wa Mashairi

Robert (1968) anaelezea mapenzi yake kwa ushairi kwa kubainisha umuhimu wake. Katika shairi "Ushairi" anasema kuwa, ushairi ni kama hirizi ya bahati kwa sababu ni kama malaika anayemsaidia katika ibada na sala. Yeye hana uwezo wa kunena wala nguvu ya kujiendesha lakini Mungu amempa uwezo wa kutunga shairi. Anaendelea kusema kuwa, watu hupenda uchumi wa mali au fedha lakini yeye anapenda ushairi ndio akasema "Bali huba yangu mimi, ni ushairi kuzidi". Anajiona yeye si kitu mbele ya mabwana walio maarufu kwa sifa na heshima ya nasaba. Lakini kwa nguvu ya ushairi, yeye anaweza kufanya mambo makuu akaonekana kama kiongozi mkuu mahali palipo na askari. Ushairi humpandisha ari, akajiona kama mtu mashuhuri na aliye madhubuti kama chuma. Pia, mshairi huweza kutambua siri za moyo wake akazuia fikira na nia au maazimio. Wasafiri wanapomtembelea na kumwambia kuwa anastahili heshima kwa kipawa chake, yeye huwajibu kuwa ni zawadi kutoka kwa Mungu. Anamshukuru Mungu kwa kipawa hicho na kuomba msamaha kwa kujisifu. Katika shairi hili mshairi anadhihirisha mapenzi yake kwa ushairi na matarajio yake kuwa ushairi uzidi kuendelea.

Pia, Robert (1969) anaendelea kubainisha umuhimu wa ushairi katika shairi “Hazina”. Anasema:

> Mashairi ni hazina, katika kila msemo,
> Huongoza kuona, mambo mengi yaliyomo,
> Katika dunia pana, mfano kama masomo,
> Tena huwafaa sana, watu wa kila makamo (Robert, 1969: 50).

Katika shairi hili lenye ubeti mmoja, mshairi analinganisha mashairi na hazina ili kudhihirisha thamani yake. Mashairi ni muhimu kwa sababu huongoza mtu kuona mambo mengi yaliyomo duniani. Kwa hivyo, hutoa mafunzo mbalimbali. Aidha, mashairi yanawafaa watu wa kila umri.

Zaidi ya hayo, katika shairi “Barua”, Robert (1969) anausifu ushairi wa Musa Rashid na ushairi kwa jumla. Katika shairi hili, mshairi anasema kuwa, alipata barua ya Musa Rashid iliyoandikwa kishairi. Anamsifu Rashid kwa utunzi wake bora. Amependezwa na beti jinsi zilivyoandikwa kwa ufasaha na maana ikajitokeza vyema. Shairi linafurahisha kwa jinsi maneno yalivyotumiwa. Kwa hivyo, Rashid anastahili kuhesabiwa miongoni mwa washairi bora.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, lugha hutumika sio tu kama chombo cha mawasiliano lakini hubainisha uwezo fulani unaomfanya mtu aonyeshe umilisi wa lugha alionao. Kwa hivyo, Musa Rashid anadhihirisha umilisi wa lugha alionao kwa kutumia lugha kwa ufasaha katika shairi.

Katika ubeti wa nne anasema:

> Masuto hayawi fumo, hasa ya wenye wazimu,
> Japo kuwa si chumo, mashairi ni matamu,

Katika kila masomo, ya watu wataalamu,
Mashairi ni kilimo, na mbegu ya fahamu (Robert, 1969: 60).

Katika ubeti huu mshairi anasema kuwa, masuto hayana hadhi yoyote hasa kutoka kwa wenye wazimu. Ingawa mashairi hayana mapato, ni matamu hasa yanapotoa mafunzo ya taaluma mbalimbali. Mashairi yanalinganishwa na kilimo kwa sababu yana mazao kwa kuwa watu hufahamu mambo mengi. Kwa mfano, kupitia shairi alipata habari kuwa mwenzake alikuwa mgonjwa. Isitoshe, katika ubeti wa saba mshairi anasema:

Nilialikwa niwemo, juzi katika karamu,
Nikakuta Harvey yumo, anaagwa na walimu,
Nikasikia msemo, wa hotuba moja tamu,
Iliyotia tetemo, kwa shairi maalumu (Robert, 1969: 60).

Katika ubeti huu mshairi anasema kwamba, alipohudhuria karamu ya walimu ya kumuaga Harvey, alipata kusikiliza hotuba moja tamu iliyotolewa kishairi. Kwa hivyo, mshairi anausifu ushairi kwa kuwa na majukumu tofauti ya kuwasilisha ujumbe na kuburudisha.

Kama nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha inavyosisitiza, lugha huwa bidhaa muhimu na yenye thamani kutokana na majukumu mengi inayotimiza katika jamii. Lugha ya Kiswahili ilitimiza majukumu tofauti katika jamii kama vile kuwasilisha ujumbe na kuburudisha hivyo basi, ikaenea kote nchini Tanganyika.

Mnyampala (1965) anausifu ushairi kwa kudhihirisha umuhimu wake katika shairi “Shairi Johari Shwari”. Katika ubeti wa kwanza anasema:

Shairi tunga tongole, kito hiki cha johari,
Shairi tuweke mbele, na moyoni tukariri,
Shairi tusome shule, tujifunze kubashiri,

> Shairi johari shwari, tangu zamani za kale (Mnyampala, 1965: 79).

Katika ubeti huu mshairi anasema kuwa, shairi ni tungo za thamani zinazosifika na kukaririwa moyoni. Tunastahili tujifunze mashairi shuleni ili tupate kuyaelewa. Ushairi umekuwepo tangu zamani na ni tungo za milele. Ushairi umelinganishwa na tungo za milele kama vile Injili na Zaburi zinazohubiriwa ulimwenguni. Ushairi si matusi bali ni kauli za upole zenye kuhubiri mazuri. Ushairi unaosifika ni ule unaoonyesha uhodari wa utunzi kwa kutumia lugha inayofaa kwani mshairi ni tajiri wa lugha. Mshairi anawashauri watunzi wa mashairi kutunga mashairi mazuri yasiozua vita au kukasirisha wengine lakini yatungwe kwa nia njema.

Mshairi anasifu kipindi cha mashairi redioni. Katika shairi "Nashangilia Unguja", Mnyampala (1965) anamwombea heri mhariri wa kipindi cha mashairi. Anaeleza kuwa anashangilia Unguja kwa kuwa na kipindi cha mashairi. Anamwomba mhariri awaletee tafrija katika kipindi cha mashairi lakini achunguze anayoyaleta kwa utaratibu yasije yakasababisha mabaya. Mashairi yanayokaririwa redioni ni ya hekima na furaha kwa sababu huimbwa yakapendeza sana. Huwaliwaza hata wenye shida wakatulia. Mshairi anamsalimu Bwana Hija na kumjulisha kuwa angetembelea Unguja mambo yasipobadilika. Shairi hili linadhihirisha mashairi yalisifika kwa kuwa na majukumu kama vile ya kuburudisha, kuelimisha na kuliwaza jamii.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, maelezo haya yanabainisha kuwa, lugha ya Kiswahili ilisifika kwa kuwa na faida yaani kuwa bidhaa muhimu katika 'soko' ama hadhira inayokusudiwa kutokana na dhima yake katika jamii.

3.5 Mchango wa Shaaban Robert katika Kueneza Kiswahili

Shaaban Robert alikuwa mshairi maarufu aliyesifika nchini Tanganyika. Kwa maoni ya Kezilahabi (1976: 1) Robert alikuwa na kipaji cha ushairi kinachoonekana katika uchaguzi wake wa maneno ya kishairi na katika matumizi yake ya picha. Kwa mfano, katika shairi "Kiswahili" (Robert, 1966: 27-31) anatumia sitiari ya titi la mama kurejelea lugha ya Kiswahili. Anasema Kiswahili ni lugha tamu iliyomkuza na haiwezi kulinganishwa na lugha nyingine yoyote. Anaisifu na kuelezea matumizi yake hasa anapojieleza kupitia ushairi. Kutokana na sera ya lugha ya kipindi cha ukoloni iliyokiunga mkono Kiswahili, Robert alikitetea kwa kutunga kazi za kifasihi ushairi ukiwepo kwa Kiswahili sanifu. Maisha ya Shaaban Robert ya kazi yalivuka mipaka ya utumishi wa serikali ya kikoloni kwa manufaa yao hadi kwenye shughuli za kukuza na kuendeleza Kiswahili kwa manufaa ya wazawa (Chuachua, 2011: 40).

Mapenzi ya Shaaban Robert kwa Lugha ya Kiswahili yanaonekana waziwazi katika mashairi yake. Kupitia mashairi yake, anaonekana ni mkuzaji na mwendelezaji madhubuti wa Kiswahili (Hassan, 2020: 199). Kutokana na diwani zake za ushairi ni dhahiri kuwa ameikuza lugha ya Kiswahili kimsamiati. Robert alikuwa mwenyekiti wa Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki kutoka mwezi wa Novemba 1961 hadi Juni 1962 alipofariki. Katika kamati hii katibu walikuwa wataalamu wa kigeni kama vile Whiteley, Jan Knappert na Allen. Kulikuwa na Waafrika wachache waliokuwa wanakamati kama vile Sheikh Saleh Farsi na Muhammed Kombo.

Kulingana na Kezilahabi (1976: 2), Robert alikuwa na uhusiano mzuri na wanakamati wenzake wa Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki alipokuwa msomaji wa miswada iliyochapishwa na jarida lililokuwa likiitwa *Swahili Journal.* Wanakamati walipenda maandishi yake sio tu kwa uzuri wake lakini kwa sababu ya msamiati wake mwingi

uliioonekana katika maandishi hayo. Kutokana na kuwepo kwake katika kamati na uhusiano wake mzuri na wanakamati waliokuwa na imani naye, Robert aliweza siyo tu kuchapisha vitabu vyake na diwani za mashairi kwa urahisi lakini pia kupata makala mengi na mawaidha ya kitaalamu.

Kutokana na maelezo hayo ni dhahiri kuwa Robert alishiriki katika uundaji wa sera ya lugha ya kabla ya uhuru wa Tanganyika. Yeye pamoja na washairi wengine wa kipindi hicho kama Saadani Kandoro, Amri Abedi, Akilimali Snow-White na Mathias Mnyampala walikuza Kiswahili kimsamiati kupitia diwani zao za mashairi zilizotungwa kwa Kiswahili sanifu. Baadhi ya maudhui yaliyozungumziwa na Robert yalihusu kanda ya Afrika Mashariki. Alipofariki washairi walihuzunika na kutunga mashairi ili kuelezea sifa zake pamoja na kudhihirisha hisia zao.

Mnyampala (1965) alitunga shairi"Watunzi Tuna Huzuni" ili kuelezea huzuni iliyowapata washairi Robert alipofariki. Mshairi anamrejelea kama rubani kwani ndiye aliyewaongoza watunzi wa mashairi. Katika ubeti wa tatu mshairi anasema:

> Bingwa lugha Kiswahili, alikuwa nambawani,
>
> Elimu ya kila hali, kila mbinu za undani,
>
> Wa Kiswahili kamili, cha lafidhi fasahani,
>
> Kifo cha Bwana Shaaban, kimetutia huzuni (Mnyampala, 1965: 150).

Katika ubeti huu, mshairi anasema kuwa, Robert alikuwa bingwa wa lugha ya Kiswahili kwani alikielewa kwa undani; lafudhi na ufasaha wake. Alikuwa mtunzi mwenye ujuzi wa kila fani kwani alitunga vitabu kumi na viwili mojawapo kikiwa ni *Adili na Nduguze.* Mshairi anakubaliana na Rais Nyerere kuwa nchi inasikitika kwa kifo cha Robert kwani alikuwa amekiinua Kiswahili. Robert alikuwa mtunzi bora aliyetumia Kiswahili kigumu

na chepesi katika vitabu vyake. Kwa hivyo, vitabu vyake vingetumika mijini na hata shuleni. Aidha, Robert alitumia Kiswahili cha kale na cha sasa katika majibu na maswali yake. Nchi ya Tanganyika ilimtegemea kwani kazi zake zilitumiwa kila mahali Afrika na hata Ulaya. Shaaban hakupenda ama kutamani ufedhuli. Alichukia wahuni na akaamua kuzama katika elimu. Alipenda ukweli na kujitenga na uongo. Vitabu alivyoviandika ni vitamu kwani yaliyomo yanapendeza. Hata hivyo, mtunzi huyu si mchoyo kwani vitabu vyake vinatumiwa katika elimu duniani kote. Mshairi anamalizia shairi lake kwa kumwomba Mungu ailaze roho ya Robert mahali pema peponi. Ingawa amefariki kimwili awe na uzima wa rohoni huko mbinguni. Katika shairi hili, ni wazi kuwa Robert alikuwa na mchango mkubwa katika kueneza lugha ya Kiswahili na katika utunzi wa kazi za fasihi ushairi ukiwepo.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Utegemezi, Waafrika wanaweza kuondoa utegemezi kwa kutetea na kudumisha waandishi wazalendo wa Afrika. Mshairi anamsifu Shaaban Robert kwa mchango wake wa kueneza Kiswahili kupitia mashairi ya Kiswahili.

Isitoshe, Mnyampala (1965) ametunga shairi lingine linaloitwa “Kifo cha Bwana Robert”. Katika shairi hili, mshairi anasema kuwa, kifo cha Bwana Robert ni hasara kwa sababu kinaathiri maenezi ya Kiswahili. Anaanza shairi lake kwa kutuma rambirambi kwa mke na watoto wa Robert. Anasema kifo cha Robert ni hasara kwa nchi kwa sababu ni kama taa ikizimika usiku katikati kwani Kiswahili kitakosa mtu wa kuzibia nyufa. Mshairi anasisitiza kuwa, Robert ndiye bingwa wa nudhuma kwani alikuwa na ufundi wa kuzipanga beti na kuzipima, mashairi yake yakawa na thamani. Wote walioyasoma mashairi yake waliyapenda. Aliheshimika kwa kuwa na sifa njema katika maandishi na mazungumzo kwani utunzi wake ni imara. Katika ubeti wa saba anasema:

Na ndiye mwenye ulama, wa Kiswahili la dhati,

Alikuwa mwanachama, Kiswahili kutafiti,

Tena alikuwa mwema, alipendwa na umati,

Kifo cha Bwana Robert, hasara kwa Kiswahili (Mnyampala, 1965: 151).

Katika ubeti huu mshairi anaeleza kuwa, Robert ni mtaalamu wa kweli wa Kiswahili. Alikuwa miongoni mwa watafiti wa Kiswahili. Kadhalika, alikuwa mwema na alipendwa na watu kwa hivyo, kifo chake ni hasara kwa Kiswahili. Aidha, katika ubeti wa nane anasema:

Vitabuvye vya hekima, alivyotunga mufti,

Katu havina kilema, na kuleta ati ati,

Ni vitabu vyenye mema, havinao usaliti,

Kifo cha Bwana Robert, hasara kwa Kiswahili (Mnyampala, 1965: 151).

Katika ubeti huu, mshairi anavisifu vitabu vya Robert kwa kuwa ni vyenye hekima na vilivyotungwa vizuri. Havina kasoro wala kutoeleweka kwani ni vitabu bora visivyo na usaliti.

Mnyampala (1965) anaeleza sifa za Shaaban Robert katika shairi "Komesheni Magombano." Katika ubeti wa sita mshairi anasema:

Mshairi tamalaki, ni Shaaban mno,

Afrika Mashariki, ndiye mwenye julikano,

Watunzi katumiliki, mkuu wa mikutano,

Komesheni magombano, watunzi ni marafiki (Mnyampala, 1965: 15).

Katika ubeti huu mshairi anasema kuwa, Robert anatamalaki eneo la Afrika Mashariki kwani anasifika sana. Yeye ndiye kiongozi wa watunzi wote anayeendesha mikutano.

Katika shairi hili mshairi analenga kubainisha umaarufu na umuhimu wa Robert katika fasihi.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, lugha hutumika sio tu kama chombo cha mawasiliano lakini hubainisha uwezo fulani unaomfanya mtu aonyeshe umilisi wa lugha alionao. Hivyo, Shaaban Robert alidhihirisha ubingwa wake katika utunzi wa kazi za fasihi. Tungo zake zilikuza na kueneza Kiswahili katika eneo la Afrika Mashariki.

3.6 Hitimisho

Sura hii imechunguza hali ya shughuli za Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki ili kutathmini jinsi zilivyochochea mabadiliko ya maudhui katika ushairi wa Kiswahili. Uchunguzi umeonyesha kuwa Kamati hiyo ilipoundwa mwaka wa 1930 ilikuwa na malengo mengi. Baadhi ya malengo hayo yalikuwa ni kusanifisha Kiswahili, kuchapisha vitabu vya Kiswahili na kuhimiza uandishi kwa kuandaa mashindano ya uandishi wa insha na vitabu. Kamati iliwahimiza na kuwasaidia waandishi wa Kiswahili washairi wakiwepo kwa kuwachapishia kazi zao asilia kwani tafsiri zilifanywa na wazungu. Kubuniwa kwa shirika la uchapishaji la E.A.L.B mwaka wa 1948 kuliwafanya Waafrika wajitegemee katika uchapishaji wa vitabu kwani hapo awali walitegemea mashirika ya kigeni kama vile Shirika la Uchapishaji la Chuo Kikuu cha Witwatersrand cha Afrika kusini. Watunzi kama Shaaban Robert waliweza kuchapisha mashairi yao yaliyotungwa kwa Kiswahili sanifu kinyume na mashairi yaliyotungwa sehemu ya pwani yaliyotumia lahaja za Kiswahili. Kama Nadharia ya Utegemezi inavyosisitiza, Waafrika wanapaswa kutumia lugha moja ya kuwaunganisha watu ili kuwa na umoja kwa lengo la kusitisha utegemezi ndiposa watunzi wa mashairi wakatumia Kiswahili. Hivyo, washairi walizingatia sera ya lugha iliyokuza na

kuendeleza Kiswahili. Shaaban Robert alichangia sana katika kupanuka kwa ushairi. Kutokana na shughuli hizo za kamati, watunzi wa mashairi walihimizwa na kushauriwa kuendeleza utunzi wa mashairi. Magazeti ya Kiswahili yalichapisha mashairi kwa hivyo, yalichangia kukuza ushairi wenye maudhui tofauti. Washairi waliunga mkono sera ya lugha ya kipindi cha kabla ya uhuru kwa sababu walishiriki katika usanifishaji wa Kiswahili kama wanakamati.

Mihimili ya Nadharia ya Utegemezi ilitumiwa kuchunguza jinsi watunzi wa mashairi walivyositisha utegemezi wa lugha za kikoloni kwa kutetea na kutukuza lugha ya Kiswahili katika mashairi. Aidha, mihimili ilitumiwa kuchunguza jinsi washairi walivyotumia Kiswahili sio tu kama chombo cha mawasiliano bali kama lugha ya kuwaunganisha Watanganyika kwa lengo la kuleta ukombozi. Vilevile, mihimili ilitumiwa kuchunguza jinsi washairi walivyotetea utamaduni wao hasa lugha pamoja na kutukuza waandishi wa Afrika. Mihimili ya Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha ilitumiwa kuchunguza sababu zilizoifanya lugha ya Kiswahili kusifika na kuwa na thamani kama bidhaa muhimu katika “soko” au jamii. Isitoshe, mihimili ilitumiwa kuchunguza majukumu ya lugha ya Kiswahili yaliyoifanya kuwa na faida katika jamii.

Katika sura ifuatayo uchunguzi ulifanywa ili kutathmini jinsi kanuni za utunzi wa mashairi zilivyochochea mabadiliko ya kimaudhui katika ushairi nchini Tanganyika.

SURA YA NNE

KANUNI ZA UTUNZI WA MASHAIRI NA MAUDHUI YA USHAIRI

4.0 Utangulizi

Sura iliyotangulia ilichunguza jinsi shughuli za Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki zilivyochochea mabadiliko ya kimaudhui ya ushairi wa Kiswahili nchini Tanganyika kati ya mwaka 1930 hadi 1960. Uchunguzi ulidhihirisha kuwa Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki ilisanifisha Kiswahili, ikachapisha vitabu vya Kiswahili na ikaandaa mashindano ya uandishi wa insha na vitabu ili kuhimiza uandishi. Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki ilikabidhi Shirika la Uchapishaji la EALB mamlaka ya utoaji na uchapishaji wa vitabu. Shirika hili liliundwa mwaka wa 1948. Makao makuu yalikuwa Nairobi na matawi madogo yalikuwa Kampala na Dar es Salaam. Mkurugenzi wa kwanza alikuwa C.G Richards aliyekua meneja wa kampuni ya Ndia Kuu Press (Chege, 1978: 128). EALB ilianzishwa ili kutosheleza mahitaji ya vitabu yaliokuwa yakiongezeka kwa haraka kati ya Waafrika walioelimika. Kwa hivyo, shirika lilitarajiwa kuchapisha na kutawanya vitabu vya fasihi kwa watu wa kawaida, vitabu vya lazima kwa shule, vitabu vya kilimo na ufundi vya watu wazima, magazeti au majarida. Pia, shirika liliwasaidia waandisho wa Kiafrika na kutoa huduma za maktaba. Vilevile, shirika lilikabidhiwa kazi ya upangaji wa mashindano ya uandishi wa Kiswahili ijapokuwa usomaji na utoaji uamuzi wa maandishi hayo ulikuwa ukifanywa na kamati. Kufikia mwaka wa 1953 waandishi wengi walikuwa wakipeleka miswada yao moja kwa moja kwa EALB bila kupata ithibati ya kamati. Isipokuwa miswada hiyo iwe ni ya vitabu vya shule, EALB haikusisitiza kuwepo kwa kibali cha kamati kabla ya kuvichapisha. Hivyo, waandishi wa Kiswahili wakiwemo watunzi wa mashairi walihimizwa kuendeleza uandishi kwa kuchapishiwa kazi zao. Baadhi ya kazi

zilizochapishwa ni *Utenzi wa Vita vya Majimaji* kilichaandikwa na Abdul Karim bin Jamahiddini kilichohaririwa na W.H. Whiteley katika mwaka wa 1957. Vitabu vingine ni *Maisha ya Siti Binti Saad* cha Shaaban Robert na *Maisha ya Hemed bin Mohammed yaani Tippu Tip kwa Maneno Yake Mwenywewe* kilichoandikiwa utangulizi wa kihistoria na kufasiriwa na Bi. Alison Smith. Vitabu hivi vilichapishwa mwaka wa 1958. Sehemu ya uchapishaji wa magazeti ya EALB ilichapisha gazeti la kila wiki lililojulikana kama Tazama (Mbaabu, 2007: 83). Kwa hivyo, waandishi wa Kiswahili wakiwepo washairi kama Shaaban Robert walichapisha kazi zao. Mashairi yaliyotungwa yalibeba maudhui ya kuhimiza utunzi wa mashairi, kutoa ushauri kwa watunzi, kueleza umuhimu wa mashairi na kutoa sifa kwa washairi maarufu kama vile Shaaban Robert.

Sura hii ililenga kuchunguza jinsi kanuni za utunzi wa mashairi zilivyochochea mabadiliko ya maudhui ya ushairi nchini Tanganyika kati ya mwaka wa 1930 hadi 1960. Baadhi ya kanuni hizo ni kuwepo kwa vina, mizani, kituo, muwala, urari, kutosheleza, kiini na lugha mwafaka. Sura hii ilibainisha athari ya kanuni za utunzi wa mashairi katika uteuzi wa maudhui ya ushairi uliotungwa katika kipindi cha ukoloni nchini Tanganyika. Sura hii ilidhihirisha kuwa, washairi walitunga mashairi yaliyohimiza utunzi wa mashairi ya arudhi na kuwashauri watunzi. Pia, mashairi yalieleza umuhimu wa ushairi pamoja na kuwasifu washairi.

4.1 Maana ya Ushairi

Dhana ya ushairi kimsingi ni pana sana na imezua mizozo na mitafaruku mingi miongoni mwa wanataaluma (Msokile, 1993: 51). Hata hivyo, kwa mujibu wa utafiti huu maoni ya washairi wa jadi au wanamapokeo ndio yatakayozingatiwa.Wataalamu mbalimbali walitoa fasili tofauti katika dibaji za diwani zao. Katika dibaji ya

Mnyampala (1965), anafafanua ushairi kuwa, ni msingi wa maneno ya hekima tangu kale. Ndicho kitu kilicho bora sana katika maongozi ya dunia kwa kutumia maneno ya mkato na lugha nzito yenye kunata iliyopangwa kwa urari wa mizani na vina maalum kwa ushairi. Shairi laweza kumliza mtu akatokwa na machozi kwa ajili ya mchomo wa hanjari la kuukata moyo na maini kwa ule mchomo na mguso wa maneno ya shairi la mshairi bora. Vilevile, shairi jingine laweza kuuburudisha moyo wa mtu akafurahi akthari ya furaha na kujiona kuwa nayo heri mithili ya mtu aliyoko peponi. Shairi lina usemi ulio mtamu sana, kwa maoni yanayopenya na mafunzo yenye uadilifu na mazingira ya dunia yalivyo.

Kutokana na maelezo haya ni wazi kuwa, Mnyampala anauona ushairi kuwa umejengwa na vitu viwili mahsusi: maneno ya hekima na sanaa yenyewe. Kulingana na Mnyampala ili maneno ya hekima yaweze kuingizwa katika ushairi, sharti yawe na lugha ya mkato, nzito, yenye kunata na ni lazima maneno yake yawe katika mpango wa urari wa vina na mizani. Pia, anasisitiza juu ya sanaa ya ushairi anaposema mambo yafuatayo:

1. Shairi liwe na Kiswahili kinachohusu mwendo wa mashairi bora.

2. Shairi liwe na urari wa mizani kamili zinazohusikana na ushairi wa kawaida kwa lugha ya Kiswahili kisichokuwa na kashfa au matusi ndani yake.

3. Shairi liwe na vina vinavyopatana, hususan mwishoni mwa kila ubeti kwa shairi lote zima ingawa vina vya katikati vikosane kwa utenzi wake.

4. Shairi kama halikulingana vina vyake yaani, mtiririko lakini liwe na muwala. Yaani liwe na maana iliyo bora sana yenye ufundisho ndani mwake, furahisho, mvuto wa maarufu au vitu vinginevyo vinavyostahili kusifiwa.

5. Lisizidi mno maneno ya kurudiarudia. Kulinganisha matuta lisiwe pyororo la mashairi bali liwe shairi kamili kama mashairi ya watu mahiri, werevu na wenye hekima.

Kwa upande mwingine, Robert (1958: 37) anafafanua ushairi kuwa, ni sanaa ya vina inayopambanuliwa kama nyimbo, mashairi na tenzi. Zaidi ya kuwa sanaa ya vina, ushairi una ufasaha wa maneno machache au muhtasari. Anaeleza kuwa, wimbo ni shairi ndogo, shairi ni wimbo mkubwa na utenzi ni upeo wa ushairi. Kina ni mlingano wa sauti za herufi. Kwa maneno mengine huitwa mizani ya sauti na ufasaha ni uzuri wa lugha. Mawazo, maono na fikira za ndani zinapoelezwa kwa muhtasari wa ushairi huvuta moyo kwa namna ya ajabu.

Kutokana na maelezo haya inadhihirika kuwa, Robert anachukulia ushairi kuwa sanaa ya lugha ambamo kuna vina au mlingano wa sauti za herufi, lugha tamu na fupi na kwamba sanaa hiyo inapobeba mawazo, maono na fikra nzito huufanya moyo uathirike vikubwa. Ni wazi kuwa, fafanuzi za Robert na Mnyampala zinaunganisha maana na dhima ya ushairi.

Abdalla (1973) anaeleza kuwa, utungo ufaao kupewa jina la ushairi si utungo wowote tu bali ni utungo ambao katika kila ubeti wake kuna ulinganifu wa vina vitukufu vilivyopangwa kimoja baada ya chenziye; wenye vipande vilivyo na ulinganifu wa mizani zisizopungufu wala zilizozidi; na vipande hivyo viwe vimetandwa na maneno ya mkato maalumu na yenye lugha nyofu, tamu na laini. Lugha ambayo ni tetelezi kwa ulimi wa kuitamka. Lugha ambayo ina uzito wa fikira, tamu kwa mdomo wa kuisema, tumbuizi kwa masikio ya kuisikia na yenye kuathiri moyo uliokusudiwa na kama ilivyokusudiwa. Maelezo haya yanasisitiza umuhimu wa vina, vipande na mizani katika

shairi. Pia, shairi lazima liwe na lugha mwafaka inayowasilisha ujumbe uliokusudiwa. Abdalla anatia mkazo mkubwa katika fani au sanaa yenyewe.

Abedi (1954:1) anaeleza kuwa, shairi au utenzi ni wimbo. Hivyo, kama shairi haliimbiki halina maana. Anaendelea kueleza kwamba, ingefaa asiyeweza kutunga mashairi sawasawa aeleze fikra zake kwa maelezo ya desturi kuliko kujitia ndani ya mkorogano wa maneno yasiyoimbika. Abedi anaeleza kuwa, jambo muhimu la kukumbuka katika utungaji ni kuwa, mawazo yazue vina, sio vina kuzua mawazo. Mtungaji hodari anao uwezo wa kuzua vina vizuri vinavyochukuzana na habari anayoieleza kwa urahisi, hata shairi lake linakuwa halina taabu, halipindipindi, nalo linakuwa kama ndiyo asili yake. Kwa hivyo, anadhihirisha umuhimu wa vina katika shairi.

Njogu na Chimerah (1999:87), wanafafanua ushairi kuwa ni sanaa ya lugha inayoeleza jambo au wazo kwa njia ya mkato na kwa namna inayoteka hisia za msomaji au msikilizaji. Maneno ya shairi huteuliwa kimakusudi na kimahsusi ili yalete taswira maalum akilini mwa msomaji au msikilizaji. Maneno hayo pia hupangwa ili yatoe mdundo fulani shairi linapoimbwa, kusemwa, kughaniwa au kusomwa. Wanaelezea uteuzi wa lugha mwafaka inayobeba mawazo ya mshairi. Aidha, wanaelezea mdundo wa shairi unaotokana na mpangilio wa maneno ambao hutokana na urari wa vina na mizani.

Kutokana na fafanuzi za washairi kama Abdilatif Abdalla, Mathias Mnyampala na Shaaban Robert inadhihirika kuwa, mawazo yao kuhusu maana ya ushairi yanafanana. Wote wanasisitiza kuwa, sanaa na maudhui ni vitu muhimu katika ushairi wa Kiswahili. Mawazo mazito na hisia za ndani wanazozizungumzia haziwezi kuitwa ushairi lakini zinahitaji kuelezewa kwa sanaa maalum yenye vina, mizani, maneno ya mkato na lugha

ya kunata yenye mpangilio unaokubalika. Kipengele cha lugha kinatiliwa mkazo na washairi hao japo kwa mitazamo tofauti. Robert anasisitiza kuwa, shairi nzuri halina budi kuwa na ufasaha wa lugha. Mnyampala anaeleza kuwa, shairi lazima litumie maneno ya mkato na lugha nzito yenye kunata. Abdilatif anaeleza kuwa, shairi lafaa litumie maneno ya mkato maalum na yenye lugha nyofu, tamu na laini. Kwa hivyo, wanamapokeo wanaeleza kwamba, lugha ya ushairi haina budi iwe ya mkato na ya ufasaha. Hivyo, ushairi ni aina ya utungo wenye sura tofauti na tungo zingine.

Mtazamo wa washairi wa Kiswahili wa jadi kuhusu maana ya ushairi ni kuwa, ushairi ni wimbo au utungo, una maneno ya hekima, lugha nzito na ya mkato, una urari wa vina na mizani na unabeba hisia yaani unaburudisha. Kwa maoni ya Mulokozi (2008: 73-74), wataalamu hawa wa ushairi wa Kiswahili hawakufafanua maana ya dhana za "lugha ya mkato" na "lugha nzito". Hata hivyo, inaelekea kuwa walikusudia lugha inayotumia maneno machache lakini yenye kubeba maana pana. Hivyo, huenda labda walikusudia lugha ya picha yenye kusheheni sitiari, ishara, udokezi na tamathali nyingine za usemi. Isitoshe, Mulokozi anaongeza kuwa, wananadharia wa jadi wanabainisha kwamba, shairi hujengwa na mbinu zifuatazo: maneno ya hekima, kiini (dhamira), lugha ya mkato, nzito, teule, hisia (kuvuta moyo), urari (wa vina, mizani, sauti na kadhalika), utoshelezo, muwala, umbo na muundo.

4.2 Kanuni za Utunzi wa Mashairi: Mtazamo wa Amri Abedi

Abedi alitoa mchango mkubwa katika kuifafanua na kuijenga Nadharia ya Kijadi ya ushairi wa Kiswahili. Kwa mujibu wa Mulokozi, mchango wake ulikuwa katika mambo mawili. Kwanza, aliainisha sifa muhimu za tungo za Kiswahili kama vile vina, mizani, kituo na kutosheleza. Kwa hivyo, alimwelekeza mwanagenzi namna ya kutunga mashairi. Pili, aliainisha aina na miundo ya utungo kama vile mashairi ya mishororo

minne katika kila ubeti na mizani kumi na sita kwa kila mshororo (Mulokozi, 2008: 79). Abedi aliyataja mashairi yasiyo na vina yanayoitwa guni ingawa hakuyashughulikia kwa kuwa si maarufu (Abedi, 1954: 18).

Washairi wa jadi wanasisitiza kuwa, urari wa vina na mizani ni roho ya ushairi wa Kiswahili. Hata hivyo, Senkoro anaeleza kuwa, vipengele vya vina na mizani haviwezi kuwa ndio uhai wa kazi yoyote ya sanaa kwani uhai hutokana na uwiano mzuri baina ya fani na maudhui (Senkoro, 1988: 12).

Mohamed (1984: v), anafafanua ushairi kama chombo mwafaka kinachomwezesha mwandishi kufumbata upana na urefu wa maisha katika maneno mateule, machache yaliyofinyangwa kisanaa. Kiwango cha kisanaa na kimaudhui cha ushairi hakikui wala hakibadiliki kutokana na dhana ya kuchukulia tu kuwa sifa kuu za ushairi wa Kiswahili ni vina na mizani, muwala na urari, kibwagizo na beti hasa zile zenye mistari minne (yaani tarbia). Ushairi hunasibika na mpangilio adimu wa maneno, midundo, teuzi za tamathali na ujenzi wa picha na ufupisho kwa matumizi ya taswira na picha: ufupisho wa wazo, dhana au jambo pana na refu katika ufinyu wa maneno yanayonata sanaa. Isitoshe, Mohamed anaeleza kuwa, ushairi si vina na mizani na wala si uhuru tu. Ni uhuru wa busara unaoshikana na hisia na ufundi wa utunzi. Lakini hii si kusema kwamba, fani na maudhui ni vitu vyenye kutengana. Hivyo, Mohamed anaoanisha fani na maudhui katika shairi (Mohamed, 2002: ix).

Kwa upande mwingine, Mazrui anaeleza kuwa, maudhui ya mashairi ni muhimu zaidi kuliko umbo lake kwani ndiyo kiini cha ushairi. Hata hivyo, umbo la mashairi daima litakuwa na umuhimu mkubwa katika kuwasilisha maudhui. Kwa hivyo, jambo linalofaa si kulitweza umbo bali ni kujenga ndoa iliyokamilika baina ya umbo na

maudhui. Anaeleza kuwa, mshairi wa Kiswahili aliyefaulu hapingwi na kanuni za arudhi katika kujenga maudhui yake. Pia, anaeleza kuwa, watu wengi ambao hawaelewi kazi ya arudhi katika ushairi ndiposa wanafikiria arudhi yenyewe kuwa ndiyo ushairi (Mazrui, 1988: xii).

Mazrui anapendekeza washairi wawe na msimamo kuhusu ushairi kwa jumla na siyo kuhusu arudhi peke yake. Anaongeza kwamba, washairi wa jadi wanachukulia kuwa, wanamabadiliko wana muundo 'mpya' katika utunzi wa mashairi kwa sababu hawajazimudu vyema mbinu za ushairi. Hivyo, wanashindwa kutunga mashairi kwa mujibu wa mbinu hizo. Hata hivyo, wanamabadiliko wanatumia lugha, jazanda na taswira katika kiwango cha juu katika utunzi wa mashairi (Mazrui, 1988: xiii).

Shariff anabainisha umuhimu wa maudhui kwa kushadidia wazo la Abedi (1954) kuwa, maudhui hutawala fani. Anaeleza kwamba, waliotangulia kutunga ushairi walitunga bila ya kalamu na karatasi na walikuwa na sababu na maudhui maalum yaliyowapelekea kutunga. Mara nyingi maudhui yalisababishwa na matokeo maalum yaliyofungamana na maisha ya watu. Ingawa walitunga kwa vina na mizani sawasawa, yaliyokuwa muhimu pale ni yale waliyonena (Shariff, 1988: 77-78). Pia, anaongeza kuwa, mtindo wa uumbaji wa 'sanaa' kwa madhumuni ya sanaa yenyewe bila ya kuwa na sababu iliyooana na maisha ya watu ni jambo geni kwa Waswahili kwani ni mtindo wa Kizungu (Shariff, 1988: 85).

Njogu na Chimerah wanaongeza kuwa, ushairi ni kongamano la fani, maudhui na muktadha wa kijamii. Mshairi huanza na wazo lakini inamlazimu alitafutie fani wazo hilo ili kulikuza na kulieleza. Kwa hivyo, kwa namna fulani, fani inabeba maudhui (mawazo). Lakini fani huathiri maudhui katika maingiliano yao. Vipengele vya fani ni

lugha, muundo wahusika na mtindo. Pia, wanaendelea kueleza kuwa, shairi halina budi kuzingatia fani na maudhui kwa sababu fani imo ndani ya maudhui na maudhui yamo ndani ya fani. Vitu hivi viwili vinaingiliana na kutegemeana ili kutoa mchango katika ukuzaji wa kazi ya sanaa. Maingiliano hayo ndiyo yanayoipa kazi ya fasihi nguvu. Kwa hivyo, muhimu si kuwa na vina au kutokuwa navyo, muhimu ni ujumi wa kazi nzima (Njogu na Chimerah, 1999: 124).

Kezilahabi anaeleza kuwa, hakuna sheria za kutunga mashairi. Kila mshairi ana njia yake ya kutunga mashairi; ana njia yake ya kutoa mawazo yake ya kishairi. Zile ambazo wataalamu wanaita 'sheria' ni yale mambo yanayofanana katika mashairi fulani kwa wakati fulani lakini si sheria (Kezilahabi, 1977: 60). Kezilahabi anaongeza kuwa, kuna washairi wa Kiswahili na wahakiki wanafikiria kuwa umbo la ushairi wa Kiswahili ni la pekee duniani. Kwao vina, mizani na muwala ni sifa za ushairi wa Kiswahili. Lakini hizi ni sifa za jumla za ushairi hata wa Kiingereza, Kilatini, Kifaransa na kadhalika. Kwa hivyo, vina na mizani peke yake havifanyi shairi likawa la Kiswahili. Anaeleza kwamba, ushairi ni tukio, hali au wazo ambalo twaonyeshwa kutokana na upangaji mzuri wa maneno fasaha yenye mizani tena kwa ufupi ili kuonyesha ukweli fulani wa maisha (Kezilahabi, 1983: 147).

Kahigi na Mulokozi wameufasili ushairi kwa jumla kuwa, ni sanaa inayopambanuliwa kwa mpangilio maalumu wa maneno fasaha. Maneno hayo ni yenye muwala kwa lugha ya mkato, picha au sitiari au ishara, katika usemi maandishi au mahadhi ya wimbo ili kueleza wazo au mawazo, kufunza au kueleza tukio au hisi fulani kuhusu maisha au mazingira ya binadamu kwa njia inayogusa moyo. Wamevitaja vipengele vya ushairi kuwa ni mpangilio wa maneno, picha tamathali za usemi, takriri na ridhimu, hisia za kishairi, fani na maudhui. Wao wanaonekana kupuuza masharti ya vina na urari wa

mizani katika ushairi, japo wanakiri umuhimu wa mizani na kuimbika (Mulokozi na Kahigi, 1979: 22-25). Wanadai kuwa, mabadiliko ya umbo la shairi la Kiswahili yamefungamana na maendeleo na mabadiliko ya historia ya jamii zetu. Wanaongeza kuwa, fasihi ni sehemu ya utamaduni wa jamii. Utamaduni huo hufungamana na muundo maalum wa uchumi na hauna budi kubadilika wakati muundo huo unapabadilika. Kwa kuwa kila kitu daima kipo katika hali ya mabadiliko, kubadilika kwa ushairi wa Kiswahili si kitu kigeni (Kahigi na Mulokozi, 1979: 2).

Kutokana na maelezo ya washairi wa jadi na wanamabadiliko, washairi wengi wanaamini kuwa, lugha ya shairi lazima iwe ya mkato. Hii inamaanisha kuwa, lugha iweze kueleza mambo mengi kwa manane machache. Pia, washairi wanasisitiza kwamba, katika ushairi fani na maudhui ni vitu muhimu na kila kimoja kina wajibu wake. Hata hivyo, kuna wanaotilia mkazo maudhui na wengine fani. Wanasisitiza kuwa, kwa upande wa maudhui, mawazo, fikira nzito au hisi za ndani ni muhimu katika ushairi. Vilevile, kwa upande wa fani wanasisitiza kuwa, ili sanaa ya ushairi iweze kushamiri sharti lugha yake iwe na mpangilio fulani. Kuhusu mpangilio, baadhi ya washairi wanabainisha kwamba, vina na mizani ndivyo vinavyojenga umbo la shairi nao wanamabadiliko kama Kahigi na Mulokozi wanasisitiza kuwa, si vitu vya lazima katika ushairi (Massamba, 1983: 58).

Katika kipindi cha Urasmi Mpya kati ya mwaka 1945 hadi1970, watunzi wapya wa fasihi ya Kiswahili waliibuka na wakataka kuzivumbua upya kunga za utunzi na kuzitumia katika utunzi wao. Wataalamu walishikilia kuzieneza kunga za utunzi na wakaziandikia na kuzihifadhi katika maandishi yao. Walichukua jukumu la kueleza kunga za utunzi na kubainisha kaida za baadhi ya bahari za kishairi. Mifano ya malenga walioibuka katika kipindi hiki ni ifuatayo: Amri Abedi, Shaaban Robert, Mathias

Mnyampala na Akilimali Snow-White. Tangulizi za diwani za wataalamu hawa zilisheheni habari kuhusu dhima, kunga na arudhi za utunzi (Shitemi, 2010: 7).

Wafula na Njogu wanaongeza kuwa, matamshi na maandishi yanayopatikana katika tangulizi za tungo za wataalamu hao zinabainisha kuwa, walitaka kuufahamu ushairi wa Kiswahili kinadharia; maana na muundo wa ushairi wa Kiswahili (Wafula na Njogu, 2007: 50). Kandoro anaeleza kuwa, wataalamu wa tungo za maandishi ya Kiswahili wanakubaliana kwamba, mashairi ya Kiswahili yana kaida zake maalum, kanuni au sheria.Yanapofuata misingi yake hiyo vizuri huelekea na kusisimua msomaji na msikilizaji katika fahamu zake (Kandoro, 1983: 117). Kulingana na Kandoro, kufanya ushairi wa Kiswahili usiwe na vina na mizani ni kuipumbaza akili isifanye kazi ya kutafuta maneno ya kusadifisha mawazo na dhana itakiwayo. Katika ushairi kuna utajiri mkubwa sana wa msamiati wa Kiswahili. Kuzikataa kanuni na sheria zinazofungamana na ushairi wa Kiswahili ni kuua hamu ya utafiti wa matumizi ya msamiati wa Kiswahili (Kandoro, 1983: 118).

Misingi inazoweza kufikia hatua ya kutambulisha shairi la Kiswahili ni kama ifuatayo:

a) Vina
b) Mizani
c) Kiini
d) Urari
e) Muwala
f) Utoshelezaji

Ufafanuzi huu wa mashairi ya Kiswahili kufuatana na misingi hiyo, ndio unatudhihirishia kanuni za ushairi wa Kiswahili, ambazo hasa ndizo zinafanya shairi liwe ni pambo la lugha. Pia, kanuni hizo hufanya shairi kuwa hazina ya ufasili iliyolimbikiza maneno adhibu ya lugha. Aidha, yanafupisha maana, yanaipa haiba lugha katika matumizi yake na kufanya mashairi yawe ni chombo cha utamaduni wa lugha pamoja na kiburudisho cha fikira. Kibao anaeleza kuwa kanuni kubwa katika shairi la Kiswahili ni sita, kanuni ambazo ndizo nguzo hasa za ushairi. Kanuni hizo ni: mizani, vina, urari, muwala, utoshelezo na kuwa na maana. Pia, kuna mambo mengine ambayo yanapaswa kufuatwa ili shairi liwe zuri zaidi na la kuvutia nayo ni manne: kichwa cha shairi, kutorudia maneno, kunga na kutochanganya dhamira (Kibao, 1983: 102).

Khan katika utangulizi wa Diwani ya *Tujifunze Mashairi* yao Mzenga Musa na Hijazy Said anaeleza kuwa, mshairi wa Kiswahili sharti azijue kanuni za kutunga mashairi na azifahamu aina mbalimbali za tungo na mambo yanayosimuliwa na kila aina. Hawezi kuanzisha mtindo wake mwenyewe wa kutunga mashairi ikiwa haandami kanuni za ushairi zinazofuatwa na kutambuliwa. Akijaribu kuleta uzushi wake atakuwa amejitoa na kujiweka kando kutoka jamii ya Waswahili wanaomheshimu na kumuenzi kama malenga wao (Khan, 1977: 3). Kwa hivyo, Khan anasisitiza umuhimu wa kuzingatia kanuni za utunzi wa mashairi.

Ruo anaeleza kuwa, kanuni za ushairi wa Kiswahili zinazojulikana ni sita. Shairi lisipokuwa na vina, mizani, urari, muwala, kibwagizo na lisilokuwa na maana basi haliwezi kuitwa shairi. Mambo mengine yanayohitajika ili shairi liwe zuri na la kuvutia ni anwani ya shairi linaloandikwa, kutorudiarudia maneno, kunga kutochanganya, dhamira, beti na lugha safi isiyokuwa na matusi ndani yake. Ni kawaida ya maumbile kwamba kila jambo linalofanywa na jamii ya watu huamuliwa namna ya kulifanya.

Hivyo, utunzi wa mashairi una kanuni zake ambazo huzingatiwa na yeyote anayeamua kutunga mashairi (Ruo, 1989: 52). Kutokana na maelezo haya, kanuni za utunzi wa mashairi zinazodhihirika ni: vina, mizani, urari, muwala, kibwagizo, maana ya shairi na kadhalika.

Suala la kusisitiza arudhi katika utunzi wa mashairi ya Kiswahili linaambatana na kipindi cha Waraabu na mfumo wa kimwinyi. Kuja kwa Waraabu na hali ya ubwanyenye kulileta "maongozo mapya" katika umbo na hata maudhui ya ushairi wa Kiswahili (Senkoro, 1987: 21). Baadhi ya athari kutokana na Uarabu ni:

1) Mashairi andishi yalichipuka kwa kutumia hati za Kiarabu.

2) Kuhifadhiwa kwa mashairi kimaandishi.

3) Kutokea kwa mashairi marefu kama vile tenzi, takhmisa na hamziya.

4) Matumizi ya arudhi yalitiliwa maanani zaidi.

5) Maudhui yalikuwa zaidi ya kikasida na kuhusu dini ya Kiislamu.

Katika kipindi hiki pia, mfumo wa kimwinyi ulianza kujikita katika asasi zote za utamaduni wa wenyeji. Hivyo, dhamira za kidini za kuendeleza maslahi ya mamwinyi na mabwenyenye pamoja na itikadi yao ya kiutumwa zikatawala. Pia, matabaka yalizuka katika jamii kukawa na wangwana na watumwa. Hivyo, utamaduni wa Waswahili ukaathirika kwa kuwa fasihi ni sehemu ya utamaduni wa jamii. Kwa hivyo, fasihi ya wakati huo ilitawaliwa na falsafa zinazojaribu kuhalalisha msisitizo kuhusu mapambo (urari wa vina na mizani) kama ilivyo katika maisha yao ya kila siku (Senkoro, 1987).

Suala la asili ya vina na mizani katika ushairi wa Kiswahili ni muhimu. Katika fasihi ya Kiswahili tanzu za mwanzo zilikuwa nyimbo na mashairi (Senkoro, 1982: 67). Syambo na Mazrui wanaongeza kuwa, ushairi ulianza na nyimbo za kale ambazo zilikuwa zikiimbwa katika hafla mbalimbali kama vile harusini, unyagoni, mavunoni na pungwani (Syambo na Mazrui, 1992: 43).

Abedi anashadidia maelezo hayo kwa kueleza kuwa, kabla watu hawajajua kusoma na kuandika, mashairi ya Kiswahili yalikuwa yanatungwa na kuimbwa katika sherehe mbalimbali. Chanzo chake ni katika magoma ya kiasili. Nyimbo hizo katika kuimbwa kwake zilikuwa hazifuati utaratibu maalum (Abedi, 1964: vi). Nyimbo zilikuwa hazina vina na mizani kama kawaida ya ushairi wa leo unavyohitaji (Massamba, 1983: 61). Ni baadaye tu ambapo manju na malenga walipoanza utaratibu wa kutumia urari wa vina vya mwisho lakini bila ulinganifu wa vina vya kati na ulinganifu wa mizani. Syambo na Mazrui wanaongeza kuwa, katika kujaribu kuongeza ladha katika nyimbo zao, manju walianza kutumia mbinu za vina na baadaye mizani. Hapa ndipo elimu ya arudhi yaani elimu ya kanuni na kawaida za ushairi ilipoanza kuwa na nguvu (Syambo na Mazrui, 1992: 43).

Chiraghdin anaeleza kuwa, jambo ambalo limeutenga ushairi wa Kiswahili na tungo nyingine ni umbo lake. Shairi la Kiswahili likikosa vina na mizani na hapo haliitwi tena shairi (Chiraghdin 1977: 10). Mulokozi anashadidia maelezo hayo anaporejelea hotuba ya Mwinyihatibu Mohamed kuhusu utunzi bora wa ushairi wa Kiswahili anaeleza kuwa, ushairi una miko, misingi, mipaka na ustadi wake kama fani nyingine za ulimwengu. Katika jumla ya miko ni miko ya vina na mizani. Katika kuchagua vina, hapo ndipo utokeapo upambanuzi wa shairi bora na shairi shafuu. Kwani mbali na kusuluhisha vina, mshairi ana kazi ya uteuzi wa vina; aepuke kurudiarudia vina vivyo kwa vivyo. Hii ni

ila kama ambavyo ni ila kubwa kurudia maneno yayo kwa yayo pasi na sababu maalum ya kishairi. Pia, shairi ambalo lina upotofu wa mizani huifuja ladha ya sauti ya shairi (Mulokozi, 2008: 73). Chiraghdin anaongeza kuwa, wakati mwingine sanaa ya ushairi hudhoofishwa ikanyimwa kanuni na misingi yake. Inachukuliwa kwa wepesi kwamba haina masharti, ustadi au mipaka yake maalum. Pengine huonekana kuwa ukamilifu wa shairi ni mizani na vina tu. Ni kweli kuwa vina na mizani ni alama ya utungaji mwema lakini huitwa baadhi tu ya kanuni za utungaji (Chiraghdin, 1977: 27). Wataalamu hawa wanasisitiza kuwa shairi la Kiswahili sharti lizingatie kanuni za utunzi wa mashairi.

Abedi anaeleza kanuni zinazofungamana na utunzi wa mashairi Abedi (1954: 16). Baadhi ya mambo anayoyaeleza ni mizani, vina, kituo na kutosheleza ndiposa akasema:

> Nimezifichua kunga, kwa watakao kujua,
> Mashairi kuyatunga, na tenzi zinozindua,
> Kwa mpango nimepanga, huenda yataelea,
> Kunga nimezifichua, kwa watakao kutunga (Abedi 1954: 4).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, amezifichua kunga za utunzi wa mashairi kama mwongozo kwa watunzi wanagenzi.

4.2.1 Vina

Kulingana na Massamba, vina ni zile sauti za kati na za mwisho (au pengine za mwisho tu) zenye kufanana katika kila mstari wa ubeti (Massamba, 1983: 93). Katika mashairi ya tarbia aghalabu vina hufanana katika ile mistari mitatu ya mwanzo tu. Maoni ya Abedi ni kwamba, vina ni silabi za namna moja zinazotokea baada ya kila mizani kadha katika mstari wa shairi. Mashairi ya mistari minne ya mizani 16 huwa na vina katika silabi ya 8 (au ya 6 pengine) na ya 16 mistari mitatu ya kwanza. Kwa desturi vina vya silabi ya 16 huwa vya namna moja katika beti zote za shairi zima, na vina vya silabi ya

8, kwa desturi inayotumika sana, huwa tofauti ubeti kwa ubeti (Abedi, 1954: 18). Kandoro (1983: 120) anaeleza kuwa, katika sanaa ya mashairi ya Kiswahili, vina ni muhimu kuwepo: ni kitambulisho cha mwisho wa kila mstari. Sauti ile ile inabainisha sura ya mashairi katika mtindo wake.

Kulingana na Mnyampala shairi bora ni lile lililohitilafiana vina; vina vya kati na vya mwisho. Shairi kama hilo hupendeza masikio mghani anapoimba. Shairi la namna hiyo hupambwa uzuri wa haiba wakati kiitikio kinapobadilisha kina cha mwisho kuja katikati. Mshairi anapopambanisha vina kuwa namna moja cha katikati na cha mwisho, shairi hata liwe zuri namna gani huharibika hasa wakati wakutia kibwagizo au kiitikio (Mnyampala, 1965: viii).

4.2.2 Mizani

Kwa mujibu wa Abedi (1954: 16**),** mizani ni vipimo vinavyopima urefu wa kila mstari katika shairi. Kila silabi moja ni mizani moja. Mathalan, tamko la “mba” au “mbu” na maneno mengine kama hayo yanaweza kutoa silabi moja au mbili kwa kadiri yanavyotamkwa. Likiwa “m-ba” au “m-bu” hutoa silabi mbili na hivyo linakuwa na mizani mbili. Hata hivyo, katika neno “nyumba” silabi ni mbili yaani nyu-mba. Kwa hivyo, “mba” ni mizani moja. Abedi anafafanua kuwa, shairi zuri ni lile lenye mizani sawa katika kila mstari kwa mfano, katika mashairi ya mistari minne, kila mstari uwe na mizani 16 bila kupungua bila kuzidi: kila mstari ukiwa na sehemu mbili zenye mizani 8 kila sehemu (Abedi, 1954: 18). Massamba anaongezea kuwa, mizani ndiyo inayoleta urari wa mapigo, kwani kila mstari watakiwa uwe na mizani sawa na mistari mingine au wakati mwingine ule mstari wa mwisho uwe na nusu ya mizani ya mstari mmoja (Massamba, 1983: 94).

4.2.3 Kituo

Mstari wa mwisho katika kila ubeti huitwa kituo. Huo huwa ama ni kiini cha habari au kimalizio; nao hubadilika. Kina cha mwisho huja kati na cha kati huenda mwisho kwa mujibu wa desturi nzuri ya utungaji (Abedi 1954: 19). Hata hivyo, kituo kinaweza kuwa na kina kimoja tu cha ubeti au kiwe na vina vya namna ya peke yake au kifuate mpango ule ule wa vina vya mistari mingine. Abedi anaeleza kuwa, kuna desturi iliyoenea zaidi ya kukifanya kituo kuwa kiini cha habari na kukileta mwisho wa kila ubeti bila kubadilisha maneno yake. Katika hali hii, maelezo ya ubeti huwa yanatimia katika mistari mitatu ya kwanza na inakuwa ni maelezo zaidi juu ya kiini hicho. Kuna wakati mstari wa mwisho unakuwa si kiini cha habari, bali kimalizio tu ambacho hakielezi habari yoyote inayosimama peke yake ikaleta maana. Inapokuwa ni hivyo, mstari wa mwisho unaweza kubadilisha maneno bila kubadilisha vina (Abedi, 1954: 21).

Maoni haya yanafafanuliwa zaidi na King'ei na Kemoli wanapoeleza kuwa, maneno ya kituo yanaweza kuwa yale yale yanayokaririwa kutoka ubeti hadi ubeti (kibwagizo) au yanayobadilikabadilika kutoka ubeti mmoja hadi mwingine (kimalizio). Mara nyingi kituo hubeba maneno yaliyo na busara na kinaeleza kiini cha habari katika shairi. Umuhimu wa kibwagizo ni kwamba, hulisisitiza jambo linaloelezwa na mshairi. Hivyo, kibwagizo huweza kuwa kinaeleza dhamira muhimu ya shairi. Kwa upande mwingine, kimalizio hufanya kazi ya kukamilisha wazo lililo katika ubeti wa shairi (King'ei na Kemoli, 2001: 11).

4.2.4 Muwala

Muwala ni mtiririko na mpangilio wa mawazo au fikira kutoka ubeti hadi ubeti zinavyopokezana kwa kufuatiliza kisa au tukio katika shairi. Kulingana na Kibao, muwala ni ufuatanisho wa habari kutoka ubeti hadi ubeti (Kibao, 1983: 105). Mtiririko

wa habari sharti uwe na mantiki na ufungamano fulani. King'ei na Kemoli wanaongeza kuwa, muwala ni mtiririko wa mawazo na fani ulio na mantiki katika shairi (King'ei na Kemoli (2001: 13). Kwa upande mwingine, Kandoro anaeleza muwala kama utaratibu wa utungo (Kandoro, 1983: 120). Kwa hivyo, muwala ni dhana inayohusu ufungamano, mwambatano na mfuatano wenye mantiki wa hoja na beti za utungo na uhusiano au upatanifu wake na umbo la utungo huo.

4.2.5 Urari

Kandoro anafafanua urari kuwa ni usawa au ulinganifu (Kandoro 1983: 120). Karibu washairi wote wa jadi wanasisitiza kuwa, urari hasa wa mizani na vina ni kipengele muhimu na cha lazima cha shairi la Kiswahili (Mulokozi, 2008: 76). Chiraghdin anaeleza kuwa, raha inayopatikana katika shairi hutokea katika kulingamana kwa vina, mizani, lugha na hisi. Mlingamano wa vina na mizani si kwa kuhesabu silabi na herufi tu bali ni zaidi ya hapo. Anaongeza kuwa, baada ya vina vya kati na vya vituo na kuhesabu silabi kuna vina vya ndani kwa ndani na mizani ya mtiririko wa herufi zinazotoa sauti ya mlingano (Chiraghdin, 1977: 3). Kutokana na maelezo hayo, dhana ya "mlingano" anayoizungumzia Chiraghdin huenda ni ile ya urari. Hivyo, urari wa vipengele mbalimbali vya shairi kuanzia sauti, vipande, mpangilio wa maneno na kadhalika ni kanuni muhimu katika ushairi wa Kiswahili (Mulokozi, 2008: 76).

4.2.6 Utoshelezaji

Kulingana na Abedi kila ubeti wa shairi la Kiswahili unapaswa ujitosheleze kadiri iwezekanavyo yaani uwe na maana kamili na usingoje kutimizwa na ubeti mwingine unaofuata (Abedi, 1954: 19). Kibao anaunga mkono maelezo hayo kwamba, shairi la Kiswahili ni lile ambalo kila ubeti unajitosheleza kamili kwa habari au ujumbe unaompa msomaji ili afahamu unamweleza nini katika ubeti ule (Kibao, 1983: 105). Kwa hivyo,

utoshelezaji ni kukamilika kwa wazo ndani ya ubeti. Kandoro anachukulia utoshelezaji kuwa ni kufaa, kuridhisha au kutimu kwa hali ya shairi (Kandoro, 1983: 120).

Maoni ya wataalamu hawa kuhusu utoshelezaji yanaangazia kiwango cha ubeti. Hata hivyo, Mulokozi (2008) anaongeza kuwa, maoni ya Abedi (1954) yanaweza yakapanuliwa na kuhusisha mishororo. Kanuni ya utoshelezaji inafanya kazi hata kwenye ngazi ya mshororo. Sharti mshororo wa shairi ujitosheleze kwa maana.

4.2.7 Kiini

Kibao anaeleza kuwa, shairi la Kiswahili sio tu lifuate kanuni bali sharti liwe na maana au kiini (Kibao, 1983: 105). Kandoro anafafanua kiini kuwa ni undani au moyo wa shairi (Kandoro, 1983: 120). Mulokozi anafafanua zaidi kwa kueleza kuwa kiini ni wazo kuu au dhamira. Hiki ni kipengele muhimu kwani bila dhamira hakuna mawazo, mafunzo, hekima na kadhalika. Vitu hivyo hutokana na dhamira ya utungo unaohusika (Mulokozi (2008: 75). Katika kubainisha umuhimu wa mawazo ya shairi, Abedi anapendekeza kwamba, mawazo ya mtungaji yazue vina, siyo vina kuzua mawazo. Anajaribu kuonyesha uhusiano uliopo wa mawazo na namna yanavyosemwa; mbinu za kuwasilisha ujumbe. Hivyo, maudhui ya shairi yafaa yaitawale fani (Abedi, 1954: 1). Msimamo huu unashadidiwa na Kandoro anaeleza kuwa, mawazo ndiyo yanayomwangazia mwandishi kuelezea anachohitaji kueleza. Bahari hii ya mawazo ataendelea kuogelea hadi kikomo cha kazi za tungo zake. Ndani ya mawazo hayo ndimo mnamoweza kubuni hatua mbalimbali za awali za mashairi (Kandoro, 1983: 116). Kwa hivyo, ni wazi kwamba, mawazo ya shairi ndio yanayolipa shairi umbo lake.

Shariff anashadidia wazo la Abedi (1954: 1) kuwa, maudhui hutawala fani. Shariff anaeleza kwamba, wanaotunga mashairi huwa na maudhui maalum yanayowapelekea kutunga yanayosababishwa na matokeo maalum yaliyofungamana na maisha ya watu.

Ingawa wanatunga kwa vina na mizani sawasawa, yaliyokuwa muhimu pale ni yale waliyoyanena (Shariff, 1988: 77-78).

4.2.8 Lugha Mwafaka

Vipengele kadha vya lugha kama vile lugha ya mkato yaani lugha yenye ufasaha wa maneno machache, lugha nzito yaani lugha yenye uzito wa fikira, msamiati, lugha teule na lugha fasaha vinaweza kuangaliwa pamoja kwa kuwa vinahusiana. Vipengele hivyo vyote vinahusu matumizi ya lugha katika ushairi (Mulokozi, 2008: 74). Kulingana na Kandoro, utungo wa shairi wenye heba ni ule ambao umbo lake limejengwa katika lugha yenye ufasaha kutokana na utajiri wa maneno anayoyajua mtunzi. Mtunzi asiyejua mbinu za lugha na msamiati, maneno ya beti za msamiati wake huwa hayanogi. Kandoro anasisitiza kuwa mtunzi sharti awe na lugha yenye ufasaha ili shairi lake lipendeze (Kandoro, 1983: 115).

Katika kufafanua maana ya shairi, Robert anaeleza kuwa ushairi una ufasaha wa maneno machache au muhtasari. Hivyo, mtunzi wa shairi sharti awe na ufasaha wa lugha (Robert, 1958: 37). Kwa upande mwingine, Abdalla (1973) anasisitiza kuwa, shairi sharti liwe na maneno ya mkato, maalum na yenye lugha nyofu, tamu na laini. Lugha ambayo ni tetelezi kwa ulimi wa kuitamka. Lugha ambayo ina uzito wa fikira, tamu kwa mdomo wa kuisema, tumbuizi kwa masikio ya kuisikia na yenye kuathiri moyo uliokusudiwa na kama ulivyokusudiwa.

Maelezo haya yanadhihirisha kuwa, mtunzi wa shairi anahitaji kuwa na msamiati wa kutosha ili aweze kuteua maneno yanayofaa kuwasilishia mawazo yake. Msamiati wa kutosha unamwezesha mtunzi kutorudiarudia maneno hayo hayo, jambo ambalo hupunguza ladha ya shairi na kumfanya msomaji asipate hamu ya kulisoma tena. Kulingana na (Kibao 1983: 99), anayetaka kujifunza ushairi ni lazima awe na msamiati

wa kutosha kwani akiwa na lugha ya kutosha ataweza kuichezea atakavyo, akinyambua maneno na kuyaweka mahala mnamofaa bila ya kupoteza dhamira ya shairi. Abedi anasisitiza umuhimu wa kujua lugha anaposema:

> Kiswahili lugha nzuri, na tamu kuitumia,
> Kuitungia shairi, kwanza shuti kuijua,
> Lugha hii ya fahari, nayo lugha kubwa pia,
> Kunga nimezifichua, kwa watakao kutunga (Abedi 1954: 4).

Katika ubeti huu, mshairi anabainisha kuwa, ujuzi wa lugha ya Kiswahili ni lazima ikiwa mtu anataka kuitungia shairi.

Kulingana na Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, lugha hutumiwa na watu kulingana na mahitaji ya kijamii au "soko" yaani hadhira inayokusudiwa. Kwa hivyo, ujuzi wa lugha ya Kiswahili ulihitajika ili kuweza kuitumia kutungia mashairi yaliyoshughulikia masuala mbalimbali yaliyofaidi jamii. Lugha ya Kiswahili ilienea kupitia ushairi katika kipindi cha ukoloni.

4.3 Utunzi wa Mashairi ya Arudhi

Robert (1969) anaeleza jinsi ya kutunga shairi la arudhi katika shairi "Ushairi." Katika ubeti wa kwanza mshairi anasema:

> Ushairi ni sudi, mwenye nao ni kipawa,
> Kipawa cha ustadi, hedaya watu kupewa,
> Waimbao wana jadi, ya kusema kwa maua,
> Maneno huyachagua, yanayokidhi kusudi (Robert, 1969: 2).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, mtunzi wa shairi ana kipawa cha ustadi na yeye ni zawadi kwa watu. Washairi wa jadi wanatunga kwa njia inayopendeza kwani huchagua maneno yanayokidhi kusudi lao. Katika ubeti wa pili mshairi anasema:

Huchagua na kupima, maneno wanayonena,
Mepesi mtu kusema, na kudhibiti maana,
Yanayoimbika vema, na sauti kulingana,
Hawayapendi sana, maneno ya kukingama (Robert, 1969: 2).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, washairi wa jadi huchagua na kupima maneno wanayonena ili wapate maana wanayolenga. Pia, washairi huweza kupata maneno yanayoimbika vyema kwa kuwa na sauti zinazolingana. Hawapendi kutumia sauti zinazokingama. Katika ubeti wa tatu anasema:

Japokuwa lina kina, neno la kukingama,
Huwa halifai sana, mashairini hukwama,
Kisha hupoteza maana, uzuri hata kima,
Shairi haliwi njema, lugha ikitatizana (Robert, 1969: 2).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, ingawa neno lina kina lakini linakingama, halifai katika shairi. Neno kama hilo hupoteza maana na uzuri wake. Hivyo, shairi halipendezi kwa sababu lugha yake inatatiza. Katika ubeti wa mwisho mshairi anasema:

Maneno yakisongana, maanaye huwa kiza,
Japo likiwa na kina, shairi linapooza,
Maneno yakikosana, hayafanyi mwangaza,
Shairi la kutatiza, halina faida sana (Robert, 1969: 2).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, maneno yakibanana maana yake haieleweki. Ijapokuwa maneno yana vina shairi huharibika. Maneno yasipoeleweka shairi halina maana. Shairi linalotatiza halina faida sana. Katika shairi hili, mshairi anadhihirisha umuhimu wa kuchagua maneno kwa makini ili kupata vina vinavyolingana. Shairi nzuri ni lile linaloimbika na linaloeleweka.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Ubidhaaishaji ya Lugha, lugha hutumika sio tu kama chombo cha mawasiliano lakini hubainisha uwezo fulani unaomfanya mtu aonyeshe umulisi wa lugha alionao. Ingawa mshairi analenga kuwasilisha maudhui yake, anastahili kufuata kanuni za utunzi wa mashairi ya arudhi jambo linalodhihirisha umilisi wake wa lugha. Hivyo, lugha ya Kiswahili ilienea kupitia mashairi.

Pia, katika shairi "Vileo" Robert (1969) anasema:

> Mtengeza *Mambo leo*, radhi niwie bwana,
> Nafasi ukiwa nayo, nipe ruhusa kunena,
> Ukiona mapoteo, shairi halina kina,
> Sahihisha kila tao, liimbike danadana (Robert, 1969: 62).

Katika ubeti huu, mshairi anamwomba radhi mhariri wa gazeti la *Mambo leo*. Angependa kumweleza kuwa akiona shairi ambalo halina vina alisahihishe katika utao ili liweze kuimbika vizuri. Vilevile, katika ubeti wa pili anasema:

> Tena litie vituo, liwe jepesi kunena,
> Lipendeze masikio, kwa sauti kulingana,
> Hata watu wasomao, wadhibiti na maana,
> Kama tembo kileo, nguvu hulevya sana (Robert, 1969: 62).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza mhariri wa gazeti la *Mambo leo* kuwa atie shairi vituo ili liwe jepesi kuneneka. Shairi litapendeza masikioni kwa sauti kulingana. Hata watu wanaolisoma watapata maana yake. Katika shairi hili, mshairi anadhihirisha umuhimu wa utunzi wa mashairi yenye vina vinavyolingana kwani shairi huimbika vizuri.

Kulingana na Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, lugha hutumiwa na watu kulingana na mahitaji ya hadhira inayokusudiwa. Hivyo, kwa kuwa watu hupenda mashairi

yanayoneneka kwa urahisi na yanayoimbika, mtunzi wa shairi anastahili kuzingatia urari wa vina. Ni kupitia mashairi ambapo lugha ya Kiswahili inaenea.

Aidha, katika shairi “Ikirari ya Mapenzi”, Robert (1968) anaelezea utunzi wa mashairi. Katika ubeti wa nne anasema:

> Utunzi na umalenga ni vitu vya taratibu,
> Ndani yake mna kunga na marudi na adabu,
> Hufunza watu kulenga na kusema na kujibu,
> Si kwamba mtu apinga kitu bila ya sababu (Robert, 1968: 80).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza utaratibu unaofaa kufuatwa katika utunzi wa mashairi. Kuna kunga na maadili yanayofuatwa. Kwa hivyo, watu hufunzwa jinsi ya kusema na kujibu washairi wengine. Hivyo, mshairi hawezi kupinga kila kitu bila sababu. Mshairi anabainisha umuhimu wa kufuata taratibu za utunzi wa mashairi. Hapa inaelekea kuwa anarejelea zile kanuni za utunzi wa mashairi. Pia, anawashauri washairi kuepukana na matusi wanapotunga mashairi.

Isitoshe, katika shairi “Barua”, Robert (1969) anamwambia somo yake Musa Rashid kwamba, amepata barua yake na akasoma yaliyomo akayaelewa. Robert anamsifu Musa kwa utunzi wake unaofuata sifa muhimu. Kwa hivyo, amelazimika kumtolea ungamo. Katika ubeti wa pili anasema:

> Nimependezwa na kimo, beti zilivyotimu,
> Tezi hata omo, zimeundwa kwa elimu,
> Na maana ndani imo, iletayo tabasamu,
> Kubwa katika midomo, kwa maneno maalum (Robert, 1969: 60).

Katika ubeti huu, mshairi anapendezwa na kimo na vile beti zimetimia kuanzia mwanzo hadi mwisho kwa sababu zimeundwa kwa ustadi. Tena, beti zimebeba maana

inayofurahisha kutokana na maneno maalumu. Mshairi anadhihirisha umuhimu wa utoshelezo wa ubeti. Zaidi ya hayo, katika ubeti wa tatu anasema:

> Umefikia kipimo, kwa watu wengi adimu,
> Bora hakina mashimo, na maneno si magumu,
> Usemapo kwa humo, ushairini haramu,
> Mimi nahesabu umo, wala hutoki mwalimu (Robert, 1969: 60).

Katika ubeti huu, mshairi anamwambia Musa kuwa amefikia kiwango cha washairi wachache mahiri. Ametunga shairi bora kwa sababu maneno si magumu. Anamwonya asije akajichukulia kuwa si mshairi. Katika shairi hili mshairi anamsifu Musa kwa kutunga beti zilizojitosheleza kimaana anaposema "beti zilivyotimu" na "maana ndani imo". Kwa hivyo, Musa amezingatia sifa muhimu ya ushairi wa arudhi yaani utoshelezaji. Pia, ametumia "maneno si magumu." Abedi (1954: 42) anapendekeza watunzi watumie lugha nyepesi kuyaeleza mambo ya kawaida. Jambo hili limezingatiwa na Musa Rashid. Isitoshe, katika ubeti wa saba mshairi anasema:

> Nilialikwa niwemo, juzi katika karamu,
> Nikakuta Harvey yumo, anaagwa na walimu,
> Nikasikia msemo, wa hotuba moja tamu,
> Iliyotia tetemo, kwa shairi maalum (Robert, 1960: 60).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, juzi alialikwa kwenye karamu moja ya walimu ya kumuaga Harvey. Alisikia hotuba tamu iliyotolewa kishairi.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Utegemezi, uteuzi na matumizi ya lugha katika jamii ndio hutambulisha jamii kwa kuihusisha na mazingira na ulimwengu kwa jumla. Hivyo, kwa kuwa mshairi alitumia lugha ya Kiswahili kutolea hotuba ya kishairi iliyozingatia kanuni za utunzi wa mashairi, alisitisha utegemezi wa lugha za kikoloni katika

mawasiliano na akaitukuza lugha ya Kiswahili. Pia, mshairi alieneza Kiswahili kupitia ushairi.

Mnyampala (1965) amependekeza utunzi wa mashairi ya arudhi. Katika shairi "Tungeni Mtiririko", anawaeleza washairi watunge mashairi ya mtiririko na "silabi kuhesabu". Hapa anamaanisha kuwa wazingatie urari wa vina na mizani. Anawaeleza watunzi wasiwe na hasira na vituko lakini wafikirie usanifu wa beti zao. Hata kama wanajibu swali wafikirie ujumbe katika beti hizo. Katika ubeti wa tano mshairi anasema:

> Kisa kilichokusibu, kipate nacho mwandiko,
> Maanaye na sababu, mwanzo ni chokochoko,
> Ni kipawa cha Wahabu, usipate masumbuko,
> Tungeni mtiririko, na silabi kuhasibu (Mnyampala, 1965: 6).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, kisa kilichompata mtunzi kinaweza kutungiwa shairi. Ingawa ni ugomvi au matatizo afikirie maana na sababu ya utunzi wake. Asipate masumbuko kwani ni kipawa cha Mungu. Mshairi anabainisha umuhimu wa maana ya shairi yaani mtunzi afikirie ujumbe wa shairi lake. Katika ubeti wa saba mshairi anasema:

> Tungozo ziwe dhahabu, zambatane na mwitiko,
> Wengi wasitaajabu, jinsi ya mtiririko,
> Liimbwapo ni taibu, lipendeze walioko,
> Tungeni mtiririko, na silabi kuhasibu (Mnyampala, 1965: 6).

Katika ubeti huu, mshairi anawashauri watunzi watunge mashairi ya thamani yanayoambatana na habari wanayokusudia. Watu wengi watashangazwa na hali ya mtiririko. Pia, watu watafurahia kwa kuwa shairi litaimbika vizuri. Hapa mshairi

anadhihirisha umuhimu wa shairi kuimbika anaposema “liimbwapo ni taibu” yaani linapoimbwa ni nzuri. Aidha, katika ubeti wa kumi mshairi anasema:

> Beti kumi kwa hesabu, hazina mchanganyiko,
> Nimemuweka Katibu, hapo kaka kitako,
> Kati “bu” imeratibu, mwisho “ko” imekuweko,
> Tungeni mtiririko, na silabi kuhasibu (Mnyampala, 1965: 6).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, ameweza kutunga beti kumi bila kuchanganya vina. Hata Katibu aliyeandikiwa ametulia. Mshairi ametumia urari wa vina vya kati na vya mwisho katika beti zote. Hivyo, anawahimiza watunzi watunge mashairi ya mtiririko yenye urari wa mizani. Katika ubeti huu, mshairi anadhihirisha umuhimu wa kutunga mashairi ya arudhi yenye urari wa vina kwa kutunga shairi la mtiririko.

Katika shairi “Dodoma Imeitika”, Mnyampala (1965) anawashukuru washairi wa Dodoma kwa kukubali kuungana na washairi wengine wa Unguja na Tanganyika. Anaeleza kuwa, ushirikiano ni muhimu kwani wataweza kufurahi na kupigana na adui pamoja. Anasisiza kuwa, utunzi si kujivuna bali ni kupendana pendo linaloleta baraka. Katika ubeti wa sita mshairi anasema:

> Hija Salehe Mwungwana, mshairi mtajika,
> Bai Mohamed Bwana, Dodoma yashangilika,
> Nilosahau majina, ni nyote kujumuika,
> Dodoma imeitika, mwaliko wa kuungana (Mnyampala, 1965: 61).

Katika ubeti huu, mshairi anawataja washairi kama Hija Salehe, Mwungwana na Bai Mohamed Bwana miongoni mwa wengine aliowasahau majina. Anafurahia kuwa washairi wameweza kuungana pamoja. Katika ubeti wa saba anasema:

Ofisi yatajazana, hata yakisomwa mwaka,

Yenye sanaa ya vina, tungo zenye kunyooka,

Mashairi twamimina, na beti kutiririka,

Dodoma imeitika, mwaliko wa kuungana (Mnyampala, 1965: 61).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, washairi wakiungana wataweza kujaza ofisi ya chama cha washairi kwa mashairi yatakayosomwa kwa muda mrefu au mwaka mzima. Mashairi yatakayotungwa yatazingatia vina na yanayopendeza. Mashairi yatakuwa mengi kwa sababu beti zitatiririshwa na washairi wa Dodoma ambao wamekubali kuungana. Mshairi anabainisha kuwa, mashairi yanayotarajiwa kutungwa ni ya arudhi ndio maana akasema “yenye sanaa ya vina” yaani yanayozingatia urari wa vina.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Utegemezi, jamii inayonuia kujikomboa kutokana na ukoloni haina budi kutumia lugha moja ya kuwaunganisha watu ili kuwa na umoja kwa lengo la kuleta ukombozi. Kwa hivyo, washairi wa Dodoma wanapoungana na kutunga mashairi kwa lugha ya Kiswahili wanasitisha utegemezi wa lugha za kikoloni na kukuza lugha ya Kiswahili ndiposa washairi wakahimizwa utunzi wa mashairi ya arudhi.

Isitoshe, katika shairi “Mzozo Wangu Patano”, Mnyampala (1965) anawashauri washairi kuwa wanafaa kupendana. Katika ubeti wa pili anasema:

Washairi hupatana, wakendesha mikutano,

Mikutano za maana, za kutengeza unono,

Unono tenzi kusana, vina vyenye mlingano,

Mzozo wangu patano, washairi hupendana (Mnyampala, 1965: 107).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kwamba, washairi hupatana na kuwa na mikutano ya maana ya kupanga mambo mazuri. Wanapanga jinsi watakavyotunga tenzi na mashairi yenye urari au mlingano wa vina. Hapa mshairi anawashauri watunge mashairi ya arudhi ndipo akasema kuwa, watunge mashairi yenye "vina vyenye mlingano." Aidha, katika ubeti wa sita mshairi anasema:

> Khalfani panga vina, ugomvi uwe mwagano,
> Gonga ujaze makana, ufanye suluhishano,
> Shikeni zenu supana, funga yenu mapigano,
> Mzozo wangu patano, washairi hupendana (Mnyampala, 1965: 107).

Katika ubeti huu, mshairi anamshauri Khalfani atunge mashairi yaani "apange vina" aachane na ugomvi. Gonga naye anaambiwa asuluhishe mambo ili waache mapigano. Mshairi anasisitiza kuwa, washairi hupendana kwa hivyo, mzozo unastahili uishe kwa mapatano. Katika ubeti huu, mshairi anawashauri washairi watunge mashairi ya arudhi kwa kumweleza Khalfani apange vina yaani atunge mashairi yanayozingatia urari wa vina. Isitoshe, katika ubeti wa kumi mshairi anasema:

> Namuomba Subuhana, alete afikiano,
> Tuache kununiana, tupatane kama ngano,
> Ndipo utunzi tanona, tuachapo utengano,
> Mzozo wangu patano, washairi hupendana (Mnyampala, 1965: 108).

Katika ubeti huu, mshairi anamwomba Mungu awasaidie washairi kuelewana na kuacha kununiana. Maoni yake ni kuwa, wakiacha utengano na kushirikiana, utunzi wa mashairi utazidi kuendelea.

Kulingana na Nadharia ya Utegemezi, jamii inayonuia kujikomboa kutokana na ukoloni haina budi kutumia lugha moja ya kuwaunganisha watu ili kuwa na umoja kwa lengo la

kuleta ukombozi. Mshairi anawahimiza washairi waungane na waendeleze utunzi wa mashairi kwa lugha ya Kiswahili. Anawaonya dhidi ya mapigano kwani kwa pamoja wangeweza kusitisha utegemezi wa lugha za kikoloni kwa kukuza Kiswahili kupitia mashairi.

> Katika utangulizi wa Diwani ya Abedi (1954), Abedi anasema amefichua kunga kwa wale wanaotaka kutunga mashairi. Anaeleza kwamba, tungo alizotunga ni kiasi tu cha anayojua kwa sababu yeye si nyakanga eti anajua kila kitu. Yale ambayo ameyaacha anaomba mabingwa wamsaidie. Ametunga mashairi ya tenzi kwa mpango ili utunzi ufahamike. Katika ubeti wa tatu mshairi anasema:
>
> Kiswahili lugha nzuri, na tamu kutumia,
> Kuitungia shairi, kwanza shuti kuijua,
> Lugha hii ya fahari, nayo lugha kubwa pia,
> Kunga nimezifichua, kwa watakao kutunga (Abedi, 1954: 4)

Katika ubeti huu, mshairi anasifu lugha ya Kiswahili kwa sababu ni tamu inapotumiwa katika utunzi wa mashairi lakini sharti mtunzi aifahamu vilivyo. Pia, lugha ya Kiswahili ni ya kifahari na imeenea sana. Katika ubeti wa nne mshairi anasema:

> Ni lugha yenye mizani, yenye vina vya kutua,
> Hii ni lugha ya shani, usiyejua tambua,
> Ole wako maskini, wa humu asoijua,
> Kunga nimezifichua, kwa watakao kutunga (Abedi, 1954: 4).

Katika ubeti huu, mshairi anasifu lugha ya Kiswahili kwa sababu ni lugha yenye mizani na vina vya kutua. Kwa wale ambao hawajui ni lugha ya ajabu. Ametumia Kiswahili kwa kutunga mashairi na tenzi kama vielelezo bora kwa wanaotaka kujua utunzi wa mashairi ya arudhi. Ameelezea mambo mazito na mepesi katika mashairi hayo. Shairi

hili linatanguliza mashairi yaliyotungwa na Abedi (1954) kama vielelezo vya mashairi yanayofuata arudhi.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, luhga hutumiwa na watu kulingana na mahitaji ya hadhira inayokusudiwa. Washairi walitumia ushairi wa Kiswahili kuwahimiza Watanganyika watunge mashairi ya arudhi na kuendeleza utunzi. Hii ilikuwa mbinu mojawapo ya kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili. Kupitia njia hii, washairi walichangia katika kusitisha utegemezi wa lugha za kikoloni katika kipindi cha ukoloni nchini Tanganyika.

4.4 Hitimisho

Sura hii imechunguza kanuni za utunzi wa mashairi na jinsi zilivyochochea mabadiliko ya maudhui ya ushairi wa Kiswahili nchini Tanzania kati ya mwaka 1930 hadi 1960. Uchunguzi umebainisha kuwa, washairi wa jadi walizingatia kanuni za utunzi wa mashairi kama alivyopendekeza Abedi (1954) katika tungo zao. Katika dibaji za diwani zao, walitoa fafanuzi mbalimbali za maana ya ushairi. Hata hivyo, walisisitiza kuwa, shairi la Kiswahili linastahili kuzingatia kanuni zifuatazo: vina, mizani, kituo, muwala, urari, kutosheleza, kiini na lugha mwafaka. Watunzi wa mashairi walihimiza na kuwashauri watunzi wengine wafuate arudhi katika utunzi wa mashairi. Hivyo, mashairi yaliyotungwa yalibeba maudhui ya kuhimiza utunzi wa mashairi ya arudhi.

Sura ifuatayo ilifanya utathmini wa jinsi harakati za upiganiaji uhuru zilivyochochea mabadiliko ya kimaudhui ya ushairi wa Kiswahili nchini Tanganyika kati ya mwaka 1930 hadi 1960.

SURA YA TANO

HARAKATI ZA UPIGANIAJI UHURU NA MAUDHUI YA USHAIRI

5.0 Utangulizi

Sura iliyotangulia ilichunguza jinsi kanuni za utunzi wa mashairi zilivyochochea mabadiliko ya maudhui katika ushairi wa Kiswahili. Uchunguzi ulibainisha kuwa maoni ya washairi wa jadi au wanamapokeo kuhusu maana ya ushairi yanashabihiana. Wanasisitiza kuwa, mashairi yafaa yazingatie kanuni za utunzi wa mashairi kama alivyopendekeza Abedi (1954). Mashairi waliyoyatunga yalibeba maudhui ya kuwashauri watunzi wapya kufuata kanuni za utunzi katika mashairi yao. Baadhi ya kanuni hizo ni shairi kuwa na vina, mizani, kituo, urari, utoshelezaji, kiini na lugha mwafaka.

Sura hii ililenga kuchunguza jinsi harakati za upiganiaji uhuru zilivyochochea mabadiliko ya kimaudhui katika ushairi wa Kiswahili nchini Tanganyika kati ya mwaka wa 1930 hadi 1960.

5.1 Vyama vya Kisiasa

Waingereza walipokuwa wanatawala nchi ya Tanganyika kuanzia mwaka wa 1918, Waafrika walilalamikia ubaguzi, mishahara duni, hali duni za maisha na kazi za lazima kutoka kwa watawala. Waafrika waliunda Chama cha Wafanyakazi wa Serikali (TTACSA) mjini Tanga katika mwaka wa 1922. Kwa mujibu wa Chachage (2003), chama hiki kilidai malipo bora ya wafanyakazi, bei bora za bidhaa za kilimo na maendeleo katika kilimo. Hata katika mwaka wa 1924 Chama cha Wakulima cha Kilimanjaro yaani (KNPA) kilibuniwa. Katika mwaka wa 1929 chama cha TTACSA kilianzisha chama cha kisiasa cha TAA. Chama cha TAA kililenga kutafuta ajira bora kwa Waafrika na kuunganisha mashirika yote ya kupigania uwakilishi wa Waafrika katika Legco (Legislative Council). Katika mwaka wa 1945 Julius Nyerere alijiunga na

TAA na katika mwaka wa 1953 alichaguliwa kuwa rais wa chama. Chama cha TAA kililenga kutafuta uhuru wa kujitawala. Katika tarehe saba, mwezi wa Julai, mwaka wa 1954 kwenye mkutano uliokuwa Dar es Salaam, mabadiliko makubwa yalifanyiwa chama cha TAA na jina lake likabadilishwa na kuwa Tanganyika African National Union -TANU (Were na Wilson, 1968: 257). Nyerere alichaguliwa kuwa rais wa chama cha TANU na Oscar Kambona akawa mhazili mkuu. Walowezi walianzisha chama cha UTP katika mwaka wa 1958 ili kupinga juhudi za TANU lakini hawakufanikiwa (Chachage, 2003).

5.1.1 Matumizi ya Kiswahili Katika Vyama vya Kisiasa

Katika Tanganyika shughuli za siasa zilipoanza kupamba moto, zilianza kwa kutumia lugha ya Kiswahili kama lugha ya mawasiliano (Massamba, Kihore na Hokororo, 1999: 22). Kiswahili kilikuwa silaha kubwa na muhimu kwani kilihusishwa na umoja, uhuru na uzalendo (Massamba, 1995: 5). Chama cha siasa kilichotangulia TANU yaani TAA kilikuwa na katiba yake iliyoandikwa kwa Kiswahili. Zaidi ya hayo, wakati chama hicho kilipokuwa na mkutano wake huko Unguja katika mwaka wa 1947, mwenyekiti wake alitoa hotuba yake kwa Kiingereza. Wajumbe wa mkutano huo walisisitiza kwamba lazima hotuba isomwe kwa Kiswahili. Kwa hivyo, Shaaban Robert alichukua madaraka na kuifasiri na toka hapo kukakatwa shauri kuwa mikutano ya TAA yote ingeendeshwa kwa Kiswahili tu (Chiraghdin na Mnyampala, 1977: 70).

Katika mwaka wa 1954 chama cha TANU kilichopigania uhuru kutoka kwa utawala wa Waingereza, kilitumia Kiswahili kama ugwe wa kuwaunganisha watu wa makabila tofauti (Rubagumya, 1990). Whiteley anaeleza kuwa, umuhimu wa Kiswahili kwa chama cha TANU ulidhihirishwa na Nyerere. Nyerere aliwahi kusema kuwa katika safari zake nyingi nchini ni mara mbili pekee aliwahi kutumia wakalimani (Whiteley,

1969: 65). Mawasiliano kati ya maofisa wa chama cha TANU na watu wa mashinani hasa wale ambao walizungumza lugha za kienyeji yalitumia Kiswahili (Bienen, 1970: 43). Ujuzi wa Kiswahili ulikuwa jambo la lazima kwa wafanyakazi wa chama cha TANU ambao waliweza kufanya kazi sehemu mbalimbali kote nchini. Nyerere pamoja na wanachama wenzake walisafiri nchi nzima wakitumia Kiswahili kuwashawishi wananchi wajiunge na harakati za kupigania uhuru. Matawi ya chama cha TANU yalifunguliwa kwanza katika maeneo ambayo wenyeji waliweza kuzungumza Kiswahili. Mikutano yote ya siasa ikawa inaendeshwa kwa Kiswahili. Kulipoanzishwa Chama cha Vijana wa TANU yaani TANU Youth League, matumizi ya Kiswahili yakapata sura nyingine kwani lugha ya Kiswahili ilikuwa ndiyo alama ya umoja, uzalendo, utanganyika na uhuru. Hata wito wa chama ukawa katika Kiswahili: Uhuru na Umoja! Clarke anaongeza kuwa, afisi za chama cha TANU zilianzishwa karibu katika kila kijiji na salamu ikawa ni "Uhuru na Kazi" (Clarke, 1960: 137). Lugha ya Kiswahili ilikuwa kama bidhaa muhimu katika soko kwa sababu ya umuhimu wake katika shughuli za kisiasa.

Aidha, chama cha TANU kiliinua elimu hasa ya watu wazima kwa kuanzisha shule za chama ili kueneza matumizi ya Kiswahili. Kiswahili kilizidi kupata nguvu kwani mwaka wa 1955 kilianza kutumiwa bungeni na ilipofika mwaka wa 1960 chama cha TANU kiliazimia kuwa Kiswahili kiwe lugha ya taifa. Tokea hapo juhudi zikawa zinafanywa ili Kiswahili kitumike katika shughuli za serikali (Chiraghdin na Mnyampala, 1977: 70)

Kulingana na Massamba (1995: 5), kama kungekuwa hakuna lugha ya mawasiliano kama Kiswahili, Mwalimu Nyerere na viongozi wenzake wa chama cha TANU wasingefanikiwa kwa haraka katika kuwahamasisha wananchi dhidi ya ukoloni.

Vilevile, ingekuwa taabu kidogo kwa Nyerere kukubalika pwani au kwingineko kusikokuwa kwao, kwani asingeweza kuongea Kiingereza au Kizanaki akaeleweka na umma. Nyerere alifanikiwa kwani aliwaunganisha viongozi wote na kuwafunza thamani na kumaliza mielekeo ya kikabila kwa kuzingatia Kiswahili kama lugha ya taifa (King'ei, 2010: 150). Maoni haya yaungwa mkono na Whiteley anapoeleza kwamba, Nyerere hakuweza kupigania uhuru kwa kujua Kiingereza lakini kwa sababu aliwakilisha umma wa Tanganyika kutokana na uwezo wake wa kuzungumza Kiswahili katika mawasiliano ya kitaifa (Whiteley, 1969: 65).

Kutokana na maelezo hayo ni wazi kuwa lugha ya Kiswahili ilikuwa chombo muhimu cha kuwaunganisha Watanganyika kisiasa katika harakati za kupigania uhuru. Kwa mujibu wa Nadharia ya Utegemezi, jamii inayonuia kujikomboa kutokana na ukoloni haina budi kutumia lugha moja ya kuwaunganisha watu ili kuwa na umoja kwa lengo la kuleta ukombozi. Kwa hivyo, lugha ya Kiswahili ilitumika kama chombo cha mawasiliano miongoni mwa Watanganyika ndiposa ikapata kuenea kote nchini.

Katika kipindi hiki cha kupigania uhuru, magazeti ya Kiswahili yalichapishwa kwa mfano, gazeti la chama cha TTACSA lililoitwa *Kwetu* na lilitoka baina ya mwaka wa 1937 na 1952 (Chiraghdin na Mnyampala, 1977: 9). Uchapishaji wa mashairi katika magazeti lilikuwa jambo la kawaida (Mbaabu, 1985: 61). Hivyo, washairi walitekeleza jukumu la kuhamasisha na kuzindua watu ili wapate nguvu mpya za mapambano dhidi ya udhalimu wa mkoloni.

5.2 Ushairi kama Chombo cha Kisiasa

Uhusiano kati ya ushairi wa Kiswahili na siasa ulianza zamani. Uhusiano huo unaweza kuangaliwa kwa pande mbili. Kwanza, kuna wanasiasa ambao walikuwa washairi kwa mfano, Fumo Liyongo, Zahid Mngumi, Muhammed bin Shee Mataka pamoja na

washairi wa kisasa kama Amri Abedi, Saadan Kandoro, Abdilatif Abdalla na Julius Nyerere. Pili, kuna washairi waliotunga mashairi ya kisiasa lakini hawakuwa wanasiasa. Kwa mfano, Muyaka bin Haji, Ali Koti, Shaaban Robert na Mathias Mnyampala (Mulokozi na Sengo, 1995: 94).

Kulingana na King'ei na Kemoli katika enzi za ukoloni na hata baada ya uhuru, ushairi ulitumiwa kama chombo cha kushajiisha wanajamii kuungana dhidi ya tawala za dhuluma. Washairi walitunga tungo za kishairi na wakati mwingine kwa kufumba kwa madhumuni ya kuwapinga dhulumati (King'ei na Kemoli (2001: 6). Pia, Mbaabu anashadidia maelezo hayo kwa kuongeza kuwa, uchapishaji wa mashairi katika magazeti ulikuwa jambo la kawaida wakati wa ukoloni (Mbaabu, 1985: 61). Hizi zilikuwa ni nyakati za udhalimu wakati washairi walitumia ishara kwa wingi ili wakoloni wasielewe ujumbe wao. Huu ulikuwa wakati wa washairi kama Shaaban Robert na Saadani Kandoro. Kezilahabi (1976: 33) anaongeza kwamba, siasa ni jambo ambalo limegusa waandishi wa Kiswahili hasa wale waliopitia enzi za ukoloni na kuingia katika uhuru.

Shaaban Robert alikuwa mshairi aliyeishi nyakati za ukoloni hivyo, hangeweza kukwepa uhalisi wa maisha ya kikoloni yaliyokuwa yakiwaonea na kuwadhulumu wananchi. Alijishughulisha na masuala ya kisiasa ya kutetea haki na kupinga unyonyaji, unyanyasaji na uovu mwingine wote (Senkoro, 1988: 106). Katika kitabu chake cha *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini*, inadhihirika jinsi alivyoupinga ubaguzi wa rangi uliomfanya Mwafrika kudunishwa, kudharauliwa na kunyanyaswa kutokana na rangi yake. Mojawapo kati ya matendo yaliyomuudhi Shaaban Robert ni ubaguzi wa rangi (Kezilahabi, 1976: 33). Wakati mwingine aliwaomba Watanganyika wa wakati huo wa ukoloni wajiunge na Chama cha Mwafrika ili wapinge dhuluma. Robert alikuwa

na ujasiri wa kuwalaumu viongozi au wakubwa wa aina yoyote ile. Alitunga mashairi ya aina nyingi kimtindo na kimaudhui, mengi ya kuutetea Uafrika na kuponda vitimbi vya wakoloni (Syambo na Mazrui, 1992: 46). Hivyo, siasa haikuachana na mashairi ya Shaaban Robert.

Kwa upande mwingine, Saadan Kandoro alijishughulisha na siasa. Katika dibaji ya diwani ya *Mashairi ya Saadani,* Mnyampala anasema kuwa Kandoro alishughulika na siasa ya kuikomboa nchi ya Tanganyika kutoka mikononi mwa wakoloni akiwa bega kwa bega na Nyerere mpaka mwisho wa ukombozi huo. Kwa mujibu wa Senkoro, Kandoro alikuwa mmoja kati ya watu waliopigania uhuru kwa njia mbili: kimatendo na kimaandishi. Kwa upande wa maandishi Kandoro anasifika kwa ujasiri wa kuandika mashairi yaliyokashifu serikali ya mkoloni wakati ambapo mkoloni alikuwa bado nchini anatawala. Ni watu wachache walioonyesha ujasiri huu wa kumpinga mkoloni (Senkoro, 1988: 53). Kulingana na Mulokozi na Sengo washairi wengi wa wakati wa ukoloni walioandika mashairi ya kisiasa walikuwa wanasiasa (Mulokozi na Sengo, 1995: 79). Walikuwa viongozi wa vyama vya kisiasa vilivyopigania uhuru wa Tanganyika. Kwa mfano, Kandoro alikuwa kiongozi wa chama cha TANU mjini Tabora na Mwanza na Akilimali Snow-White alikuwa kiongozi wa Ujiji. Vilevile, Amri Abedi alikutana na Julius Nyerere kabla ya uhuru na akamsaidia kuunda chama cha TANU, chama ambacho kilikuja kuwa cha kitaifa (Knappert, 1979: 284).

5.3.1 Dhuluma za Kikoloni

Kandoro (1966) anaeleza jinsi wakoloni walivyowanyanyasa Waafrika katika kipindi cha utawala wa Waingereza. Katika shairi “Tumshukuru Manani”, Kandoro anaeleza jinsi alivyofurahi walipopata uhuru kwani walikuwa utumwani. Anaeleza madhila waliyoyapata. Katika ubeti wa pili anasema:

Tabu nyingi tulitiwa, sharia ziso imani,

Ubaguzi ukatiwa, hata vyoo safarini,

Sisi tulibaguliwa, hata kula hotelini,

Tumshukuru Manani, uhuru tumejaliwa (Kandoro, 1966: 146).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, mkoloni aliunda sheria ambazo hazikuwa na maana. Waafrika walibaguliwa katika sehemu nyingi kwa mfano, hotelini na misalani. Kwa hivyo, anamshukuru Mungu kwa kuwajalia uhuru. Pia, katika ubeti wa tatu mshairi anasema:

Tulifanywa ni wakiwa, tungemlilia nani,

Tukisema hutishwa, tutatiwa gerezani,

Ndivyo tulivyotumiwa, kama punda mizigoni,

Tumshukuru Manani, uhuru tumejaliwa (Kandoro, 1966: 146).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza jinsi walivyotishwa kuwa wangefungwa gerezani ikiwa wangelalamika kwa kufanyizwa kazi kama punda. Mambo mengine waliyofanyiwa ni kuwa, walipokuwa kifungoni walipewa chakula kidogo kama vile ndege anavyotiliwa mtama kifungoni. Pia, walilazimishwa kulipa kodi la sivyo wangefungwa kamba shingoni na kupitishwa mitaani. Isitoshe, katika ubeti wa sita mshairi anasema:

Shuleni hatukutiwa, ili tuwe ujingani,

Fusi hatukupatiwa, kutiwa utajirini,

Kucha kutwa hukomewa, kama majitu haini,

Tumshukuru Manani, uhuru tumejaliwa (Kandoro, 1966: 146).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kwamba, hawakuruhusiwa kusoma shuleni ili waendelee kuwa wajinga. Hata pesa wasingepata wasije wakawa matajiri.Waliteswa kama wahalifu. Wakoloni waliwawekea vizuizi wasipate uhuru hasa miongoni mwa

wasomi. Walifukuza watu mijini. Vilevile, Waafrika walipofunguliwa mashtaka walitozwa faini kubwa. Matatizo haya yote yanadhihirisha kuwa, Waafrika waliteseka katika kipindi cha ukoloni.

Akilimali (1963) anaeleza dhuluma alizopata kutoka kwa wakoloni katika shairi "Nafingwa Ningali Hai". Mshairi anatamani kueleza anayoyapitia lakini haruhusiwi kusema. Kwanza, anazungumzia ubaguzi wa rangi unaomfanya akose anachotaka. Pia, sheria ambazo hazifuatwi kwa hivyo, hawawezi pata maendeleo. Aidha, ingawa ana uwezo wa kuwa kiongozi, anazuiwa asifanikiwe. Anapata hata vitisho asije akasema yale anayoyapitia. Katika ubeti wa tano anasema:

> Napigwa pigo la goti, miguu nimelemewa
> Kilicho changu sipati, naomba bila kupewa
> Nafingwa kama kijiti, nanyimwa kwa kuonewa
> Nafingwa ningali hai, kinywa nazibwa kunena (Akilimali, 1963: 47).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kwamba, anapigwa magoti na kulemazwa miguu. Vitu vilivyo vyake hapati, akiomba hapati wala hapewi. Anazuiwa kwa kiboko kwa hivyo, ananyimwa kwa kuonewa. Mshairi anasisitiza kuwa ingawa yuko hai anazibwa mdomo asiweze kusema anayoyapitia.

Fauka ya hayo, katika shairi "Walimwengu Tutendeje?" Kandoro (1963) anaeleza shida zilizoingia nchini na hawajui watafanya nini. Katika ubeti wa kwanza mshairi anasema:

> Nchi yaingia shida, shida imebisha hodi,
> Juhudi na jitihada, bali shida inazidi,
> Wanadamu tunakonda, shida zafyonza miradi,
> Nafingwa ningali hai, kinywa nazibwa kunena (Akilimali, 1963: 71).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, nchi yao imepata shida. Ingawa wanatia bidii shida zinawazidi kwani wananchi wanasononeka kwa sababu miradi yao imeharibika. Kwa hivyo, anaomba ushauri kuhusu shida waliyoipata. Shida iliyoko ni kulipa kodi jambo linaloathiri miradi yao. Anamalizia shairi kwa kueleza kwamba, wanapotaka kupanda miche mashambani nguruwe wanawawinda kwa sababu ni maadui wao. Wanapata shida pale nguruwe wanawashinda nguvu. Mshairi anafananisha wakoloni na nguruwe wanaozuia wananchi kuleta maendeleo kwa kuwadhulumu.

Isitoshe, katika "Utenzi wa L", Kandoro (1966) anaeleza jinsi alivyokwenda Mwanza kujaribu kuzungumza na serikali ya mkoloni iliyokuwa inawaumiza. Katika ubeti wa kumi na nne mshairi anasema:

Kwamba inatuumiza
Ng'ombe zetu kupunguza
Nilikuwa naeleza
Nikisema tafadhali (Kandoro, 1966: 89).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, Watanganyika walikuwa wanapunguziwa idadi ya ng'ombe waliofuga. Kwa hivyo, walikuwa wanaomba wakoloni wawaruhusu wafuge idadi ya ng'ombe wanayotaka. Aidha, katika ubeti wa kumi na tano mshairi anasema:

Ng'ombe ushuru kutoza,
Pamba bei kupunguza,
Ushuru pamba kutoza,
Ni mambo ya idhilali (Kandoro, 1966: 89).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kwamba, Watanganyika walitozwa ushuru kwa kufuga ng'ombe. Pia, walipunguziwa bei ya pamba kwa kutozwa ushuru. Katika shairi hili, mshairi anabainisha madhila waliyoyapata kutoka kwa wakoloni.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, watu hutumia lugha kulingana na mahitaji ya kijamii au "soko" yaani hadhira inayokusudiwa. Kwa hivyo, washairi walitumia lugha ya Kiswahili kuelezea dhuluma za kikoloni kwa lengo la kuwahamasisha Watanganyika kupigania ukombozi.

Mnyampala (1965) anaeleza jinsi siasa zilivyokuwa wakati wa mkoloni. Katika shairi "Zama Zetu za Siasa", analinganisha jinsi siasa ilivyokuwa wakati wa ukoloni na wakati wa sasa. Anaeleza kwamba, huwezi kuiga siasa ya zamani ya wendawazimu kwa sababu wakati huu siasa inahitaji upole na tahadhari. Katika ubeti wa tatu mshairi anasema:

> Zama zile zimepita, za watu kuwanyanyasa,
> Zile zama za kututa, na kunyang'anya mapesa,
> Hizi zama za matata, kuchunguzana makosa,
> Zama hizi za siasa, ni zama za tahadhari (Mnyampala, 1965: 149).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kwamba, nyakati za zamani zimepita ambapo watu walinyanyaswa kwa vile wakoloni walijitajirisha kwa kuwanyang'anya watu pesa kwa kuwatafutia makosa. Zilikuwa nyakati zenye visa na mikasa zilizojaa dhuluma. Kwa upande mwingine, anaeleza kuwa, siasa za wakati huu ni tofauti kwani watu hushikilia haki na hawana dhuluma. Anasisitiza siasa za wakati huu zinahitaji tahadhari. Mshairi anabainisha dhuluma walizozipata Watanganyika wakati wa ukoloni. Aidha, katika ubeti wa nne mshairi anaongeza kuwa:

> Zino zama za kuteta, zenye visa na mikasa,
> Sizo zama za kupata, kwa dhuluma na kutesa,
> Ni zama za kuambata, yenye haki inopasa,
> Zama hizi za siasa, ni zama za tahadhari (Mnyampala, 1965: 149).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, nyakati za ukoloni zilikuwa zenye visa na mikasa. Zilikuwa nyakati za mateso kwani hungeweza kupata chochote kwa haki.

Aidha, katika shairi "Uhuru Una Kiungo", Mnyampala (1965) anasisitiza kuwa, uhuru una kipengele kinachofuta kodi inayolipwa na wanyonge. Anawaeleza wanaume wote wafurahi, wapumzike na wang'ae kama mpingo kwa sababu ya kupata uhuru uliowaondolea wanyonge kodi. Anawaeleza wajinyooshe lakini wasiseme maneno yaliyowaumiza. Anawashauri watu walime wapate fedha kwa sababu wamefanyiwa mipango. Tena, wapeleke watoto shuleni wakasome hadi kiwango cha juu. Maelezo haya yanabainisha kuwa, Watanganyika walilazimishwa kulipa kodi, hawakupata faida kutokana na kilimo na walinyimwa elimu na utawala wa mkoloni. Katika ubeti wa mwisho mshairi anasema:

> Hapo ilikuwa ngome, asolipa kodi ni msungo,
> Alitandikwa akome, na gereza kifungo,
> Hebu sasa tupime, Dola sasa si kiungo?
> Uhuru una kiungo, wanyonge kufutwa kodi (Mnyampala, 1965: 143).

Katika ubeti huu, mshairi anasema kuwa, kulikuwa na sera kwamba asiyelipa kodi alikuwa amekiuka sheria. Kwa hivyo, alipigwa na kufungwa gerezani. Mambo yamekuwa tofauti baada ya kupata uhuru kwani wanyonge wamefutiwa kodi. Shairi hili linabainisha kuwa kabla ya uhuru Waafrika walidhulumiwa kwa sababu walilazimishwa kulipa kodi. Wanyonge walioshindwa kulipa waliteswa kwa kupigwa na kufungwa gerezani.

Robert (1967) amekashifu ubaguzi wa rangi uliofanywa na wakoloni dhidi ya Waafrika. Katika shairi "Rangi Zetu", mshairi anaeleza kwamba, rangi ni pambo la binadamu alilopewa na Mungu lakini si alama ya maafa. Rangi si alama ya uchafu wala si ishara

ya machungu, dhambi au upungufu lakini ni sifa au urembo kutoka kwa Mungu. Anaeleza kuwa, wajinga hudhani rangi ni kashifa lakini Mungu hupamba mbingu, viumbe na mataifa kwa rangi tofauti. Katika ubeti wa kumi na mbili mshairi anasema:

> Rangi kwa shairi langu, tungo yenye kuarifu,
> Kila walipo wenzangu, jambo hili maarufu,
> Rangi kugawa mafungu, huonyesha upungufu,
> Rangi heba ya Mungu, Mwenyezi Mkamilifu (Robert, 1967: 19).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, ametunga shairi la rangi ili kufahamisha wenzake jambo muhimu. Anaeleza kwamba, kubagua watu kwa misingi ya rangi huonyesha upungufu kwani rangi inadhihirisha sifa ya Mungu. Mshairi anabainisha kuwa, kudharau na kuonea wivu kwa sababu ya rangi ni upuzi wa mtu. Mshairi alilenga kukashifu ubaguzi wa rangi uliofanywa na wakoloni kwa Waafrika.

Pia, Robert (1968) anaendelea kukashifu ubaguzi katika shairi "Kama Upinde wa Mvua". Mshairi anasema:

> Dunia wenyewe watu, wamepewa kutumia,
> Hii ni heshima kwetu, tumshukuru Jalia,
> Wanyama ni washirika wenye kucha na pembe,
> Na ndege wanaoruka na jamii ya viumbe,
> Wanaokwenda kwa tumbo au kwa kurukaruka,
> Ama walio na umbo ambalo huajibika.
> Na baharini samaki ambao huzama mbizi,
> Vitu havihesabiki, vyenye roho na pumzi,
> Vitu hitilafu rangi kama upinde wa mvua (Robert, 1968: 44).

Katika shairi hili, mshairi anaeleza kuwa, binadamu amepewa dunia na Mungu kwa ajili ya matumizi yake. Humu duniani kuna wanyama, ndege, samaki na viumbe wengine

kadha wa kadha. Kwa hivyo, Mungu amewaumba viumbe walivyo na rangi au sura tofauti kama upinde wa mvua kwa kusudi la kuupamba ulimwengu. Viumbe hao wote hupata riziki kila siku kutoka kwake pasipo kusahaulika hata kidogo. Anaendelea kueleza kuwa, binadamu atarudi kwa Mungu na kuingia katika utukufu wake mkubwa usiopimika. Watu wote wataishi maisha ya furaha. Katika shairi hili, mshairi anapinga ubaguzi kwa misingi ya rangi au sura. Kwa kutumia mifano ya viumbe walioumbwa na Mungu, anabainisha kuwa, ingawa watu wana rangi tofauti, wote ni viumbe wa Mungu na anawajali. Mshairi anamtetea Mwafrika kwa kubaguliwa na wakoloni.

Isitoshe, katika shairi "Kuondoana Njiani", Robert (1968) anatetea usawa kwa kupinga ubaguzi. Anaeleza kwamba, wanafanya kazi nyingi lakini hazina faida. Kwa mfano, watu wanauza kangara lakini hawana mapato. Anapinga tabia zinazozuia wengine kufanikiwa. Watu wa bara wanafanya kazi kwa bidii bila faida. Watu wa pwani wakihama hawawezi kurudi kwao kwani wanahangaika bila faida. Hata ukifanya kazi kwa bidii, tajiri hupata cheo lakini huongezwi mshahara. Unapochelewa kazini unaogopa kwa sababu tajiri hukuita kwa haraka na kukufokea kwa hasira. Mnyonge hana hasira la sivyo angepigana na tajiri wake. Hata mtu akifanya kazi miaka kumi, haongezwi mshahara hata senti lakini anajipa moyo. Anakemewa kila siku kwa hivyo, hana raha kazini. Mwaka unapoisha hakuna kupandishwa cheo ila anakuwa tu mtumwa.

Katika ubeti wa kumi mshairi anasema:

> Kutumiwa kama nyara, mimi furaha sinayo,
> Takwenda nayo ahera, machungu niliyo nayo,
> Kuna maamuzi bora, ya dhuluma kama hiyo,
> Tutaenda ndivyo sivyo tuondoane njiani (Robert, 1968: 87).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kwamba, hana furaha bali ana machungu atakayokwenda nayo ahera. Hajui maamuzi bora ya dhuluma wanazotendewa Waafrika na wakoloni. Katika shairi hili, mshairi anabainisha dhuluma wanazopata Waafrika wanaowafanyia kazi wakoloni. Wanafanya kazi nyingi isiyo na malipo na wananyimwa haki za wanyakazi kama kuongezwa mshahara baada ya wakati fulani.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, watu hutumia lugha kulingana na mahitaji ya jamii inayokusudiwa. Washairi walitumia lugha ya Kiswahili kuelezea madhila yaliyowakumba Watanganyika wakati wa ukoloni kwa lengo la kuwahamasisha kupigania uhuru wao. Matumizi ya Kiswahili katika ushairi yalieneza lugha ya Kiswahili.

5.3.2 Utetezi wa Haki

Mnyampala (1965) anatetea haki za wafanyakazi. Katika shairi "Watumishi Tusimame", Chama cha Wafanyikazi kinahimizwa kudai haki kutoka kwa matajiri ambao ni wakoloni. Katika ubeti wa pili mshairi anasema:

> Hebu tudai tajiri, mbele yake tulalame,
> Jioni alfajiri, tumwambie ayapime,
> Maombi si kukasiri, ya mapigano kwa sime,
> Watumishi tusimame, haki tudai tajiri (Mnyampala, 1965: 43).

Katika ubeti huu, mshairi anawashauri watumishi wa wakoloni wadai haki kila wakati yaani "jioni alfajiri" kwa kumwomba tajiri apime wanayoyasema. Waombe haki bila hasira au kupigana kwa sime. Pia, mshairi anawaomba wafanyakazi wasiwe na kiburi lakini wasimame kama wanaume. Wasiwe wajeuri kama paka shume ila wadai mapato siku zote mbele ya mfalme. Katika ubeti wa mwisho mshairi anasema:

> Tusivunje itibari, tukisimama kinyume,

Dai letu ni dhahiri, mali nasi tuichume,

Kila alotuajiri, dai mate asiteme,

Watumishi tusimame, haki tudai tajiri (Mnyampala, 1965: 43).

Katika ubeti huu, mshairi anawashauri wafanyakazi wasivunje muamana kwa kusimama kinyume. Madai yao ni dhahiri ili waweze kuchuma mali. Kila aliyewaajiri asije akatupilia mbali madai yao. Kwa hivyo, anasisitizia wafanyakazi kuendelea kudai haki zao. Katika shairi hili, mshairi anawahimiza Waafrika waendelee na mapambano ya kutafuta haki za wafanyakazi.

Robert (1968) anahimiza watu waingie vitani wapambane na wakoloni. Katika shairi "Kufua Moyo", mshairi anaeleza kwamba, siku panga itakapochomolewa mashujaa wataenda vitani na kusababisha machafuko. Ardhi italowa kwa mmiminiko wa damu. Hii ndio siku watu mashuhuri watajipambanua kwa matendo. Watu watajikusanya pamoja na kujiuliza kama ni bora kufa kwa vita au kufa kwa maradhi ya sondo. Katika ubeti wa tatu mshairi anasema:

Uvundo wa mashujaa,

Ni sawa na manukato,

Marashi katika pua,

Hauna harufu nzito,

Ama rihi ya maua,

Njema isiyo fukuto,

Nyingi katika hewa,

Na ardhi yenye woto,

Ni fahari maridhawa,

Kwa wazee na watoto (Robert, 1968: 49).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, uvundo wa maiti ya mashujaa ni sawasawa na manukato au marashi au harufu nzuri ya maua katika pua za watu. Uvundo wa mashujaa

hauna harufu ya karaha wala fukuto. Harufu hii nzuri hujaa tele katika hewa na katika ardhi yenye mimea. Mauti ya mashujaa huacha fahari kubwa kwa watu wote na ni urithi unaopendelewa na watu. Ni urithi wa majohari yaliyo bora katika ulimwengu. Mauti ya vitani hufanana na ndoto katika usingizi. Katika shairi hili, mshairi anawahimiza watu wapambane na adui vitani. Mshairi angependa Waafrika wapambane na watawala wa kikoloni ndiposa akasema bora kufa kwa vita. Anawasifu mashujaa wa Kiafrika kwa kusema kuwa hata uvundo wa maiti zao ni manukato kwa watu kumaanisha wasiogope kufia vitani. Aidha, anawatia shime kwa kubainisha kuwa, hawatawahi kusahaulika kwa kujitolea kwao katika mapambano.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Utegemezi, jamii inayonuia kujikomboa kutokana na ukoloni haina budi kutumia lugha moja ya kuwaunganisha watu ili kuwa na umoja kwa lengo la kuleta ukombozi. Mshairi ametumia lugha ya Kiswahili kuwahimiza Watanganyika wapambane na wakoloni.

Kwa kuelezea sifa za ushujaa, Kandoro (1966) anawatia moyo Waafrika kutetea haki zao. Katika shairi “Shujaa Haogopi Kitu Kilicho Chake”, mshairi anaeleza kwamba, shujaa hakubali kudhulumiwa na kunyang’anywa kitu chake. Yeye ana ujasiri wa kutetea halali yake. Shujaa ni hodari wa kutafuta haki yake kwa hivyo, haogopi. Hata kama ni mtoto akishikwa hufanya utukutu. Yeye hupigania mji wake usitekwe na huokoa vitu vyake au vyao. Katika ubeti wa mwisho anasema:

> Hodari nyumbani kwake, huwakaribisha watu,
> Hutetea nchi yake, asiichafue mtu,
> Yu tayari peke yake, kuutembelea mwitu,
> Shujaa haogopi kitu, kilicho halali yake (Kandoro, 1963: 66).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, shujaa huwa hodari hata nyumbani kwake anapowakaribisha watu. Hutetea nchi yake isije ikaharibiwa na watu. Huwa tayari hata kwenda msituni kupigana kwa sababu anatetea kilicho chake. Katika shairi hili, mshairi anawahimiza Waafrika watetee nchi yao bila kuogopa. Pia, Waafrika wasiruhusu wakoloni kuharibu nchi au kuteka nyara miji yao lakini wafanye vyovyote vile kulinda nchi yao.

Isitoshe, katika shairi "Ondoka Nchini Mwetu", Kandoro (1966) anadhihirisha hisia zake kuhusu utawala wa Mwingereza nchini Tanganyika na Afrika kwa jumla. Katika ubeti wa kwanza mshairi anasema:

> Raia tumekutana, mbele ya wakubwa wetu,
> Raia tumeungana, kuunda taifa letu,
> Na sisi tuwe mabwana, kutawala nchi yetu,
> Ondoka nchini mwetu, mwishoni mwa mwaka huu (Kandoro, 1966: 141).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kwamba, raia wa Tanganyika wameungana ili walinde taifa lao na waweze kujitawala. Anaeleza kuwa, wanachama wa Chama cha TANU wanawaomba Waingereza waondoke nchini Tanganyika. Pia, Waafrika wote wameungana na kuwaomba Waingereza watoke Afrika. Anaongeza kuwa, nchi ya Uingereza na hata Uchina zinajua sheria na kwamba Tanganyika si nchi yao kwa hivyo, hakuna haja ya kuifanya kuwa yao. Mzee Kenyatta alikuwa amenyamazishwa na jambo hilo linawauma sana kwani alikuwa anawaomba Waingereza waondoke Kenya. Watanganyika wote wangependa kuwa huru ili wajitawale kama nchi ya Ghana. Anamalizia shairi kwa kueleza kwamba, Waingereza wakiondoka kwa amani, Afrika itakuwa huru na wote watafurahia kwani si vizuri kudhulumu wengine. Katika shairi hili, mshairi anahamasisha Waafrika wakatae utawala wa Mwingereza kwa kusisitiza

kuwa, Waingereza wanastahili waondoke nchini Tanganyika kufikia mwishoni mwa mwaka.

Vilevile, katika shairi “Kujitawala”, Kandoro (1966) anawahimiza wananchi wavumilie mpaka waweze kujitawala kwani kupata uhuru si jambo rahisi. Ikiwa wanataka kujitawala inabidi wajitolee kabisa lakini si kuishi maisha ya raha. Pia, wanastahili wafikirie jinsi ambavyo wangeandika mipango yao ipelekwe Buckingham ili kuonyesha kuwa, wako tayari kujitawala. Wanastahili walinde na kuheshimu watu wote wawe maskini au tajiri na wasidhulumu matajiri. Anawaomba watu wasaidiane ili chama cha TANU kiheshimike na waungane waombe wapate kujitawala. Wakifanya hivyo, Tanganyika itatukuka duniani kote. Anamalizia shairi kwa maombi kwamba, wakituma wajumbe kuomba uhuru wapate bila shida. Katika shairi hili, mshairi anawahamasisha Watanganyika waungane na chama cha TANU waweze kutetea haki yao ya kujitawala. Ana matumaini kwamba wakiomba uhuru kwa Waingereza watapata.

Katika “Utenzi wa L”, Kandoro (1966) anaeleza kuwa, walipotaka kujitawala walimtuma mjumbe kwa waziri msifika huko Uingereza kuwasilisha maombi yao. Mshairi anasema mnyonge anapodai haki na mwenye nguvu hataki, vita hutokea. Hivyo, Wazungu walifika katika ofisi yake wakawakamata na kutwaa kila kitu hata mali yake wakiwa na Bwana Munanka. Hata hivyo, katika ubeti wa thelathini na saba anasema:

> Lazima tuwe imara,
> Itabadilika kura,
> Yataafiki majira,
> Tule ngano na samli (Akilimali, 1966: 91).

Katika ubeti huu, mshairi anawashauri Watanganyika wasibabaike kwa madhila waliyonayo. Anapendekeza wawe imara kwani mabadiliko yatatokea wakati ukifika na wapate uhuru. Mshairi anawahimiza Watanganyika waendelee na mapambano ya kupigania uhuru.

Kulingana na Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, lugha huwa kama bidhaa muhimu kutokana na majukumu inayochangia na kutimiza miongoni mwa wanajamii na mikakati yao ya kuendeleza maisha. Lugha ya Kiswahili ilikuwa muhimu kwa sababu ilitumika kuwahamasisha Watanganyika waungane na watetee haki zao. Kwa hivyo, Kiswahili kilienea kote nchini Tanganyika.

5.3.3 Umoja na Ushirikiano wa Waafrika

Akisisitiza umuhimu wa Watanganyika kuungana ili kupambana na mkoloni, Robert (1966) katika shairi lake "Chama cha Waafrika", anabainisha umuhimu wa mapambano. Anaeleza kuwa, baada ya kuwaza amegundua upekee hauna faida hasa wakati wa shida. Hivyo, ikiwa wananchi wanataka kujitawala lazima washirikiane. Katika nchi ya Tanganyika kuna chama ambacho kinalenga kupigania nchi na kumaliza matatizo yake. Wananchi wanastahili kujiunga na Chama cha Waafrika cha Watanganyika kwa sababu ni shirika linalotukuka linalonuia kuzuia mateso kwa wananchi. Chama pia kinaeleza serikali ya Waingereza shida wanazopitia wananchi. Hivyo, kazi yake ni halali japo wananchi wakinyamaza wataangamia. Mshairi anawahimiza wananchi waungane kwa sauti moja ili Waingereza wajue kuwa wanawaumiza. Baadhi ya shida za wananchi ni kubezwa kwa kazi zao, jambo linalowachukiza. Anawahimiza Waafrika waelewe mashaka waliyonayo waweze kutafuta suluhisho. Katika ubeti wa mwisho mshairi anasema:

All come on, kila mwenyeji aweza,

Do his turn, Tanganyika kuikuza,

Know each grain, uzito inaongezeka,

African Association, naam mwangaza (Robert, 1966: 10).

Katika ubeti huu, mshairi anawaita wenyeji wa Tanganyika waweze kushiriki kuikuza Tanganyika. Kila mtu ana mchango wake ulio muhimu. Kwa hivyo, Chama cha Waafrika kitafanikiwa. Katika shairi hili, mshairi anabainisha umuhimu wa kujiunga na Chama cha Waafrika. Pia, anawahimiza Watanganyika waungane katika harakati za ukombozi.

Kwa upande mwingine, Mnyampala (1965: 147), anawashauri watu waungane waweze kupambana na wakoloni. Katika shairi"Muungano Utupambe" mshairi anamwomba Mungu awaondolee mizozo ili mataifa yasigombane. Anasisitiza kuwa, viumbe wote wanastahili waungane pamoja. Pia, waondoe ugomvi na machukizo kama watoto wadogo waweze kuishi kwa amani na waasi wasije wakafurahi. Anapendekeza muungano kwa Wakenya ili waondoe serikali za majimbo na kuwa na umoja. Watanganyika waungane na Unguja na Rhodesia wasiwabague hata kidogo. Waafrika wanapodai haki wanaodaiwa waweze kuwasikiliza wasiwapuuze ama kuwa wajeuri. Mshairi angependa kuona Mreno ameondoka katika nchi anazotawala na kuwaachia wenyeji utawala. Anamaliza shairi kwa kumwomba Mungu awaondolee mikwaruzo na mabomu wanayorushiwa wasalimike. Katika shairi hili, mshairi analenga kuwahimiza Waafrika washirikiane popote walipo ili wakabiliane na matatizo yao.

Pia, katika shairi "Mwaka uwe wa Heri", Mnyampala (1965) anaeleza matarajio yake kuwa, Watanganyika watakuwa huru. Anaiombea nchi yake baraka na neema tena wasiwe na minong'ono bali wawe na usalama. Mshairi angependa wawe na mapatano, huruma na imani na waache dhuluma. Anaeleza kwamba, vita havina salama kwa hivyo,

waachane na maandamano waweze kumaliza njaa nchini. Elimu iendelezwe kama njia ya kukabiliana na ujinga. Katika ubeti wa sita anasema:

> Shirika uwe mfano, kwa Tanganyika mzima,
> Tuyaache matetano, magombano siyo mema,
> Bora mashirikiano, ndilo jambo lilo jema,
> Mwaka uwe na neema, wenye heri na fanaka (Mnyampala, 1965: 5).

Katika ubeti huu, mshairi anawashauri Watanganyika washirikiane waache kugombana kwa sababu ushirikiano ni jambo njema. Anasisitiza kuwa, wakifanya hivyo mwaka utakuwa na neema, wenye heri na fanaka. Shairi hili linadhihirisha kuwa, Watanganyika wakipatana mwaka utakuwa wa baraka.

Isitoshe, katika shairi "Shirika ni Kustawi", Mnyampala (1965) anasisitiza kuwa, ushirikiano huleta mafanikio na kufarakana ni vibaya. Anasema kwamba, anayeacha wengi ni mchawi kwa sababu shirika ni nzuri. Katika ubeti wa tatu anasema:

> Maneno haya muhimu, msijifanye viziwi,
> Sijifanye madhalimu, kuchomana kama biwi,
> Huo huitwa wazimu, pendo halihalibiwi,
> Shirika ni kusitawi, vibaya kufarakana (Mnyampala, 1965: 24).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kwamba, maneno anayoyasema ni muhimu wasikose kuyasikia. Anasema ni wazimu kuharibu upendo kwa kuchomana kama takataka. Mapenzi yakiwepo shirika linadumu na watu huishi kwa furaha. Mshairi angependa Mdigo na Msandawi washike hatamu wawaheshimu wakubwa na watu wa rika zote. Pia, waache chuki na kiburi lakini wawe na heshima ili shirika listawi. Katika shairi hili, mshairi anabainisha umuhimu wa ushirikiano katika jamii.

Katika shairi “Mungu Ondoa Tatizo”, Mnyampala (1965) anamwomba Mungu awaondolee mizozo ili majirani waelewane na waungane. Katika ubeti wa kwanza mshairi anasema:

> Jirani wana gombano, kutwa kucha ni mzozo,
> Kwani hawana patano, wagomba mfululizo,
> Hawaishi mikwaruzo;
> Mikwaruzo mashindano, kuonyeshana uwezo,
> Hawatamani mwungano, ambao kwao ni nguzo,
> Mola ondoa mizozo, majirani wafaulu (Mnyampala, 1965: 129).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, majirani wanagombana na kushindana kila mmoja akionyesha uwezo wake. Hawataki muungano ambao ni nguzo muhimu. Mshairi anamwomba Mungu awaondolee mizozo ili waweze kufaulu. Anataja kisiwa cha Unguja kama sehemu yenye mzozo. Nchi ya Kenya inajivuna kwa kupinga yaliyoamuliwa katika mkutano uliokuwa Cairo na kuvunja moyo kiongozi Jomo Kenyatta. Nchini Uganda kuna upinzani kwa sababu Buganda na Bunyoro kuna magombano, jambo linalomwathiri Lukiko. Nchini Kongo vita vinaendelea kwa hivyo, vifo ni vingi. Nchi ya Zambia (Nyasaland) ina uongozi bora wa Banda anayewabembeleza wananchi ili wapate uhuru. Mshairi anaisifu nchi ya Tanganyika kwani kuna maridhiano na anaomba mizozo isitokee. Anamalizia shairi kwa kueleza kuwa, ugomvi unaleta maangamizi kwa hivyo, wananchi washirikiane kwa kusuluhisha matatizo yao. Katika shairi hili, mshairi anawahimiza Waafrika wa nchi mbalimbali kushirikiana na kuepuka mizozo wapate kufanikiwa katika kutatua matatizo yao.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Utegemezi jamii inayonuia kujikomboa kutokana na ukoloni haina budi kutumia lugha moja ya kuwaunganisha watu ili kuwa na umoja kwa lengo la kuleta ukombozi. Lugha ya Kiswahili ilitumika kuwahimiza Watanganyika na

Waafrika kwa jumla washirikiane katika harakati za ukombozi. Hivyo, kupitia mashairi, lugha ya Kiswahili ilienea.

5.3.4 Kupigania Utamaduni wa Waafrika

Abedi (1954) anapigania utamaduni wa Kiafrika kwa kukashifu tabia ya wanawake wa Afrika ya kuvaa mavazi ya kigeni katika shairi lake "Nguo Ziteremsheni Yapungue Maasia." Katika ubeti wa kwanza mshairi anasema:

> Sitara kubwa kuvaa, vazi refu miguuni,
> Msiige bila njia, mabibi kunradhini,
> Vazi refu kulivaa, ni sitara muilini,
> Nguo ziteremsheni, yapungue maasia (Abedi, 1954: 52).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, ni heshima kuvaa nguo ndefu hadi miguuni. Wanawake wasiige mavazi ya wengine yanayosababisha maovu. Mtu anapovaa nguo ndefu anaheshimu mwili wake. Nguo baya ni baya hata kama imetoka uzunguni. Muumini akivaa anakuwa mwovu na itabidi arudi kwa Mungu. Nguo fupi zikivaliwa zinachochea tamaa ya wanawake bali kanzu ndefu zinafanya wanaume waende macho yakiwa chini. Kwa sababu ya kuvaa nguo fupi, watu wengi huko Uropa hugongwa na magari hata Waganda wameumia pia. Mshairi anauliza kama ni vyema watu kungoja walemazwe kisha waanze kuvaa nguo ndefu kwa lengo la kuficha huo ulemavu. Anamalizia shairi kwa kueleza kwamba, ni tabia njema kuvaa nguo ndefu kwani hukinga homa mwilini. Mshairi anadhamiria kuonya wanawake dhidi ya kuiga tabia za kigeni kama vile kuvaa nguo fupi zinazowafedhehesha na kuwadunisha mbele ya macho ya umma. Anasema "baya ni baya tambua ingawa la uzunguni" kuonyesha kuwa uvaaji wa nguo fupi si utamaduni wa Waafrika bali ni wa Wazungu. Pia, ni kinyume cha mafunzo ya kidini kwa hivyo, akamshauri muumini anayevaa nguo fupi kumrudia Mungu ndiposa akasema "hujahoji kwa hatua, bibi rudi kwa Manani".

Aidha, katika shairi “Wakudao Magotini Hawachelei Khasar”, Abedi (1954) anaendelea kukashifu tabia ya wanawake ya kuvaa nguo fupi. Anasisitiza kuwa, wanapopandisha nguo mpaka magotini hawaogopi hasara. Anashangaa jinsi buibui na kanga ndefu hupandishwa mpaka magotini na ni nguo za heshima. Mshairi analenga kutaja maovu yaliyopo nchini kwa sababu yanaleta hasara, ukware na ushetani. Kwa mwanamke kuvaa shungi linalofunika sura ni jambo zuri lenye shani kwani hapauki ngozi kwa kuchomwa na jua. Vilevile, hupunguza kutamaniwa na kuzuia fikira mbaya matokeo yake mwanamke anaheshimika. Katika ubeti wa nane anasema:

> Kuiga bila fikira, ni ujahili yakini.
> Huzivaa kaputura, mabibi wa Uzunguni,
> Je, hili ni busara, kwa kuwako Uzunguni?
> Wakudao magotini, hawachelei khasara (Abedi, 1954: 54).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa wanaoiga tabia za Wazungu bila kufikiria kweli ni wajinga. Anajiuliza kama ni jambo la busara kuvaa kaputura kama wanawake wa Kizungu. Anasisitiza kuwa, wanaovaa nguo fupi hawaogopi hasara. Isitoshe, katika ubeti wa tisa mshairi anasema:

> Kwao sio masikhara, chupi tupu kiunoni,
> Zinawatwaa kamera, utupu pasipo soni,
> Haya je ni busara, kwa kuwa ya Uzunguni?
> Wakudao magotini, hawachelei khasara (Abedi, 1954: 54).

Katika ubeti huu, mshairi anakashifu tabia ya wanawake ya kuvaa nguo zinazoonyesha nguo za ndani. Anauliza kama ni jambo la busara kuvaa hivyo hata kama utamaduni huo ni wa Wazungu. Anatilia mkazo kuwa, wanaovaa nguo fupi hawaogopi hasara. Katika shairi hili, mshairi anatetea utamaduni wa Waafrika kwa kuwaonya wanawake

wa Afrika wasiige tabia za Wazungu. Anawaeleza wanawake kuwa, wanajikosesha heshima na kusababisha maovu mengi wanapoiga mavazi ya Wazungu.

Isitoshe, katika shairi "Njema Haina Mkosi Japo aivae Koja", Abedi (1954) anaendelea kukashifu wanawake wanaovaa nguo fupi. Anasisitiza kuwa, Wahindi wakivaa nguo fupi huwa ni njema kwao lakini ni balaa kwa Waafrika. Katika shairi hili, mshairi anazungumzia mavazi ya wanawake. Anasema wanawake kuvaa nguo fupi ni ujinga na ushetani. Katika ubeti wa tatu mshairi anasema:

> Nawe binti wa Ujiji, nguo fupi si libasi,
> Usijitie ujaji, hujui kukata kesi,
> Wacheni ya ufujaji, tumche Mola Qudusi,
> Njema haina mkosi, japo aivae Koja (Abedi, 1954: 55).

Katika ubeti huu, mshairi anawashauri wanawake wa Ujiji waachane na nguo fupi ili waweze kumcha Mungu. Anawaambia wasifanye maamuzi mabaya yasiyowafaidi tena, hayo si mavazi yao ila ni ya Wahindi. Mshairi anawahimiza manju wapige vita mavazi ya aibu. Anawataka wanawake wasishiriki maovu bali wafuate ushauri wake. Wafuate mwongozo mwema waweze kumrudia Mungu na kuacha ushetani. Mshairi anawaomba wanawake wasimtusi kutokana na msimamo wake wala wasitetee maovu. Katika Shairi hili, mshairi anautetea utamaduni wa Mwafrika kwani mshairi anaonya wanawake wa Afrika wasiige mavazi ya Wahindi hata kama ni mazuri kwa Wahindi.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Utegemezi, Waafrika wanapaswa kutetea na kudumisha utamaduni wao ili kuondoa utegemezi wa utamaduni wa kigeni. Watunzi wa mashairi walihimiza Watanganyika wadumishe utamaduni wao kwa kukashifu utamaduni wa Kizungu hasa unaohusu mavazi.

5.3.5 Sifa za Viongozi Bora

Suala la uongozi limeshughulikiwa na Akilimali (1963). Katika shairi "Manahodha Kuwa Wengi", mshairi anaelezea sifa za viongozi bora. Anaeleza kuwa, ingawa kiongozi amesoma na kuihitimu mitihani ya Ulaya, lakini akiwa mkaidi au mpinzani nchini, nchi haitaendelea ndiposa akasema "meli haitaelea". Anasisitiza kuwa, viongozi wakiwa wengi na wenye maoni tofauti wanaweza kuharibu nchi.Viongozi wakibishana na kushindana wanaweza kuathiri nchi isipate maendeleo. Katika ubeti wa tatu mshairi anasema:

> Awe fundi yakini, hodari alosomea,
> Mjuzi wa kila fani, hana linampotea,
> Kama hataki maoni, hana budi kukosea,
> Manahodha kuwa wengi, ni kuzamisha mashua (Akilimali, 1963: 29).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kwamba, ikiwa kiongozi ni hodari na ni msomi mwenye ujuzi mwingi lakini hataki maoni ya wengine, atafanya makosa. Anasisitiza kuwa, viongozi wakiwa wengi wanaweza wakaharibu nchi. Kusoma sana si ajabu lakini cha muhimu ni mtu kutokuwa mbishi na kutotumia nguvu katika utawala la sivyo anakwamiza maendeleo ya nchi. Mungu ndiye hujua kiongozi mwema bali watu humjua anapofanya kazi kwa mwaka mmoja. Wananchi hawafaidi chochote kiongozi anapotawala na nchi isipate maendeleo kwani wao hutaka mabadiliko. Shairi hili linadhihirisha umuhimu wa kiongozi bora kwa sababu huleta maendeleo nchini.

Katika shairi "Kila Mpenda Rushuwa", Akilimali (1963) anawaonya viongozi dhidi ya kuchukua hongo kwani itawatia jela. Anaeleza kuwa, tamaa nyingi ya pesa ni hatari kwani itamtia mtu jela. Jela yenyewe ina matatizo mengi hivyo, si ya kuchezewa. Hata wale wenye nguvu hutulia wanapotiwa gerezani. Wanaokula hongo wafaa wajihadhari kwani itawaletea shida. Mtu anastahili aridhike na anachokipata hata kama ni kidogo

bila kutamani cha mwingine asije akajidhuru. Kuna viongozi wengine wasiogopa Mungu kwa sababu wanaagiza wafanyakazi wawaletee rushwa. Katika ubeti wa sita anasema:

> Kuna wengi mahakimu, haki wanazopinduwa,
> Yatima kuwadhulumu, kwa kupapia rushuwa,
> Kwa kutaka darahimu, aso haki anapewa,
> Kila mpenda rushuwa, jela inamkonyeza
> (Akilimali,1963: 23).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, kuna mahakimu wengi wanaodhulumu mayatima kwa kuwanyima haki. Mahakimu wanapewa pesa na asiye na haki anapewa huku yatima akinyimwa haki yake. Katika shairi hili, mshairi anabainisha athari za rushwa kwani mhusika huishia gerezani. Hivyo, analenga kuwaonya viongozi yaani "wenye vyeo" kama vile mahakimu wajihadhari kwani rushwa itawatia gerezani. Vilevile, mshairi anawaonya wanaotaka hadhi au utukufu kwa njia isiyo halali kuwa watapatwa na maafa.

Katika shairi "Kila Mtaka Uluwa", Akilimali (1963) anaeleza kuwa, mtu anayetaka cheo kwa kasi hujitia kwenye matatizo kwa sababu hawezi kukaa na kutulia bali hujitia hatiani. Anaendelea kueleza kwamba, ameona watu wengi zaidi ya mia wanaopoteza pesa zao wakitafuta vyeo au ufalme. Katika ubeti wa tatu mshairi anasema:

> Kupata huwa si nguvu, si vishindo na ghasia,
> Kwataka uvumilivu, uukosapo tulia,
> Autakae kwa nguvu, jela inamngojea,
> Kila mtaka uluwa, dunia aichukia (Akilimali, 1963: 19).

Katika ubeti huu, mshairi anashauri kuwa, kutafuta vyeo hakuhitaji nguvu, vishindo au ghasia bali kunataka uvumilivu. Mtu anapokosa cheo anastahili atulie la sivyo akitumia nguvu atatiwa gerezani. Anasisitiza kuwa, anayetaka utukufu au cheo kwa njia isiyofaa

anajitia matatani. Mshairi analenga kuwashauri wanaotaka uongozi kwamba watumie njia halali na wanapokosa vyeo hivyo wakubali wameshindwa.

Kwa upande wake, Robert (1968) anaangazia suala la uongozi katika shairi lake "Kashata na Ladu". Mshairi analinganisha serikali za wanyama, ndege na wadudu na serikali za watu. Anaeleza kuwa, wanyama, ndege na wadudu wana serikali zilizo na fahari iliyo kama ibada ya dini. Ingawa watu ni wenye busara hawawezi kuchukua madaraka na kuheshimika kuliko wanyama na wadudu. Vinywa vya watu vimefunuka wazi na kitu kilicho kitamu kimekuwa kichungu kwao. Hawana heshima ila wana uchafu. Madhara na dhuluma imekuwa kama miungu ya kuabudu. Mambo kama haya hayana heri bali ni ya kuharibu binadamu. Hizi ni nyakati za kuangamiza watu hali bado wazima na wenye nguvu za kuabudu Mungu. Kwa watu hawa maudhi na uadui huonekana matamu kama kashata na ladu. Katika shairi hili, mshairi anazungumzia serikali mbovu zinazoongozwa na watu. Serikali ambazo ni duni kuliko zile za wanyama, ndege na wadudu. Mshairi anadhihirisha kuwa, viongozi huendeleza dhuluma na kuangamiza watu. Hivyo, watu hawawezi kuwaheshimu kwa sababu wanafurahia uadui.

Fauka ya hayo, katika shairi "Kosa Ndogo", Robert (1968: 50) anabainisha athari za makosa ya viongozi. Anaeleza kuwa, ni jambo lisilo la maana kutangaza habari ya kosa la mtu mdogo au wa kawaida kwa sababu tendo lake ni kama la mwendawazimu ambalo wenye akili timamu hawawezi kulipatiliza. Walakini, kosa la kiongozi hutangazwa katika ulimwengu kwa maandiko ya herufi kubwa. Mtu mdogo hana nafasi ya kutenda mambo makubwa. Makosa makubwa hufanywa na viongozi ingawa hufichwa kwa uangalifu mkubwa. Kwa hivyo, walimwengu hutukuza wahalifu wakubwa na kuaibisha maskini ndiposa akasema "wakubwa wenye hatia wakazidi kutukuka". Viongozi

huwadhulumu maskini ili wafaidi cha maskini lakini hawafanywi chochote kwani maskini hawana uwezo wa kutenda lolote. Hivyo, maskini wanaishi katika unyonge lakini hawana la kutenda. Katika shairi hili, mshairi anabainisha maonevu kwa wanyonge. Viongozi wanawadhulumu wanyonge lakini wanatukuzwa ila wanyonge wanaoneshwa kuwa ndio wenye kosa.

Aidha, katika shairi "Uasi", Robert (1968: 34) analinganisha serikali na dini. Anaeleza kuwa, waasi wa serikali ni wengi kuliko waasi wa dini. Sababu ni kwamba, ingawa kuna watu wengi wasioenda kusali wana imani ya dini pasipo kasoro mioyoni mwao. Serikali ina watu wasio na maadili wasioheshimika na wanaofanya mambo ya matata, ugomvi, dhuluma, ubatili na hawana wema wowote. Kwa hivyo, watu wa jinsi mbalimbali huona hakuna ukweli katika serikali na kuamua kuitoroka. Katika shairi hili, mshairi anakashifu uongozi kwa sababu viongozi hawana maadili lakini wana maovu mengi.

Isitoshe, katika shairi "Vivuli", Robert (1968: 55) anaelezea hali ya kisiasa duniani. Anaeleza kuwa, kumetokea watu wenye kucha na mikono kama sumu wenye mazoea mabaya ya kusababisha machafuko na uhalifu na hatia. Mapenzi hayapatikani tena ila mapendeleo yasiyo na haki. Uchafu ndio uliobakia sasa katika pembe zote ulimwenguni. Kila mtu analia kwa ukosefu wa rai ya tendo na mwendo. Vitisho vinazidi kuongezeka kwani viongozi wanatisha kwa namna wanavyoongoza mataifa yao. Hivyo, hakuna amani kwani migongano ya mataifa makubwa yameleta machafuko na maangamizo makubwa duniani. Katika shairi hili, mshairi anabainisha uhasama na machafuko ya kisiasa duniani yanayosababishwa na viongozi.

Kulingana na Nadharia ya Ubidhaaishaji wa lugha, lugha inayochukuliwa kuwa yenye faida katika jamii huenea. Lugha ya Kiswahili ilitumiwa kuelezea sifa za viongozi bora

huku ikikashifu viongozi wabaya. Matokeo yake ni kuwa lugha ya Kiswahili ilienea kote nchini Tanganyika.

5.3.6 Uzalendo

Suala la uzalendo limeshughulikiwa na Akilimali (1963) katika shairi "Kila Ndege na Tundule." Mshairi anatumia jazanda ya ndege kuashiria mwenyeji wa lugha fulani na tundu kurejelea lugha asilia. Anaeleza kuwa, hata lugha iwe nzuri namna gani lakini ni ya kigeni, haiwezi ikampendeza mtu aliye na lugha yake asilia. Anasisitiza kuwa, kwa mtu aliye na lugha yake, lugha nyingine ni karaha. Lugha ya kigeni haimpi raha na uhuru wa kujieleza. Anaionea fahari lugha yake ya asili. Mwenyeji wa lugha hata akapewa maneno tofauti hatapenda kuyatumia kwani ni lugha ya kuazima siyo yake. Huweza kutoa sauti nzuri akaimba kwa lugha yake mpaka akasifika nyumbani kwao. Akitumia lugha ya kigeni huwa kama yatima asiye na kwao yaani asiye na lugha yake ya asili. Katika ubeti wa tano mshairi anasema:

> Tundu jingine uchuru, ndege hataita mama,
> Ndege hawi na uhuru, ndege hapati karama,
> Japo atajikusuru, hasikiziki kalima,
> Kila ndege na tundule, tundu jingine karaha (Akilimali, 1963: 20).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kwamba, lugha geni si ya mama na ni kama adui kwa sababu inamnyima uwezo wa kuomba hata akijilazimisha kwa taabu, kauli yake haieleweki. Anasisitiza kuwa, kila mtu ana lugha yake asilia inayompendeza lakini lugha zingine ni shida. Kwa jumla, hata wakalazimishwa kuitumia, marafiki wanapata taabu kwani hawasikilizani. Katika ubeti wa saba mshairi anasema:

> Rabi naomba kabuli, tujalie heri njema,
> Tuzidishe ikibali, tujifunze taaluma,
> Tuishi na Kiswahili, lugha ngeni kuzitema,

> Kila ndege na tundule, tundu jingine karaha (Akilimali, 1963: 20).

Katika ubeti huu, mshairi anamwomba Mungu akubali maombi yao awajalie heri njema. Awazidishie ukubalifu ili waweze kujifunza taaluma ya Kiswahili na kuachana na lugha za kigeni. Katika shairi hili, mshairi anadhihirisha mapenzi yake kwa lugha ya Kiswahili; lugha yake ya asili. Anabainisha kuwa, lugha ya Kiswahili ndio njema na haiwezi kulinganishwa na lugha nyingine za kigeni.

Suala la uzalendo linadhihirika pia katika shairi "Kila Mdharau Chake" ambapo Akilimali (1963) anaonya anayedharau lugha yake kuwa ataangamia. Amelaaniwa kwa kukidharau, kukikana na kukitupa kilicho chake na kupendelea cha mwingine. Inaelekea mshairi anarejelea anayedharau lugha yake ya asili hasa Kiswahili. Anaendelea kueleza kuwa, mtu asiringe na kujivuna kwa kutumia lugha ya mwingine kwa sababu anajiharibia jina na amelaaniwa na Mungu. Katika ubeti wa tatu mshairi anasema:

> Chako japo si cha mana, kibaya mtu ni chake,
> Kitunze na kukinena, na ukipe hadhi yake,
> Kisifu ukipe jina, kipambe na kipambike,
> Kila mdharau chake, kuzimu enda kuona (Akilimali, 1963: 21).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kwamba, hata kama lugha yako ya asili (Kiswahili) haina maana, bado ni yako. Kwa hivyo, mwenyeji anastahili aitunze, ainene na aipe hadhi yake. Pia, anastahili aisifu na kuipamba lugha yake. Anasisitiza kuwa, anayedharau lugha yake ataangamia. Kila lugha ina hadhi yake, iwe ya Kiingereza au ya Kiswahili na katu haiwezi kufanana na nyingine. Hivyo, mtu hafai kudharau lugha yake. Mshairi anawaomba watu wadumishe Kiswahili na kukipa hadhi yake wasije

wakapata laana kutoka kwa Mungu. Katika shairi hili, mshairi anaisifu na kuitetea lugha yake ya Kiswahili ili idumishwe na kupewa hadhi yake.

Aidha, katika shairi "Kiswahili", Akilimali (1963) anaendelea kuisifu lugha ya Kiswahili. Anaeleza kuwa, Kiswahili ni lugha yake ya asili aliyoizungumza tangu utotoni hadi utu uzima. Anaipenda kwa sababu ni tamu kama zamaradi. Pia, mshairi anajieleza vizuri bila hofu kwa kuwa ana ufasaha wa lugha. Katika ubeti wa tatu anasema:

> Ingawa najitahidi, kujifunza kila somo,
> Lugha za kila biladi, ni kwa kutafuta chumo,
> Bali sipati muradi, ila naambua zumo,
> Ni bure yangu juhudi, kusema sipati kimo! (Akilimali, 1963: 27).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kwamba, ingawa anajitahidi kujifunza na kusoma lugha za nchi zingine, hafanikiwi. Yeye hufanya hivyo apate pato ila hapati matilaba yoyote. Mshairi anamalizia shairi lake kwa kuwaomba watu waondoe vikwazo vinavyozuia lugha ya Kiswahili kuenea nchini kote. Katika shairi hili, mshairi anaisifu lugha ya Kiswahili kwani hawezi kuilinganisha na lugha nyingine.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Utegemezi, ukoloni unahusu kusambaratisha ama kutothamini kwa makusudi utamaduni wa jamii. Washairi walisitisha utegemezi wa lugha za kikoloni kwa kuthamini na kutukuza lugha ya Kiswahili katika kazi zao.

Kwa upande mwingine, Robert (1966) anashadidia maoni ya Akilimali ya kuisifu na kuitukuza lugha ya Kiswahili. Katika shairi lake "Kiswahili", Robert anatumia sitiari ya "titi la mama" kubainisha utamu na uzuri wa Kiswahili tofauti na lugha nyingine. Katika ubeti wa tatu mshairi anasema:

Lugha yangu ya utoto, hata leo nimekua,
Tangu ulimi mzito, sasa kusema najua,
Sawa na manukato, moyoni mwangu na pua,
Pori, bahari na mto, napita nikitumia,
Titi la mama litamu, jingine halishi hamu (Robert, 1966: 27).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, Kiswahili ni lugha yake tangu utotoni hadi utu uzima. Ni lugha anayoipenda ndiposa akaifananisha na manukato yanayopendeza. Anaitumia popote anapopitia kwa sababu ni tamu kuliko lugha nyingine. Ingawa lugha nyingine zinampa ujira anaelewa kuwa, mwacha mila ni mtumwa. Hawezi kujieleza vyema kwa lugha za kigeni tena akizizungumza anabezwa. Lugha ya Kiswahili ni nyepesi kutumia katika mawasiliano. Ni mojawapo ya lugha kuu duniani kwani haijapungua kwa chochote. Ni lugha inayokopa maneno sawasawa na lugha zingine duniani. Hata hivyo, inaweza kutumika kama lugha ya kufundishia. Umuhimu wake ni kuwa, hutumiwa kutoa taarifa katika mataifa mengi. Kwa hivyo, ikiwa itakufa watu wengi wataumia. Anaitumia kutungia mashairi yanayobeba mawazo yake. Hivyo, Kiswahili ni lugha muhimu sana kwake. Katika shairi hili mshairi anaisifu na kuitukuza lugha ya Kiswahili huku akidhihirisha umuhimu wake katika jamii.

Suala la uzalendo limeshughulikiwa pia na Mnyampala (1965). Katika shairi lake "Lugha Yetu Kiswahili", anaisifu lugha ya Kiswahili. Katika ubeti wa kwanza anasema:

Siachi kuisifia, lugha yetu Kiswahili,
Wewe twajivunia, twaitumia kuwili,
Kama wali na samli;
Samli wali kitia, utadharau ugali,
Asokula hujutia, moyonimwe umdhili,

> Lugha yetu Kiswahili, twazama na kuibuka (Mnyampala, 1965: 123).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kwamba, ataisifu na kujivunia lugha ya Kiswahili. Anaifananisha na wali uliotiwa samli kwa kuwa ni lugha tamu. Wasioitumia hujuta kwani ina manufaa mengi. Kiswahili ni lugha njema katika mawasiliano hasa kwa wageni. Tena, inatumiwa shuleni, bungeni na katika biashara. Kadhalika, Kiswahili hutumika kama lugha ya kufundishia masomo ya kiufundi. Aidha, hutumiwa katika dini hasa kwa kusali. Kwa hivyo, Kiswahili ni lugha yenye majukumu mengi katika jamii.

Fauka ya hayo, Mnyampala (1965) anaendelea kusifu lugha ya Kiswahili katika shairi "Kimefuzu Kiswahili". Mshairi anaeleza furaha aliyonayo kwa Kiswahili kuteuliwa kitumike katika Baraza kuu. Hivyo, anapendekeza washerehekee na wailinde kama tumbuu. Katika ubeti wa tano anasema:

> Tuisomee Juzuu, sala zote kila hali,
>
> Tumepanda kisuguu, lugha yetu tuijali,
>
> Itembee kwa miguu, toka hapa hadi mbali,
>
> Kwa kufuzu Kiswahili, wananchi tumefurahi (Mnyampala, 1965: 155).

Katika ubeti huu, mshairi anapendekeza Kiswahili kitunzwe na kiombewe kiweze kuenea kote nchini. Mshairi anaendelea kueleza kuwa, lugha nyingine hazifai kwani hawawezi kujieleza vilivyo hata wanapotosha kauli kwa kutozijua vyema. Anamalizia shairi kwa kuwaomba Watanganyika waendelee kutumia methali, simo na vitendawili vya Kiswahili; lugha yao iliyo tamu. Katika shairi hili, mshairi anaisifu na kuitukuza lugha ya Kiswahili.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Utegemezi, Waafrika wanapaswa kutetea na kudumisha utamaduni na lugha yao ili kuondoa utegemezi wa lugha za kikoloni. Watunzi wa mashairi walitetea lugha ya Kiswahili kwa kuisifu na kuitukuza huku wakisitisha

utegemezi wa lugha za kikoloni katika mawasiliano. Jambo hili lilieneza lugha ya Kiswahili kote nchini.

Abedi (1954) ameshughulikia suala la uzalendo kupitia shairi lake "Uhuru jambo Halisi". Katika shairi hili anadhihirisha mapenzi kwa nchi yake inayotawaliwa na mkoloni anayewanyima uhuru. Anaeleza kuwa, nchi ikiwa nzuri lakini wananchi wakose uhuru, huwa na taabu sana. Watu wote wakubwa kwa wadogo huhitaji uhuru kwani ni kipawa kutoka kwa Mungu. Wakoloni wanawalaghai ili wapate kuwatawala na kuwakandamiza ndiposa akasema "mwenye nguvu anasubu, mnyonge hana nafasi." Ingawa wakoloni wameelimika, elimu yao haiwafaidi kwani hata katika kanisa hakuna usawa. Wakoloni wanaendeleza ubaguzi wa rangi kwani Mwafrika akifanya makosa anaadhibiwa vikali tofauti na mkoloni. Waafrika wanadharauliwa kwa matusi kama mahabusu katika nchi yao. Katika ubeti wa nane mshairi anasema:

> Nchi hii mahabubu, haki ni nchi ya sisi,
> Vile kuwapa karibu, sisi tumekuwa fisi,
> Sasa ni kheri kilabu, wapendwa kuliko sisi,
> Uhuru jambo halisi, kuukosa ni taabu (Abedi, 1954: 99).

Katika ubeti huu, mshairi anakiri kuwa, anaipenda nchi yake kwa sababu ana haki ya kuishi. Hata hivyo, wamekuwa waoga kama fisi kwa wakoloni kuwepo nchini. Hivyo, angependa wapate uhuru kwani wakiukosa watapata shida. Mshairi anabainisha uzalendo kwa taifa lake. Anaendelea kueleza kuwa, mtu anapotawaliwa akili na kunyamazishwa hawezi kuendelea kwani huwa mwoga. Anawaomba Watanganyika waungane waweze kupigania uhuru. Ana matumaini kuwa siku moja watakuwa huru. Katika shairi hili, mshairi anadhihirisha uzalendo kwa nchi yake kwa kuwa tayari kuipigania ipate uhuru.

Uzalendo kwa taifa ni suala linaloangaziwa na Akilimali (1963: 83) katika shairi lake "Lipende Taifa Lako". Mshairi anaeleza kuwa, mtu anapopenda taifa lake kwa dhati na kuisherehekea, hata yeye anasifika kwa kuwa mzuri. Anashauri kila mtu alipende taifa lake na alitumikie. Mtu anapopenda taifa lake anazingatia hadhi yake kwa kuiona kama ngome madhubuti. Pia, handanganyi watu kwamba, anapenda taifa kwani huo ni unafiki. Anawashauri watu wasiogope kifo kwa ajili ya taifa. Vilevile, wazingatie umoja kwa sababu ni muhimu unashinda hata kito cha thamani. Anatahadharisha watu wasikubali kukashifu taifa lao hata wakipigwa au kubadili taifa kwa mali heri hata wafe. Anawahimiza wapiganie taifa lao kwa kuwa wanateswa na wageni kwani hata wakifa watasifika kwa kujitolea kwao. Kuifia nchi yako ni sawa na kwenda peponi. Anahitimisha shairi kwa kusema kwamba, upendo ni kama utabibu kwani huleti madhara yoyote. Katika shairi hili, mshairi anawahimiza watu wapende taifa lao na kujitolea kulipigania na kulitumikia.

Kulingana na Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, lugha hutumiwa na watu kulingana na mahitaji ya jamii iliyokusudiwa. Washairi walitumia lugha ya Kiswahili kubainisha umuhimu wa uzalendo kwa taifa la Tanganyika. Hivyo, kupitia kwa ushairi lugha ya Kiswahili ilienea kote nchini.

5.3.7 Mchango wa Chama cha TANU katika Kuunganisha Wananchi

Kandoro alikuwa mmoja wa watu kumi na saba walioanzisha chama cha TANU (Kandoro 1966: 146). Hivyo, aliwahimiza Waafrika waungane ili kutetea uhuru wa Watanganyika. Katika shairi "Waafrika Njooni", Kandoro (1966) anawaita Watanganyika wajiunge na chama cha TANU. Anawasihi wasikae ujingani lakini wafahamu chama chao ni kimoja tu na ni cha TANU. Anaeleza lengo kuu la chama hicho ni kuunganisha watu wa makabila tofauti ili wapiganie uhuru. Nchi ya

Tanganyika ikijitawala itatukuka duniani. Anawashauri watazame nchi ya Ghana inayojitawala na walinganishe na hali zao. Watu wanapotawaliwa hawana maendeleo kwani hawaelezi waongozwe kivipi wala hawaoni rasilmali zao zikitumiwa na wengine. Katika ubeti wa saba mshairi anasema:

> Mpeni nguvu mwenzetu, Bwana Nyerere mpeni,
> Mpenu umoja wenu, umoja wenu mpeni,
> Mkombozi wangu wenu, ututowe utumwani,
> Waafrika njoni, njoni muandike TANU (Kandoro, 1966: 140).

Katika ubeti huu, mshairi anawashauri Watanganyika wamuunge mkono Bwana Nyerere kiongozi wa TANU. Anamchukulia Nyerere kuwa mkombozi ambaye angewatoa utumwani mwa mkoloni kutokana na uongozi wake bora. Hivyo, anasisitiza kuwa, Watanganyika wanastahili wajiunge na chama cha TANU. Anamalizia shairi kwa kuwahimiza wapiganie uhuru. Katika shairi hili, mshairi anadhihirisha umuhimu wa Watanganyika wa kujiunga na chama cha TANU ili kupigania uhuru wao.

Mnyampala (1965) anasifu chama cha TANU kutokana na ushindi wake katika uchaguzi kwenye shairi “Kura Tumezifagia”. Mshairi anaeleza kuwa, lisije likaonekana kama jambo ndogo chama cha TANU kushinda kwa kura tatu na kupata wawakilishi serikalini. Wapinzani kutoka vyama vingine vya kisiasa vya Wahindi na Wazungu walishindwa. Mshairi ana matumaini kuwa hata katika uchaguzi mwingine chama cha TANU kitashinda. Anawaeleza Watanganyika kwamba, watajionea waliyoahidiwa kuwa TANU ingeshinda bila kuguna. Anawaeleza kuwa, wanachama hawangesinzia au kulala ndipo wakapata mwamko mpya wa kutia bidii zaidi ili wawe washindi. Katika ubeti wa nane mshairi anasema:

> Kaditama kuonyana, na kudai uhuria,

Uhuru wenye kufana, ambao twatazamia,

Na tushukuru sana, Mungu akitujalia,

TANU imezifagia, kura tatu kazi bure (Mnyampala, 1965: 32).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, amemaliza kuonya watu na sasa anadai uhuru ambao wanatazamia. Watashukuru Mungu sana akiwajalia uhuru. Anasisitiza kuwa, chama cha TANU kimeweza kujishindia kura tatu kwa urahisi. Katika shairi hili, mshairi anabainisha mafanikio ya chama cha TANU kwa kushinda kura tatu. Pia, anadhihirisha matarajio yake kuwa, chama cha TANU kitakuwa chombo cha kudai uhuru.

Robert (1966) anawaomba Watanganyika wajiunge na chama cha TANU. Katika shairi "Chama cha Waafrika", anaeleza kuwa watu wanapaswa waungane kama wanataka kujitawala. Tanganyika ina chama ambacho kingeweza kutumika kuwaondolea dhiki zilizowakumba. Kila mtu anaombwa ajiunge na Chama cha Waafrika ambacho kingetumika kuelezea wakoloni matakwa yao. Waafrika wangefanikiwa ikiwa wangekuwa na umoja katika kutetea haki zao. Katika ubeti wa saba mshairi anasema:

Shime Waafrika, kutafuta mwangaza,

Fahamuni mashaka, daima yatufingiza,

Vyama vingine kushika, siwezi kukataza,

Ila cha Waafrika, nakiona ni kikuza (Robert, 1966: 10).

Katika ubeti huu, mshairi anawahamasisha Watanganyika wapiganie haki zao wajiondolee mashaka. Mshairi anaeleza kwamba, hawezi kuwakataza kujiunga na vyama vingine ila kile Chama cha Waafrika anakiona kuwa bora. Mshairi anamalizia shairi lake kwa mwito kwa Watanganyika wote kutimiza wajibu wao na kujiunga na Chama cha Waafrika. Katika shairi hili, mshairi anawahimiza Watanganyika wajiunge na Chama cha Waafrika ili waweze kupigania uhuru.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Utegemezi jamii inayonuia kujikomboa kutokana na ukoloni haina budi kutumia lugha moja ya kuwaunganisha watu ili kuwa na umoja kwa lengo la kuleta ukombozi. Lugha ya Kiswahili ilikuwa lugha ya mawasiliano katika shughuli za chama cha TANU. Kiswahili kilitumika kuwahimiza Watanganyika wajiunge na chama cha TANU na washirikiane katika harakati za ukombozi. Hivyo, kupitia mashairi, lugha ya Kiswahili ilienea.

5.3.8 Madaraka ya Kujitawala

Mnyampala (1965: 131) anaelezea furaha aliyokuwa nayo nchi ya Tanganyika ilipopata madaraka tarehe kumi na moja, mwezi wa Oktoba. Katika shairi "Siku ya Historia", anaeleza kuwa, ataikumbuka siku ambayo nchi yake ilipiga hatua ikikaribia kupata uhuru. Waliitazamia siku ya kupata madaraka kwa sababu gavana alikuwa amewaahidi. Walikuwa wamezuiwa hivyo, wananchi walipigania madaraka hayo lakini kwa sasa wamefanikiwa. Waliitarajia nchi yao kuwa huru mwaka uliofuata. Wangetundika bendera yao na kutungua ya wakoloni na kuiweka sandukuni. Uchungu waliokuwa nao ulikuwa umekwisha kwa sababu wangejitawala. Mshairi anawahimiza Watanganyika wafanye kazi mashambani kwani wangepata fanaka kwa kujichumia mali. Kwanza, mwezi wa Oktoba walikuwa na nguvu kwa sababu hakukuwa na wakuwazuia. Nchi ya Tanganyika ilikuwa inaheshimika kwa kuwa na kiongozi bora aliyewaunganisha watu wote. Nchi ilisifika Ulaya hata India. Mshairi ana matumaini kuwa, hawangemaliza mwaka bila kujipatia uhuru. Katika shairi hili, mshairi anadhihirisha matumaini ya Watanganyika ya kupata uhuru baada ya kuwa na madaraka.

Aidha, katika shairi "Ni Madaraka Kamili", Mnyampala (1965: 139) anasherehekea kupatikana kwa madaraka kamili. Anamshukuru Mungu kwa kuwapa kiongozi wasiendelee kunyanyaswa. Wameweza kuwashinda watawala waliowadhulumu na

kufurahi kwamba, hawatatawaliwa tena. Mshairi analiombea Baraza la Majilisi liweze kushamiri kwa sifa njema na busara. Anatamani mwezi wa Disemba ufike wabadili bendera ya mkoloni na kutundika ya Watanganyika. Migogoro yote ingeisha na nchi ingekuwa nzuri kama asali. Mshairi anaisifu nchi ya Tanganyika inayosifika kote duniani. Wananchi wanampenda rais wao Nyerere na wanamwomba Mungu amzidishie ukweli. Wanamwombea afya njema na ufanisi wa kila aina kwa sababu ni kiongozi stadi na mwema, mwenye bidii kwa maombi na kusali. Mshairi anatamani Disemba ifike haraka wapate uhuru kamili. Katika shairi hili, mshairi anabainisha furaha yake kwa nchi yake kupata madaraka kamili.

Suala la madaraka nchini Tanganyika linaangaziwa pia katika shairi "Mpya Sasa Tanganyika". Katika shairi hili, Mnyampala (1965: 97) anaeleza kwamba, nchi mpya imeumbika kwa hivyo, ana haki ya kufurahi kwani ya kale yametoweka. Mshairi anahimiza majirani wa Tanganyika wakazanie siasa njema ili Mungu awajalie madaraka. Anawaita watu waje waone kuwa nchi yao iliyodharauliwa sasa inatukuka. Anawaonya majirani wasiwaonee wivu kwa sababu mambo yao yako shwari. Mshairi anaeleza kuwa, angeitungia shairi nchi yake ndio wale wako mbali wasikie kwamba imepata madaraka. Anawaomba wajivunie na kuiombea nchi ya Tanganyika. Mshairi angependa nchi za Uganda, Kenya na Unguja zipate madaraka pia. Anaeleza kuwa nchi ya Tanganyika ilidharauliwa ndio maana Wadachi na Waingereza waliigombania waitawale lakini sasa ni nchi mpya. Tanganyika ilibaki nyuma ikilinganishwa na Nyasa na Rhodesia lakini sasa ina hadhi yake. Anamwomba Mungu amzidishie umri Bwana Nyerere kwa kuokoa Tanganyika. Anawahimiza Watanganyika waitikie mwito wa Nyerere wa kushangilia Tanganyika. Anahitimisha shairi kwa kuwashauri Watanganyika kuungana mpaka wapate uhuru kamili. Katika shairi hili, mshairi

anabainisha furaha yake kwa Tanganyika kupata madaraka na kutangulia nchi nyingine za Afrika Mashariki.

Vilevile, katika shairi “1960 Madaraka Tumebeba” suala la madaraka limefafanuliwa. Mnyampala (1965: 91) anaeleza kuwa, huu ndio mwaka wa kumpamba Nyerere kwa sababu ni kipenzi chao. Amewaongoza vyema mpaka wakapata madaraka na kilichobaki ni uhuru kamili. Alisikiliza hotuba alipokuwa Lejiko ilipotangazwa kuwa, wangepewa madaraka ndipo akafurahi sana. Safari ya kutafuta madaraka ilikuwa ya shida lakini sasa yote yamekwisha. Watanganyika walikuwa na katiba yao ambayo ingewaongoza na mambo yanayohusu dhuluma na ukiukaji wa haki yalikuwa yamefika mwisho. Anawashauri Watanganyika waanze kulima mapori ili wapate chakula cha kutosha na wastawishe masoko ya mazao yao. Nchi ingepata utajiri kutokana na kilimo na shaba. Kwa hivyo, nchi ingetukuka. Anamalizia shairi kwa kuwataka wananchi washukuru Nyerere kwa mchango wake. Pia, wananchi washangilie kwa kuwa hawangehangaika tena. Katika shairi hili, mshairi anadhihirisha furaha waliokuwa nayo Watanganyika kwa kupata madaraka huku wamengoja uhuru kamili.

5.3.9 Sifa kwa Kiongozi Nyerere

Nyerere alikuwa kiongozi wa chama cha TANU kilichopigania uhuru nchini Tanganyika**.** Mnyampala (1965: 102), anamsifu Nyerere na kumtakia mema. Katika shairi “Twaomba Ubarikiwe”, mshairi anamwombea Nyerere na jamii yake wabarikiwe. Mshairi anatanguliza utungo wake kwa kulishukuru gazeti la *Kiongozi* kwa kuwafahamisha waziwazi familia ya Nyerere. Anamtaja Nyerere kama kiongozi mwenye huruma aliyetaka Watanganyika waokolewe. Anamwombea abarikiwe na afanikiwe maishani. Anamtambua Mama Maria kwa kuwa mwangalizi na mlezi mwema nyumbani kwake. Hivyo, anastahili kuheshimiwa na kuombewa kheri njema.

Andrea ni kifungua mimba wa Nyerere anayefaa kupewa madaraka. Bi. Anna anaombewa asipate matatizo yoyote na asichukiwe na mtu. Alselmi anaombewa akue vyema, John apate elimu aweze kuyafumbua mafumbo na Karoli afanikiwe. Mshairi angependa pasitokee mtu mbaya au mwongo wakuwaliza machozi watoto wa Nyerere. Anamlaani mtu wa tabia kama hiyo. Anapomalizia shairi lake, anaiombea jamii yote ya Nyerere iongezewe maisha na ifaulu katika shughuli zao. Tena, anampongeza Nyerere kwa kulinyanyua taifa lao. Katika shairi hili, mshairi anabainisha mapenzi yake kwa Nyerere kwa mchango wake nchini Tanganyika. Hivyo, anaomba Mungu ambariki pamoja na familia yake.

Fauka ya hayo, Mnyampala (1965: 137) anamsifu kiongozi Nyerere katika shairi lake "Mungu Mwongoze Rubani" kwa kutumia sitiari ya rubani kuashiria kiongozi Nyerere. Katika shairi hili, mshairi anaeleza kuwa, wanakaribia kupata uhuru licha ya matatizo waliyoyapata. Nyerere alikuwa kiongozi mwema aliyesimama imara. Watanganyika walimwamini kama kiongozi wao ambaye angeongoza safari ya kupigania uhuru mpaka ikamilike salama. Waliyapitia mengi ambayo yangewakwamiza njiani lakini hakuna jambo lingewapepesuka pembeni. Ijapokuwa walipigania uhuru, hakuna mtu aliyeumia na damu haikumwagika. Ingawa kiongozi Nyerere hakugombea uongozi, hakuna mtu hata mmoja aliyediriki kumpokonya uongozi. Watu wote walijiweka kando na kungoja awaongoze. Katika ubeti wa nane mshairi anasema:

> Rubani wetu tukuka, akujalie Manani,
> Maisha kuongezeka, Nyerere mwenye hisani,
> Iongoze Tanganyika, nakutilia ubani,
> Tumbwi letu la Rubani, lasogea ukingoni (Mnyampala, 1965: 137).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kwamba, hatachoka kumwombea Nyerere hadi wapate uhuru na kutundika bendera ya nchi yao mlingotini. Jambo hili litawafurahisha wananchi wote. Anamalizia shairi kwa kuwaomba wananchi washirikiane la sivyo hawangefanikiwa. Katika shairi hili, mshairi anamsifu Nyerere kwa uongozi bora.

Isitoshe, katika shairi "Duri Nadawiri Zari", Mnyampala (1965) anamsifu Mheshimiwa Nyerere. Mshairi anaeleza kuwa, siku ya uhuru tarumbeta zitavumishwa na bendera kupangwa na askari huku wananchi wakisherehekea. Pia, kiongozi Nyerere ataheshimika kwa kupambiwa taji sawa na Watemi mashuhuri. Nyerere amekumbana na matatizo mengi na kushambuliwa na maadui lakini aliweza kuwashinda. Kwa hivyo, anapambiwa taji la heshima na hilo linajulikana mjini Ujiji na kote nchini. Waimbaji maarufu wangemsifu kwa nyimbo waziwazi vitongojini hadi mjini huku wameandamana na watunzi wa mashairi. Mshairi hawataki wajeuri wenye viburi wanaovunja sheria na amri lakini anataka watu wanaomwogopa Mungu. Nyerere ni hodari kama simba popote anapokwenda kwani amewashinda viongozi wengine kwa kazi yake njema. Katika ubeti wa nane mshairi anasema:

> Wageni nasi wenyeji, na sote tunakukiri,
> Wako mwema wongozaji, Mkuu wetu Waziri,
> Ombi letu twataraji, uzidishiwe umri,
> Duri nadawiri zari, apambwe Mheshimiwa (Mnyampala, 1965: 142).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, wageni na hata wenyeji wanakiri kuwa waziri wao mkuu alikuwa kiongozi mwema. Kwa hivyo, wanamwombea Mungu amzidishie umri. Anasisitiza kuwa, Mheshimiwa Nyerere anastahili kupambwa kwa taji linalopendeza. Mshairi anaeleza kuwa, Nyerere amepewa kipaji na Mungu cha kuweza kushindana na wanasiasa wengine. Ameweza kuwashinda kwa sababu ya ujasiri wake.

Mshairi anawaomba watu wamwombee heri adumu na asipate shari. Pia, aweze kuwa kiongozi aliyefaulu mwenye maarifa yaliyokithiri. Katika shairi hili, mshairi anamsifu kiongozi Nyerere kwa ushujaa na uongozi bora.

Kulingana na Nadharia ya Utegemezi, Waafrika wanapaswa kutetea na kudumisha siasa zao ili kuondoa utegemezi wa utawala wa kikoloni. Washairi wa Kiswahili walimtukuza na kumsifu Nyerere kutokana na mchango wake katika harakati za kupigania ukombozi wa nchi ya Tanganyika.

5.3.10 Hamu ya Kupata Uhuru

Abedi (1954: 98) anadhihirisha hamu ya kupata uhuru katika nchi ya Tanganyika. Katika shairi "Uhuru Jambo Halisi", Mshairi anasisitiza umuhimu wa uhuru na kuukosa ni taabu. Anasema hata tundu liwe la dhahabu na lenye milango iliyotengenezwa kwa mbao za mpingo, ndege akiwa ndani na kufanywa mahabusu huiona adhabu. Mshairi anatumia jazanda ya tundu na ndege kumaanisha kuwa mtu akifanywa mahabusu katika nchi yake hukosa raha na hutaka kuwa huru. Uhuru ni kipaji kutoka kwa Mungu kwa watu wote. Mshairi anaeleza kwamba, wakoloni waliwalaghai wakawafilisi na kushika uongozi huku wanafanyizwa kazi za kuwalinda. Hali ya utumwa haijaisha kwa sababu bado wanateswa na wenye nguvu yaani wakoloni na ukilalamika unazidishiwa shida. Elimu waliyoitoa ni ya bure kwani ni ya kupumbaza umma. Usawa umepotea hata ndani ya kanisa. Mwafrika anabaguliwa na Wazungu kupendelewa. Waafrika wanadharauliwa na kujibiwa kwa maneno ya matusi. Nchi hii ya Waafrika ni nzuri lakini Waafrika wanachukuliwa kama fisi. Waafrika wametawaliwa akili kwa sababu hawapewi nafasi ya kujieleza lakini wanaendelea kunyanyaswa. Waafrika wamekuwa kama wageni katika nchi yao na kuwa na woga kama fisi. Mshairi angependa Waafrika waungane upesi ili wapiganie haki. Viongozi wenye ustadi wa kuhutubu wajieleze kwa

Wazungu kwamba, wanataka uhuru. Mshairi ana matumaini kuwa, kuna siku itafika wananchi wajitawale na dhiki na wasiwasi zifike mwisho. Katika shairi hili, mshairi anabainisha matatizo wanayoyapata Waafrika kama vile ubaguzi, ukiukaji wa haki na unyanyasaji. Anatamani wapate uhuru ili matatizo yao yaishe.

Pia, katika shairi "Kiwakacho Huzimika", Abedi (1954) anamwomba Mungu awajalie uhuru. Katika shairi hili, mshairi anaeleza kuwa, ana huzuni na roho yake inataabika lakini anaamini kuwa kila jambo lina mwisho wake. Amepata huzuni hata vitamu vimekuwa chungu kwa kufikiri sana akipanga na kupangua. Anashangazwa na jinsi wanavyodhulumiwa. Mshairi anaeleza kuwa, waovu wako huru lakini wao ni wema na wamefungiwa. Anawaeleza wakoloni kuwa hawatalipiza kisasi mbali watamwomba Mungu awasaidie. Mshairi anamwomba Mungu amsamehe dhambi na kujibu maombi yake. Anaamini kuwa, Mungu ni mwenye nguvu na hakuna asiloliweza kwa hivyo, atamzidishia wema wake. Katika ubeti wa mwisho anasema:

> Nalia naomboleza, Rabi Muweza sikia,
> Nikuambayo timiza, ya Huru msafi nia,
> Ambaye atanipoza, na fani zote kujua,
> Kiwakacho huzimika, na ina mwisho dunia (Abedi, 1954: 104).

Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kuwa, anamlilia Mungu anayeweza yote amtimizie maombi yake ya kupata uhuru. Kwa kupata uhuru, atatulia na kuendelea na kazi yake vyema. Anaamini kila jambo lina mwisho wake. Katika shairi hili, mshairi anadhihirisha hisia zake kutokana na unyanyasaji. Mshairi anamwomba Mungu awajalie uhuru ili waishi maisha mema.

Isitoshe, katika shairi "Uhuru Uwe wa Kheri", Abedi (1954: 144) anabainisha hamu na matumaini ya Watanganyika ya kupata uhuru. Anasisitiza kuwa angependa uhuru uwe

wa kheri na udumu kwa amani. Mshairi anamwomba Mungu awaondolee unyanyasaji kwa kuwa ni mwenye uwezo ili Tanganyika iwe shwari na wanawake na wanaume wote watashangilia. Pia, anamwomba Mungu awaondolee majuto Tanganyika iweze kukua na kuwa huru. Anaeleza kuwa uhuru wameupata bila shida na kwa upole pasipokuwa na vita. Anamsifu kiongozi Nyerere kwa kutokuwa mkali ama mjeuri bali amefaulu kutokana na umahiri wake. Mshairi angependa kusitokee mizozo ama wageni kupokwa mali kwani wangehatarisha maisha kwa ubaradhuli wao. Anawashauri Watanganyika wasiwe na kiburi na kufoka kama fahari lakini wawe na heshima; wawe watu mashuhuri. Pia, wasiwe majahili kama watu wa Kongo kwa sababu si halali. Aidha, mshairi anawashauri wajiepushie ajali za barabarani na wajihadhari yasizuke machachari. Walakini, wawe watu wenye akili wanaowasifu mawaziri waliowaongoza katika safari ya kutafuta uhuru. Anamalizia shairi kwa matumaini kuwa, watafaulu daima. Mambo yamekuwa dhahiri kwa sababu serikali mpya imeundwa. Katika shairi hili, mshairi anabainisha kuwa uhuru umepatikana ndipo akasema “uhuru umewasili, pasipokuwa na dosari” lakini unastahili udumu kwa amani.

Kulingana na Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha, lugha hutumiwa na watu kulingana na mahitaji ya jamii iliyokusudiwa. Washairi walitumia lugha ya Kiswahili kubainisha hamu waliyokuwa nayo ya kupata uhuru wa Tanganyika. Hivyo, kupitia kwa ushairi lugha ya Kiswahili ilienea kote nchini.

Mnyampala (1965: 136) anadhihirisha hamu ya kupata uhuru nchini Tanganyika. Katika shairi “Mungu Zidisha Uhai”, anamwomba Mungu awazidishie uhai ili waione siku ya uhuru. Anaeleza kuwa Waswahili wote wanafurahi kwa sababu nchi ya Tanganyika imetoka katika shida. Anamshukuru Mungu kwa wema wake na kumwomba awaruhusu wawe na uhuru. Wanaingojea kwa hamu siku njema matumaini yao yatakapotimizwa

watu wote wafurahi. Dhuluma na vitisho vitakuwa vimeisha kwa sababu watakuwa wamepata walichokipigania kwa muda. Anaeleza kuwa, tarehe moja, mwezi wa Mei imewasili na udhalili umeisha. Sasa wanangojea Disemba wabadili bendera ya mkoloni na kuitundika ya Watanganyika. Watakapopata uhuru kamili mwezi wa Disemba watarukaruka kwa furaha. Anawashauri Watanganyika waimbe nyimbo kwa zumari washerehekee kila sehemu nchini. Pia, anawaeleza wasali wasipate huzuni na wamwombee kiongozi Nyerere awe hai mpaka mkoloni aondoke nchini mwao. Udhalimu utakuwa umeisha na watu wa jamii zote watafurahi. Katika shairi hili, mshairi anadhihirisha hamu ya Watanganyika ya kupata uhuru.

5.4 Hitimisho

Sura hii imechunguza harakati za upiganiaji uhuru na jinsi zilivyochochea mabadiliko ya maudhui katika ushairi wa Kiswahili. Uchunguzi umeonyesha kuwa washairi wengi wa wakati wa ukoloni walikuwa wanasiasa walioongoza vyama vya kisiasa. Pia, kuna mashairi ya kisiasa yaliyotungwa na washairi wasiokuwa wanasiasa. Hivyo, washairi hawakujitenga kisiasa kwani kuna wale walioshiriki au kuandika kuhusu harakati za ukombozi wa Watanganyika. Vyama vya kisiasa vilitumia lugha ya Kiswahili kama chombo cha kuwaunganisha Watanganyika kisiasa. Uchapishaji wa mashairi katika magazeti ulikuwa jambo la kawaida ili kuhamasisha na kuzindua watu wapiganie uhuru. Utunzi wa mashairi kwa Kiswahili sanifu ulichangia maenezi ya Kiswahili kote nchini Tanganyika. Mashairi yalibeba maudhui mbalimbali yakiwemo: dhuluma za kikoloni, utetezi wa haki, umoja na ushirikiano wa Waafrika, kupigania utamaduni wa Waafrika, sifa za viongozi bora, uzalendo, chama cha TANU chaunganisha wananchi, madaraka ya kujitawala, sifa kwa kiongozi Nyerere na hamu ya kupata uhuru.

Katika sura ifuatayo, muhtasari, matokeo, mchango na mapendekezo ya utafiti yalitolewa.

SURA YA SITA

MUHTASARI, MATOKEO, MCHANGO NA MAPENDEKEZO

6.0 Utangulizi

Katika sura iliyotangulia mtafiti alichunguza jinsi harakati za upiganiaji uhuru zilivyochochea mabadiliko ya kimaudhui ya ushairi wa Kiswahili nchini Tanganyika kati ya mwaka 1930 hadi 1960. Katika sura hiyo ilibainika kuwa, katika kipindi cha ukoloni washairi wengi walikuwa wanasiasa walioongoza vyama vya kisiasa na wengine waliandika mashairi ya kisiasa ingawa hawakuwa wanasiasa. Vyama vya kisiasa vilitumia lugha ya Kiswahili kuwaunganisha Watanganyika katika harakati za kupigania ukombozi. Mashairi yalichapishwa magazetini ili kuwahamasisha Watanganyika kupigania uhuru. Mashairi yalitungwa kwa Kiswahili sanifu, jambo lililoeneza lugha ya Kiswahili kote nchini Tanganyika. Mashairi yaliyotungwa yalibeba maudhui mbalimbali yakiwemo: dhuluma za kikoloni, utetezi wa haki, umoja na ushirikiano wa Waafrika, utamaduni wa Waafrika, sifa za viongozi bora, uzalendo, chama cha TANU, madaraka ya kujitawala, sifa kwa kiongozi Nyerere na hamu ya kupata uhuru.

Sura hii ililenga kujadili muhtasari wa tasnifu, matokeo ya utafiti, mchango wa utafiti, changamoto na mapendekezo ambayo yatachochea tafiti za baadaye.

6.1 Muhtasari wa Tasnifu

Katika tasnifu hii, utafiti amechunguza matukio yaliyochochea mabadiliko ya kimaudhui ya ushairi wa Kiswahili nchini Tanganyika kati ya mwaka 1930 hadi 1960. Katika sura ya kwanza, utangulizi wa tasnifu umetolewa na suala la utafiti limebainishwa ambalo ni kuchunguza matukio yaliyochochea mabadiliko ya kimaudhui ya ushairi wa Kiswahili nchini Tanganyika kati ya mwaka 1930 hadi 1960. Utafiti umebainisha jinsi uchunguzi huo ulifanywa kupitia Diwani za mashairi zifuatazo: *Koja*

la Lugha (1969), *Kielezo cha Fasili* (1968), *Masomo Yenye Adili* (1967), *Pambo la Lugha* (1966), *Mashairi ya Saadan* (1966), *Diwani ya Mnyampala* (1965), *Diwani ya Akilimali* (1963) and *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri* (1954). Malengo ya utafiti yamebainishwa ambayo ni:

1. Kueleza jinsi sera ya lugha ya kipindi cha ukoloni ilivyochochea mabadiliko ya kimaudhui ya ushairi wa Kiswahili nchini Tanganyika kati ya mwaka wa 1930 hadi 1960.
2. Kubainisha jinsi shughuli za Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki zilivyochochea mabadiliko ya maudhui ya ushairi wa Kiswahili nchini Tanganyika kati ya mwaka wa 1930 hadi 1960.
3. Kufafanua jinsi kanuni za utunzi wa mashairi zilivyochochea mabadiliko ya kimaudhui ya ushairi wa Kiswahili nchini Tanganyika kati ya mwaka wa 1930 hadi 1960.
4. Kueleza jinsi harakati za upiganiaji uhuru zilivyochochea mabadiliko ya kimaudhui ya ushairi wa Kiswahili nchini Tanzania kati ya mwaka wa 1930 hadi 1960.

Kadhalika, utafiti umejadili upeo na mipaka ya utafiti huu. Pia, utafiti umejadili yaliyoandikwa kuhusu mada ya utafiti ili kubainisha pengo lililotokana na tafiti za awali. Vilevile, utafiti umejadili misingi ya nadharia zilizoongoza utafiti huu ambapo mihimili ya Nadharia ya Utegemezi kama anavyoeleza Ngugi wa Thiong'o katika kitabu chake *Decolonising the Mind: The Politics of Language in African Litereture* (1986) imeelezwa. Aidha, mihimili ya Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha kama anavyoeleza Pierre Bourdieu katika kitabu chake *Language and Symbolic Power* (1991) imebainishwa. Isitoshe, utafiti ameeleza mbinu zilizotumiwa katika utafiti ambapo

imebainishwa kuwa, utafiti huu ni wa maktabani. Pia, sampuli iliteuliwa kwa kutumia mbinu kusudio. Uteuzi wa watunzi wa mashairi pamoja na diwani zilizoshughulikiwa ulifanywa kwa kutumia mbinu kusudio. Tena, maelezo kuhusu ukusanyaji wa data, namna data ilivyochanganuliwa na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo yametolewa.

Katika sura ya pili, utafiti umejadili dhana ya sera ya lugha na upangaji wa lugha. Pia, hatua za upangaji wa lugha zimeelezwa. Vilevile, utafiti umejadili sera ya lugha ya kipindi cha utawala wa Wajerumani kati ya mwaka 1895 hadi 1918 katika utawala na elimu. Aidha, utafiti umejadili sera ya lugha ya kipindi cha utawala wa Waingereza kati ya mwaka 1918 hadi 1961. Dhana ya maudhui katika ushairi imefafanuliwa. Utafiti umebainisha jinsi watunzi wa mashairi walivyoeleza sifa na umuhimu wa Kiswahili nchini Tanganyika katika mshairi yao. Isitoshe, utafiti umedhihirisha jinsi washairi walivyotumia ushairi kama chombo cha umma cha kujieleza.

Katika sura ya tatu, utafiti umejadili shughuli za Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki. Utafiti umeelezea shughuli za usanifishaji wa Kiswahili, mashindano ya uandishi na kuundwa kwa shirika la uchapishaji wa vitabu la EALB ili kubainisha athari yake juu ya ubunifu wa maudhui ya ushairi wa Kiswahili. Fauka ya hayo, utafiti umebainisha jinsi watunzi wa mashairi walivyohimiza utunzi wa mashairi, kutoa ushauri kwa watunzi wa mashairi, kuelezea umuhimu wa mashairi pamoja na kuelezea mchango wa washairi katika jamii

Katika sura ya nne, utafiti umefafanua maana ya ushairi kwa kuzingatia maoni ya washairi wa jadi. Pia, utafiti umejadili kanuni za utunzi wa mashairi kwa kuzingatia

mtazamo wa Amri Abedi kama anavyoeleza katika kitabu chake *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri* (1954). Aidha, utafiti umebainisha jinsi washairi walivyohimiza utunzi wa mashairi ya arudhi katika mashairi yao.

Katika sura ya tano, utafiti umebainisha jinsi harakati za upiganiaji uhuru zilivyochochea mabadiliko ya kimaudhui katika ushairi wa Kiswahili nchini Tanganyika kati ya mwaka 1930 hadi 1960. Utafiti umejadili jinsi vyama vya kisiasa vilivyobuniwa na matumizi ya Kiswahili katika shughuli za vyama hivyo. Pia, utafiti umebainisha matumizi ya ushairi kama chombo cha kisiasa. Utafiti umebainisha jinsi ushairi ulivyotumiwa kudhihirisha dhuluma za kikoloni, kutetea haki, uzalendo, umoja na ushirikiano wa Waafrika, kupigania utamaduni wa Waafrika, kuhimiza Watanganyika kujiunga na chama cha TANU, kusifu viongozi bora kama Nyerere na kuelezea hamu ya kupata uhuru.

Sura ya sita ni hitimisho la tasnifu. Hitimisho limetoa muhtasari wa kila sura. Maelezo yametolewa kulingana na malengo ya utafiti. Matokeo ya utafiti yametolewa kulingana na malengo ya utafiti. Hatimaye, sura hii imeeleza mchango, changamoto na mapendekezo ya utafiti ambao unaweza kufanywa katika siku za baadaye.

6.2 Matokeo ya Utafiti

Katika utafiti huu, utafiti ulidhamiria kutimiza malengo ya kueleza jinsi sera ya lugha ya kipindi cha ukoloni ilivyochochea mabadiliko ya kimaudhui ya ushairi wa Kiswahili nchini Tanganyika kati ya mwaka wa 1930 hadi 1960. Pia, utafiti ulilenga kubainisha jinsi shughuli za Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki zilivyochochea mabadiliko ya maudhui ya ushairi wa Kiswahili. Vilevile, utafiti ulilenga kudhihirisha jinsi kanuni za

utunzi wa mashairi zilivyochochea mabadiliko ya kimaudhui ya ushairi wa Kiswahili nchini Tanganyika. Aidha, utafiti ulilenga kueleza jinsi harakati za upiganiaji uhuru zilivyochochea mabadiliko ya kimaudhui ya ushairi wa Kiswahili nchini Tanganyika kati ya mwaka wa 1930 hadi 1960.

Kuambatana na lengo la kwanza, utafiti umebainisha namna sera ya lugha ilivyochochea mabadiliko ya kimaudhui katika ushairi wa Kiswahili nchini Tanganyika kati ya mwaka 1930 hadi 1960. Utafiti umebainisha kuwa, sera ya lugha nchini Tanganyika ilikuwa tofauti katika kipindi cha utawala wa Wajerumani na cha Waingereza. Wajerumani walitumia Kiswahili katika utawala na elimu. Walijifunza Kiswahili kabla ya kuja Tanganyika kama watawala. Waafrika walilazimika kujifunza Kiswahili ili wapate ajira ya ngazi ya chini katika serikali ya Mjerumani. Wawakilishi wa watawala yaani Akida, Jumbe na Liwali walitakiwa kujifunza Kiswahili. Kiswahili kilitumika kama lugha ya mawasiliano kati ya watu na kama lugha rasmi katika utawala wa wilaya. Hata hivyo, ujuzi wa lugha ya Kiingereza ulihitajika katika ajira ya ngazi ya juu. Wajerumani walianzisha shule zilizofundishwa kwa Kiswahili katika fani tofauti kama vile uashi na useremala. Pia, Waafrika wachache walifunzwa wapate kuhudumu katika utawala wa Kijerumani kwa kufanya kazi ndogondogo kama za ofisini, mahakamani na za ulinzi. Vitabu na magazeti ya Kiswahili yalichapishwa, jambo lililoeneza lugha ya Kiswahili kote nchini Tanganyika. Katika kipindi cha utawala wa Waingereza, Kiswahili kilitumika katika utawala wa wilaya na mikoa lakini Kiingereza kiliteuliwa kama lugha rasmi. Katika elimu, Kiswahili kilitumika kama lugha ya kufundishia shule za viwango vya msingi lakini Kiingereza kilitumika katika shule za sekondari na vyuo. Kiswahili kilipewa hadhi ya chini kwa sababu kilitumiwa na watu wa tabaka la chini. Kwa hivyo,

Watanganyika walikichukulia Kiswahili kuwa lugha ya hadhi ya chini na Kiingereza lugha ya hadhi ya juu ndiposa watunzi wa mashairi wakakitetea kwa kukitukuza na kukisifu katika mashairi yao.

Utafiti umebainisha kuwa, watunzi wa mashairi ya Kiswahili katika kipindi cha ukoloni walijitahidi kukuza Kiswahili. Walikisifu, wakakitukuza na kuelezea umuhimu wake kwa Watanganyika. Baadhi ya mashairi yaliyotungwa katika kipindi hiki yalibeba maudhui ya kutetea na kutukuza lugha ya Kiswahili na kuhimiza Watanganyika waikuze na kuieneza kote nchini.

Katika kushughulikia lengo la pili, utafiti umebainisha jinsi shughuli za Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki zilivyochochea mabadiliko ya kimaudhui ya ushairi wa Kiswahili nchini Tanganyika kati ya mwaka 1930 hadi 1960. Utafiti umeonyesha kwamba, nchi za Afrika Mashariki ziliungana na kuanzisha Kamati ya Lugha (ya Kiswahili) ya Afrika Mashariki ili kusanifisha na kuikuza lugha ya Kiswahili. Usanifishaji wa Kiswahili ulichochewa na hali ya kuwepo kwa lahaja nyingi za Kiswahili. Kulikuwa na haja ya kuwa na lahaja moja au lugha ambayo ingetumika kufundishia shuleni, kutumika katika maandishi na kueleweka na kila aliyekifahamu Kiswahili. Pia, kamati ililenga kuchapisha vitabu vya Kiswahili na kuhimiza uandishi kwa kuandaa mashindano ya insha na vitabu. Waandishi chipukizi walihimizwa na kusaidiwa kwa kuwachapishia kazi zao asilia. Aidha, kulibuniwa shirika la uchapishaji la EALB lililowafanya Waafrika wajitegemee katika uchapishaji wa tungo zao kwa Kiswahili sanifu.

Utafiti umebaini kuwa, kutokana na shughuli hizo za kamati, watunzi wa mashairi walihimizwa na kushauriwa kuendeleza utunzi wa mashairi. Hivyo, mashairi yalibeba

maudhui ya kuhimiza utunzi wa mashairi, ushauri kwa watunzi wa mashairi, umuhimu wa mashairi na mchango wa mshairi maarufu Shaaban Robert katika kueneza Kiswahili.

Kwa kuzingatia lengo la tatu, utafiti umechunguza jinsi kanuni za utunzi wa mashairi zilivyochochea mabadiliko ya maudhui ya ushairi wa Kiswahili nchini Tanzania kati ya mwaka 1930 hadi 1960. Utafiti umedhihirisha kwamba, mtazamo wa washairi wa jadi au wanamapokeo kuhusu maana ya ushairi unabainisha baadhi ya kanuni za utunzi wa mashairi. Kanuni hizo ni kuwepo kwa vina, mizani, kituo, muwala, urari, kutosheleza, kiini na lugha mwafaka. Baadhi ya kanuni hizo zilipendekezwa na kuelezwa na Abedi katika diwani yake: *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri* (1954).

Utafiti umebainisha kuwa, kulitokea msisimko wa utunzi wa mashairi yaliyozongatia kanuni za utunzi wa mashairi baada ya uchapishaji wa diwani ya Abedi (1954). Mashairi yaliyotungwa yalibeba maudhui ya kuhimiza utunzi wa mashairi ya arudhi.

Kuambatana na lengo la nne, utafiti umechunguza namna harakati za upiganiaji uhuru zilivyochochea mabadiliko ya kimaudhui katika ushairi wa Kiswahili nchini Tanganyika. Utafiti umedhihirisha kuwa, katika kipindi cha utawala wa Waingereza nchini Tanganyika, Waafrika walilalamikia ubaguzi na unyanyasaji kutoka kwa watawala. Waliunda vyama vya wafanyakazi na baadaye vyama vya kisiasa ili kutetea haki zao. Kiswahili kilitumika kama chombo cha mawasiliano na kama ugwe wa kuwaunganisha Watanganyika kote nchini. Chama cha TANU kilitumia Kiswahili kuwashawishi watu washiriki katika harakati za kupigania ukombozi.

Utafiti umebainisha kuwa, kuna uhusiano kati ya ushairi na siasa. Katika kipindi cha kupigania uhuru, kuna washairi wanasiasa waliotunga mashairi ya kisiasa. Tena, kuna washairi waliotunga mashairi ya kisiasa ingawa hawakuwa wanasiasa. Mashairi yaliyotungwa katika kipindi cha ukoloni yalibeba maudhui mbalimbali. Baadhi ya maudhui hayo ni dhuluma za kikoloni, utetezi wa haki, umoja na ushirikiano, kupigania utamaduni wa Waafrika, sifa za viongozi bora, uzalendo, mchango wa chama cha TANU katika kuunganisha wananchi, Madaraka ya kujitawala, sifa kwa Kiongozi Nyerere na hamu ya kupata uhuru.

6.3 Mchango wa Utafiti

Utafiti huu umechangia katika ufahamu wa utunzi wa utanzu wa fasihi unavyoathiri namna lugha ilivyo katika kipindi maalum cha wakati. Utafiti huu umedhihirisha kwamba, utunzi wa mashairi kwa Kiswahili sanifu katika kipindi cha ukoloni ulibainisha hadhi ya juu ya lugha ya Kiswahili. Kiswahili kilipewa hadhi ya juu kuliko lugha zingine za kienyeji kutokana na majukumu yake katika jamii kwa kutumika kama chombo cha umma cha kujieleza.

Kadhalika, utafiti huu umechangia katika kubainisha uhusiano kati ya utunzi wa mashairi na maenezi ya Kiswahili. Utafiti umebainisha kuwa, utunzi wa mashairi umechangia maenezi ya Kiswahili na uzalendo kwa sababu Kiswahili kilisifiwa kama lugha ya kuunganisha Watanganyika kote nchini. Washairi walikitetea na kukisifu Kiswahili katika mashairi yao huku wakieleza umuhimu wake katika jamii.

Aidha, utafiti umechangia katika kubainisha kuwa, masuala ya fasihi ya Kiswahili na historia ya lugha yanachangia usanifishaji wa lugha. Utafiti huu umedhihirisha kuwa,

Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki ilipoundwa katika mwaka wa 1930 ilihimiza uandishi wa vitabu vya Kiswahili. Waandishi wa Kiswahili wakiwemo washairi walitunga mashairi ya kuhimiza utunzi kwa Kiswahili sanifu. Hata msamiati wa Kiswahili ulipanuka kwa kuweka kamusi ndogo ya msamiati uliotumika katika Diwani zao kama vile Abedi (1954).

Kupitia kwa utafiti huu imebainika kuwa lugha ikiwa moja katika jamii inawasaidia wanajamii kutimiza mahitaji yake katika utawala, elimu na biashara. Utafiti huu umedhihirisha kuwa, lugha huwa kama bidhaa muhimu katika ‘soko’ au kwa hadhira iliyokusudiwa kutokana na majukumu inayochangia na kutimiza miongoni mwa wanajamii na mikakati yao ya kuendeleza maisha. Utafiti umebainisha kuwa, sera ya lugha ya kipindi cha ukoloni iliunga mkono matumizi ya Kiswahili nchini Tanganyika. Lugha ya Kiswahili iliteuliwa na wakoloni; Wajerumani na Waingereza kwa kuwa ilikuwa imeenea nchini Tanganyika tofauti na lugha zingine za kienyeji. Lugha ya Kiswahili ilitumika katika utawala wa mikoa, kutolea mafunzo ya kidini, kushughulikia kesi za Waafrika mahakamani na kama lugha ya kufundishia shuleni na vyuo vya kiufundi miongoni mwa matumizi mengine. Matokeo yake ni kwamba, watunzi wa mashairi walijitahidi kuikuza kwa kutunga mashairi kwa Kiswahili sanifu ili kubainisha hadhi yake.

6.4 Changamoto za Utafiti

Ugonjwa wa korona ulipozuka katika mwaka wa 2020, shughuli za masomo zilisimama kwa muda kwa sababu vyuo vikuu vilifungwa. Mtafiti hakuweza kuingia maktabani kusoma lakini alilazimika kusoma kwa mtandao tu. Hata hivyo, vyuo vikuu vilipofunguliwa mtafiti alipata nafasi ya kusoma katika maktaba za TATAKI, Chuo

Kikuu cha Kenyatta, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Pia, ilikuwa ni changamoto kupata magazeti yaliyoandikwa katika kipindi cha ukoloni maktabani ili kuchunguza ushairi ulioandikwa. Magazeti mengi yaliyopatikana yalikuwa na habari za kilimo na biashara mada ambazo hazikufaa utafiti huu. Hata hivyo, vitabu, majarida na tasnifu zinazohusiana na utafiti huu zilizopatikana maktabani zilisomwa. Ingawa matatizo haya yalisababisha kuchelewa kukamilika kwa kazi hii, mtafiti aliweza kukamilisha utafiti huu.

6.5 Mapendekezo ya Utafiti

Utafiti huu umezingatia matukio yaliyochochea mabadiliko ya kimaudhui ya ushairi wa Kiswahili nchini Tanzania kati ya mwaka wa 1930 hadi 1960. Hiki ni kipindi cha kabla ya uhuru wa Tanzania. Kwa hivyo, mtafiti anapendekeza kwamba, utafiti wa baadaye ufanywe kuhusu kipindi cha baada ya uhuru wa Tanzania. Aidha, tafiti zaidi zinaweza kufanywa kwa kuzingatia diwani zingine za watunzi walioteuliwa.

Kazi hii imeongozwa na mihimili ya Nadharia ya Utegemezi na Nadharia ya Ubidhaaishaji wa Lugha. Tafiti zaidi zinaweza kufanywa kwa kuzingatia nadharia hizo katika Diwani za watunzi wengine wa mashairi ya Kiswahili ili kuendeleza suala la mabadiliko na maendeleo ya maudhui ya ushairi wa Kiswahili. Pia, inapendekezwa na mtafiti kwamba, utafiti zaidi ufanywe kwa kuzingatia nadharia hizo katika tanzu zingine za fasihi.

Utafiti huu umezingatia kipengele cha maudhui katika ushairi uliotungwa katika kipindi cha ukoloni. Hivyo, tafiti zaidi zinaweza kufanywa kwa kuangazia masuala mengine kama vile mtindo katika ushairi wa kipindi cha ukoloni.

Isitoshe, tafiti zingine zinaweza kufanywa kuhusu athari ya Sera ya Lugha katika utunzi na uchapishaji wa vitabu ili wachapishaji wawe na uelewa wa lugha ya kuzingatia katika utunzi kwa sababu sera ya lugha huathiri maenezi ya lugha. Pia, utafiti utazifaidi taasisi zinapofanya maamuzi kuhusu upangaji wa lugha nchini.

MAREJELEO

Abdalla, A. (1973). "Taaluma ya Lugha ya Kiswahili" katika Makala ya Kongamano la Chama cha Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Haijachapishwa).

Abdulaziz, M. H. (1979). *Muyaka: 19th Century Swahili Popular Poetry*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Abdulaziz, M. H. "Tanzania's National Language Policy and the Rise of Swahili Political Culture" katika Whiteley, W. (Mhr) (1971). *Language Use and Social Change- Problems of Multilingualism with Special Reference to East Africa*. International African Institute: Oxford University Press. kur. 160-178

Abedi, K. A. (1954). *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*. Nairobi: EastAfrican Literature Bureau.

Akilimali, K. H. (1963). *Diwani ya Akilimali*. Nairobi: East African Literature Bureau.

Bienen, H. (1970). *Tanzania: Party Transformation and Economic Development*. Princeton: Princeton University Press.

Block, D. (2010). Globalisation and Language Teaching. In Coupland N. (mhr.). *Handbook of Language and Globalisation.* Oxford: Blackwell. kur. 287-304

Bourdieu, P. (1991). *Language and Symbolic Power*. United States of America: Harvard University Press.

Brock-Utne, B. na Holmarsdottir, H. (2004). "Language Policies and Practices in Tanzania and South Africa: Problems and Challenges" katika International Journal of Educational and Development. University of Oslo. Na. 24 kur. 67-83.

Buliba, A. Njogu, K. na Mwihaki, A. (2006). *Isimu Jamii kwa Wanafunzi wa Kiswahili*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Cameron, D. "The Commodification of Language: English as a global Commodity" katika Nevalainen T. and Traugott E. (Whr). (2012). *The Oxford Handbook of the History of English*. Oxford: Oxford University Press. kur. 352-361.

Chachage, C. (2003) "Globalisation and Democracy Governance in Tanzania" in Development Policy Management Forum (www). http://www.dpmf.org/publications/occassional%20papers/occasionalpaper10.pdf (Pdf documents, opens new windows) accessed 23 Feb 2010

Chacha, N. C. (1987). Meaning and Interpretation of Swahili Poetry: A Potrayal of a Changing Society. Tasnifu ya Shahada ya Uzamifu. Marekani: Chuo Kikuu cha Yale.

Chege, J. (1978). *Copyright Law and Publishing in Kenya*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Chiraghdin, S. (Mhr) (1977). *Malenga wa Mrima: Abjadi ya Mwinyihatibu Mohamed*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

Chiraghdin, S. na Mnyampala, M. (1977). *Historia ya Kiswahili*. Nairobi: Oxford University Press.

Chuachua, R. (2011). *Itikadi katika Riwaya za Shaaban Robert.* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

Clarke, P. H. (1960). *A Short History of Tanganyika: Mainland of Tanzania*. Tanzania: Longman.

Cooper, R. (1989). *Language Planning and Social Change*. Cambridge: Cambridge University Press.

Dos Santos, T. **"**The Structure of Dependence**"** katika Fann, K. na Hodges, D. (Mhr) (1971). *Reading in U.S Imperialism*. Boston: Porter Sargent. uk. 226.

Dubhashi, P. (1986). *Policy and Performance: Agriculture and Rural Development in Post- Independence India*. New Delhi: Sage.

East African Literature Bureau. (1950). Nairobi: The Report of the East African Literature Bureau.

Eleuthera, S. (2007) "Language Policy for Education and Development on Tanzania."

Tasnifu ya B.A ya Chuo cha Swarthmore. htt://scholarship.tricolib.brynmawyr.edu//

Fanon, F. (1952). *Black Skins, White Masks*. New York: Grove Press.

Fasold, R. W. "Language Policy and Change: Sexist Language in the Periodic News Media" katika Lowenberge, P. H. (Mhr) (1988). *Language Spread and Language Policy: Issues, Implications and Case Studies*. Washington D.C: Gearge University Press. uk. 187.

Fergusson, C. "Language Development". Katika Fishman, J. Fergusson, C. na Das Gupta, J. (Whr.) (1968). *Language Problems of Developing Nations*. New York: Wiley. uk. 3

Gibbe, G. A. na Mvungi, M. (1987). *Fasihi Simulizi Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: Standard Publishing Company Limited.

Gorman, T. P. "The Development of Language Policy in Kenya with Particular Reference to the Education System" katika Whiteley, W. (Mhr.) (1974). *Language in Kenya*. Nairobi: Oxford University Press. uk. 425

Gunder Frank, A**.** "The Development of Underdevelopment" katika Cockcroft, J. Gunder Frank, A. na Dale, J. (Whr) (1972). *Dependence and Underdevelopment*. Gardencity, New York: Achor Books. uk.3

Hassan, R. "Nafasi ya Shaaban Robert Katika Kukuza na Kuendeleza Kiswahili: Uchunguzi wa Mashairi Teule" katika Jarida la CHALUFAKITA (2020), Juz. Na.2 uk.193

Haugen, E. (1966) "Linguistics and Language Planning." katika Bright, W. (Mhr)

Sociolinguistics Proceedings of the UCLA Sociolinguistics Conference 1964. Mouton: The Hague, kur. 50-71

Haugen, E. (1983). "The Implementation of Corpus Planning: Theory and Practice" Katika Cobarrubias, J. na Fishman, J. A. (Whr) *Progress in Language Planning: International Perspectives.* New York: Mouton, kur. 269-290

Heller, M. (2010). “Commodification of Language”. Annual Review of Anthropology. Juz. Na.39 kur.101-114

Iliffe, J. (1969). *Tanganyika under German Rule, 1905-1912*. London: Cambridge University Press.

Iliffe, J. (1979). *A Modern History of Tanganyika*. London: Cambridge University Press.

Ingham, K. (1962). *A History of East Africa*. London: Longman.

Ipara, I. O. na Maina, G. (2008). *Fani ya Isimujamii kwa Shule za Sekondari*. Nairobi: Oxford University Press.

Kandoro, S. “Hatua Mbalimbali za Kubuni na Kutunga Mashairi ya Kiswahili” katika

Makala ya Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili: Fasihi III (1983). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. kur. 114-120

Kandoro, S. A. (1966). *Mashairi ya Saadani*. Dar es Salaam: Mwananchi Publishing Ltd.

Kaniki, M. H. (1980). *Tanzania under Colonial Rule*. London: Longmans.

Kezilahabi, E.”Uchunguzi katika Ushairi wa Kiswahili.” *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III: Fasihi* (1983). Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. kur. 145-163

Kezilahabi, E. “Mashairi ya Kiswahili” katika Topan, F. M. (1977). *Uchambuzi wa*

Maandishi ya Kiswahili Kitabu cha Pili. Dar es Salaam: Oxford University Press. kur. 60-61

Kezilahabi, E. (1976). *Ushairi wa Shaaban Robert*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Khan, K. katika Mzenge, M. na Hijazy, S. (1977). *Tujifunze Mashairi*. London: Macmillan Press Limited.

Kiango, J. “Ukuzaji wa Lugha ya Kiswahili katika Karne ya 21” katika Kihore, Y. M. na Chuwa, A. R. (2004). *Kiswahili katika Karne ya Ishirini na Moja*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. kur. 65-67

Kibao, S. A. “Namna ya Kujifunza, Kuliandika na Kulifumbua Shairi la Kiswahili” katika *Makala ya Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili: Fasihi III* (1983). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. kur.102-105

King’ei, K. (2010). *Misingi ya Isimujamii*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma ya Kiswahili.

King’ei, K. na Kemoli, A. (2001). *Taaluma ya Ushairi*. Nairobi: Acacia Stantex.

Kisia, A. na Mwarandani, B. (2007). *Uketo wa Ushairi kwa Shule za Upili*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Knappert, J. (1979). *Four Centuries of Swahili: A Literary History and Anthology*. London: Heinemann.

Kuvuna, S. Mvati, M. na Maliachi, P. (1992). *Nuru ya Ushairi kwa Shule: Mwongozo na Uchambuzi*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Kyamba, A. N. (2018). “Mwingilianomatini katika Ushairi wa Mathias Mnyampala”**.** Tasnifu ya Shahada ya Uzamifu. Eldoret: Chuo Kikuu cha Moi. (Haijachapishwa)

Kyamba, A. N. (2016). “Muundo wa Mashairi katika *Diwani ya Mnyampala* (1965) na Nafasi Yake katika Kuibua Maudhui” katika Kioo cha Lugha, Juz Na. 14.

Dar es Salaam: Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. kur. 108-111

Lo Bianco, J. “Language Policy and Planning” katika Hornberger, N. na Mckay, S. (2010)

(Whr) *Sociolinguistics and Language Education*. Clevedon: Multilingual Matters. kur. 143-176

Malik, N.” Extention of Kiswahili during the German Colonial Administration in

Continental Tanzania (Former Tanganyika) 1885-1917 katika *Afrikanistische Arbeitspapiere* (AAP) (1996) kur. 155-159

Marcia, W. “Swahili Language Policy 1890-1940” katika *Swahili XXXV* (1965) (1)kur. 40-49

Marshall, A. T. (2015). “Kiswahili and Decolonization: The Inter-Territorial Language

Committee and Successor Organizations, 1930-1970”. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili. Washington, DC: Chuo Kikuu cha Marekani. (Haijachapishwa)

Masinde, E. W. (2003). “Ushairi wa Kiswahili: Maendeleo na Mabadiliko ya Maudhui”. Tasnifu ya Shahada ya Uzamifu. Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Masinde, E. W. (1992). “Mashairi Huru: Uchambuzi wa Dhamira na Mtindo. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili. Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Massamba, D. P, Kihore, Y. M na Hokororo, J. I. (1999). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA) Sekondari na Vyuo.* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Massamba, D. P. “Kiswahili Kama Lugha ya Mawasiliano” katika Mlacha S. A. (1995). *Kiswahili katika Kanda ya Afrika Mashariki: Historia, Matumizi na Sera*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. kur.5

Massamba, D. P. “Utunzi wa Ushairi wa Kiswahili.” *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III: Fasihi* (1983). Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. kur. 54-95

Mathooko, P. M. (2007). *Isimu Jamii: Misingi na Nadharia*. Nairobi: Njigua Books.

Maxon, R. M. (1986). *East Africa: An Introductory History*. Morgantown: West Virginia University Press.

Mazrui, A. (1988). *Chembe cha Moyo*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mazrui, A. na Mazrui, A. (1995). *Swahili State and Society: The Political Economy of an African Language*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mbaabu, I. (2007). *Historia ya Usanifishaji wa Kiswahili***.** Chuo Kikuu cha Dar es Salaam:Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mbaabu, I. (1996). *Language Policy in East Africa: A Dependency Theory Perspective in Africa.* Nairobi: Educational Research Publications.

Mbaabu, I. (1991). The Impact of Language Policy on the Development of Kiswahili in

Kenya 1930-1990. Tasnifu ya Shahada ya Uzamifu. Washington D.C: Chuo Kikuu cha Howard. (Imechapishwa)

Mbaabu, I. (1985). *New Horizons in Kiswahili: A Synthesis in Developments, Research And Literature*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Mbaabu, I. (1978). *Kiswahili Lugha ya Taifa*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Mkude, D. "Ujenzi wa Demokrasia na Sera ya Lugha nchini Tanzania Kiswahili /Kiingereza Dhidi ya Lugha za Jumuiya Ndogondogo" katika Tumbo- Masabo, Z. na Chidu, E. (1999). *Kiswahili katika Elimu*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TUKI. kur.14-18

Mnyampala, M. (1965). *Diwani ya Mnyampala*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Mnyampala, M. (1964). *Waadhi wa Ushairi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mogeni, M. E. (2015). "Fani na Maudhui katika Magazeti ya Taifa Leo"**.** Tasnifu ya Shahada ya Uzamili. Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Mohamed, S. A. (2002). *Jicho la Ndani*. Nairobi: Longhorn.

Mohamed, S. A. (1990). *Mbinu na Mazoezi ya Ushairi*. Nairobi: Evans Brothers.

Mohamed, S. A.(1984). *Kina cha Maisha*. Nairobi: Longhorn.

Momanyi. C. (1991). Matumizi ya Taswira kama Kielelezo cha Uhalisi katika Utenzi wa Al inkishafi. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili. Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Morrison, D. R. (1976). *Education and Politics in Africa: The Tanzanian Case***.** London: Hurst.

Moyd, M. R. (1996). "Language and Power: Africans, Europeans and Language Policy in German Colonial Tanganyika"**.** Tasnifu ya Shahada ya Uzamili. Florida: Chuo Kikuu cha Florida.(Haijachapishwa)

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mulokozi, M. M. "Nadharia ya Jadi ya Ushairi wa Kiswahili: Je Upo?" katika Ogechi, N.O. na Simala, K. I. (Whr) (2008). *Nadharia katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika*. Eldoret: Moi University Press. kur. 72-79

Mulokozi, M. M. (1999). *Tenzi Tatu za Kale.* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TUKI.

Mulokozi, M. M. na Sengo, T. Y (1995). *History of Kiswahili Poetry A.D1000-2000: A Report.* University of Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research.

Mulokozi, M. M. na Kahigi, K. K. (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Mwansoko, H. J. "Swahili Terminological Modernisation in the Light of the Present Language Policy of Tanzania" katika Rubagumya C. (Mhr) (1990). *Language in Education in Africa: A Tanzanian Perspective*. Clevedon, Philadelphia*:* Multilingual Matters Limited. kur. 133-142

Mwanzi, H. O. (1986). *Language Policy in Primary Schools in Kenya***.** KERA Research Report Na. 15. Bureau of Educational Research: Nairobi: Kenyatta University.

Ndwiga, P. N. (2013). "Mtindo Katika Mashairi ya Diwani ya Karne Mpya".Tasnifu Ya Shahada ya Uzamili. Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Ngugi, T. (1986). *Decolonising the Mind: The Politics of Language in African Literature*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Njogu, K. S. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nsekela, A. J. (1965). *Minara ya Historia ya Tanganyika: Tanganyika Hadi Tanzania*. Dar es Salaam: Longman Tanzania.

Nyongesa, D. M. (2015). "Mtindo na Dhamira katika Mashairi ya Washairi Chipukizi Kutoka Bungoma". Tasnifu ya Shahada ya Uzamili. Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Orodho, J. (2009). *Elements of Education and Social Science Research Methods*. Maseno, Kenya: Kanezja Publisher.

Park, J. and Wee, L. (2012). *Markets of English: Linguistic Capital and Language Policy in a Globalizing world.* United Kingdom: Routledge.

Petzell, M. "The Linguistic Situation in Tanzania." katika *Moderna Sprak* 2012:1 University of Gothenburge.

Polome, E. C. (1967). *Swahili Language Handbook*. Washington DC: Centre for Applied Linguistics.

Polome, E. C. na Hill, C. P. (Mhr). (1980). *Language in Tanzania*. Oxford: Oxford University Press

Ratcliff, B. (1942) "History, Purpose and Activities of the Inter- Territorial Language Committee" katika I.L.C Bulletin Na.16, kur. 1-8

Robert, S. (1969). *Koja la Lugha*. Nairobi: Oxford University Press.

Robert, S. (1968). *Kielezo cha Fasili*. Nairobi: Nelson.

Robert, S. (1967). *Masomo Yenye Adili*. Nairobi: Nelson.

Robert, S. (1966). *Pambo la Lugha*. Nairobi: Oxford University Press.

Robert, S. (1958). "Hotuba Juu ya Ushairi" JEASC 28/1: kur 37-42

Rodney, W. (1972**).** *How Europe Underdeveloped Africa*. Nairobi: East African Educational Publishers Limited.

Roy-Campbell, Z. M. (2001). *Empowerment through Language: The African Experience*: *Tanzania and Beyond*. Trenton, NJ: Africa World Press.

Roy-Campbell, Z. M. (1995). "Does Medium of Instruction Really Matter? The Language

Question in Africa: The Tanzanian Experience." Katika Utafiti (New Series) Juzuu. 2 Na. 1 na 2. Michigan State University Libraries. kur. 22-38

Rubagumya, C. M. (1990) "Language in Tanzania" katika Rubagumya C. M. (Mhr)

Language In Education in Africa: A Tanzanian Prespective. Clevedon, Inc: Multilingual Matters. kur. 5-14

Rubagumya, C. M. (1990). *Language in Education in Africa: A Tanzanian Perspective*. Clevedon, Philadelphia: Multilingual Matters Limited.

Rubagumya, C. M. na Lwaitama, A. F. "Political and Economic Dimensions to Language

Policy Options in Tanzania" katika Rubagumya, C. (Mhr) (1990). *Language in Education in Africa: A Tanzanian Perspective* Clevedon, Philadelphia: Multilingual Matters Limited. kur.143-150

Rubin, J. na Jernuudd, B. (1971) (Whr.) *Can Language be Planned? Sociolinguistic: Theory in Developing Countrie*: Hawaii: Honolulu.

Rugemalira, J. M, Rubagumya, C. M, Kapinga, M. K, Lwaitama, A. F. na Tetlow, J. G. "Reflections on Recent Developments in Language Policy in Tanzania" katika Rubagumya, C. M. (Mhr) (1990). *Language in Education in Africa*: *A Tanzanian Perspective*. Clevedon, Philadelphia: Multilingual Matters Limited. kur.25-35

Ruo, K. R. (1989). *Nguzo za Ushairi wa Kiswahili*. Nairobi: Macmillan Publishers Limited.

Senkoro, F. E. (2011). *Fasihi.* Dar es Salaam: KAUTTU Limited.

Senkoro, F. E. (1988).*Ushairi: Tahakiki na Nadharia*. Dar ea Salaam: Dar es Salaam University Press.

Senkoro, F. E. (1987). *Fasihi na Jamii*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

Senkoro, F. E. (1982). *Fasihi*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

Shariff, I. N. (1988). *Tungo Zetu.*Trenton: The Red Sea Press.

Shitemi, N. L. (2011) "Kubidhaaisha na Kuwezesha Lugha kama Sarafu ya Kiuchumi na Kijamii: Kielelezo cha Taaluma za Kiswahili na Tafsiri" katika Mhadhara wa Uzinduzi Eldoret: Chuo Kikuu cha Moi. kur. 4-5.

Shitemi, N. L. (2010). *Ushairi wa Kiswahili Kabla ya Karne ya Ishirini.* Eldoret: Moi University Press.

Spolsky, B. (2004). *Language Policy.* : Cambridge: Cambridge University Press.

Sunkel, O. (1969). "National Development Policy and External Dependence in Latin America". Journal of Development Studies. Juz.6, Na.1 uk.23

Syambo, B. K. na Mazrui, A. M. (1992). *Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake.* Nairobi: Phoenix Publishers Limited.

Were, G. S. na Wilson, D. A. (1968). *East Africa through a Thousand Years*: *AD 1000 to the Present Day.* London: Evans Brothers Limited.

Whiteley, W. (1969). *Swahili: The Rise of a National Language*. London: Methuen.

Yunus, M. K. (2013). "Masuala ya Kisiasa katika Ushairi wa Kandoro: Mifano Kutoka Katika Mashairi Yake"**.** Tasnifu ya Shahada ya Uzamifu. Dae es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. (Haijachapishwa)

Viambatisho

Kiambatisho A: Mashairi ya Mathias Mnyampala

Diwani: ***Diwani ya Mnyampala*** **(1965)**

1.Lugha Yetu Kiswahili

Siachi kuisifia, lugha yetu Kiswahili,
Wenyewe twajifunia, twaitumia kuwili,
Kama wali kwa samli;
Samli wali kitia, utadharau ugali,
Asokula hujutia, moyonimwe umdhili,
Lugha yetu Kiswahili, twatazama na kuibuka.

Twatazama twaibukia, kutoa zetu kauli,
Fumbo mbizi twazamia, kuwazunguka jahili,
Kwa nisai na rijali,
Rijali wakinyatia,wakaulize maswali,
Kwa mashehe hupitia, hadi wakalipa mali,
Lugha yetu Kiswahili, twatazama na kuibuka.

Lugha yetu twapatia, utamu kama asali,
Hakuna wa kuchukia, wenyewe si mabahili,
Maneno hayo kubali;
Uyakubali sawia, kila njia kila hali,
Kila mtu mahamia, na mwenyeji hujabadili,
Lugha yetu Kiswahili, twatazama na kuibuka.

Tunaijua kwa nia, wenye nguvu na dhahili,
Shairi twaitungia, kwa upole na ukali,
Ya heshima kujidhili,
Jidhili njema tabia, wanadamu kuwajali,
Acha wenye kutania, kufata ubaradhuli,
Lugha yetu Kiswahili, twazama na kuibuka.

Kiswahili ni Rupia,tukisema kwa akili,
Kiswahili twavukia, tuende ng'ambu ya pili,
Muungwana na Mjoli,
Mjoli huwa huria, akakipata kibali,
Uhuru huufikia, kwa Mola hutawakali,
Lugha yetu Kiswahili,twazama na kuibuka.

Popote twaitumia, Barazani na sikuli,
Kunena na kutubishia, sukali na pilipili,

Na mengine mengi pia;
Pia tunashuhudia, yaletayo mushikeli,
Hata kama twasinzia, daima kila pahali,
Lugha yetu Kiswahili,twazama na kuibuka.

Ni lugha ya biladia, alotujalia Jalali,
Wahabu katujalia, katupa katusabili,
Kakamilisha kamili;
Kamili katupambia, kumbuka zake fadhili,
Lugha yatusaidia, mara kumi twabadili,
Lugha yetu Kiswahili, twazama na kuibuka.

Ufundi twajifunzia, usonara wa vipuli,
Na kuijua dunia, ya haramu na halali,
Ya sadaka na kusali;
Kusali kusujudia, Mungu atupe kubuli,
Hotuba twahotubia, yale maneno ya kweli,
Lugha yetu Kiswahili, twazama na kuibuka.

Kiswahili narudia, bora sana Kiswahili,
Maghani twakiimbia, hadi nyingine shughuli,
Kwa mafumbo na methali;
Methali zenye wasia, nazo ardhilihali,
Mpaka tukajifia, kifo kikitukabili,
Lugha yetu Kiswahili, twazama na kuibuka.

Lugha haina udhia, hutamkwa kwa sahali,
Matajili huchumia, wanapositahamili,
Kila pembe huwasili;
Huwasili huwajia, nchini wakaitaali,
Hadi wakafurahia, wasichukie muhali,
Lugha yetu Kiswahili, twazama na kuibuka.

2. Kimefuzu Kiswahili

Asante Waziri Mkuu, ombi letu kukubali,
Kwa Mungu tunarukuu, twamujudu kuwili,
Twainua mikono juu, kumshukuru Jalali,
Kwa kufuzu Kiswahili, wananchi tumefu rahi.

Tumeipata nafuu, kukubali Kiswahili,
Na kianze mwaka huu, Jamhuri kiwasili,

Katika Baraza Kuu, na pengine tujadili,
Kwa kufuzu Kiswahili, wananchi tumefurahi.

Tutafanya Sikukuu,tushukuru serikali,
Mababu na vijukuu, wanawake na rijali,
Hata hao vitukuu, wale wanotukabili,
Kwa kufuzu Kiswahili, wananchi tumefurahi.

Tuvike yake kumbuu, lugha yetu ya halali,
Ilindwe kama tumbuu, tuseme yenye akili,
Tuunge na vitunguu, tukaange kwa samli,
Kwa kufuzu Kiswahili, wananchi tumefurahi.

Tuisomee Juzuu, Sala zote kila hali,
Tumepanda kisuguu, lugha yetu tuijali,
Itembee kwa miguu, toka hapa hadi mbali,
Kwa kufuzu Kiswahili, wananchi tumefurahi.

Lugha nyingine tutuu, chungu kama pilipili,
Huchoma kama tanuu, lile la moto mkali,
Hutwangusha chini puu, kutoijua kamili,
Kwa kufuzu Kiswahili, wananchi tumefurahi.

Tuliivamia Vuu, nayo hatujui kweli,
Twajua kijuu-juu, twakwamakwama mahali,
Sasa tuipe Khuluu, lugha yenye mushikeli,
Kwa kufuzu Kiswahili, wananchi tumefurahi.

Sio lugha ni kizuu, yatutia udhalili,
Kinywani ina mabuu, yatupotosha kauli,
Hutuletea kiruu, kutamka yatudhili,
Kwa kufuzu Kiswahili, wananchi tumefurahi.

Na wakati sasa huu, afadhali tubadili,
Tuitie na buluu, iwe nyeupe mithali,
Ile yavunja vifuu, tulipojibu maswali,
Kwa kufuzu Kiswahili, wananchi tumefurahi.

Kaditama tunukuu, zile mbinu za methali,
Sidharau kuu-kuu, simo na vitendawili,
Tuunge kwa karafuu, lugha yetu ni asali,
Kwa kufuzu Kiswahili, wananchi tumefurahi.

4. Tutalea Mwana Gani?

Shairi ninakutuma, wende njia ya hewani,
Uvume toka Mrima, mpaka huko Ziwani,
Umjibu wa Kigoma, Snow White jirani,
Tutalea mwana gani, iwapo wana twanyonga?

Nasema ima fa ima, nakujibu la kipini,
Bure umenilawama, tuingie ugombani,
Ninakujibu kwa wema, wapime bara na pwani,
Tutalea mwana gani, iwapo wana twanyonga?

Maneno bila kupima, kinyume huja huzuni,
Tujitiapo ulama, mfano mwana zuoni,
Mbele huja kutukwama, na tukajuta “kwa nini!”
Tutalea mwana gani, iwapo wana twanyonga?

Mtu haewzi kulima, pasi kufyeka porini,
Na kulimia mapema, kupalilia shambani,
Mambo hayo ni lazima, ndipo ale kivulini,
Tutalea mwana gani, iwapo wana twanyonga?

Kwanza kupanda mtama, unapofukia chini,
Ulinde na kutazama, kwa kanga na hao nyuni,
Hatapata raha njema, hadi mwisho mavunoni,
Tutalea mwana gani, iwapo wana twanyonga?

Umethamini ya nyuma, ya mafunzo sitahani,
Umesahau ya bima, ya kumuomba Manani!
Jambo bora ni rehema, tusichojua tumboni,
Tutalea mwana gani, iwapo wana twanyonga?

Watu hutafuta pema, waingie furahani,
Na hitaji la kuchuma, watoke masikini,
Mafunzo huja hatima, bada ya kuzaa Joni,
Tutalea mwana gani, iwapo wana twanyonga?

Watu hufunga ndarama, wakaenda ugangani,
Huifunga nayo ndama, ya kupeleka dawani,
Watokane na kilema, kukosa mwana nyumbani,
Tutalea mwana gani, iwapo wana twanyonga?

Mwanamke hawi mama, hadi kamzaa Dani,
Kwani mwana ndilo Boma, na stara maishani,
Hutokana na lawama, la watu kumlaani,
Tutalea mwana gani, iwapo wana twanyonga?

Aszaa ni nakama, sikitiko duniani,
Ana huzuni daima, humuomba Rahamani,
Tuache anojinyima, kwa sharia za kidini,
Tutalea mwana gani, iwapo wana twanyonga?

Mwana kukosa heshima, ni huluka akilini,
Wengi huja wakakwama, nyumbani hata shuleni,
Huwapiga na kuuma, wasiweze asilani,
Tutalea mwana gani, iwapo wana twanyonga?

Hapo ndio kaditama, nakutoa ujinga,
Tumia yako kalmia, maneno yenye kiini,
Uliza wenye hekima, na utapewa yakini,
Tutalea mwana gani, iwapo wana twanyonga?

5. Yaliyopita Yamepita

Hapana cha upinzani, cha ugomvi na matata,
Watunzi na ubishani, vile watunzi kuteta,
Sasa wanayo imani, umoja wamelumbata,
Ya ugomvi yamepita,na tutunge ya Uhuru.

Ya Uhuru yatungeni, ya ugomvi yamepita,
Tanganyika nchi amani, nchi haina wasalata,
Washairi unganeni, na utunzi kutakata,
Ya ugomvi yamepita, na tutunge ya Uhuru.

Bwana Gonga muhisani,mtunzi mwenye kunata,
Khamisi bini Amani, mwenye tungo za kukata,
Ugomvi jama achene, tungeni ya kumemeta,
Ya ugomvi yamepita, na tutunge ya Uhuru.

Msanifu Makarani, mwenye tungo za kuvuta,
Bwana Miraji rubani, mtunzi usiye sita,
Pia na Makwayasoni, mtunzi mwenye mafuta,
Ya ugomvi yamepita, na tutunge ya Uhuru.

Bwana juma Ujijini, na Adamu nawambata,
Mheshimiwa wa Dini, Sheikh Amri Kaluta,
Wambieni suluhuni, Madaraka tumepata,
Ya ugomvi yamepita, na tutunge ya Uhuru.

Nawe Bwana Damiani, shauri hili kamata,
Na kule magharibi, na Idrissa kakita,
Waaseni ya uhuni, waungwana kutafuta,
Ya ugomvi yamepita, na tutunge ya Uhuru.

Mandevu wa Buguruni, na Shaha wanaye Chata,
Kazimoto na Imani, Kiwato na Chamatata,
Tanganyika tukuzeni, kiwango tumekigota,
Ya ugomvi yamepita, na tutunge ya Uhuru.

Mwaruka na Selemani, waacheni kuwasuta,
Na Palla wa Uteteni, Bini Mchuchuli Sheta,
Na adui pendaneni, hata kama ni msuta,
Ya ugomvi yamepita, na tutunge ya Uhuru.

Shinyanga ni Khalfani, fundi kucheza karata,
Na Unguja kisiwani,washairi bora sita,
Kwa umoja shikaneni, pamoja kujipakata,
Ya ugomvi yamepita, na tutunge ya Uhuru.

Tama Bwana Shaaban, na Saidi msojuta,
Mahamudu Hamduni, na Snow mwenye kuseta,
Nawe Bwana Saadani, na Kurumbiza fuata,
Ya ugomvi yamepita, na tutunge ya Uhuru.

6. Chama na Kibarikiwe

Chama nakifunga kamba, kambaye inakishiwe,
Chama natia uvumba, ubani kifukiziwe,
Chama tusije kugomba, kisha kisahauliwe,
Chama na kibarikiwe, kisitawi na kupendwa.

Chama vema kukipamba, kipambwe kinadhifiwe,
Chama kisije kuyumba, twaomba kibarikiwe,
Chama Ya Rabbi Muumba, bariki kifanikiwe,
Chama na kibarikiwe, kisitawi na kupendwa.

Chama kiwe kama mwamba, mapao pia yatiwe,
Chama ni nguzo ya nyumba, iliyojengwa kwa mawe,
Chama ndivyo kinaomba, Inshallah kijaliwe,
Chama na kibarikiwe, kisitawi na kupendwa.

Chama shairi kuimba, na wengi yatamaniwe,
Chama watunzi kuchimba, tungo njema zitakiwe,
Chama lugha na kilemba, vidarane vyongokewe,
Chama na kibarikiwe, kisitawi na kupendwa.

Chama kichukue mimba, kizae tuongezewe,
Chama kiwe kama temba, mayai yaanguliwe,
Chama nacho kitagumba, mitato zitatuliwe,
Chama na kibarikiwe, kisitawi na kupendwa.

Chama kipige marimba, milio zifurahiwe,
Chama kizidishe namba, watunzi wanyanyuliwe,
Chama kipate wa Pemba, na Unguja kisifiwe,
Chama na kibarikiwe, kisitawi na kupendwa.

Chama kifike kimamba, matawi yafunguliwe,
Chama kifike Bukwimba, Kigoma na Kiserawe,
Chama kisilete kufumba, kieleze waelewe,
Chama na kibarikiwe, kisitawi na kupendwa.

Chama kimepanda shamba, ni lazima lilimiwe,
Chama kijaze mitumba, jazo lisipungukiwe,
Chama mwisho kujigamba, watunzi sifa wapewe,
Chama na kibarikkiwe, kisitawi na kupendwa.

Chama kiwe kama Simba, amtishae nguruwe,
Chama kiwe kama Mamba, majini aheshimiwe,
Chama kipate kuvimba, kuyavunja matumbawe,
Chama na kibarikiwe, kisitawi na kupendwa.

Chama kwa Bwana Mkamba, na wengine kipokewe,
Chama nawe kumbakumba, siachie wenginewe,
Chama macho nayafumba, Tama shairi na liwe,
Chama na kibarikiwe, kisitawi na kupendwa.

7. Mwananchi Usonge Mbele

Nimeazimu kutunga, tungo njema za kikale,
Nazitunga u malenga, zafasaha ilo tele,
Waliotumia wahenga, kugangua wenye ndwele,
Mwananchi usonge mbele, songa usirudi nyuma.

Pasiwe mtu kupinga, mwananchi usonge mbele,
Tena usifanywe bunga, na kama juzi na vile,
Mwananchi itoe kunga, kwa lafidhi ya upole,
Mwananchi usonge mbele, songa usirudi nyuma.

Songa maovu kikinga, yasijeleta upele,
Songa mbele ukiringa, na mwendo wa polepole,
Upole ndio uganga, kushinda sime, mishale,
Mwananchi usonge mbele,songa usirudi nyuma.

Usinje macho kufunga, kisha usione pale,
Dhiki isije kusonga, kukuangushia mvule,
Wadudu ondoa janga, asifungwe mikatale,
Mwananchi usonge mbele, songa usirudi nyuma.

Mwananchi ninakupunga, mbele sikupate ole,
Kwa madawa kukufunga, acha nikuchanje chale,
Nina kilemba cha kanga, bakora yangu ni kole,
Mwananchi usonge mbele, songa usirudi nyuma.

Ninakuvika ushanga, pambo bora litoshile,
Shingoni zisije nyonga,zikafisha kama Yule,
Zisikufanye muhanga, kuwafia kole kole,
Mwananchi usonge mbele, songa usirudi nyuma.

Maombi ndio upanga, na silaha za milele,
Hata shinda kukutinga , usijepiga kelele,
Bwana Mungu takuchunga,panda mpaka kilele,
Mwananchi usonge mbele, songa usirudi nyuma.

Kitu chochote hukonga, ama chombo na wimbile,
Bwana Mungu huyapanga, kama safu za vidole,
Kwani yeye si mjinga, mweledi wa maumbile,
Mwananchi usonge mbele, songa usirudi nyuma.

Mwananchi litoe mwanga, ling'ae na vigelegele,
Ukweli hutauvunga, ufiche ukweli ule,
Uwachongee mizinga, waonje asali wale,
Mwananchi usonge mbele, songa usirudi nyuma.

Tamati beti kupanga, ombezi sisahawile,
Ninasema utajenga, wanavyojenga wavyele,
Na utakuwa nyakanga, sifa kila utenzile,
Mwananchi usonge mbele, songa usirudi nyuma.

8. Mwananchi Utabalaji

Risala imetufika, imenea kila mji,
Mwananchi amezalika, nasi tumlishe uji,
Nasi tumefurahika, tunaipiga buruji,
Mwananchi utabalaji, kiza kuu litoweke.

Na kiza litatoweka, huko mpaka Ujiji,
Mwananchi kuangazika, pasiwepo ufujaji,
Kundini kuhesabika, kwake Kondoo na miraji,
Mwananchi utabalaji, kiza kuu litoweke.

Leo kumepambazuka,mwananchi utabalaji,
Tabalaji ukimulika, mjini na vitongoji,
Bahari tupate vuka, tufike na Msumbiji,
Mwananchi utabalaji, kiza kuu kitoweke.

Penye tope za masika, na pepo za maleleji,
Penye wimbi kachafuka, penye mashaka ya mbwoji,
Mwananchi kinusurika,epuka mbele ya mbwiji.
Mwananchi utabalaji kiza kuu litoweke.

Mwananchi utapendeka, kwa wageni na wenyeji,
Mwananchi takamilika, pasi mtu mhojaji,
Tusomapo tukicheka, mamuma na wasomaji,
Mwananchi utabalaji, kiza kuu litoweke.

Mwananchi pata baraka, twasali waombeaji,
Mwananchi shika shirika, siwepo mchukiaji,
Ndipo utaneemeka, unapopata mtaji,
Mwananchi utabalaji, kiza kuu litoke.

Pasije baya kuzuka, kufuja utangazaji,
Wasije wakapotoka, sababu ya usemaji,
Twaomba ukitukuka, pata mwema mwongozaji,
Mwananchi utabalaji, kiza kuu litoke.

Hakuna la kuchujuka, tupo nasi wapambaji,
Daima tutaandika, tupo sisi wandikaji,
Habari ziso na shaka, kwani wapeleleji,
Mwananchi utabalaji, kiza kuu litoweke.

Mwananchi umeumbika, nasifu Mtengenezaji,
U mwepesi kusomeka, na vyepesi kwa mwuzaji,
Kurasa zimepanuka, kutimiza mahitaji,
Mwananchi utabalaji, kiza kuu litoweke.

Kaditama tamatika, hapa mwisho wa wimbaji,
Nakuombea Rabuka, pata mema makuzaji,
Hunalo la kusumbuka, kua tukuvike Taji,
Mwananchi utabalaji, kiza kuu litoweke.

9. Mwananchi Kua Salama.

Shangilika bilkuli, mwananchi mwenye heshima,
Shangilika kila hali, wengine wasije hama,
Shangilika sibadili, kauli wala mtima,
Mwananchi kua salama, wakuombea baraka.

Shangilika kwa kauli, isikufike na kama,
Shangilika bulburi, utoe habari njema,
Hapa kwetu uwasili, tukusome na mapema,
Mwananchi kua salama, twakuombea baraka.

Wasili hapa jamali, mwananchi mwenye hekima,
Kurasazo tusabili,tujisomee nudhuma
Uwafunze majahili, watokane na zahama,
Mwananchi kua salama, twakuombea baraka.

Kukuacha ni muhali, washairi wa Dodoma,
Na tupo kumi na mbili, na wengine wanasoma,
Watunzi wenye akili, watungaji wenye mandhuma
Mwananchi kua salama, twakuombea baraka.

Raisi ni jitukali, naye Farahani Juma,
Nyamaume ni mkali,mabishano utakwama,
Hawa ni mafundi kweli, watunzi wenye adhima,
Mwananchi kua salama, twakuombea baraka.

Wa tungo kama asali, watungaji wanachama,
Shabani Musa taili, mtunzi mwenye karama,
Bini Omari samili, mtunzi bora na mwema,
Mwananchi kuwa salama, twkuombea baraka

Sitafanya taghafali, wengine kuacha nyuma,
Watunzi wenye kibali, tena wenye takirima,
Mary Mangwale jabali, nuru wenye huruma
Mwananchi kua salama, twakuombea baraka

Wenye tungo la sahali, Mwanoga mwenye azima,
Mbwana asiye bahili, Shabani Saidi hima,
Juma Ngolo wajadilihao wendeshaji vyuma,
Mwananchi kua salama, twakuombea baraka.

Yako ardhilihali, hiyo uliyoisema,
Dodoma imeijali, imo katika kupima
Ramadhani tafadhali, tuma tungo Mzizima,
Mwananchi kua salama, twakuombea baraka.

Tamati natawakali, kwa Mola mwenye rehema,
Mungu chukua kubuli, nakuomba nainama,
Hassan toa dalili,mwananchi akue vema
Mwananchi kua salama, twakuombea Baraka.

10. Johari Ninakupamba

Kila pambo na fanie, falau kuwa ni nyumba,
Kila kito na hadhie, falau kuwa ni gamba,
Pambo la tungo tungie, tenzi watu wakaimba,
Johari ninakupamba, pambo la waraka tenzi.

Kila pambo wasifie, falau kuwa kamba,
Kamba bora ifungie, kikumba fanya mitumba,
Japo marashi rashie, lawaridi na uvumba,
Johari ninakupamba, pambo la waraka tenzi.

Tenzi Mwananchi ridhie, ndio johari napamba,
Kurasani nipambie, kati kati nikiwamba,
Niwambe kikukalie, kiache kuyumba yumba,
Johari ninakupamba, pambo la waraka tenzi.

Mwananchi ujivalie, wakusifu hata shamba,
Na watu washangilie, shangwe iende sambamba,
Ndipo wakukimbilie, pasi na watu kugomba,
Johari ninakupamba, pambo la waraka tenzi.

Kupendwa usichukie, wa huko wala wa Zomba,
Harufu iwanukie, ifike hadi Kimamba,
Shairi wakutungie, hata wale wa Msimba,
Johari ninakupamba, pambo la waraka tenzi.

Pambo nikusabilie, kukuvika watalumba,
Lulu hii itumie, wasifu wa Bukwimba,
Yapendeza uzurie, hapana atayefumba,
Johari ninakupamba, pambo la waraka tenzi.

Shingoni mwako kitie, haidhuru kikuomba,
Haidhuru usinzie, hata Jini kukukumba,
Katu usiwaachie, radhi lindi wakichimba,
Johari ninakupamba, pambo la waraka tenzi.

Kito hicho jivunje, wapigie na marimba,
Shingoni mwako ifie, Yakuti niliyoremba,
Alimasi wafichie, wasijue yake namba,
Johari ninakupamba, pambo la waraka tenzi.

Makombo uwatupie, masalio ya makomba,
Mavumbi wakung'utie, na masazo yake pamba,
Uwachie wagombanie, kama panya na usumba,
Johari ninakupamba, pambo la waraka tenzi.

Wadudi akujalie, uwashinde wale Simba,
Pambo acha walilie, siwajali kwaumemba,
Nakuombea Jalie, akubariki Muumba,
Johari ninakupamba, pambo la waraka tenzi.

11. Kiongozi Mtukufu

Kuchapo nakuchelee, tupokee mtukufu,
Tusome tuendelee, na wambali watusifu,
Na heko watutolee, kwa upendo kamilifu,
Kwa sifa na utukufu, *Kiongozi* wendelee

Walimwengu wasifie, kwa sifaa takilifu,
Waasi wakurudie, hali mpya badilifu,
Kwa zumariwakwimbie, wamekuwa sadikifu,
Kwa sifa na utukufu, *Kiongozi* wendelee.

Uzuri wako pekee,hapana ulinganifu,
Kila mara utokee,zidi usiwe pungufu,
Tama tukupokee,kila mwezi maradufu
Kwa sifa na utukufu, *Kiongozi* wendelee

Kiongozi wendelee,sifaa zako sufufu,
Hasidi wachekelee, wakufanye maarufu,
Na watoto uwalee,uwafundishe wongofu,
Kwa sifa na utukufu, *Kiongozi* wendelee.

Walofungwa wafungue,kuacha uharibifu,
Msalaba tuuchukue, kwa mateso na sumbufu,
Jema baya tutambue, na tusome misahafu,
Kwa sifa na utukufu, *Kiongozi* wendelee.

Nyoyo zisitulegee, kwa juhudi jikalifu,
Na pasaka isogee, kwa siku zake tawafu,
Ni karibu tutegee, na tuyaache machafu,
Kwa sifa na utukufu, *Kiongozi* wendelee.

Aprili zisitulegee,na pasaka takatifu,
Pasaka tushangilie, na tujipange kwa safu,
Tuimbe atusikie, Alleluya suluhifu,
Kwa sifa na utukufu, *Kiongozi* wendelee.

Ni haki tufurahie, siku hii tambulifu,
Wengine watangazie, wauache uhalifu,
Mungu tusimuambae, tumfuate Latifu,
Kwa sifa na utukufu, *Kiongozi* wendelee.

Akili situfungulie, macho tusiwe vipofu,
Rabbi utuhurumie, hapa penye uumbufu,
Mbingu utufungulie, na mengine tahafifu,
Kwa sifa na utukufu, *Kiongozi* wendelee.

Kandatamati tupambie, ndiwe wetu msanifu,
Kiongozi tuambie, mema yasiyo tukifu,
Mashairi tutilie, yenye heshima hawafu,
Kwa sifa na utukufu, *Kiongozi* wendelee.

12. Tuongoze kwa Mteremo.

Kiongozi ja mrua, Gazeti lenye nderemo,
Naliombea dua, lizidishe chake kimo,
Kimo bora cha kukua, kwa kurasa za masomo,
Kila habari zenye simo, tuongoze kiongozi.

Ongoza hatuchafua, kubadilisha misemo,
Yalofichwa hufichua, na kuacha ya mivumo,
Kila siriwagundua, ya kuwasha na michomo,
Kila la wema liwemo, tuongoze kiongozi.

Tanua mbawa tanua, usihofu mitutumo,
Walio chini nyayua,vijana na wa makamo,
Mwele apate fua, umtoke mtetemo,
Yake karikenye yamo, tuongoze kiongozi.

Kilichogoba nasua, tusomapo yaliomo,
Twakiri una satua, katika fitina hyumo
Tanganyika kuchafua, kwa ghasia na migomo,
Ya tuangaze ya mumo, tuongoze kiongozi.

Kua nimekuteua, ushike sana milimo,
Ya maarifa panua, ya Elimu na Kilimo,
Hali ya nchi pindua, usawazishe vipimo,
Mashairi ya mzamo, tuongoze kiongozi.

Hapa basi napumua,naufunika mdomo,
Kuna kitu nakijua,kile kiletacho chumo,
Aridhi tukitifua, tachuma hadi kikomo,
Ya milima ya mwinamo, tuongoze kiongozi.

13. Usitunge Uchokozi.

Ahasante Bwana Mbwana,kwa fumbo la utetezi,
Kila tambo na maana, humtakamtambuzi,
Umechinja na kuchuna, wamtaka mtumbuzi,
Usitunge uchokozi, kutaja mtu na jina.

Tambo moja hupishana, maana ya ugunduzi,
Wengine hupotezana, Mkoche kuwa mnazi,
Mtabaki kuzozana, na ubishi wa bazazi,
Usitunge uchokozi, kutaja mtu na jina.

Wafumba fumbo mchana, lifumbuliwe na jozi?
Kupima pana na refu,ukuta tia timazi,
Kumbuka utaachana, urudi kuwa bomozi,
Usitunge uchokozi, kutaja mtu na jina.

Halimashauri tuna, Sheikh Kombo mwangalizi,
Watu wanapogusana, kwa matusi na utwezi,
Mwenyewe ndiye supana, kufunga na mfunguzi,
Usitunge uchokozi, kutaja mtu na jina.

14. Washairi Hupendana.

Penda- chako najituma, kuwaandisi waungwana,
Naandisi kwa heshima, japo wakinitukana,
Tusi huleta zahama, tena huvuta laana,
Washairi hupendana, kashifa si ushairi.

Kashifa ina unyama, desturi ya vitwana,
Huweka heshima nyuma, kuwa hatuna maana,
Si utunzi wa hekima,hujengi jengo nakana
Washairi hupendana,kashifa si ushairi.

Kukashifu si kilema, kazi yao kutetana,
Kashifa haina wema, daima ni kuzozana,
Hamtapata ulama, kwani bure mwajiona,
Washairi hupedana, kashifa si ushauri,

Tusi huzidi husuma, na kuzii kutengana,
Nyoyo zao huwachoma, kusifu na kujivuna,

Mwisho hupata nakama, wakalia na kuguna,
Washairi hupendana, kashifu si ushairi.

Pendana kama Dodoma, sisi tunavyopendana,
Twafanya pendo lazima, na umoja kusikana,
Kimshambulia Juma, kundi lote mwapambana,
Washairi hupendana, kashifu si ushairi.

Dodoma watunzi hima, wapendana sana sana,
Tuwavute wa Mrima, mpate nanyi patina,
Na Unguja wadhama, sote tuje kuungana,
Washairi hupendana, kashifu si ushairi.

Mnakiharibu chama, vile mkibeuana,
Ndipo mwaivunja njama, kwalo zogo kuzozana,
Wengine watatulema, kwamba akili hatuna
Washairi hupendana, kashifu si ushairi.

Mwandike yenye mitima, maarifa kupeana,
Wafurahi wakisoma, wazee na wavulana,
Msitunge ya kukwama, mioyoni yakabana,
Washairi hupendana, kashifu si ushairi.

Fundisha watu kulima, maana kufundishana,
Fundisha watu kupima, mizani kufata vina,
Fundisha watu kufuma, fulana ama kusana,
Washairi hupendana, kashifu si ushairi.

Hapa ndiyo kaditama, wachokozi nawaona,
Wengine watu wazima, wanajifanya vijana,
Jambo hililingekoma, chama chetu kingefana,
Washairi hupendana, kashifu si ushairi.

15. Mzozo Wangu Patano

Siku zote ninaguna, huchungulia makano,
Hutokana na vijana, wasopenda shirikiano,
Daima wakizongana, hadi kwa utukanano,
Mzozo wangu patano, washairi hupendana.

Washairi hupatana, wakendesha mikutano,

Mikutano za maana, za kutengeza unono,
Unono tenzi kusana, vina vyenye mlingano,
Mzozo wangu patano, washairi hupendana.

Washairi hupendana,na hushikana mikono,
Haviji kubagukana, fitina na minong'ono,
Hakika si maungwana, mshairi mzozano,
Mzozo wangu patano, washairi hupendana

Tafadhali sihiyana, waase hao watano,
Nao nawapenda sana,wana uheshimiano,
Kwangu ubaya hawana, kuwa wana ukinzano,
Mzozo wangu patano, washairi hupendana.

Adam tumeonana, na kwa mashauriano,
Zungumzo limefana, kisha kwa mtulizano,
Ubaya kwake hakuna, hapendi machokozano,
Mzozo wangu patano, washairi hupendana.

Khalfani panga vina, ugomvi uwe mwagano,
Gonga ujaze makana,ufanye suluhishano,
Shikeni zenu supana, funga yenu mapigano,
Mzozo wangu patano,washairi hupendana

Na Makarani mwanana, fanyeni uhusiano,
Naye miraji hatakana, azidi shambuliano,
Walimwengu hukwaana, mwisho masameheano,
Mzozo wangu patano, washairi hupendana.\

Kwa marefu na mapana, mwache yenu matukano,
Kwayo kukashifiana, matusi na mfyonyano,
Ni tabia ya utwana, yenye rangi ya manjano,
Mzozo wangu patano, washairi hupendana.

Ya IIIahi ya Rabana, wajalie mapatano,
Wapeane muawana, yenye upenzi maneno,
Mawaidha kupeana, wasia na tangamano,
Mzozo wangu patano, washairi hupendana.

Namuomba Subuhana, alete afikiano,
Tuache kununiana, tupatane kama ngano,
Ndipo utunzi tanona,tuachapo utengano,

Mzozo wangu patano, washairi hupendana.

15. Bure Wanajikalifu.

Miraji Zodo mpenzi, hakika umwadilifu,
Nasifu wako utunzi, na vitendo kuvisifu,
Umewaonya wapinzi, waache zao kashifu,
Waipate tahafifu, wakikiri kuungana.

Umewaonya kitanzi, waogope kwa hawafu,
Umemulika kurunzi, wajione hitilafu,
Wajiondoe vibanzi, katika macho mabofu,
Wajiunga kisiafu, tuache kubagukana.

Adam apate gunzi, apasugwe pachafu,
Wawekwe katika konzi, kufanya usuluhifu,
Umoja huwa ni kanzi, zinapotunzwa sarafu,
Tujiunge kwa sufufu, tungo njema kuzisana.

Kanzi linaye mlinzi, si nyumbaya uhalifu,
Hapazuki na udwanzi, hali mbaya badilifu,
Si ulevi wa ulanzi, kuharibu utukufu,
Wamebaki wapungufu, hawataweza kunona.

Msikonde kama panzi, alokufa kinyamafu,
Mjipatie visunzi, na nyoyo vichefuchefu,
Ziwachome zetu tenzi, hali ziwe kudhoofu,
Mpaka mje hii safu, tukaacha kugombana.

Tamati tuna mianzi, ilonyoka na mirefu,
Mpanzi Mkurugenzi, kulinda hii tarafu,
Mlinziwe wa Makenzi, awajua maarufu,
Si vema kujikalifu,wasanifu hupatana.

16. Pendo- Chako Nimefurahi

Kukaa nanyi rafiki, kama leo sijawahi,
Sijawahi kudiriki,kuja kwenu wasabahi,
Mapendo nimehakiki, kwangu yana masilahi,
Penda – chako nafurahi, kwa Washairi wa Dar.

Sisemi kwa kujinaki, penda – chako nafurahi,
Nimefurahi kwa haki, kuchangamka wajihi,

Japo mimi ni kaniki,tambara liso na zihi,
Penda – chako nafurahi, kwa Washairi wa Dar.

Penzi lenu nasadiki, ni njema halikirihi,
Asemayye wazandiki, Mwenyezi amjeruhi,
Na mimi pia sichoki, kuwaombea IIIahi,
Penda – chako nafurahi, kwa Washairi wa Dar.

Na Mungu awabariki, vita mfanye suluhi,
Mapenzi kwenu yabaki, na itoweke kebehi
Uhuru tuumiliki, kuchao na asubuhi,
Penda – chako nafurahi, kwa Washairi wa Dar.

Kaditama siandiki, nakuoneni malihi,
Tusi sasa hamtaki, mambo mumetanabahi
Nawaombea Maliki, naomba kwenu nasahi
Penda – chako nafurahi, kwa Washairi wa Dar.

17. Shairi Johari Shwari

Shairi tunga tongole, kito hki cha johari,
Shair tuweke mbele, na moyoni tukariri,
Shairi tusome shule, tujifunze kubashiri,
Shairi johari shwari, tangu zamani za zale.

Shairi tangu za kale, walimwengu wahubiri,
Shairi ni ya milele, kwa Enjili na Zaburi,
Shairi niza wavyele, Abasi, Abubakari,
Shairi johari shwari, tangu zamani za zale.

Shairi niwasomele, wanaoleta kiburi,
Shairi si maumbile, matusi na machachari,
Shairi haliwi vile, shairi halina shari,
Shairi johari shwari, tangu zamani za zale.

Shairi halina ndwele, kugangua na tungari,
Shairi kauli pole, kuhubiri kwa shuwari,
Shairi siyo kelele, za matusi na jeuri,
Shairi johari shwari, tangu zamani za zale.

Shairi panda kilele, kuonyesha uhodari,
Shairi huchanjwi chale, kusudi uwe mahiri,

Shairi njoo ulole, linavyotungwa shairi,
Shairi johari shwari, tangu zamani za zale.

Shairi ni mgolole, kuitandua nadhiri,
Shairi ni kolekole, wengi katika bahari,
Shairi hasa taile, linotungwa kwa nadhari,
Shairi johari shwari, tangu zamani za zale.

Shairi ni pole pole, nenda mwendo wa saburi,
Shairi lina vidole, na kucha za msumari,
Shairi si magogole, yanayoleta khatari,
Shairi johari shwari, tangu zamani za zale.

Shairi neema tele, ushairi ni bohari,
Shairi lugha ikele, mshairi ni tajiri,
Shairi hizi na zile, zataka uziashiri,
Shairi johari shwari, tangu zamani za zale.

Shairi halina ole, kama vita vya hanjari,
Shairi halina yule, kilea kumuadhiri,
Shairi ja watu wale, wanaozuwia siri,
Shairi johari shwari, tangu zamani za zale.

Shairi na nikomile, nakutakeni kheri,
Shairi ukate kile, kinoleta kukasiri,
Shairi tushike ile, nia njema na dhamiri,
Shairi johari shwari, tangu zamani za zale.

18. Nashangilia Unguja

Salamu kwa mhariri, naja ninajikongoja,
Nakuletea habari, za kheri na zenye haja,
Na nakuombea kheri, si kama ninakufuja
Nashangilia Unguja, kipindi cha mashairi.

Kipindi cha mashairi, tuletee tafrija,
Kichungue kwa saburi, pasipokuwa haraja,
Isijepatwa na shari, yaletwayo na viroja,
Nashangilia Unguja, kipindi cha mashairi.

Mashairi twakariri, na yekimana faraja,
Huimbwa kama zomari, ipendezavyo wambeja,

Hata wimbi wa bahari, hutulia likangoja,
Nashangilia Unguja, kipindi cha mashairi.

Kaditama mshairi, nisalimu Bwana Hija,
Unguja yakusaburi, hata nasi tunakuja,
Bali tumwombe Kahari, mambo yasije kangaja
Nashangilia Unguja, kipindi cha mashairi.

19. Watunzi Tuna Huzuni

Ya IIIahi ya jalali, muumba wetu manani,
Muondolee thakili, mja wako Shaabani,
Alipwe yake fadhili, na kumuweka peponi,
Kifo cha Bwana Shaaban, kimetutia huzuni.

Kimetukata makali, na kututia huzuni,
Huzuni na udhalili, kwetu washairi nchini
Kupata pevu ajali, ya kifo chake Rubani,
Kifo cha Bwana Shaaban, kimetutia huzuni.

Bingwa lugha Kiswahili, alikuwa nambawani,
Elimu ya kila hali, kila mbinuza undani,
Wa Kiswahili kamili,cha lafidhi fasahani,
Kifo cha Bwana Shaaban, kimetutia huzuni.

Mtunzi mwenye akili, kila hali kila fani,
Vitabu kumi na mbili, kavitunga maishani,
Kimojawapo ni Adili, nao nduguze manyani,
Mola muweke peponi, mpenzi wetu Shaaban.

Ni hasara nakubali, kama walivyobaini,
Nyerere yake kauli, kangia sikitikoni,
Kusikitika hili, Kiswahili kuwa chini,
Watunzi tu msibani, tumepatwa na huzuni.

Kiswahili cha asili, na kingine cha kubuni,
Cha kuunga kwa achali, hupendeza sikizoni,
Kigumu na cha sahali, katumia vitabuni,
Mjini hata shuleni, mtunzi wetu Shaaban.

Akitumia kuwili, cha leo na cha zamani,

Kwa mujibu na maswali, na maneno ya kilingeni,
Huenda kila mahali, Afrika na Landani,
Nchi ilimtumaini, mpenzi wetu Robert.

Hakupenda ufedhuli, wala hakuutamani,
Alichukia jahili, ajifanyaye mhuni,
Na alijitenga mbali, akazama elimuni,
Amjaze rehemani, Shaaban Robert.

Alipendelea kweli, wongo kwake nuksani,
wala hakuwa bahili, kwa elimu duniani,
Na vitabuvye asali, kwayo yaliyomo ndani,
Kifo cha Bwana Shaaban, kimetutia huzuni.

Kaditama kwa dalili, atapokewa Lijani,
Amefariki kwa mwili, na uzima u rohoni.
Kisomo cha tahalili, peleka rohoye mbinguni,
Mola amweke peponi, Shaaban Robert.

20. Kifo cha Bwana Robert

Rambirambi nazituma, kwakeye Bibi Robert,
Nazituma kwa huruma, kujizuia sipati,
Kwao watoto na mama, walolia kwa sauti,
Kifo cha Bwana Robert, hasara kwa Kiswahili.

Ni hasara kwa nchi nzima, ninayasemakwa dhati,
Ni kama taa kuzima, usiku wa katikati,
Kiswahili tainama, kwa kukosa kalafati,
Kifo cha Bwana Robert, hasara kwa Kiswahili.

Umkaribishe pema, Jaala Wabarakati,
Apate kwako rehema, umjalie bahati,
Mkidhi yao neema, huko peponi aketi,
Kifo cha Bwana Robert, hasara kwa Kiswahili.

Japo dunia kahama, kwa kumfika mauti,
Japo kaacha yatima, wavulana na benati,
Namuombea salama, mwondolee vizingiti,
Kifo cha Bwana Robert, hasara kwa Kiswahili.

Ndiye bingwa wanudhuma, fundi kuzipanga beti,

Mjuaji wa kupima, mashairiye yakuti,
Kila aliyeyasoma, hakukuta tofauti,
Kifo cha Bwana Robert, hasara kwa Kiswahili.

Kajipatia heshima, na sifa njema thabiti,
Kuandika na kusema, yeye hakuwa katiti,
Imara alisimama, kwa utunzi madhubuti,
Kifo cha Bwana Robert, hasara kwa Kiswahili.

Na ndiye mwenye ulama, wa Kiswahili la dhati,
Alikuwa mwanachama, Kiswahili kutafiti,
Tena alikuwa mwema, alipendwa na umati,
Kifo cha Bwana Robert, hasara kwa Kiswahili.

Vitabuvye vya hekima, alivyotunga mufti,
Kati havina kilema, na kuleta ati ati,
Ni vitabu vyenye mema, havinao usaliti,
Kifo cha Bwana Robert, hasara kwa Kiswahili.

Maisha yetu hukoma, unapofika wakati,
Na kama maji huzama, kulitimiza shariti,
Walimwengu hulalama, na kuupata kibuhuti,
Kifo cha Bwana Robert, hasara kwa Kiswahili.

Tulobaki twainama, na lini yetu sanati,
Njia tupate yandama, kuifuata sirati,
Tunamuomba Karima, tufanikiwe jahati,
Mwondolee vizingiti, apumzike Shaaban.

Hapa ndipo kaditama, nakifunga kidawati,
Machungu yanipa homa, chini napiga magoti,
Namuomba Allahuma, Jalia Wabarakati,
Namtakia bahati, akaribishwe peponi.

21. **Komesheni Magombano**

Mwache mkiki-mkiki, ugomvi na matetano,
Nakanya hamkanyiki, mnazidi mzozano,
Nasema halisimbuki, simbiko kwazo mifano,
komesheni magombano, watunzi ni marafiki.

Nipigwe sikasiriki, nawakanya maashindano,

Shindano halitatiki, kidimbwi ndani ya chano,
Ninyukwe sitetereki, haja yangu muungano,
Komesheni mangombano, watunzi ni marafiki.

Dhihaka huleta chuki, na huvuta utengano,
Tengano huleta dhiki, ingiapo minong'ono,
Na ngoma haichezeki, wingiapo mpambano,
Komesheni mangombano, watunzi ni marafiki

Jitukali hashindiki, na bomu za mabishano,
Nyamaume harudiki, kashika safu ya tano,
Waloanzisha sabiki, sasa wana tulizano,
Komesheni mangombano, watunzi ni marafiki.

Nyamaume ni rafiki, Jitukali naye mno,
Nuru ndiye mshiriki, binti wetu shikamano,
Amri simfariki, msimulizi wa ngano,
Komesheni mangombano, watunzi ni marafiki.

Mshairi tamalaki, ni Shaaban mnono,
Afrika Mashariki, ndiye mwenye julikano,
Watunzi kaumiliki, mkuu wa mikutano,
Komesheni mangombano, watunzi ni marafiki.

Tafuta neno la haki, tuepuke ukinzano,
Tuwavutehalaiki, tupate mwongezekano,
Twongezeke tuwe laki, tuwe na afikiano,
Komesheni magombano, watunzi ni marafiki.

Snow haambiliki, kwa wembe miburuzano,
Mandevu alaidiki, na ndevu hana makano,
Mlanzi hatataniki, ubishi na jibizano,
Komesheni magombano, watunzi ni marafiki.

Robati naye hataki, hakubali ridhiano,
Hakubali haridhiki, ridhaa ya maoano,
Na Kiwato hafutiki, atajwa uchokozano,
Komesheni magombano, watunzi ni marafiki.

Mwinyihatibu handaki, maficho ya mapigano,
Mtu-Chake na mswaki, huku asafisha meno,
Huo ukali wa nyuki, wa mbio mfukuzano,

Komesheni magombano, watunzi ni marafiki.

Si furahi sitosheki, jambo hili mng'ang'ano,
Penzi halitakasiki, lasinzinsha kama pono,
Pono huwa haamki, hadi pigo kwa mguno,
Komesheni magombano, watunzi ni marafiki.

Tusifanye uzandiki, vijembe mikwaruzano,
Hivyo huleta hamaki, na kutiana mikono,
Nayo siyo itifaki, iletayo husiano,
Komesheni magombano, watunzi ni marafiki.
Tamai mashabiki, uwacheni mzongano,
Kioa ukitaliki, ni lenu sikilizano,
Kiacheni kisa hiki, kimechakaa mshono,
Komesheni magombano, watunzi ni marafiki.

22. Tungeni Mtiririko

Mhariri mahabubu, pokea wangu mwandiko,
Napenda kuwahutubu,washairi walioko,
Si kama nawaghailibu,na kujitia vituko
Tungeni mtirirko, na silabi kuhasibu.

Msichukue ghadhabu, kwa mabavu na vituko,
Lichungulie taratibu, usanifu beti zako,
Kama wajibu jawabu, ukae kwanza kitako,
Tungeni mtirirko, na silabi kuhasibu.

Nisikie masharubu, wape habari wa keko,
Mwinginw sikughilibu, na vingine lisiweko,
Sitoke kwenye kilabu, ukajidai mwandiko
Tungeni mtirirko, na silabi kuhasibu.

Uliza kwanza swahibu, umwendee kwa kicheko,
Pekee taliharibu, likose hata mwitiko,
Bali wepuke kidhabu,huyo awe sumu kwako,
Tungeni mtirirko, na silabi kuhasibu.

Kisa kilichokusibu, kipate nacho mwandiko,
Maanaye na sababu, mwanzo ni chokochoko,
Ni kipawa cha Wahabu,usipate masumbuko
Tungeni mtirirko, na silabi kuhasibu.

Mwendo huo siharibu,vinginevyo lisiweko,
Ukianza na Hatibu, simwite tena Maiko,
Na uzuri wa dhahabu, sitie mchanganyiko,
Tungeni mtirirko, na silabi kuhasibu.

Tungozo ziwe dhahabu, zambatane na mwitiko,
Wengi wasitaajabu, jinsi ya mtiririko,
Liimbwapo ni taibu, lipendeze walioko,
Tungeni mtirirko, na silabi kuhasibu.

Asiliye ughaibu, moyoni ndilo chimbuko,
Yaliimbwa na mababu, hao waliokuweko,
Hawakulewa sharabu, waliotunza tambiko,
Tungeni mtiririko, na silabi kuhasibu.

Walotunga ya thawabu, na matusi yasiweko,
Watunzaji wa medhehebu, na dini na zilizoko,
Kumtukuza wahabu, majambo mtakasiko,
Tungeni mtiririko, na silabi kuhasibu.

Beti kumi kwa hesabu, hazina mchanganyiko,
Nimemuweka Katibu, hapo kaka kitako,
Kati`bu' imeratibu, mwisho `ko' imekuweko,
Tungeni mtiririko, na silabi kuhasibu.

23. Dodoma Imeitika.

Shairi nenda kunena, kwa wale waheshimika,
Useme asante sana, kwa upole kitamka,
Hapana budi hapana, tena wasiwe na shaka,
Dodoma imeitika, mwaliko wa kuungana.

Mwaliko wa kuungana, Bwana jaha alotaka,
Hili jambo la maana, na si jambo la dhihaka,
Vema kushirikiana, twache walohadaika,
Dodoma imeitika, mwaliko wa kuungana.

Ni bora kushikamana, Unguja na Tanganyika,
Kwa marefu na mapana, tufurahi na kucheka,
Tucheke na kuwaguna, wale waliobaguka,
Dodoma imeitika, mwaliko wa kuungana.

Hatuwezi kuachana, kwa tisho la paparika,
Tuzidi kuambatana, japo pirika pirika,
Na wale tukishindana, wasopenda kushindika,
Dodoma imeitika, mwaliko wa kuungana.

Kwa vita vya kupigana, adui walochimbuka,
Chimbuko kutetana, na kitali kikafika,
Penzi halina fitina, ya kuharibu shirika,
Dodoma imeitika, mwaliko wa kuungana.

Hija Salehe mwungwana, mshairi mtajika,
Bai Mohamed Bwana, Dodoma yashangilia,
Nilosahau majina, ni nyote kujumuika,
Dodoma imeitika, mwaliko wa kuungana.

Ofisi yatajazana, hata ikisomwa mwaka,
Yenye sanaa ya vina, tungo zenye kunyooka,
Mashairi twamimina, na beti kutiririka,
Dodoma imeitika, mwaliko wa kuungana.

Utunzi si kujivuna, kama alivyo ‘Mnyuka’,
Watunzi ni kupendana, pendo huleta Baraka,
Bali si kubeuana, kuitana nyangarika,
Dodoma imeitika, mwaliko wa kuungana.

Takuja tembeleana,ninyi nasi kadhalika,
Bora kuamkiana, na hamu zitakatika,
Kwa mikono kushikana, ndipo nyuso takunjuka,
Dodoma imeitika, mwaliko wa kuungana.

Naomba Maulana, mapenzi kushamilika,
Yashike na kushibana, hapana kuvurugika,
Kaditama naagika, na mlango kufunguka,
Dodoma imeitika, mwaliko wa kuungana.

24. Zama Zetu za Siasa

Zamani za mazezetna, leo si za kufuasa,
Si zamani za kung’eta, ulimaji wa sesa,
Zama hizi za kutota, zataka upole sana,

Zama hizi za siasa, ni zama za tahadhari.

Ni zamani za kunyata, kula mboga ya msusa,
Hizi ni zama za kwata, na vichwa kuvitikisa,
Sizo zama za kubwata, za maneno ya ufyosa,
Zama hizi za siasa, ni zama za tahadhari.

Zama zile zimepita, za watu kuwanyanyasa,
Zile zama zakututa, na kunyang'anya mapesa,
Hizi zama za matata, kuchunguzana makosa,
Zama hizi za siasa, ni zama za tahadhari.

Zino zama za kuteta, zenye visa na mikasa,
Sizo zama za kupata, kwa dhuluma na kutesa,
Ni zama za kuambata, yenye haki inopasa,
Zama hizi za siasa, ni zama za tahadhari.

Zama hizi za kujuta, zama zetu za Siasa,
Sizo za kufurukuta, na za macho kupepesa,
Ni zamani za kukata, makali na kuyatosa,
Zama hizi za siasa, ni zama za tahadhari.

Ni zama hizi za kufuata, haki zao watu hasa,
Ni zamani za kufuta, mawazo yenye anasa,
Sizo zama za kuchota, wala dhuluma kunusa,
Zama hizi za siasa, ni zama za tahadhari.

Sizo zama za mafuta, za kucheza kibemasa,
Wala sizo za kuota, za njozi za kutomasa,
Si zama za kuokota, kujipatia halasa,
Zama hizi za siasa, ni zama za tahadhari.

Si zama za kujiita,lile jina la Mtesa,
Wala sizo za kukita, kupata mali kwa visa,
Hizi zama za kusita, za rai na kupapasa,
Zama hizi za siasa, ni zama za tahadhari.

Wangapi yamewapata,kwa kutafuta ukwasa,
Kuona vyameremeta,mijimali na vipusa,
Siasa iliwakuta,sasa wacheza kibisa,
Zama hizi za siasa, ni zama za tahadhari.

Kaditama nimegota, tujihadhari kabisa,
Haki yetu kukamata, hata kama vile tosa,
Kama twapenda kuseta, dunia itatususa,
Zama hizi za siasa, ni zama za tahadhari.

25. Uhuru una Kiungo

Chekelea wanaume, wenye meno na mapengo,
Shukurani muiname, mpunzishe maungo,
Na miili zitereme, mng'ae kama mpingo,
Uhuru una kiungo, wanyonge kufutwa kodi.

Leo pateni unyeme, nyoosheni zenu shingo,
Maneno tena siseme, yalowavunja vibyongo,
Leo hebu msimame, nyosheni yenu migongo
Uhuru una kiungo, wanyonge kufutwa kodi.

Limeni fedha mchume, mumefanyiwa mipango,
Shuleni wana wasome, yakifikie kiwango,
Kirudi nchini watame, yamekwisha masimango,
Uhuru una kiungo, wanyonge kufutwa kodi.

Hapo ilikuwa ngome, aso kodi ni msungo,
Alitandikwa akome, na gerezani kifungo,
Hebu sasa tupime, Dola sasa si kiungo?
Uhuru una kiungo, wanyonge kufutwa kodi.

26. Watumishi Tusimame

Kala natunga shairi, chama kukitia shime,
Ili nipate hubiri, japo mimi si mtume,
Bali ninayo fahari, hili langu niliseme,
Watumishi tusimame, haki tudai tajiri.

Hebu tudai tajiri, mbele yake tulalame,
Jioni alfajiri, tumwambie ayapime,
Maombi si kukasiri, ya mapigano kwa sime,
Watumishi tusimame, haki tudai tajiri.

Tumika siwe kiburi, simama u mwanamume,

Acha usiwe jeuri, kama Yule paka-shume,
Pato udai dahari, mbele yake mfalme,
Watumishi tusimame,haki tudai tajiri.

Tusivunje itibari, tukisamama kinyume,
Dai letu ni dhahiri, mali nasi tuichume,
Kila alotuajiri, dai mate asiteme,
Watumishi tusimame,haki tudai tajiri.

27. Muungano Utupambe

Wahabu mwenye uwezo, muumba vyote viumbe,
Ndiwe muwekaji nguzo, tangu pembe hadi pembe,
Tuondolee mizozo, mataifa wasigombe,
Sisi sote tu viumbe, tuunganike pamoja.

Twondolee matatizo, ghururi isitumbe,
Ugomvi na machukizo, mfano wana wakembe,
Tuletee matulizo, tufurahi yatupambe,
Sisi sote tu viumbe, tuunganike pamoja.

Zisijezuka michezo, kama zile kina Tshombe,
Wenye kuleta utwezo,kuiondoa halambe,
Amani iwe enezo, na waasi wasitambe,
Sisi sote tu viumbe, tuunganike pamoja.

Mwungano uwe mkazo, Kenya wapate ulumbe,
Waondolee vikwazo, vya Majimbo kwa wajumbe,
Waunge mapendekezo, ya umoja wa kamambe,
Sisi sote tu viumbe, tuunganike pamoja.

Tanganyika ni igizo, kushikamana iwambe,
Hilo liwe elekezo, na Unguja waliombe,
Na Rhodesia agizo, wasibagukane chembe,
Sisi sote tu viumbe, tuunganike pamoja.

Utupe mema mawazo, siwe kama wanywa pombe,
Twondolee angamizo, la mchezo wa kizembe,
Tujalie ya tulizo, si ya ukali kwa wembe,
Sisi sote tu viumbe, tuunganike pamoja.

Wenye haki wadaizo, ingawaje ni kikombe,

Na hao wadaiwazo, macho yao wasifumbe,
Wasifanye mapuuzo, vichwani waote pembe,
Sisi sote tu viumbe, tuunganike pamoja.

Mreno silete bezo, na nchi zile azisombe,
Ondowe tama hizo, dunia isimchambe,
Ni lipi liwe pendezo, amwachie Bwana Gwambe,
Sisi sote tu viumbe, tuunganike pamoja.

Twahitaji barakazo, tusiombe kwa ubembe,
Tuziombe kwa chetezo, kila sala tuichimbe,
Twategemea mwongozo, wa arusi na wapambe,
Sisi sote tu viumbe, tuunganike pamoja.

Kaditama tupe pozo, nasi maovu tusambe,
Twondolee mikwaruzo, kwa mabomu watutimbe,
Tupe mema mzo mzo, tusalimike viumbe,
Sisi sote tu viumbe, tuunganike pamoja.

28. Mwaka Uwe wa Heri.

Mwaka uwe na unono,wa Baraka na neema,
Isiwepo minong'ono, hayo huleta husuma,
Tuyavune na mavuno, na nchini pawe salama,
Mwaka uwe wa neema, wenye heri na fanaka.

Sipunguze mapatano, bali tujaze huruma,
Si imani ya maneno, njiani tukiloloma,
Imani mwafikiano, na tuitupe dhuluma,
Mwaka uwe wa neema, wenye heri na fanaka.

Pasiwe miburuzano, kwa vitara na zahama,
Rabbi punguza mbano, vita havina salama,
Heri fanya mapatano, bora na yenye heshima,
Mwaka uwe wa neema, wenye heri na fanaka.

Ugogo na iwe nono,njaa nchini kutuhama,
Ifupishe mwandamano, njaa inavyotuuma,
Furaha kuwa miguno, wana kwa watu wazima,
Mwaka uwe wa neema, wenye heri na fanaka.

Elimu uwe mfano, wa mwanga ulio mwema,

Giza na liwe mwagano, mwanzo wa kulisukuma,
Siwe kama konokono, asofunzwa taalamu,
Mwaka uwe wa neema, wenye heri na fanaka.

Shirika uwe mfano,kwa Tanganyika mzima,
Tuyaache matetano, magombano siyo mema,
Bora mashirikiano, ndilo jambo lilo jema,
Mwaka uwe wa neema, wenye heri na fanaka.

29. Shirika ni Kustawi

Mhariri mahashumu, pambo la shina matawi,
Wasema wataalamu, muacha wingi mchawi,
Shirika kweli ni tamu, baya halihesabiwi,
Shirika ni kusitawi, vibaya kufarakana.

Kuandika nina hamu,kisha tena sichelewi,
Japo mimi si mwalimu, lau heshima sipewi,
Una wengi mahasimu, na kundini sitakiwi,
Shirika ni kusitawi, vibaya kufarakana.

Maneno haya muhimu, msijifanye viziwi,
Sijifanye madhalimu, kuchomana kama biwi,
Huo huitwa wazimu,pendo haliharibiwi,
Shirika ni kusitawi, vibaya kufarakana.

Tuliepuke shutumu, kwani hutafanikiwa,
Jamani hayo haramu, kwa Mola hupokelewi,
Kwetu sote ndio sumu, na kuharibu hukawi,
Shirika ni kusitawi, vibaya kufarakana.

Bora mapenzi yadumu, shirika itasitawi,
Na tuishi tabasamu, kwa neema kama Fiwi,
Tutaipata naimu, ikiwa hatuchezewi
Shirika ni kusitawi, vibaya kufarakana.

Hebu tushike hatamu, Mdigo na Msandawi,
Wakubwa tuwaheshimu, kama mtoto na chuwi,
Wazee nanyi ghulamu, hata viluwiluwi,
Shirika ni kusitawi, vibaya kufarakana.

Sote inatulazimu, kama hudharauliwi,

Mzima na mwenye pumu, baya huyu hatendewi,
Kila mtu ana zamu, kama moja hazuliwi,
Shirika ni kusitawi, vibaya kufarakana.

Ijapokuwa vigumu, kiburi hakitakiwi,
Ye yote kila makamu, chuki haithaminiwi,
Asiyejua kukimu, nyumbani hafurahiwi,
Shirika ni kusitawi, vibaya kufarakana.

Sijifanye mahamumu,kwamba hubanduliwi,
Heshima tuikasimu, kitunza husumbuliwi,
Paka wakati utimu, furaha husulibiwi,
Shirika ni kusitawi, vibaya kufarakana.

Kaditama takadamu, moyo kaupake kiwi,
Tuliambae hujumu, tuukoke usodawi,
Tuipate jukumu, maishayo huchukiwi,
Shirika ni kusitawi, vibaya kufarakana.

30. Kura Tumezifagia

Utungaji wenye kina, wananchi nawatungia,
Natunga yenye maana, hakuna wakubishia,
Abishaye tamsana, kama neno ababia,
Tanu imezifagia, kura tatu kazi bure.

Kura tatu nazikana, tena zisije tukia,
Zisije kuonekana, uknda huu wasia,
Wasia wangu wabana, nabana nakuzingia,
Tanu imezifagia, kura tatu kazi bure.

Kura tatu si mwanana, kwa mwenendo wa tabia,
Si mwendo mwema nakana, nakana nakuchukia,
Chukio la kuuchana,shimoni kuufukia,
Tanu imezifagia, kura tatu kazi bure.

Si tabia ya mwungwana,mimi najikatalia,
Vitabu tulobishana, si vema kuchanganyia,
Wavichanganya vitwana, na mabwana kupangia,
Tanu imezifagia, kura tatu kazi bure.

Leo si kundanganyana, senti tuite Rupia,

Danganyo ni kutupana, siwezi na nitalia,
Huko mbele takutana, mlango kitufungia,
Tanu imezifagia, kura tatu kazi bure.

Je sasa mumeona, hayo tuloahidia?
Tuliahidi kuvuna, ushindi kujipatia,
Twapata bila kuguna, mpaka yametimia,
Tanu imezifagia, kura tatu kazi bure.

Kwa marefu na mapana, wala hatutasinzia,
Usingizi wa manna, na ugolo kubugia,
Tumeamka mchana, na macho twawakazia,
Tanu imezifagia, kura tatu kazi bure.

Kaditama kuonyana, na kudai Uhuria,
Uhuru wenye kufana, ambao twatazamia,
Na tutashukuru sana, Mungu akitujalia,
Tanu imezifagia, kura tatu kazi bure.

31. Siku ya Historia

Ni siku ya kukumbuka, nyandiko nayandikia,
Ni siku ya kulimbuka, hatua kuifikia,
Kizingiti tumevuka, imebaki kuingia,
Siku ya Historia, Oktoba Edashara.

Ni hii naiandika, siku ya Historia,
Ni siku ya madaraka, tuliotukitazamia,
Hapa kwetu Tanganyika, nyoyo zikitamania,
Siku ya Historia, Oktoba Edashara.

Leo yametimilika,tulivyo kisimulia,
Gavana alotamka,alipotuahidia,
Hivi leo tumefika, hayo kutumainia,
Siku ya Historia, Oktoba Edashara.

Mlango umefunguka, tulipofungiwa njia,
Kwa kelele tukitaka,wananchi tukililia,
Sasa hatuna mashaka, mavuno tajivunia,
Siku ya Historia, Oktoba Edashara.

Mwakani tutaishika, nchi yetu kuwa huria,
Bendera taitundika, juu itaning'inia,
Ya wageni kutunguka, sandukuni kuitia,
Siku ya Historia, Oktoba Edashara.

Jipu limetutumbuka, mwilini lilovimbia,
Mili zilisawajika, na nyusoni kufifia,
Inshallah yatatoweka, viti tutavikalia,
Siku ya Historia, Oktoba Edashara.

Tushike shoka kufyeka, na jembe kupalilia,
Twende mwendo patashika, mabonde kujilimia,
Tutaipata fanaka, na mali kujichumia,
Siku ya Historia, Oktoba Edashara.

Oktoba ni mpaka, hapana wa kutania,
Oktoba tumechoka, mwingine kutupimia,
Oktoba tumeshika, nguvu twajichukulia,
Siku ya Historia, Oktoba Edashara.

Nchi yetu ni heshimika, ya Mwongozi asilia,
Watu wameunganika, katu hawana udhuia,
Po pote tunasifika, Ulaya hadi India,
Siku ya Historia, Oktoba Edashara.

Twamshukuru Rabuka, Muumba nchi na dunia,
Taifa kusalimika, wa mbali wakasifia,
Hatutamaliza mwaka, Uhuru tajipatia,
Siku ya Historia, Oktoba Edashara.

32. Ni Madaraka Kamili

Twakushukuru Mkwasi, Muumba wetu jalali,
Kwa kuishika Turusi,Utemi wetu halali,
Tuushike wadinasi, ututoke udhalili,
Madaraka ya kamili, Mei mosi tumefika.

Tumewashinda wasasi, kesho hawatutawali,
Madhila ya wasiwasi, vitanzi kutukabili,
Bali tuepuke mikosi, mitato tuzijadili,
Madaraka ya kamili, Mei mosi tumefika.

Zimefurahi nafusi, kwa madaraka kamili,
Mioyo kuwa shumusi, mwanga washinda kandili,
Twafurahi wafuasi, jamii ya waswahili,
Madaraka ya kamili, Mei mosi tumefika.

Baraza la Majilisi, naliombea kubuli,
Lishami kwa nemusi, tangu mosi hadi pili,
Kebeneti ya weusi, mwongozi mwenye akili,
Madaraka ya kamili, Mei mosi tumefika.

Desembakadamnasi, bendera tuibadili,
Na mambo tukidurusu, ni nani dume fahari?
Hata Januari mosi, tufunge kufuli,
Madaraka ya kamili, Mei mosi tumefika.

Migogoro ziwe basi, zifungwe mbaya kauli,
Zikomeshwe tetesi, na chungu ya pilipili,
Nchi nayo ipigwe pasi, na iwe kama asali,
Madaraka ya kamili, Mei mosi tumefika.

Tanganyika nchi fususi, wajua kila pahali,
Mwongozi wetu Raisi, wananchi wanamjali,
Twakuombea Qudusi,akuzidishe ukweli,
Madaraka ya kamili, Mei mosi tumefika.

Heko Nyerere kapasi, heko yake stahili,
Heko mwongozi farisi, heko wetu jamili,
Heko mpasi khalisi, kwa maombi na kusali,
Madaraka ya kamili, Mei mosi tumefika.

Pepo zivume za kusi, na matlai kuwili,
Za umande zije Rasi, na unenepeshwe mwili,
Na upate ufanisi, kila mwendo kila hali,
Madaraka ya kamili, Mei mosi tumefika.

Kaditama uandishi, nakuimbia Yaleli,
Nakuimbia kiasi, ya Uhuru kuwasili,
Desemba njoo upesi, wa nyota njema sahali,
Madaraka ya kamili, Mei mosi tumefika.

33. Mpya Sasa Tanganyika

Nakuja nisimulie, kwa moyo kufurahika,
Shairi niwaimbie, hewani kusikilika,
Ni haki nifurahie, nchi mpya imeumbika,
Mpya sasa Tanganyika, ya kale imetoweka.

Jirani mkazanie, siasa njema tamka,
Vijembe situtupie, kwamba tunahangaika,
Shika chombo uvukie, tajaliwa na Rabuka,
Mpya sasa Tanganyika, ya kale imetoweka.

Njooni muangalie, nchi yetu imegeuka,
Njooni mshuhudie, nchi ilodharaulika,
Njooni muisifie,sasa inavyotukuka,
Mpya sasa Tanganyika, ya kale imetoweka.

Acha tuwatangulie, mlivyo mkitucheka,
Njoo mwone uzurie, kila jambo laongoka,
Ngoa msitulilie, kwa mwendo wetu kunyoka,
Mpya sasa Tanganyika, ya kale imetoweka.

Utenzi niitungie, nchi sahibu Tanganyika,
Walo mbali wasikie, kwamba tuna madaraka,
Nchi yetu tujivunie, tuiombee Baraka,
Mpya sasa Tanganyika, ya kale imetoweka.

Uganda na ikisie, jinsi iloheshimika,
Na Kenya tufuatie, tunayajua hakika,
Unguja tusikawie, haikuwa na mashaka,
Mpya sasa Tanganyika, ya kale imetoweka.

Tanganyika siitie, ilikuwa nyangarika,
Wengi waidharawie, na haikuhesabika,
Ndo nchi wagombanie, dachi, Ngereza kateka,
Mpya sasa Tanganyika, ya kale imetoweka.

Nyasa haina fanie, mpaka huko Lusaka,
Rhodesia ya kusinie, pote ilelimika,
Tanganyika ibakie, nyuma ilicheleweka,
Mpya sasa Tanganyika, ya kale imetoweka.

Ni nani atutanie, kuwa haya twaropoka?
Ni nani atubishie, mtu alodanganyika?
Inayo kubwa hadhie, imegota na mpaka,
Mpya sasa Tanganyika, ya kale imetoweka.

Wadudi amjalie, Bwana Nyerere msifika,
Umri amzidishe, maisha kuongezeka,
Baraka umjalie,Tanganyika kuokoka,
Mpya sasa Tanganyika, ya kale imetoweka.

Nasi tusilimatie, sauti yake kusika,
Tuidake turidhie, mwito wake kuitika,
Sote tuishangilie, pamoja kwa ushirika
Mpya sasa Tanganyika, ya kale imetoweka.

Tama uma siwachie, paka safari kufika,
Tushike tusisinzie, pamoja kuunganika,
Gavana asaidie, Bendera kuitundika
Mpya sasa Tanganyika, ya kale imetoweka.

34. 1960 Madaraka Tumebeba

Huu ndio mwaka wako, uvikwe chako kikuba,
Eleka yako mbeleko, tulee wana kwa huba,
Tamba kule utabarako, Nyerere mahabuba,
Madaraka tumebeba, baki uhuru kamili.

Nilikuwako Lejiko, kuisikiza hotuba
Likatolewa tamko, tulifurahi si haba,
Kuondoa sikitiko, yatimizwe matilaba,
Madaraka tumebeba, baki uhuru kamili.

Safari na masumbuko, kama tabu na misiba,
Mabonde na miinuko, vipeto nazo kuruba
Leo letu limbuko, umekwisha mkataba,
Madaraka tumebeba, baki uhuru kamili.

Japo misukosuko, mambo ya kigoba-goba,
Yenye tabu na vituko, kwa ujuvi na ujuba,
Tumekivuka kivuko, mkoba tumeubeba,
Madaraka tumebeba, baki uhuru kamili.

Tumepata farijiko, kubeba wetu mkoba,
Limetoka badiliko, nahubiri kwa katiba,
Sote tunatoa heko, twashukuru kwa haiba
Madaraka tumebeba, baki uhuru kamili.

Limeitika tambiko, shetani aliloziba,
Limekwepa hadaiko, kudhulumiwa kibaba,
Inaondoka haiku, haki yetu kutuiba,
Madaraka tumebeba, baki uhuru kamili.

Tusijekaa kitako, pori tupige dharuba,
Panga tutie matiko, na kazi ndio kushiba,
Mapori kwa mfyeko, kuitafuta rutuba,
Madaraka tumebeba, baki uhuru kamili.

Tusitawishe masoko,kwa mazao na viliba,
Nchi ipate tajiriko, kwa ukulima na shaba,
Ndipo ipate tukuko, na kuondoka kalaba,
Madaraka tumebeba, baki uhuru kamili.

Vimepungua vituko, afadhali kama buba,
Limeanza pukutiko, kama kuepuka waba,
Tumewapita wa huko, imekuwa mara saba,
Madaraka tumebeba, baki uhuru kamili.

Jamani tutie mbeko, tushukuru yeye baba,
Cha kwako kiwe ni chako, cha asili na nasaba,
Katu hakina ponyoko, utakipata suhuba
Madaraka tumebeba, baki uhuru kamili.

Tama cheleko cheleko, wa hapa hata Bukoba,
Lipu lipu mlipuko, shangilieni mazuba,
Ondoeni hangaiko, leo tumelipa tiba,
Madaraka tumebeba, baki uhuru kamili.

35. Twaomba Ubarikiwe.

Ahasante kiongozi, yapasa ushukuriwe,
Umetupa utambuzi,kusudi tuzinduliwe,
Tumjuwe waziwazi, Bwa Nyerere na wanawe,

Twaomba ubarikiwe, na jamii yako pia.

Ewe wetu muongozi, twaomba ubarikiwe,
Mwongozi mwenye mbawazi, upendaye twokolewe,
Akubariki Mwenyezi, shabaha ufanikiwe
Twaomba ubarikiwe, na jamii yako pia.

Maria mama azizi, kwetu sidharauliwe,
Wewe ndiwe mwangalizi, kheri njema ujaliwe,
Nyumbani ndiwe mlezi, lazima uhesimiwe,
Twaomba ubarikiwe, na jamii yako pia.

Andrea ni muhozi, madaraka na apewe,
Ni yeye mtangulizi, wa kwanza ahesabiwe,
Mfugunzi wa kizazi, halafu afuatiwe,
Twaomba ubarikiwe, na jamii yako pia.

Wa pili ndiye mwombezi, Bi Anna ahifadhiwe,
Pasitoke kumuhizi, moyo wake uchukiwe,
Asipate matatizi, mitato zitatuliwe,
Twaomba ubarikiwe, na jamii yako pia.

Tatu bila pingamizi, mwingine na azaliwe,
Anselmi mgunduzi, kaptikana sikawe,
Kua uote mizizi, kinyume vingine siwe,
Twaomba ubarikiwe, na jamii yako pia.

Nne kaja mwamuzi, kumpata mwinginewe,
Pasi kupata simazi, John ikawa na awe,
Elimu mzama mbizi, mafumbo yafumbuliwe,
Twaomba ubarikiwe, na jamii yako pia.

Tano Karoli mbalamwezi, dunia afanikiwe,
Mja ipima timazi, pabovu pabomolewe,
Kaja kuhimiza kazi, na uvivu uondolewe,
Twaomba ubarikiwe, na jamii yako pia.

Pasizuke wachafuzi, wa tabia kama mwewe,
Ambao ni wabazazi, hao ni walaaniwe,
Bana walie machozi, wajilaumu wenyewe,
Twaomba ubarikiwe, na jamii yako pia.

Tamati bila ajizi, maisha muongezewe,
Pia na kupnda ngazi, kufaulu ukidhiwe,
Tena nakupa pongezi,nchi inyanyuliwe,
Twaomba ubarikiwe, na jamii yako pia.

36. Duri Nadawiri Zari

Zijevumishwa Buruji, siku yetu ya Uhuri,
Beramu na kudariji, kuwapanga Asikari,
Ananchi kuwafariji, kutuliza yao mori,
Duri nadawiri zari, apambwe mhesimiwa.

Zari hupambiwa Taji, za Watemi mashuhuri,
Kama Nyerere yu gwiji, kaonyesha uhodari,
Nyotaye itabalaji, ya Jaha alfajiri,
Duri nadawiri zari, apambwe mhesimiwa.

Ameyashinda maleleji, ya dharuba za bahari,
Wamemtema walaji, wa mapanga na hanjari,
Na hila za kuhariji, walaili walaili wanahari
Duri nadawiri zari, apambwe mhesimiwa.

Nimpambe msanaji, duri nadawiri zari,
Liwake kama siraji, Alimasi na johari,
Nuru ifike Ujiji, kila pahari dhahiri,
Duri nadawiri zari, apambwe mhesimiwa.

Hapo waimbe wimbaji, waziwazi si kwa siri,
Vitongojini na miji, tufungamane sanjari,
Papo nasi watungaji, tumwimbie mashairi,
Duri nadawiri zari, apambwe mhesimiwa.

Hatutaki wafujaji, wajeuri na viburi,
Hatutaki wavunjaji, wa sheria na Amri,
Wapole tunahitaji, wamwogopao Kahari,
Duri nadawiri zari, apambwe mhesimiwa.

Wewe ni samba wa maji, baharini hadi pori,
Wa Bara na Msumbiji, kwako wanayo fahari,

Umeshinda wawindaji, wasasi na Takisiri,
Duri nadawiri zari, apambwe mhesimiwa.

Wageni nasi wenyeji, na sote tunakukiri,
Wako mwema wongozaji, Mkuu wetu Waziri,
Ombi letu twataraji,uzidishiwe umri,
Duri nadawiri zari, apambwe mhesimiwa.

Mungu kakupa kipaji, Mwumba wetu wa dahari,
Kushindana naWambuji, kwa siasa ya nadhari,
Umekuwa mshindaji, ajiri ya ujasiri,
Duri nadawiri zari, apambwe mhesimiwa.

Kaditama wasomaji, bora tumwombee kheri
Adumu utawalaji, mbele asipate shari,
Afaulu uchungaji, maarifa kukithiri,
Duri nadawiri zari, apambwe mhesimiwa.

37. Mungu Zidisha Uhai.

Chekelea bilkuli, mfurahike Magai,
Jumla ya Waswahili, na makabila Mapai,
Tanganyika nchi jamali, imetoka vurumai,
Mungu zidisha uhai, tuone siku tukufu.

Mungu chukua kibuli, wemao hauchakai,
Si kama wa ngulumbili, watenda mzaizai,
Tupate chako kibali, pasi wewe hatukai
Mungu zidisha uhai, tuone siku tukufu.

Siku njema tusabili, tutimize matumai,
Uhuru wetu rijali, ule tulotukidai,
Sasa siku yakabili, mfuhaike kwa chai,
Mungu zidisha uhai, tuone siku tukufu.

Yamekatika makali, vitisho vya kuzirai,
Tumefungua kufuli, tulipotumia rai,
Rai iliyo halali, kwayo hatukurufai
Mungu zidisha uhai, tuone siku tukufu.

Tarehe imewasili, mosi ya mwezi wa Mei,
Ututoke udhalili, na mtu hatuhadai,

Desemba tuibadili, Bendera imekinai,
Mungu zidisha uhai, tuone siku tukufu.

Uhuru wetu kamili, Desemba hatushangai,
Siusemi kwa dalili, la hakuna ulaghai,
Kuruka hapo muhali,Tanganyika twajidai
Mungu zidisha uhai, tuone siku tukufu.

Valieni suruali, imbeni nyimbo kwa nai,
Nchini na kila pahali,kwa masuti na matai,
Kuleni embe kwa wali, na keki za mayai,
Mungu zidisha uhai, tuone siku tukufu.

Tule wali wa samli, kwa matunda ya Papai,
Kwa mikate na asali, ambavyo havitukwai,
Kaimbeni wanawali, wa furaha hanyamai
Mungu zidisha uhai, tuone siku tukufu.

Watanganyika tusali, situfike jitimai,
Tumwombee mfadhili, Nyerere mwenye urai,
Azidishwe mara mbili, Makoloni Bai-Bai
Mungu zidisha uhai, tuone siku tukufu.

Tamati yangu kauli, ya kweli si puruzai,
Tuondowe ujahili, kwetu hayo hayafai,
Tutende yenye akili, wa Sonjo na Umasai
Mungu zidisha uhai, tuone siku tukufu.

38. Uhuru Uwe wa Kheri

Kwa Mola twatawakali, Bwana mwenye Amri,
Mungu chukua kubuli, ombi la hili shairi,
Tutokwe na udhalili, utubariki Kahari,
Uhuru uwe wa kheri, na udumu kwa amani.

Uwezo unao Jalali, wa kutukinga na shari,
Tuepukwe na thakili, walaili wanahari,
Yetu ardhilihali,Tanganyika iwe shwari,
Uhuru uwe wa kheri, na udumu kwa amani.

Tufarijike rijali, na nisai kuwa kheri,
Barakazo tusabili, nasi tuone fahari,

Shangwe yetu bilkuli, iwe njema ya johari,
Uhuru uwe wa kheri, na udumu kwa amani.

Majuto situkabili, Tanganyika inawiri,
Tupate hiki kibali, tuitimize nadhili,
Ombi nchi yetu jamili, Tanganyika kuwa huri,
Uhuru uwe wa kheri, na udumu kwa amani.

Uhuru umewasili, pasipokuwa na dosari,
Kwa upole na sahali, kwa madai ya saburi,
Hakikuzuka kitali, kupigana kwa hanjari,
Uhuru uwe wa kheri, na udumu kwa amani.

Nyerere siye mkali, kama wale majeuri,
Na hiyo siyo kauli, ya siasa ya kiburi,
Amefaulu kamili, kwa kudai kimahiri
Uhuru uwe wa kheri, na udumu kwa amani.

Pasizuke mushikeli, wa mizozo na kikiri,
Wageni kupokwa mali, maisha kuwa hatari,
Huo ni ubaradhuli, ni kujipalia nari
Uhuru uwe wa kheri, na udumu kwa amani.

Tusijivune muhali, viburi tusishamiri,
Kufoka kama fahali, tujidai mahodari,
Ya heshima tuyajali, tutakwa mashuhuri,
Uhuru uwe wa kheri, na udumu kwa amani.

Pasizuke makatili, kama Kongo kukithiri,
Kujifanya majahili, mpole kuwa kufari,
Haitakuwa halali, tulinde yetu nadhari,
Uhuru uwe wa kheri, na udumu kwa amani.

Tuepushie ajali, za kupondwa na magari,
Taabu za kila hari, yafaa tujihadhari,
Kauli tusibadili, yazuka machachari,
Uhuru uwe wa kheri, na udumu kwa amani.

Tuwe wenye akili, tuwasifu Mawaziri,
Ambao walihimili, kuiongoza safari,
Sifa wanastahili, bahari walivinjari,
Uhuru uwe wa kheri, na udumu kwa amani.

Tama naona dalili, tutafaulu dahari,
Mambo yamekuwa kweli, na leo ni dhahiri,
Imeundwa serikali, ya Matumbi imejiri,
Uhuru uwe wa kheri, na udumu kwa amani.

39. Kukuzwa Twafurahia

Hadi nyoyo zimepanda, nafsi kufurahia,
Kiongozi umetanda, tuliivyo tukililia,
Ama kweli umeshinda, sote tunashangilia,
Kukuzwa twafurahi, Kiongozi twakupenda.

Kila sehemu utande, hapa hadi Tunisia,
Hata kusini uende, na maonyo kuwambia,
Madhila yote ushinde, wadilifu kufatia,
Kukuzwa twafurahi, Kiongozi twakupenda.

Utambe hadi Malindi, pasipo kulimatia,
Onyesha wako ufundi, hata na Kongo pitia,
Hata Ruanda Urundi, Ghana hadi Nigeria,
Kukuzwa twafurahi, Kiongozi twakupenda.

Onyesha wako upendo, na upole kazania,
Uwaonyeshe matendo, ya siku za Uhuria,
Waonyeshe nyendo, maungwana kufikia,
Kukuzwa twafurahi, Kiongozi twakupenda.

40. Mungu Ondoa Tatizo

Jirani wana gombano, kutwa kucha ni mizozo,
Kwani hawana patano, wagomba mfululizo,
Hawaishi mikwaruzo;
Mikwaruzo mashindano, kuonyeshana uwezo,
Hawatamani mwungano, ambao kwao ni nguzo,
Mola ondoa mizozo, majirani wafaulu.

Yaacheni matetano, rekebisheni mawazo,
Uacheni utengano, unaoleta utwezo,
Acheni huo mchezo;
Mchezo wa mzongano, kujiletea tatizo,
Fateni wetu mfano, na kwenu liwe igizo,

Mola ondoa mizozo, majirani wafaulu.

Unguja kuna kinzano,hadi yaleta chukizo,
Huwahi na matukano, na kashifa kwa chagizo,
Hakuna njema pendezo;
Pendezo la mlingano, kuviepuka vikwazo,
Acheni yenu maneno, ya utesi na mabezo,
Mola ondoa mizozo, majirani wafaulu.

Kenya nako majivuno, kupingana welekezo,
Wa Cairo Mkutano, yalosemwa kwa mkazo,
Kwa lile lenye katazo;
Katazo mfungamano, nchiini na liwe enezo,
Kuagiza wezekano, Jomo atoke himizo,
Mola ondoa mizozo, majirani wafaulu.

Uganda pia pinzano,kukutana na ufyonzo,
Buganda ubagukano, itoke kwa nyinginezo,
Waifanye msambazo;
Msambazo na makano, na Lukiko mahimizo,
Na Bunyoro magombano, na Majimbo upotezo
Mola ondoa mizozo, majirani wafaulu.

Ya Congo tuna miguno, makubwa ya mzo mzo,
Ya kuzuka mapitano, kwa zao tamaa hizo,
Ikawa vifo msozo;
Msozo kwa mapambano , kama watu hawanazo,
Hawaishi mauwano, UNO hana wendekezo,
Mola ondoa mizozo, majirani wafaulu.

Nyasaland si mbanano,Banda ana muongozo,
Mwongozo wake mnono, si mkali una pozo,
Siasa ya bembelezo;
Bembelezo la mshono, mbele na wapate tuzo,
Baada ya suiku tano, mapitano na fukuzo,
Mola ondoa mizozo, majirani wafaulu.

Sisi tuna ridhiano, ndilo letu pendekezo,
Yasizuke mazozano, ya kupigana kwa tezo,
Tukisogeze chetezo;
Chetezo tusali mno, tuombe kwa mpaazo,
Na tuinuwe mikono, Wahabu abarikizo,

Mola ondoa mizozo, majirani wafaulu.

Tama siumane meno, ugomvi wa angamizo,
Pendeni shirikiano, msifanye mapuuzo,
Mwajiletea vikwazo;
Vikwazo vya mgongano, unaoleta mivizo,
Fanyeni sulubishano, epukeni maapizo,
Mola ondoa mizozo, majirani wafaulu.

41. Komesheni Magombano

Mwache mkiki-mkiki, ugomvi na matetano,
Nakanya hamkanyiki, mnazidi mzozano,
Nasema halisumbuki, simbiko kwazo mifano,
Komesheni magombano, watunzi ni marafiki.

Nipigwe sikasirikii, nawakanya mashindano,
Shindano halikatik, kidimbwi ndani ya chano,
Ninyukwe sitetereki, haja yangu muungano,
Komesheni magombano, watunzi ni marafiki.

Dhihaka huleta chuki, na huvuta utengano,
Tengano huleta dhiki, ingiapo minong'ono,
Na ngoma haichezeki, wingiapo mpambano,
Komesheni magombano, watunzi ni marafiki.

Jitukali hashindiki, na bomu za mabishano,
Nyamaume harudiki, kashika safu ya tano,
Waloanzisha sabiki, sasa wana tulizano,
Komesheni magombano, watunzi ni marafiki.

Nyamaume ni rafiki, Jitukali naye mno,
Nuru ndiye mshiriki, binti wetu shikamano,
Amri simfariki, msimiulizi wa ngano,
Komesheni magombano, watunzi ni marafiki.

Mshairi tamalaki, ni Shaaban mnono,
Afrika Mashariki, ndiye mwenye julikano,
Watunzi katumiliki, mkuu wa mikutano,
Komesheni magombano, watunzi ni marafiki.

Tafuta neno la haki, tuepuke ukinzano,

Tuwavute halaiki, tupate mwongezekano,
Twongezeke tuwe laki, tuwe na afikiano,
Komesheni magombano, watunzi ni marafiki.

Snow haambiliki, kwa wembe miburuzano,
Mandevu alaidiki, na ndevu hana makano,
Mlanzi hatataniki, ubishi na jibizano,
Komesheni magombano, watunzi ni marafiki.

Robati naye hataki, hakubali ridhiano,
Hakubali haridhiki, ridhaa ya maoano,
Na Kiwato hafutiki, atajwa uchokozano,
Komesheni magombano, watunzi ni marafiki.

Mwinyihatibu handaki, maficho ya mapigano,
Mtu- Chake na mswaki, huku asfisha meno,
Huo ukali wa nyuki, wa mbio mfukuzano,
Komesheni magombano, watunzi ni marafiki.

Si furahi sitosheki, jambo hili mng'ang'ano,
Penzi halitakasiki, lasinzisha kama pono,
Pono huwa haamki, hadi pigo kwa mguno,
Komesheni magombano, watunzi ni marafiki.

Tusifanye uzandiki, vijembe mikwaruzano,
Hivyo huleta hamaki, na kutiana mikono,
Nayo siyo itifaki, iletayo husiano,
Komesheni magombano, watunzi ni marafiki.

Tamai mashabiki, uwacheni mzongano,
Kioa ukitaliki, ni lenu sikilizano,
Kiacheni kisa hiki, kimechakaa mshono,
Komesheni magombano, watunzi ni marafiki.

42. Mzozo Wangu Patano

Siku zote ninaguna, huchungulia makano,
Hutokana na vijana, wasopenda ushirikiano,
Daima wakizongana, hadi kwa utukanano,
Mzozo wangu patano, washairi hupendana.

Washairi hupatana, wekendesha mikutano,

Mikutano za maana, za kutengeza unono,
Unono tenzi kusana, vina vyenye mlingano,
Mzozo wangu patano, washairi hupendana.

Washairi hupendana, na hushikana mikono,
Haviji kubagukana, fitina na minong'ono,
Hakika si maungwana, washairi mzozano,
Mzozo wangu patano, washairi hupendana.

Tafadhali Sihiyana, waase hao watano,
Nao nawapenda sana, wana uheshimiano,
Kwangu ubaya hawana, kuwa wana ukinzano,
Mzozo wangu patano, washairi hupendana.

Adam tumeonana, na kwa mashauriano,
Zungumzo limefana, kasha kwa mtulizano,
Ubaya kwake hakuna, hapendi machokozano,
Mzozo wangu patano, washairi hupendana.

Khalfani panga vina, ugomvi uwe mwagano,
Gonga ujaze makana, ufanye suluhishano,
Shikeni zenu supana, funga yenu mapigano,
Mzozo wangu patano, washairi hupendana.

Na Makarani mwanana, fanyeni uhusiano,
Naye Miraji hatakana, azidi shambuliano,
Walimwengu hukwaana, mwisho masameheano,
Mzozo wangu patano, washairi hupendana.

Kwa marefu na mapana, mwache yenu matukano,
Kwayo kukashifiana, matusi na mfyonyano,
Ni tabia ya Utwana, yenye rangi ya manjano,
Mzozo wangu patano, washairi hupendana.

Ya illahi Rabana, wajalie mapatano,
Wapeane muawana, yenye upenzi maneno,
Mawaidha kupeana, wasia na tangamano,
Mzozo wangu patano, washairi hupendana.

Namuomba Subuhana, alete afikiano,
Tuache kununuiana, tupatane kama ngano,
Ndipo utunzi tanona, tuachapo utengano,

Mzozo wangu patano, washairi hupendana.

43. Mungu Mwongoze Rubani

Twakaribia kufika, safari ya Bandarini,
Bahari kuu kuvuka, na wimbi za Baharini,
Twaomba kusalimika, salama usalimini,
Tumbwi letu la Rubani, lasogea ukingoni.

Ewe fundi msifika, Nahodha wetu Rubani
Tangu uliposhika, kuliendesha majini,
Katu hukupepesuka, kwa mawimbi kilindini,
Tumbwi letu la Rubani, lasogea ukingoni.

Safari hatuna shaka, Rubani tunakwamini,
Si fundi wa kutishika, wa wasiwasi moyoni,
Ukishika umeshika, hadi tufike fukweni,
Tumbwi letu la Rubani, lasogea ukingoni.

Mail inane tabaka, tusimame ukingoni,
Maili hizo hakika, si nyingi kama mwanzoni,
Tunamuomba Rabuka, tukasimame Gatini,
Tumbwi letu la Rubani, lasogea ukingoni.

Mapito yalinyooka, hatukukwama njiani,
Wala hatukuzunguka, tufike hapa tabani,
Hakuna kilichozuka, tupepesuke pembeni,
Tumbwi letu la Rubani, lasogea ukingoni.

Damu haikumwagika, kwa kukwaruzwa mwilini,
Na nyongo kwa kutapika, mivurugiko tumboni,
Nani alitaabika, kwa hofu ya mawimbini
Tumbwi letu la Rubani, lasogea ukingoni.

Katu hakuhusudika, kugombea usukani,
Nani alipaparika, kupokonya mkononi?
Sote tulisubirika, tukajiweka kandoni,
Tumbwi letu la Rubani, lasogea ukingoni.

Rubani wetu tukuka, akujalie Manani,
Maisha kuongezeka, Nyerere mwenye hisani,
Iongoze Tanganyika, nakutilia ubani,

Tumbwi letu la Rubani, lasogea ukingoni.

Kukwombea sitachoka, hadi tufike mwishoni,
Wa bendera kutundika, icheze mlingotini,
Wananchi kufurahika, warukeruke kwa shani,
Tumbwi letu la Rubani, lasogea ukingoni.

Namaliza kuandika, nawaaga kwa herini,
Watu tunaohusika, kutolewa utumwani,
Chombo chetu ushirika, vingine hiwezekani,
Tumbwi letu la Rubani, lasogea ukingoni.

Kiambatisho B: Mashairi ya Shaaban Robert

(i) Diwani: Koja la Lugha **(1969)**

1. Wafu Wenye Sauti

Bwana Mwalimu Kihere, niawini mpwao,
Naona kiherehere, piga ramli na bao,
Usiseme kazi bure, itatukuka kaziyo,
Upesi jibu lichore, ueleze watu hao.

Abushiri wa Mbwana, tunga kwa vituo,
Mistari pima sana, pasiwe ipitanayo,
Kisha iwe na maana, ueleze watu hao,
Po pote ulipoona, miujiza kama hiyo.

Haya bin Hanasa, kina cha *Mambo Leo*,
Kujibu kutakupasa, unitoke mshangao,
Ajabu ya hiki kisa, sioni wake upeo,
Mfu asemaje hasa, akashinda wazikao?

Tena Mzee Waziri, stadi wetu wa leo,
Simulia kwa shairi, Mombo mji ukaao,
Namna ya wasafiri, wazikao kama hao,
Tunga kwa mistari, isiyopitana cheo.

Fundo niliyofunda, yataka wafunguao,
Abdi bin Matunga, haraka nijibu leo,
Wengine wakitunga, sitakasirika nao,
Mimi kinanitinga, kisa cha mfu huyo.

Nikiwaza ya maiti, na watu wamzikao,
Naapa kuwa sipati, usingizi nitakao,
Wafu wenye sauti, bado kukutana nao,
Nataka madhubuti, kwa watu waelewao.

Madhubuti nataka, ili nitulize moyo,
Daima nasumbuka, kutafuta siri hiyo,
Leo nipeni hakika, msomao *Mambo Leo*,
Kwayo nilipofika, nitangoja wajibuo.

2. **Moyo Unapopenda**

KUTUNGA na kukusifu, ni alama ya kupenda,
Wala usitie hofu, jambo hili nikitenda,
Nalitenda kwa unyofu, wala usidhani inda,
Na njia japo ndefu, mimi sitachoka kwenda.

Njia hiyo sitachoka, japo milima ‘tapanda,
Nitapanda nikishuka, nifike ninakokwenda,
Hauchoshwi na mashaka, moyo unapopenda,
Nguvu mpya huzuka, ikahimiza kushinda.

3. **Gazeti Halina Nafasi**

AHSANTE Bwana Edi, salamu nimeziona,
Nitafanya jitihadi, utenzi uzidi tena,
Beti elfu idadi,zimekwisha patikana,
Na nyingine zaidi, kiwandani nazisana.

Nasikitika gazeti, sasa nafasi halina,
Karatani hatupati, zimekuwa shida sana,
Tunazopata katiti, hazitoshi kama jana,
Zikichapwa nyingi beti, habari zitabanana.

Moyoni ninayo dhati, nafasi ikija tena,
Likikua gazeti, kwa urefu na upana,
Nitazizidisha beti, na kuzidi kukazana,
Ahadi hii thabiti, akiniweka Rabana.

Tumwombe Mungu wetu, upepo uwe mwanana,
Ushindi uje kwetu, Hitler apate laana,

Na mfalme wetu, apewe amani tena,
Turudiye raha zetu, za usiku na mchana.

Hitler na wenzake, nataka wapigwe sana,
Hata walalamike, *nguvu hatuna tena*,
Tunataka tuandike, sasa vita hapana,
Tendo hili lifanyike, ninakuomba Rabana.

4. Kundi

KUNDI moja wanakaa, wadudu wadogo sana,
Na ndege wenye manyoya, kundi moja hupatana,
Wanadamu vibaya, kutengana kwa fitina,
Kwani hatuna haya, siku zote kugombana?

Hatukuumbwa na kucha, mfano kama wa simba,
Wala meno yenye ncha, kama panya au mamba,
Sababu gani twaacha, alivyotaka Muumba,
Ambaye tunamcha, na daima kumwomba?

Mtu hakupewa pembe, aina kama ya mbogo,
Hafanani na ng'ombe, mtu hata kidogo,
Twaigaje nyama kumbe, wanavyofanya zogo,
Kama wana wakembe, kugombana kwa madogo?

Hasara na majuto, huja kwa tunayotenda,
Hupenya katika keto, kutia moyo madonda,
Nyayoni hatuna kwato, namna kama ya punda,
Hupigaje teke zito, kupigwa usikopenda?

Mwilini hatuna miba, kama mfano wa nungu,
Twafanyaje ghiliba, izae mambo machungu,
Yanayoleta misiba, kuwadhuru walimwengu,
Kwa choyo cha kushiba, kuwania kubwa fungu?

Vinywani hatuna sumu, mshabaha kama nyoka,
Mtu hufanyaje hamu, akataka kugeuka,
Awe si binadamu, Muumba alivyotaka,
Kusudi adhulumu, na kuvunja ushirika?

Wala hatuna mikonga, mfano kama wa tembo,
Hutamanije kutunga, kuburuga kila jambo,
Kwa kusudi la kugonga, wenzetu kwa makumbo,

Na kuwavutia janga, tufananao kwa umbo?

Sisi wanadamu, ni wasafiri pamoja,
Na vitu vilivyo humu, hatuchukui kimoja,
Tutaacha vinadumu, safari yetu ikija,
Kwa hakika ni wazimu,hiki choyo kutufuja.

Huko tunakokwenda, ukizuka ushahidi,
Kuwa nani ametenda, mambo yasiyo muradi,
Nani atakayependa, kushuhudiwa hasidi,
Hitler utakonda, jambo hili likibidi.

16. Hazina

MASHAIRI ni hazina, katika kila msemo,
Huongoza kuona, mambo mengi yaliyomo,
Katika dunia pana, mfano kama masomo,
Tena huwafaa sana, watu wa kila makamo.

17. Barua

Musa Rashid somo, barua nimefahamu,
Nimesoma yaliyomo, hata nikahitimu,
Kwa kutunga nawe umo, katika sifa muhimu,
Kukutolea ungamo, hapa imenilazimu.

Nimependezwa na kimo, beti zilivyotimu,
Tezi hata omo, zimeundwa kwa elimu,
Na maana ndani imo, iletayo tabasamu,
Kubwa katika midomo, kwa maneno maalumu.

Umefikia kipimo, kwa watu wengi adimu,
Bora hakina mashimo, na maneno si magumu,
Usemapo kuwa humo, ushairini haramu
Mimi nahesabu umo, wala hutoki mwalimu.

Masuto hayawi fumo, hasa na wenye wazimu,
Japo kuwa si chumo, mashairi ni matamu,
Katika kila masomo, ya watu wataalamu,
Mashairi ni kilimo, na mbegu ya fahamu.

Nimepatwa na mshomo, kwa kusikia muamu,
Kuwa kitandani yumo, kwa maradhi kumsumu,
Ipe kabuli midomo, Bwana Mungu mkirimu,
Atoke katika shimo, kijana tena adumu.

Mrefu kwa kipimo, mkono wako Karimu,
Mwokoe asiwemo, ndani ya dhiki ngumu,
Dunia haina shimo, usiloweza hukumu,
Kutoka kiliyomo, na kuamuru kudumu.

Nilialikwa niwemo, juzi katika karamu,
Nikakuta Harvey yumo, anaagawa na walimu,
Nikasikia msemo, wa hotuba moja tamu,
Iliyotia tetemo, kwa shairi maalumu.

Nitafuliza msemo, hata beti zitimu,
Nyuma kusibaki zumo, kushutumu wanadamu,
Kuhesabiwa kuwamo, katika choyo si tamu,
Sifa mbaya siyo chumo, kuwania mwanadamu.

Beti nane kwa kipimo, shairi lako mwalimu,
Ni hili chake kimo, beti tisa zimetimu,
Kuzidisha msemo, sasa hailazimu,
Basi hiki ni kikomo, pamoja na wasalamu.

18. Ushairi

Ushairi ni sudi, mwenye nao ni kipawa,
Kipawa cha ustadi, hedaya watu hupewa,
Waimbao wana jadi, ya kusema kwa maua,
Maneno huyachagua, yanayokidhi kusudi.

Huchagua na kupima, maneno wanayonena,
Mepesi mtu kusema, na kudhibiti maana,
Yanayoimbika vema, na sauti kulingana,
Hawayapendi sana, maneno ya kukingama.

Japokuwa lina kina, neno ya kukingama,
Huwa halifai sana, mashairini hukwama,
Kisha hupoteza maana, uzuri hata kima,
Shairi haliwi jema, lugha ikitatizana.

Maneno yakisongana, maanaye huwa kiza,
Japo likiwa na kina, shairi litapooza,
Maneno yakikosana, hayafanyi mwangaza,
Shairi la kutatiza, halina faida sana.

19. Vileo

Mtengeza *Mambo Leo*, radhi niwie Bwana,
Nafasi ukiwa nayo, nipe ruhusa kunena,
Ukiona mapoteo, shairi halina kina,
Shahihisha kila tao, liimbike dana dana.

Tena litie vituo, liwe jepesi kunena,
Lipendeze masikio, kwa sauti kulingana,
Hata watu wasomao, wadhibiti na maana,
Kama tembo kileo, nguvu hulevya sana.

Watu nguvu walewao, daima huchokozana,
Mambo hasa wapendayo, mzozo na kuuana,
Amani kwao chukio, hawapendi kuiona,
Kama bangi kileo, mali hulevya sana.

Mali nayo ni kileo, lakini bahati ina,
Watu walewao hiyo, hudai sana ubwana,
Huwadharau wenzao, ambao kitu hawana,
Kama mvinyo kileo, elimu hulevya sana.

Elimu wailewao, ajabu ukiwaona,
Hujifanya kama wao, mfano wao hapana,
Hapa nawapa funuo, kiza huzaa mchana,
Kama kasumba kileo, uwezo hulevya sana.

Uwezo aliye nao, ana shani kubwa sana,
Hutaka ayasemayo, hata ikiwa fitina,
Yawe katika sikio, wimbo wenye maana,
Kama divai kileo, Mapenzi hulevya sana.

Mapenzi pia kileo, lakini ni bora sana,
Huunga watu ambao, nasaba moja hawana,
Yakipenya watu hao, hujiona walingana
Kama pombe kileo, sifa hulevya sana.

Hakika sifa kileo, wazi bila kubishana,

Kunguru ana mlio, usiopendeza sana,
Aliposifiwa nao, hadhari hakuiona,
Kama kangara kileo, dharau hulevya sana.

Dharau ndicho kileo, kizuio cha kuona,
Huziba na masikio, ikabaki kujivuna,
Hali ujivuniayo, pengine hayana maana,
Kama moshi ni kileo, nasaba hulevya sana.

Wale wajinasibuo, kabila na uungwana.
Na wale wadunishwao, kama walio na laana,
Adam baba yao, chini alipatikana,
Kama mbege ni kileo, neema hulevya sana.

Sisemi kuwa vileo, vimeniashiki sana,
Na watu watumiao, kupatiliza nakana,
Wengi hushinda wao, kuwashinda shida sana,
Nimevisema vileo, kuonya si kubishana.

Ningeandika vileo, vyote nilivyoviona,
Nikawapa waimbao, lakini nafasi sina,
Hali namna hiyo, mwaelewa waungwana,
Mtu akiwa nayo, mengi hawezi kunena.

Basi natia komeo, Mungu tupe mwanana,
Tupe mambo tuwezayo, yasiwe mazito sana,
Vikitokea vileo, kutaka kugombana,
Vitukute tuna ngao, na zana za kupigana.

20. Tabia

Kioo kwa binadamu, katika hii dunia,
Watakao tufahamu, wanatazama tabia,
Tabia jambo muhimu, tunza na kuangalia,
Utatukuka jina, kwa uzuri wa tabia.

Sidanganywe na pumzi, haikawi kukimbia,
Yakakutoka mapenzi, watu ukawachukia,
Jifunze uwe azizi, mahali ukiingia,
Utatukuka jina, kwa uzuri wa tabia.

Fanya adabu kwa watu, adabu husaidia,
Adabu libasi kwetu, kashifa inazuia,

Kisha hutukuza utu, jambo hili huwaniwa,
Utatukuka jina, kwa uzuri wa tabia.

Adabu ni mtumishi, milele husaidia,
Faida yake haishi, kila siku huzidia,
Adabu ina uchechi, watu huifurahia,
Utatukuka jina, kwa uzuri wa tabia.

Wapo watu maskini, hawana cha kutumia,
Lakini wana thamani, kwa ubora wa tabia,
Watu hao duniani, ni chumvi ya kutumia,
Utatukuka jina, kwa uzuri wa tabia.

Wapo wenye milki, watakavyo hutumia,
Lakini si marafiki, kwa ubaya wa tabia,
Hao hawachukuliki, hatari kukaribia,
Utatatukuka jina, kwa uzuri wa tabia.

Tena wapo wanyonge, ambao ni maridhia,
Hawadhuru kama nge, wala hawana udhia,
Wajipatiao tonge, kwa njia yenye sharia,
Utatukuka jina, kwa uzuri wa tabia.

Kisha wapo wenye nguvu, wajinga kuitumia,
Wajitiao ubovu, kwa mambo ya kurukia,
Wakamuliwapo mbavu, huilaumu dunia,
Utatukuka jina, kwa uzuri wa tabia.

Zaidi yake wadogo, waelekevu wa njia,
Wajipatiao togo, kwa mambo yenye murua,
Hawashikwi na mitego, waendapo hupokewa,
Utatukuka jina, kwa uzuri wa tabia.

21. Wema

Panda mbegu ya wema, yaote mapendeleo,
Panda mbegu ya heshima, ili uvune cheo,
Uovu si mbegu njema, zao lake machukio,
Tena hupata lawama, apandaye mbegu hiyo.

Panda ungoje majira, usivune mbio mbio,
Hapati mazao bora, mwenye pua na choyo,
Haraka ina hasara, wamesema wasemao,

Wengi wamedorora, kwa kupuuza yapasayo.

(ii) Diwani: *Kielezo cha Fasili (*1968)

1. Ushairi.

Ushairi kwangu mimi kama hirizi ya sudi,
Ni malaika huhamikwa faraza za fuadi,
Na ambaye hunihami katika kila juhudi;
Juhudi za maandami ya sala na ya uradi,
Hapana shaka hatami, kwa uwezo wa Wadudi,
Katika dhambi sizami za weusi kufanidi,
Ama mithili ya lami, na mbaya kwa kuhusudi,
Zenye moto wenye ndimikwa mtu kama zawadi;
Nami dhalili situmi, nilipeni kwa Wadudi?
Mimi ni mtu sisemi, sina nguvu sijimudi,
Basi kwani siungami, hirizi hii wahedi,
Ina sudi kwangu mimi nyingi hazina idadi,
Naifunga haizami kwa mkufu na udodi,
Au madini za Shami zenye nguvu maujudi,
Na dhahabu adimi, ghali katika biladi.
Wengi hupenda uchumi, na mali au nakidi,
Bila huba yangu mimini ushairi kuzidi;
Na nini mtu kamani mbele yao maseyidi,
Maarufu kwa uvumi na wenye sifa za jadi.

Kwa nguvuye ushairi natema moto na radi,
Vitu vilivyo hatari iwapo sikujirudi,
Unidhanie amri mahali penye junudi,
Pia natema johari na mvua yenye samadi,
Na madini ya fahafi, bei kubwa kwa nakidi,
Mfano kama tajiri, ingawa sina wahedi,
Kitu ila ufakiri, kama kwamba ni ahadi,
Na mudawe umejiri kutimizwa imebidi,
Na hunipandisha ari nikajiona seyidi,
Ama mtu mashuhuri imara kama hadidi,
Sitetemeki kwa hari, hofu wala kwa baridi,
Na bahari na mapori ya giza kama fuadi,
Ndani yaliyo na siri hupata nikaidadi,
Nikazuia dhamiri na nia na makusudi.
Huja kwangu wasafiri, kuzuru na kuradidi-
“Kipawa chako kizuri, na heshima hukubidi, ”
Jibu langu nkariri, “Hidaya yake Wadudi,”

Niwie radhi Jabali kwa kujinadijinadi,
Lakini kwa kukukiri, kukushukuru yanibidi.

2. Kama Upindi wa Mvua.

DUNIA wenyewe watu, wamepewa kutumia,
Hii ni heshima kwetu,tumshukuru Jalia,
Wanyam ni washirika wenye kucha na pembe,
Na ndege wanaoruka kwa jamii ya viumbe;
Waoenda kwa tumbo au kwa kurukaruka,
Ama walio na umbo ambalo huajabika.
Na baharini samaki ambao huzama mbizi,
Vitu haviheshabiki, vyenye roho na pumzi.
Vitu hitilafu rangi kama upindi wa mvua,
Mungu ameumba vingi kupamba hii dunia;
Na vyote hutazamia kupatariziki kwake,
Bila kusahauliwa, tazama ajabu yake!
Katutukuza si haba, kisha tutarudi kwake,
Kwa mapenzi na mahaba katika miliki yake,
Kubwa isiyopimika; mafundi hawaiwezi,
Na kulikotutanika mito yote ya mapenzi.
Kulikokutana heri, misiba hakuna tena,
Kila namna fahari, maisha ya kujivuna.
Kila mtu apendeza, kucheka hatahayari,
Na nyuso zitaangaza kama nuru ya sayari.
Watu wote wawe radhi; hapana mwenye kununa,
Hakutakuwa faradhi, kufa mama wala mwana.
Mikono watashikana, wanawake kwa waume,
Na wote kubusiana, wacheke wajitazame.

3. Kuondoana Njiani

KAZI zili nz ujira, na wingi wa visituo,
Na watu kungorangora, kuhimiza watendao;
Sasa hutumwa fikira, vitu vindani ya moyo,
Tutatenda ndivyo sivyo tuondoane njiani.

Kazi za sasa hasara, kwa jamii wafanyao,
Nyingi kukuru kakara, hazitimizi cha jio;
Hata wauza kangara, hawaoni pato lao;
Tutatenda ndivyo sivyo tuondoane njiani.

Hulia watu wa bara, kupoteza jasho lao,
Wenye nguvu wadorora, wako wapi wachumao?
Wengi pwani husowera, hawawezi rudi kwao,
Tutatenda ndivyo sivyo tuondoane njiani.

Na wa pwani wakigura, kuelekea machweo,
Huselea kuzurura, hawapati marejeo;
Hakuna tena ujara, yamebaki masumbuo,
Tutatenda ndivyo sivyo tuondoane njiani.

Fanya kazi kwa imara, tajiri apate cheo,
Kichwa kiote kipara, macho uvae vioo;
Kuzidishwi mshahara, wala huna fanikio,
Tutatenda ndivyo sivyo tuondoane njiani.

Ukichelewa ni ghera,tajiri hukwita mbio,
Hukufokea hasira, na mengi masumbulio;
Mnyonge hana harara, pangalishikanwa koo,
Tutatenda ndivyo sivyo tuondoane njiani.

Juu miaka ashara, mwendo wako huwa huo,
Huoni hata ishara, ya senti izidivyo;
Mungu mwingi wa busara, hutuliza watu hao!
Tutatenda ndivyo sivyo tuondoane njiani.

Huzindishiwi ijara, na kila siku kemeo,
Za kuudhi na kukera, furaha tembe hunayo;
Unyonge una madhara, tupeni pole tunayo,
Tutatenda ndivyo sivyo tuondoane njiani.

Mwaka ukizinga dira, hupandi huna pandio,
Watu wote wakubera, na hali kazi unayo;
Tazameni masihara, ya kutumwa na wenzio!
Tutatenda ndivyo sivyo tuondoane njiani.

Kutumiwa kama nyara, mimi furaha sinayo,
Takwenda nayo ahera, machungu niliyo nayo;
Kuna maamuzi bora, ya dhuluma kama hiyo,
Tutatenda ndivyo sivyo tuondoane njiani.

Matajiri watang’ara, safari hyo ijayo,

Nikisifu usogora, tabia na mwendo wao;
Leo siwezi kuchora, picha mfano wa hiyo,
Tutatenda ndivyo sivyo tuondoane njiani.

22. Kufua Moyo

Siku ya panga kufuta,
Mashujaa kwenda kondo,
Siku ya kuja matata,
Na fadhaa na mshindo
Siku ya watu kuteta,
Kufua moyo mfundo,
Siku ya nchi kutota,
Kwa damu kwenda mkondo
Siku ya kung'ara nyota,
Za watenzi wa matendo,
Na siku ya kujivuta,
Wa kati na kando kando;
Bora ni kufa kwa vita,
Au ni kufa kwa sondo?

Uvundo wa mashujaa,
Ni sawa na manukato,
Marashi katika pua,
Hauna harufu nzito;
Ama rihi ya maua,
Njema isiyo fukuto,
Nyingi katika hewa,
Na ardhi yenye woto;
Ni fahari maridhawa**,**
Kwawazee na watoto,
Na urithi wenye hawa,
Kama hazina ya vito,
Ghali katika dunia;
Kufa vitani ni ndoto.

5. Kashata na Ladu

Serikali za wanyama, na ndege ama wadudu,
Ndani zina taadhima, kama kwamba maabudu;
Na watu wenye hekima, siku hizi hawamudu,
Madaraka na heshima, heri mnyama na dudu;
Vinywa vimewaachama, tamu imekuwa ngwadu.

Na heshima imehama, baki taka na mashudu,
Na madhara na dhuluma, miungu ya kuabudu,
Na mambo haya si mema, watu yanawahusudu;
Hizi husemwa ni zama, za watu kufa kibudu-
Kufa wangali wazima, na nguvu za kusujudu,
Na maudhi na hasama, kwao kashata na ladu.

6. Kosa Dogo

KOSA la mtu mdogo kutangazwa si muhimu,
Hasara yake kidogo, kama mwendawazimu.
Kosa la mtu mkubwa wajibu kulitangaza,
Kwa herufi kubwa kubwa na wino wa kuangaza.
Mdogo hatendi jambo duniani lenye kimo,
Kulitangaza uchimbo, makubwa yakiwa yamo.
Dunia huharibiwa kwa makosa ya wakubwa,
Lakini husetiriwa, kwa bidii yakazibwa.
Si kinyume cha dunia wadogo kuadhirika,
Wakubwa wenye hatia wakazidi kutukuka !

Wakubwa wanafaidi, wadogo wadhulumiwa,
Na mtu akifanidi maisha huwa mabaya.
Dunia inavyokwenda mtu akiifanidi,
Na mambo inayotenda hutatizika zaidi.
Hudharau maji male yawezayo meza vyombo,
Ikapiga makelele kwa wasio na matumbo.
Wadogo wana madhila lakini watafanyaje-
Kama makosa chakula, twambieni huliwaje?
Huliwa kwa kupendeza aula kwa gagamizi,
Na watu wasioweza kubwa ila la upuzi?

7. Uasi

WAASI wa serikali, wengi kuliko wa dini,
Wengi hawendi kusali, lakini wana imani,
Ambayo kwamba kamili, bila kasoro moyoni.
Kama haba ya adili, serikali huwa chini,
Ikawa yatenda feli, za shari na nuksani,
Na dhuluma na batili, na uhaba wa hisani;
Na jinsi mbalimbali, za watu ulimwenguni,
Kama hawaoni kweli, ni wepesi wa kuhuni;
Kitu duni serikali, iwapo mbele ya dini!

8. Vivuli

WENYE kucha na maganda na sumu ya kuulia,
Wamo katika mkondo na tufani ya tabia,
Na ghasia ya matendo, uhalifu na hatia.
Hapana chembe upendo kwa uaili na ria,
Pamebakia uvundo kila pembe ya dunia.
Si wa tendo wala mwendo, kila mmoja alia,
Na kila saa mshindo wa tisho unazidia.
Kwa uovu wa mwenendo, vivuli vinatishia,
Hapana mla mawindo, kila pori lakimbia;
Hata zamani za kondo haya hayakutukia,
Samba na ndovu na nondo, woga umewaingia!

9. Ikirari ya Mapenzi

NASHUKURU mhariri, majibu yana thawabu,
Athumani mashuhuri, naomba tena jawabu;
Kwa kunipa ikirari, mapenzi kuyanasibu,
Ni mekundu ama zari, kipawa ama nasibu?

Ni baridi ama hari, kweli ama ukidhabu,
Machungu ama sukari, amani ama harubu;
Ghasia ama ni shwari, furaha au ghadhabu,
Ni kitu cha kusaburi, au mara kinaghibu?

Nami kuitwa mjinga, sioni kwamba ajabu,
Mimi mjinga naringa, werevu wana taabu;
Hawapati la kutunga, wala la kuliratibu,
Na kila wanalolenga, haliwapi matulubu.

Utunzi na umalenga ni vitu vya taratibu,
Ndani yake mna kunga na marudi na adhabu;
Hufunza watu kulenga na kusema na kujibu,
Si kwamba mtu apinga kitu bila ya sababu.

Baba na mama si wezi, kuwaheshimu wajibu,
La kulipa hatuwezi, tusiwe watu harabu;
Wa kufundisha upuzi, na mambo yenye aibu,
Ni watu bora wazazi kwetu kuliko dhahabu.

Kwamba wazazi azizi,yamo katika vitabu,
Na radhi zao hirizi, dawa yetu mujarabu;
Adili humwiti mwizi, mama yake wala abu,
Na mwerevu ni mapenzi, si mtovu wa adhabu.

10. Ubora Wetu

Kuwa mbali na umaskini ni haliiliyo njema mno,
Na afya kama haba mwilini ni taabu haina mfano.
Kuwa na rafiki sheriani uborawe si wa mlingano,
Hushinda fedha ya mfukoni isiyoweza kutenda neon,
Na laity si machukiano tungalikuwa wote peponi!

Amani yetu haba moyoni kwa uadui na magombano,
Kama hatuna matumaini na ukunjufu na tangamano.
wa imani katika pori la makindano,
ni thamani kwa kukosa masikilizano,
mapatano, na leo huwaje nuksani!

11. **Heshim**a

Kama heshima ni kosa mtu kuitaradhia,
Bora nife hivi sasa, nitengane na dunia,
Ama niwe nayo hisia katika kuheshimiwa.
Hayapendezi maisha kwa mtu bila heshima,
Kipi cha kufurahisha katika dunia nzima,
Kuliko kujipandisha cheoni na kusimama?
Jambo lenye kuchukiza mtu ni kukosa cheo,
Kufanywa kuwa mwapuza hauridhi wake moyo;
Heshima inapendeza kila mtu kuwa nayo.
Heshima jambo azizi kwa mume na mwanamke,
Umpaye hakuenzi katika maisha yake,
Kukusahau hawezi kwa wazo na tendo lake.

(iii) Diwani: *Masomo Yenye Adili (*1967)

1. Rangi Zetu.

RANGI pambo lake Mungu, rangi haina kashifa,
Ni wamoja walimwengu, wa chapati na wa mofa;
Walaji ngano na dengu, wazima na wenye kufa,
Rangi pambo lake Mungu, si alama ya maafa.

Hupamba Nyota na Mbingu, na mawaridi na afu,
Rangi adhama ya Mungu, na mwilini si uchafu;
Si dalili ya machungu, dhambi wala upungufu,
Rangi heba yake Mungu, Mwenyezi Mkamilifu.

Ni urembo wake Mungu, mwenye miliki ya sifa,
Na pambo la malimwengu, shahada ya taarifa;
Wajinga wa ulimwengu, rangi hudhani kashifa,
Rangi pambo lake Mungu, si alama ya maafa.

Twajua Mwenyezi Mungu, kwa mambo mabadilifu,
Shani zake na mizungu, ni Bwana wa wasanifu;
La Ardhi na la Mbingu,neno lake husadifu,
Rangi heba yake Mungu, Mwenyezi Mkamilifu.

Hashindwi kupamba Mbingu, viumbe na mataifa,
Kila tendo lake Mungu, hutendwa kwa maarifa;
Hubadili walimwengu, kwa kuzaliwa na kufa,
Rangi pambo lake Mungu, si alama ya maafa.

Hashindwi Mwenyezi Mungu, fupi kulipa urefu,
Hashindwi na walimwengu, watawaliwa na ufu;
Hashindwi katika Mbingu, kwa rai na utukufu,
Rangi heba yake Mungu, Mwenyezi Mkamilifu.

Wa sharabu na wa kungu, dhaifu na wenye sifa,
Dufu na wenye mizungu, sura moja na halafa;
Kama si wachaji Mungu, rangi hazina sharafa,
Rangi pambo lake Mungu, si alama ya maafa.

Rangi marembo ya Mungu, kwa viumbe hitilafu,
Mafundi wa ulimwengu, huiga kwake unyofu;
Wa feli na wa mizungu, hekima na usanifu,
Rangi heba yake Mungu, Mwenyezi Mkamilifu.

Nyingi anasa za Mungu, ndani ya kila taifa,
Mtukufu wa mizungu, laiki wa kila sifa;
Na kazi ya mlimwengu, ni lawama na kashifa,
Rangi pambo lake Mungu, si alama ya maafa.

Ndiye Mrembo wa Mbingu, samawati na wangafu,
Hupamba hata mawingu kwa zari safu kwa safu;
Kadhalika walimwengu kwa rangi za hitilafu,
Rangi heba yake Mungu, Mwenyezi Mkamilifu

Marembo tangu na tangu, utukufu wa sharafa,

Fahari ya ulimwengu, na mbingu yetu ghorofa;
Yote mapamboye Mungu, mwenye hakika ya sifa,
Rangi pambo lake Mungu, si alama ya maafa.

Rangi kwa shairi langu, tungo yenye kuarifu,
Kila walipo wenzangu, jambo hili maarufu;
Rangi kugawa mafungu, huonyesha upungufu,
Rangi heba yake Mungu, Mwenyezi Mkamilifu

Hupendwa utungo wangu, kwa wingi wa maarifa,
Kwa kujuvya walimwengu, mfano walao dhifa;
Yote mahaba ya Mungu, rangi zetu si kashifa,
Rangi pambo lake Mungu, si alama ya maafa.

Ni mwema utungo wangu, kwa vikuba na mikufu,
Uimbwapo walimwengu, wenye fahamu husifu;
Nawapa wapenzi wangu, rafiki waaminifu,
Rangi heba yake Mungu, Mwenyezi Mkamilifu.

2. Uzuri

Uzuri wa uso mwema,
Unavuta vitu vyote,
Vya macho ya kutazama,
Unapopita popote,
Walakini kwa kupima uzuri wa umbo bora.

Uzuri kupita huu,
Katika hii dunia,
Nawapa msisahau,
Ni uzuri wa tabia,
Ni johari ya heshima duniani kila mara.

Umbo pamoja na suara,
Huwa katika maficho,
Kwa mtu mwenye fikira,
Lakini kasoro macho,
Kwa hivi watu husema si uzuri wa imara.

Tazama! Dunia nzima,
Huendeshwa na tabia,
Kama tabia si njema,
Si ajabu kupotea,

Kitu kilicho adhama ni tabia ya busara.

Kwa kutengeneza tabia,
Rai yangu na fikira,
Vyuo katika dunia,
Vingekuwa na tijara,
Kwa kuwa nayo daima sera ya tabia bora.

(iv) Diwani: *Pambo la Lugha* (1966)

1. Chama cha Waafrika.

Upeke faida yake, nimekaa nikawaza,
Heri leo nitanuke, haifai kuitunza,
Upeke ni makeke, hasa siku za giza,
Itakapo watu wake,nchi kuiongoza.

Tanganyika ina chama, kale kimeanza,
Kusudile ni jema, chataka wanaoweza,,
Wote mkisimama, kazi hii kufanyiza,
Itafuata heshima, dhiki kuzituza.

Chama cha Waafrika, jina limetokeza,
Kila Mtanganyika , wajibu kujiingiza,
Kutendwa kwa shirika, hili latukuza,
Kusudile mashaka,kuzuia kutumeza.

Taabu zilizo kali, wajibu kuelezwa,
Ifahamu Serikali, Dola ya Kiingereza,
Waume wenye akili, na wake wanaowaza,
Kazi hii halali, kimya kinaangamiza.

Tuungane kwa sauti, bila mtu kuiza,
Ifike kuliko kiti, Dola iwe yawaza,
Kuwa uko umati, mashaka yawaumiza,
Kando mtu asiketi, mwendo unafuliza.

Taabu za wenyeji, kila siku hujikuza,
Hufanywa si wahitaji, kazi zao hubezwa,
Hili halifariji, moyoni linachukiza,
Heri kwetu haiji, bila umoja kukaza.

Shime waafrika, kutafuta mwangaza,
Fahamuni mashaka, daima yatufingiza,
Vyama vingine kushika, siwezi kukataza,
Ila cha Waafrika, nakiona ni kikuza.

All come on, kila mwenyeji aweza,
Do his turn, Tanganyika kuikuza,
Know each grain, uzito inaongeza,
African Association, naam mwangaza.

2. Kiswahili

Titi la mama litamu, hata likiwa la mbwa,
Kiswahili naazimu, sifayo inayofumbwa,
Kwa wasiokufahamu, niimbe ilivyo kubwa,
Toka kama chemuchemu, furika palipozibwa,
Titi la mama litamu, jingine halisi hamu.

Toka kama mlizamu, juu kwa wingi furika,
Mfano wa Zamzamu, yenye rutuba Makka,
Uonyeshe na muhimu, kwa wasiokutamka,
Hata wafanye hamu, mapajani kukuweka,
Titi la mama litamu, jingine halisi hamu.

Lugha yangu ya utoto, hata leo nimekua,
Tangu ulimi mzito, sasa kusema najua,
Sawa na manukato, moyoni mwangu na pua,
Pori, bahari na mto, napita nikitumia,
Titi la mama litamu, jingine halisi hamu.

Sababu ya kupenda, lafidhi yangu natoa,
Natumia toka ganda, na kiini chanelea,
Lugha nyingine nakonda, wakati nikitumia,
Mbele nikitaka kwenda, ulimi wangu hukwaa,
Titi la mama litamu, jingine halisi hamu.

Ujira mwema napewa, kwa lugha za kigeni,
Na bidii natoa, nyingi nisiwekwe chini,
Lakini juu ya haya, nawaza mwangu moyoni,
Mwasi wa kutumia, lugha yake maskini,
Titi la mama litamu, jingine halisi hamu.

Usemi na akili, ni pambo vikilingana,
Kwa lugha ya Kiswahili, sina cha kunibana,
Kama natoa kauli, na fikira kufanana,
Lugha nyingine bahili, ujima kwangu hazina,
Titi la mama litamu, jingine halisi hamu.

Lugha kama Kiarabu, Kirumi na Kingereza,
Kwa wingi zimeratibu, mambo ya kupendeza ,
Na mimi nimejaribu, kila hali kujifunza,
Lakini sawa na bubu, nikizisema nabezwa,
Titi la mama litamu, jingine halisi hamu.

Kila mtu lugha yake, ndiye mtumishi mwema,
Lugha nyingine makeke, mviringo kazisema,
Kila mkuu na pake, hana hadhi akihama,
Kiswahili nivike, joho lako la heshima,
Titi la mama litamu, jingine halisi hamu.

Natoa na kubakisha, kwa lugha ya Kiswahili,
Naweza na kujibisha, swali bila shikeli,
Kwa lugha nyingine yesha, rai niweze hili,
Lakini nakopesha, kulipwa sina dalili,
Titi la mama litamu,jingine halisi hamu.

Kila lugha ina roho, nyingine kama wajua,
Bali kilemba na joho, hupata mtu mzawa,
Na hili kama hoho, huwasha na kusumbua,
Nimechoshwa na uroho, sasa nataka pumua,
Titi la mama litamu, jingine halisi hamu.

Katika maamkizi, mepesi sana na mema,
Lugha zote haziwezi, nyingine kudai kima,
Kama kile azizi, kwa Kiswahili kusema,
Shikamoo kwa mzazi, ama mtu wa heshima,
Titi la mama litamu, jingine halisi hamu.

Mfano neno la *jambo,* mkato wa una jambo,
Jibu lake *si jambo*, tafsiri sina jambo,
Tazama hili pambo, lizindishavyo urembo,
Wa kuulizana mambo, kwa usemi wenye umbo,
Titi la mama litamu, jingine halisi hamu.

Lugha kuu za dunia, jumla kumi na mbili,
Na hizo huhesabiwa, pamoja na Kiswahili,
Kwa haja kuwaridhia, watu mbalimbali,
Kwayo hakikupungua, yanipasa kukijali,
Titi la mama litamu, jingine halisi hamu.

Lugha ngeni ni elimu, hili sana naelewa,
Sitishiwi na ugumu, kwa kujifunza najua,
Lakini ilivyo tamu, lugha ya kulelewa,
Kusema yalazimu, kila hali yo yote kuwa,
Titi la mama litamu, jingine halisi hamu.

Mtu kwa usemi wake, wanyama milio yao,
Samba kwa ngurumo yake, tisho kuu kwa kondoo,
Bali kwa makinda yake, hupendeza masikio,
Na tai kwa wimbo wake, mbalimbali na jogoo,
Titi la mama litamu, jingine halisi hamu.

Kiswahili kikikopa, lugha nyingine pia,
Ambazo zimenenepa, jambo hili hutumia,
Ama siyo zimetupwa, kwa kukosa manufaa,
Kiswahili kikikopa, si ila ndiyo tabia,
Titi la mama litamu, jingine halisi hamu.

Ng'ombe akiita dama, husemwa kuwa alia,
Akipigwa kulalama, ng'ombe hatujasikia,
Ukosefu wa hekima, juu ya mambo haya,
Husemwa kwa lawama, japo lugha si mbaya,
Titi la mama litamu, jingine halisi hamu.

Kiswahili tajiri, kwa fasaha na methali,
Na mimi nafikiri, wakati hauko mbali,
Kitaweza kufasiri, elimu mbalimbali,
Kwa akili na uzuri, kiwape watu fadhili,
Titi la mama litamu, jingine halisi hamu.

Maneno bila hesabu, bado watu kuandika,
Ni hazina ya dhahabu, inangoja kutumika,
Nami nadhani karibu, siku njema itafika,
Yawe katika vitabu, na vinywa kuyatamka,
Titi la mama litamu, jingine halisi hamu.

Maneno ya uthabiti, maelezo ya jinsi,
Nyingi na tofauti, kwa fasaha na wepesi,
Kama lulu na yakuti, johari na almasi,
Yenye ladha ya sauti, bado kuona kamusi,
Titi la mama litamu, jingine halisi hamu.

Yaandikwe yote haya, kwa uzuri taratibu,
Yalingane sawasawa, na uzito wa dhahabu,
Ambao wengi hutoa, kwa kununua vitabu,
Mtenda mema dunia, zawadi yake thawabu,
Titi la mama litamu, jingine halisi hamu.

Mtenda mema dunia, huwa mbali na aibu,
Wasanifu mambo haya, nataka ningejaribu,
Bahati itawendea, labda ya kuratibu,
Pungufu kuwa sawa, lugha iwe dhahabu,
Titi la mama litamu, jingine halisi hamu.

Kiswahili kina sifa, kwa nahau na maana,
Hufanya na mataifa, mengi kusikilizana,
Kikitoa taarifa, kwa wengi huwa bayana,
Na iwapo kitakufa,roho nyingi zitanuna,
Titi la mama litamu, jingine halisi hamu.

Lugha hii ni ya mbele, ingawa leo i nyuma,
Walakini polepole, sifa yake itavuma,
Kitu bora milele, hubatilisha lawama,
Na kufikia kilele, cha fahari na heshima,
Titi la mama litamu, jingine halisi hamu.

Kiswahili Mto Nili, kwa kazi ya ushairi,
Ambao hutoa mbali, rutuba hata Misri,
Masika na jua kali, kila siku husafiri,
Na kwa kazi mbalimbali, msaadawe mzuri,
Titi la mama litamu, jingine halisi hamu.

Hata tele likijaa, titi jingine si zuri,
Mtoto mwenye njaa, kunyonya hana uhuri,
Na lugha sawasawa, ni kaidi kwa amri,
Kama hakuzizoea, mtu mwanzo wa umri,
Titi la mama litamu, jingine halisi hamu.

Nashukuru fahari, sikuumbwa kwa bubu,
Jambo ambalo sikiri, kulisema ni wajibu,
Titi jingine si zuri, hili nimelijaribu,
Cheo changu na ari, nikaona laharibu,
Titi la mama litamu, jingine halisi hamu.

Kiswahili kunena, nenda demani na joshi,
Lugha geni hubana, kwa hivi hazinitoshi,
Na iwapo nazinena, fikira yangu haishi,
Bure nafua sana, mawazo hazisafishi,
Titi la mama litamu, jingine halisi hamu.

Mzoevu wa kazi, uvivu kwake hudhuru,
Kukaa bure hawezi, ndipo nikajikusuru,
Kuandika beti hizi, kama zitapata nuru,
Ndiyo yangu mapenzi, zikikosa haidhuru,
Titi la mama litamu, jingine halisi hamu.

Bado kwenda nitakavyo, ila nataka pumua,
Maneno yaliyo ovyo, moja sitaki kutiwa,
Hapa katika urovyo, shabaha ikawa mbaya,
Huu mwanzo wa mchovyo, nataka kuogelea,
Titi la mama litamu, jingine halisi hamu.

Kila kitu wastani, mwanzoe mwendo tambazi,
Na mimi Shaaban, mwendo wa mbio siwezi,
Kwa hali kuwa duni, sishi vikwi na machozi,
Bali nina shukurani, mtenda hili Mwenyezi,
Titi la mama litamu, jingine halisi hamu.

3. Udugu

Barua imewasili, Mpwapwa ninakokaa,
Leo nasema kweli, huna haja ya fadhaa,
Neno langu sibadili, udugu nimeradhia,
Kati ya sisi wawili, hili litaendelea.

Mkataa wingi mchawi, hili si masihara,
Wala nyumba haiwi, kwa jingo moja imara,

Ndugu hakataliwi, kumkataa hasara,
Wingi ni ustawi, upeke una madhara.

4. Mwananke si Kiatu

Chama kutaka utii, kichekesho si kweli,
Chama hutaka ridhai, mapatano ya kamili,
Yapimwe yasirufai, mume kwa mke ratili,
Halidi natumai, bure umekwenda mbali.

Vyama tofauti, kila hama mbalimbali,
Utii huja kati, kwa chama cha serikali,
Mume na mke sharti, mapenzi yakabili,
Huchukiza tasiliti, kusema lile na hili.

Wanawake wana laana, jibu lake ufedhuli,
Tena mimi naona, lawama lastahili,
Kuwa hujui kunena, u mchache wa akili,
Wanawake bora sana, ni hazina ya awali.

Laana ni kosa moja, kubwa katika kauli,
Ambalo limefuja, maneno na kubadili,
Mwanamke ana haja, ya usawa wa hali,
Mke hazai kioja, ila kwa mbegu dhalili.

Mwanamke ana ila, hupati wa kukubali,
Kusikia kwa muhula, mimi bado neon hili,
Wala hapana mahala, asipooneka ghali,
Bibi ni mtawala, nyumbani kila mahali.

Japo nakaa mekoni,tungo hainishughulishi,
Uliza mimi ni nani uelewe na asili,
Halafu uje wanjani, tuonyeshane kitali,
Ukiwa Shiraziani, na mimi ni Mswahili.
Majivuno na togo, nasikia huku mbali,
Ni kazi ya Kidigo, karibu kila mahali,
Sogea upate pigo, neon langu sibadili,
Wachukuaje mzigo, hali nawwe si hamali?

Vishindovyo si kitu, Vyangu vikikabili,

Usilaghai watu, juu ya kitu cha mali,
Mwanamke ndicho kitu, bora hakina badili,
Ila kufanywa kiatu, hili hatalikubali.

Si wajibu kusema, mke hana fadhili,
Wapo waume si wema, tia katika akili,
Na mabaya yauma, hapana wa kuhomili,
Ukivunja heshima, mke naye hunakili.

Bure kutaja sharia, mume anazobadili,
Hodi! Hodi! Kutokea, bwana huanza awali,
Bibi akiandamia, adhabu hastahili,
Mke hachungi murua, mume akiwa katili.

Wakatabahu natuza, yaumiza tasihili,
Bibi kwa Waingereza, bora kweli kweli,
Waungwana wakubeza, usemapo ufedhuli,
Hapa natangaza, hili lende hata mbali.

5. Mume na Mke

Wimbo wangu nahofia, kuwa utapata haba,
Watu wa kukupokea, wakuimbe kwa mahaba,
Lakini ingawa haya, naona kwangu msiba,
Mafichoni kukutia, na kuacha kukuimba.

Nikiacha kukuimba, lazima utapotea,
Pengine ziko nyumba, tayari kukupokea,
Uzuri wako kufumba, naona si maridhawa,
Na kila mtu kugomba, nadhani haitakuwa.

Utakuta marafiki, wimbo kukupa malazi,
Kwao usione dhiki, upewe hata mapenzi,
Ukae na kubariki, kwao bila simangizi,
Kwayo sina haki, kusema kwimba siwezi.

Wajibu upasao, wimbo nakujulisha,
Kuwa nataka leo, mbali kukusafirisha,
Kwa watu wakupendao, uishi mapya maisha,
Na kwa wakuchukiao, ubora wako fundisha.

Ya juu ni dibaji, sasa nataka kariri,

Nilivyoona ujaji, ghafla alfajiri,
Wa wimbo nikahitaji, niandike dhahiri,
Nataka wasomaji, wasahihishe dosari**.**

Ee wimbo una ujmbe, nakutaka usafiri,
Ili wende kila pembe, ukatangaze habari,
Kuwa katika viumbe, mume na mke johari,
Tangu hili liumbwe, maisha yana fahari.

Toka zama za mitume, hawa wana utumishi,
Wa maisha yasizame, watu wapya wanaishi,
Pekee mwanamume, hili katu hadumishi,
Apatae ufalme, malkia hadunishi.

Mwanamke shetani, watu wengine wanena,
Kuja kwake duniani, kuwa ameleta laana,
Nami kwa yakini, juu ya hili nabishana,
Kuwa ana thamani, na mwanamume walingana.

Kwa nguvu nakaidi, hoja hii ya kijinga,
Kisha nina jitihadi, mahali inapojenga,
Isistawi Zaidi, sababu haina mwanga,
Giza lake uhasidi, huvutia watu janga.

Huvutia watu janga, wasipatane maneno,
Mwanamke kumtenga, kuwa duni ya kifano,
Na mimi hapa napinga, kufanya mapigano,
Kwamba huu ujinga, naupatiliza mno.

Naupatiliza sana, ujinga huu mbaya,
Uharibiwe shina, matawi moto kutiwa,
Mwanamke si laana, mwenzetu wa dunia,
Na haki ya pepo ana, kumuumbua hatia.

Mwanamke ni mwili, damu yetu na mfupa,
Kweli ya neno hili, moyo umepiga chapa,
Na kila mwenye akili, yamkini hataapa,
Kuwa hii ni batili, leo isemwayo hapa,

Umbo la fahari, kama la mwanamke!
Hasa mimi sifikiri, kuwa kusudi lake,
Ni kuleta hatari, kwa mume asumbuke,

Ila kuzidisha heri, wote waneemeke.

Umbo la kupendeza, kama la malaika!
Nashangaaa kuwaza, moyoni nina shaka,
Kuwa ameleta giza, katika ushirika,
Badala ya mwangaza, njia ya kuokoka!

Sura ya kufurahisha, kama ile ya pepo,
Inayopamba maisha,duniani tukaapo,
Kusema yalaanisha, akili yangu haipo,
Haipo nakanusha, neon hili kwa kiapo.

Umbo la uzuri, madaha na mapendezi,
Linaloleta fahari, kupunguza simanzi,
Mwanamke kufikiri, ameumbwa kuhizi,
Katika moyo kukiri, mimi nina kizuizi.

Umbo la takaso, kama mbingu na mwezi,
Pole bila tikiso, na nyota zilizo wazi,
Kusema lina mateso, kukubali siwezi,
Siwezi kuvunja uso, aibu kama masinzi.

Ardhi inapopita, upande wetu wa giza,
Mbinguni ziko nyota, zitupazo mwangaza,
Kama nyota amepata, macho ya kupendeza,
Kusema ana matata, kila mtu latatiza.

Latatiza jambo hili, hasa naona si wazi,
Tena lina kejeli, wingi wa maangamizi,
Wawezao sema kweli, wasitende ajizi,
Kufanya tasihili, kuling'oa na mizizi,

Hili sasa ling'olewe, kati yetu lisemee,
Mume na mkewe, maisha washarikie,
Mke na mumewe, watoto wema walee,
Wote heshima wapewe, umoja wetu ukue.

Umoja wetu ukue, kwa hali na mapatano,
Kila mtu atumie, mguu kwa mkono,
Kuinua mwenziwe, wote tuvune mavuno,
Ya furaha tutumie, pato la wote unono.

Pato la wote zuri, na mke hustahili,
Kuhesabiwa johari,roho na kiwiliwili,
Kashifa ya dhahiri, kwa yeyote hubadili,
Tumaini na fahari, hii hasara kamili.

Pendo lake twataka, si faida kuumbua,
Sababu twasetirika, wakati tunapopewa,
Mwanamke mshirika, hapa katika dunia,
Kudhani kanajisika, ni ufupi wa kujua.

Mwanamke mshirika, tumkosapo twagaya,
Kati yetu kuondoka, ukiwa ungetokea,
Taabu kuu kuzuka, kuliko kiu na njaa,
Na bilashi kumpaka, aibu ni kupotea.

Burashi yetu ya lami, lazima kuzuiwa,
Mwanamke arihami, kukeni kwa uzawa,
Kukashifu haitami, tena si weleke,
Nasabaye haihami, si nguo ya kuvua.

Nakana kuwa anao, udhia na ukorofi,
Hapasiwi shambulio, kushitakiwa ulafi,
Sababu ana mazao, hasa ambayo si ghafi,
Yaletayo fanikio, kwetu bora na safi.

Wajibu ni kushukuru, mazao anayozaa,
Mwanamke si kufuru, kaja kusaidia,
Mume usimdhuru, upeke wa dunia,
Uko wapi udhuru, mwema wa kumuumbua?

Ikisemwa wafanana, naona ingefaa,
Mume na mke hawana, ovu linalowagawa,
Ila ushirika wana, katika hii dunia,
Na peponi naona, wote wataamriwa.

Kulaumu mwanamke, mimi hasa nasita,
Kuwa an makeke,vile vile nateta,
Wokofu wetu na wake, lazima kutafuta,
Wote tusetirike, tutengane na matata.

Hali itakavyokuwa, kuzaliwi bila mama,
Jambo la kuajabia, kama hili la athama,

Huwaje tena likawa, badala ya heshima,
Kila pembe kulaniwa, kuwa lina lawama!

Kila anayewaza, hili moyo hutatiwa,
Dunia ina giza, mashehe washeni taa,
Watu wanaoviza, mke wapate elewa,
Ni neno la kuchukiza, sikio, jicho na pua.

Mwanamke mtukufu, sawa na mwanamme,
Ulimwengu waarifu, mwenye akili apime,
Maneno ya uumbufu, watu bure wasiseme,
Akiwa na udhaifu, bia na mwanamume.

Kutajataja daima, mwanamke kwa ubaya,
Hufanya awe nyuma, ashindwe kuendelea,
Hili halina wema,pingamizi ya stawa,
Kubatilishwa lazima, lisiwe ni mazoea.

Lazima libatilishwe, liondoke nchi zetu,
Wanawake wasitishwe, kuwa hawawezi kitu,
Wala wasidunishwe, kufanywa chini ya watu,
Ila wakaribishwe, waongeze nguvu yetu.

Nguvu yetu ni haba, yataka mwingi msaada,
Ama kaka na baba, watashindwa kila muda,
Mbele ya kila msiba, kama mama na dada,
Hawasimami mraba, washinde kwa jitihada.

Mke nyumbani faraja, kushinda mtumishi,
Mshahara hana haja, na kazi haimchoshi,
Hutu mika bila tija, pato halimshawishi,
Hutimiza na haja, hata mwisho wa kuishi.

Mtenzi wa kama hili, dunia bado kuona,
Kwa hivi astahili, mwanamke uungwana,
Asidhaniwe dhalili, fadhiliye bora sana,
Tena kwa kila hali, ana cheo cha bayana.

Cheo chake maarufu, katika kila taifa,
Kapewa si mpungufu, akili na maarifa,
Japo umbole dhaifu, kazi yake ina sifa,
Hili hasa huarifu, hastahili kashifa.

Mama wa mitume, ya sifa na manabii,
Mashujaa, wafalme,, mashehe na mawalii,
Wanawake kwa waume, wenye roho za utii,
Vinywa bure visiseme, kudai ni maadui.

Hapana sifa ya yoyote, mke akosayo haki,
Mume na mke wote, wanaishi kirafiki,
Hapana ila yoyote, mume asiyoshariki,
Wokofu haki ya wote, mwanamke hanyimiki.

Maovu ya mwanamke, pamoja na mwanamume,
Mwanamume kazi yake, kumwinua asizame,
Chini huyu mwenzake, kwa hofu ateteme,
Hata wote wasafike, sifa yao isimame.

Sasa nimefika hapa, tatua ili niheme,
Niandike akinipa, Mungu mengine mpime,
Imara bila kunepa, kila karne wasome,
Bila watu kuyatupa, upya wake usikome.

Allah nipe zaidi, nifapo nyuma yaishi,
Machoni yawe waridi, puani yawe marashi,
Ama kama mkadi, porini wenye nakshi,
Kila mtu afaidi, raha yake na nemshi.

Kutaja jiina kanuni, kila mfanyaji kazi,
Hata kama ni duni, mficha jina ni mwizi,
Na mimi ni Shaaban, Robert waziwazi,
Dhaifu na maskini, umbo jeusi la ngozi.

Umbo ngozi nyeusi, sina hadhi na cheo,
Muumba wangu hakosi, ameona hali hiyo,
Nastahili halisi, kwa hivi sina kilio,
Na moyo haunighasi, kudai nisiyo nayo.

Kiambatisho C: Mashairi ya Akilimali Snow- White

Diwani: Diwani ya Akilimali (1963)

1. Kiswahili

Kiswahili sina budi, kukipa sana makamo,
Ni lugha yangu ya jadi, kwa uzawa nimo humo,
Yanipatia muradi, na kunikuzia kimo,
Nitokapo ni jadidi, pia heshimani nimo.

Katika yangu fuadi, napenda bila kikomo,
Kukipenda sina budi, kwa fasaha na upimo,
Tamu kama zamaradi, kwa fasaha iliyomo,
Kwa maneno nafanidi, bila kuwa mtetemo.

Ingawa najitahidi, kujifunza kila somo,
Lugha za kila biladi, ni kwa kutafuta chumo,
Bali sipati muradi, ila naambua zumo,
Ni bure yangu juhudi, kusema sipati kimo!

Jama tufanye tikadi, tuyafukie mashimo,
Ambayo yaloshitadi,kuificha lugha humo,
Na walio mahasidi, washone yao midomo,
Lugha nchini izidi, pasipo kuwa ukomo.

2. Nafingwa Ningali Hai.

Lini nipate sauti, ninene ilivyokuwa,
Hali mbele sijivuti, nipate kujikunjuwa,
Nafingwa kama mauti, kwa rangi niliopewa,
Nafingwa ningali hai, kinywa nazibwa kunena.

Sendi mbele sijivuti, mbele sifiki hatuwa,
Nitakacho sikipati,kwa sawa inavyokuwa,
Sheria hawazifati, majini zamiminiwa,
Nafingwa ningali hai, kinywa nazibwa kunena.

Wapi niende kuketi, nipate kimo kukuwa,
Hali mbele sijivuti, njiani ninaziwiwa,
Mabwana nipeni kiti, mwenyewe nimesha kuwa,
Nafingwa ningali hai, kinywa nazibwa kunena.

Nafingwa sina sauti, kunena ninaziwiwa,
Pasina ya tafauti, nakatazwa kwa ukiwa,
Vipi natiwa kijiti, sauti sije sikiwa,
Nafingwa ningali hai, kinywa nazibwa kunena.

Napigwa pigo la goti, miguu nimelemewa,
Kilicho changu sipati, naomba bila kupewa,
Nafingwa kama kijiti, nanyimwa kwa kuonewa
Nafingwa ningali hai, kinywa nazibwa kunena.

Nanyimwa kwa tashititi, kukicha kuahidiwa,
Sababu ni rikuruti, sina ninachotongowa,
Ni vipi tepe sipati, au lini nitapewa?
Nafingwa ningali hai, kinywa nazibwa kunena.

Japo navuta sauti, kauli kutaka towa,
Natishwa Snowaiti, kwa rangi niliopewa,
Kwa kunifunga kijiti, bila sababu kujuwa,
Nafingwa ningali hai, kinywa nazibwa kunena.

3. **Walimwengu Tutendeje?**

Nchi yaingia shida, shida imebisha hodi,
Juhudi na jitihada, bila shida inazidi,
Wanadamu tunakonda, shida zafyonza miradi,
Walimwengu tutendeje, nchi yaingia shida.

Tangu kuingia shida, hali yetu haizidi,
Hata ile ya kaida, shida imeishadidi,
Dhiki kwetu yatuganda, yatuganda kama kodi,
Walimwengu tutendeje, nchi yaingia shida.

Shida kwetu imeranda, yaranda kifudifudi,
Shida haina pakwenda, ila kwetu inazidi,
Dhiki yaturondaronda, yafyonza yetu miradi,
Walimwengu tutendeje, nchi yaingia shida.

Kila twataka kupanda, miche shambani izidi,
Nguruwe wanatuwinda, jinsi walivyo hasidi,
Shida mara hutushinda, walimwengu kutuzidi,
Walimwengu tutendeje, nchi yaingia shida.

4. Manahodha Kuwa Wengi.

Japo awe Kapiteni, Kemburiji kasomea,
Amevaa darubini, supana kachomekea,
Akiwa na mkinzani, meli haitaelea,
Manahodha Kuwa Wengi**,** ni kuzamisha mashua.

Huzama ikaenda chini, meli ikadidimia,
Kutoka ikawa kani, kwa ubishi kutumia,
Si mazuri ukindani, utapoteza njia,
Manahodha Kuwa Wengi**,** ni kuzamisha mashua.

Awe ni fundi yakini, hodari alosomea,
Mjuzi wa kila fani, hana linampotea,
Kama hataki maoni, hana budi kukosea,
Manahodha Kuwa Wengi**,** ni kuzamisha mashua.

Kusoma sana si shani, shani ni mtu kujua,
Na usiwe mbishani, kukinda hutaambua,
Nguvu inafaa nini, ni kuzamisha mashua,
Manahodha Kuwa Wengi**,** ni kuzamisha mashua.

Asingeitwa Manani, kama hangepambanua,
Wa juu akawa chini, na wa chini akajua,
Mwaka mwema kazini, ndiyo mwendo wa mashua,
Manahodha Kuwa Wengi**,** ni kuzamisha mashua.

Rai itafaa nini, meli ishapo titia,
Japo ushike sukani, na winchi kunyanyulia,
Lishindwalo Kapiteni, taliweza baharia?
Manahodha Kuwa Wengi**,** ni kuzamisha mashua.

5. Kila Mpenda Rushuwa

Natunga nikiwaasa, msije kujijutia,
Mitego sije wanasa, mkaja kuangamia,
Tamaa nyingi za pesa, gereza zitawatia,
Kila mpenda rushuwa, jela inamkonyeza.

Jela inakukonyesha, kama hutajiziwia,
Haina ndugu gereza, jela si ya kuchezea,
Inajuvya na kupoza, wenye nguvu kutulia,
Kila mpenda rushuwa, jela inamkonyeza.

Rushuwa si kitu chema, walaji jihadharini,
Mkila zitawakwama, zitawatoka puwani,
Wazilao hulalama, si mimi wala fulani,
Kila mpenda rushuwa, jela inamkonyeza.

Ridhika na upatacho, kama moja au mbili,
Usitaraji mkocho, apatao Bwana Ali,
Tama zako za macho, zitakuletea mbuli,
Kila mpenda rushuwa, jela inamkonyeza.

Nimeona kemu kemu, wenye vyeo kutumia,
Maleba wakiwahimu, rushuwa kuwaletea,
Muogopeni Karimu, Leba haombwi rushua,
Kila mpenda rushuwa, jela inamkonyeza.

Kuna wengi mahakimu, haki wanazopinduwa,
Yatima kuwadhulumu, kwa kupapia rushuwa,
Kwa kutaka darahimu, aso haki anapewa,
Kila mpenda rushuwa, jela inamkonyeza.

6. Kila Ndege na Tundule

Tundu liwe la johari, la lulu au la chuma,
Ndege humo hunawiri, tunduni ataparama,
Haishi akishamiri, uzima wake wa dema,
Kila ndege na tundule, tundu jingine karaha.

Tundu jingine si zuri, hawi na raha daima,
Ndege hawi na uhuri, kukonda kutamwandama,
Tundu njema la fahari, ni chali chake cha zama,
Kila ndege na tundule, tundu jingine karaha.

Muwekee kila tunda, mwanzo chenga na mtama,
Ndege kula hatapenda, kula huona nakama,
Ndege hawezi kuranda, tunduni mwa kuwazima,
Kila ndege na tundule, tundu jingine karaha.

Sauti njema ya hiba, ya ndege iweze vuma,
Ndege aweze kuimba, kwa raha musitakima,
Awe kwa mama na baba, kwingine huwa yatima,
Kila ndege na tundule, tundu jingine karaha.

Tundu jingine uchuru, ndege hataita mama,
Ndege hawi na uhuru, ndege hapati karama,
Japo atajikusuru, hasikiziki kalima,
Kila ndege na tundule, tundu jingine karaha.

Kwa jumla twahisabu, tangu kondoo na ndama,

Kufugwa kwawapa tabu, hawaridhiki daima,
Bali kati mawahibu, hatusikizi kusema,
Kila ndege na tundule, tundu jingine karaha.

Rabi naomba kabuli, tujalie heri njema,
Tuzidisha ikibali, tujifunze taaluma,
Tuishi na Kiswahili, lugha ngeni kuzitema,
Kila ndege na tundule, tundu jingine karaha.

7. Kila Mdharau Chake

Kuzimu wenda kuona, kila mdharau chake,
Cha kwake akakikana, kutumai cha mwenzake,
Fahamu anayo lana, mpiga chake mateke,
Kila mdharau chake,kuzimu enda kuona.

Siringe na kujivuna, chako ukakipa teke,
Unavunja lako jina, ili watu wakucheke,
Ama lana kwa Rabana, kila mdarau chake
Kila mdharau chake,kuzimu enda kuona.

Chako japo si cha mana, kibaya mtu ni chake,
Kitunze na kukinena, na ukipe hadhi yake,
Kisifu ukipe jina, kipambe na kipambike,
Kila mdharau chake,kuzimu enda kuona.

Awe Fatu na Amina, au Asha ndugu yake,
Katu hawatafanana, kila mtu hadhi yake,
Kila mjuzi wa mana, huwa hadharau kwake,
Kila mdharau chake,kuzimu enda kuona.

Tama naomba amina, kilicho chetu tushike,
Kidumu na kulingana, na tukipe hadhi yake,
Ama lana kwa Rabana, kila mdharau chake,
Kila mdharau chake,kuzimu enda kuona.

8. Lipende Taifa Lako

Ulipendapo taifa, kwa moyo wako wa dhati,
Kisha na kulipa dhifa, na yake kuyazingatia,

Jua kwamba hiyo sifa, ni yako mtanashati,
Lipende taifa lako, kisha ulitumikie.

Penda litie moyoni, hadhiye uizingati,
Matendo ni shukurani, yenye ngome madhubuti,
Ufapo huzikwi chini, japo iweje laiti,
Lipende taifa lako, kisha ulitumikie.

Sipende kwa uzandiki, ukadanganya umati,
Matendo usidiriki, na njia usizifati,
Huo ndiyo unafiki, kupita uafiriti,
Lipende taifa lako, kisha ulitumikie.

Ewe rafiki jelisi, songea nikupe kiti,
Nikwambie ya hususi, kichwani mwako yaketi,
Kufa kwa wingi arusi, waogopaje mauti,
Lipende taifa lako, kisha ulitumikie.

Nisemayo tekeleza, yashike kwa ithibati,
Wema wako tengeneza, kwa kila hali na dhati,
Umoja kitu cha kwanza, washinda hata yakuti,
Lipende taifa lako, kisha ulitumikie.

Usipende kukubali, japo kwa kutiwa jiti,
Kwa Taifa lako hili, kukashifiwa laiti,
Usibadili kwa mali, heri ubaki maiti,
Lipende taifa lako, kisha ulitumikie.

Pigana ridhika kufa, kama kufanywa busati,
Kukashifiwa Taifa, na mtoka Masikati,
Kufa miliki ya sifa, unapofia umati,
Lipende taifa lako, kisha ulitumikie.

Heri mauti kubaki, au kuwa mahututi,
Kama kuwa laizeki, mchache waithibati,
Kufia yako miliki, sawa na kwenda janati,
Lipende taifa lako, kisha ulitumikie.

Kumbuka kila wajibu, pambo la mti makuti,
Na pendo la utabibu, kila dhara halileti,
Usishahau sahibu, wasia wangu dhibiti,
Lipende taifa lako, kisha ulitumikie**.**

9. Jirani Yako ni Ndugu Yako

Mfanye ndugu mwamini, jirani nyumba ya pili,
Simtiye mtihani, jirani ni ndugu kweli,
Chako kiwe cha jirani, na chake usithakili,
Jirani yako ni ndugu, allaalla na jirani.

Siri yako ya moyoni, mno inayo kudhili,
Ambiwaye ni jirani, jirani si mtu mbali,
Jirani ndio mwamini, jirani ni mfadhili,
Jirani yako ni ndugu, allaalla na jirani.

Fanya ukimthamini, jirani uwa wa pili,
Peaneni la undani, japo siri na ajali,
Ni ndugu yako jirani, si vyema kumfidhuli,
Jirani yako ni ndugu, allaalla na jirani.
Pendaneni na jirani, japo kijitu dhalili,
Sahani moja kuleni, nahari hata laili,
Cheko njema peaneni, na muwe watu wa kweli,
Jirani yako ni ndugu, allaalla na jirani.

Si vizuri utetani, na kuchunguana hali,
Japo takupa majani, kula sione muhali,
Utesi na nukusani,hutenganisha wawili,
Jirani yako ni ndugu, allaalla na jirani.
Yafanye uyathamini, majani pasi muhali,
Yatafuneni majani, japo kuwa kwa ugali,
Mridhi wako jirani, moyoni stahamili,
Jirani yako ni ndugu, allaalla na jirani.

Ni ndugu yako jirani, msikindani kwa hali,
Akupacho mkononi, twaa mikono miwili,
Wa kadha na shukurani, mtolee kwa Jalali,
Jirani yako ni ndugu, allaalla na jirani.

Pendaneni na jirani, jirani ni ndugu kweli,
Penye shida ya jirani, wewe uwe wa awali,
Usijitenge pembeni, wakite watu wa mbali,
Jirani yako ni ndugu, allaalla na jirani

Mengi ndugu msidhani, kusema sina akili,

Ni mausi nawapeni, jirani ni mfadhili,
Mke wa wako jirani, haipasi kumfeli,
Jirani yako ni ndugu, allaalla na jirani.

Tamati nashukurani, kwako bwana Jitu Kali,
Picha yako Tazamani, yanirufai akili,
Ni kama Hururaini, Mafunda hana mithali,
Jitukali Hamduni, allaalla na jirani.

10. Udugu

Udugu kweli haiba, pambo zuri la moyoni,
Ikiwa nyote mwashiba, mtakuwa furahani,
Mtaishi kwa mahaba, bila kuwa nukusani,
Udugu bila ya hivyo, asili hampatani.

11. Hujafa Hujaumbika

Mwanadamu hasifiki, ushupavu na kiburi,
Kiburi huzaa chuki, majitapo si mazuri,
Ulimwengu hautaki, jambo lenye taksiri,
Hujafa hujaumbika, jilinde na majitapo.

Si wajibu upasao, vilema havikasiri,
Hujajua maishao, viwaje vitashamiri,
Anayedharau hao, mwisho wake huwa mori,
Hujafa hujaumbika, jilinde na majitapo.

Jilinde ukijiweka, makazi yalo mazuri,
Mdogo muite kaka, na mzee kumkiri,
Hapo utasalimika, dunia taona nzuri,
Hujafa hujaumbika, jilinde na majitapo.

Hautakupa salama, usinune na jeuri,
Usinyanyase vilema, vilivyo umba Kahari,
Hujafa huna salama, mtu hakosi dosari.
Hujafa hujaumbika, jilinde na majitapo.

Cheko njema ni hazina, iwezayo kusafiri,
Inaathiri mwanana, inaleta kila kheri,
Watu wanaojivuna, si watu nyama wa pori,
Hujafa hujaumbika, jilinde na majitapo.

Ni wengi nimewapima, wasio na tafakuri,

Wanapojigamba vyema, wanazidisha kiburi,
Wenzao wawita nyama, bileshi kwa ujeuri,
Hujafa hujaumbika, jilinde na majitapo.

Hasa appate kiatu, rangi mbili zilo nzuri,
Aona watu si kitu, kama mijiti na porti,
Mbora asiye na kitu, alo na heshima nzuri,
Hujafa hujaumbika, jilinde na majitapo.

Kama mume na mke, hujizidisha fahari,
Apatapo nguo yake kaeni vyema tayari,
Hasemi nao wenzake, siku hiyo kwa vizuri,
Hujafa hujaumbika, jilinde na majitapo.

Sisemi kama hujui, na huwezi tafakuri,
Kiburi hakiinui, kuwa nacho si fahari,
Kinazaa uadui, huzaa chuki kiburi,
Hujafa hujaumbika, jilinde na majitapo.
Kaditama wanachama, tupunguzeni kiburi,
Kiburi si mwendo mwema, si ungwana kiburi,
Mwisho wake ni hasama, kiburi huleta shari,
Hujafa hujaumbika, jilinde na majitapo.

12. Kila Mtaka Uluwa

Hautampa nafasi, kukaa na kutulia,
Sitoshe hivyo si basi, hatia utamtia,
Waotakao kwa kasi,kiwaka chawangojea,
Kila mtaka uluwa, dunia aichukia.

Nimeona wengi wengi, Zaidi kuliko mia,
Wapotezao shilingi, kwa vyeo kuviwania,
Wengi hutaka ukingi, viti bora kukalia,
Kila mtaka uluwa, dunia aichukia.

Kupata huwa si nguvu, si vishindo na ghasia,
Kwataka uvumilivu, uukosapo tulia,
Autakae kwa nguvu, jela inamngojea,
Kila mtaka uluwa, dunia aichukia.

Kiambatisho D: Mashairi ya Saadani Kandoro

Diwani: *Mashairi ya Saadani* (1966)

1. **Tukifanye Chama Chetu Watungaji Mashairi**

Watungaji mashairi, naeleza haki yetu,
Natoa langu shauri, lipenye akili zetu,
Mimi nimetafakari, tukifanye chama chetu,
Tukifanye chama chetu, watungaji mashairi.

Tukingonja kusubiri, kutendewa kazi zetu,
Ni kama twajihasiri, kuzuia mwendo wetu,
Tukutane tufikiri, tufanye gazeti letu,
Tukifanye chama chetu, watungaji mashairi.

Wenzangu tujisitiri, tusitiriwe na watu,
Utungaji mashairi, wahifadhi lugha yetu,
Tusimame kiamiri, kujenga muruwa wetu,
Tukifanye chama chetu, watungaji mashairi.

Tujitoe kwa hiari, tuikuze lugha yetu,
Mafunzo yenye hiari, yawe gazetini mwetu,
Na mafunzo ya hatari, tutupe ndani ya mwitu,
Tukifanye chama chetu, watungaji mashairi.

Na tusimame tayari, kwa mapenzi kila mtu,
Tuufanye uhodari, tuzitoe mali zetu,
Ukinunua sukari, mpaka ulipe kitu,
Tukifanye chama chetu, watungaji mashairi.

Mko wapi washairi, enye watungaji wetu,
Nakuombeni mkiri, muendeshe nchi yetu,
Wakati waliasiri, tusichekwe na wenzetu,
Tukifanye chama chetu, watungaji mashairi.

Ni nane awe amiri, aanzishe wito wetu,
Tumchague dhamiri, atangaze mambo yetu,
Mji gani wa shauri, iwepo ofisi yetu,
Tukifanye chama chetu, watungaji mashairi.

Kaditama shairi, kaelewa kila mtu,

Nimeeleza dhahiri, nami sikuficha kitu,
Kwa kweli nipo tayari, tuanzishe kazi yetu,
Tukifanye chama chetu, watungaji mashairi.

2. Shujaa Haogopi Kitu Kilicho Halali Yake

Nisarayo mnyashike, hili shairi letu,
Akuitae mwitike, tuendeshe mamabo yetu,
Shujaa na kitu chake, hadhulumiwi na mtu,
Shujaa hahofu kitu, kilicho halali yake.

Hodari kwa haki yake, hapendi ipate kitu,
Tena hageuki kike, japokuwa mwana kwetu,
Japo mtoto mshike, atafanya utukutu,
Shujaa haogopi kitu, kilicho halali yake.

Hupendezwa kiongoke, cha kwake au cha kwetu,
Hupendezwa moyo wake, usitekwe mji wetu,
Japokuwa muudhike, yeye haogopi kitu,
Shujaa haogopi kitu, kilicho halali yake.

Hodari nyumbani kwake, huwakaribisha watu,
Hutetea nchi yake, asichafue mtu,
Yu tayari peke yake, kuutembelea mwitu,
Shujaa haogopi kitu, kilicho halali yake.

3. Haki Huvunja Milima

Hakika nimebairi, walimu walivyosema,
Edita usinihini, shairi litoe hima,
Kiongozi wa jeshini, haliogopi lawama,
Haki huvunja milima, niliambiwa shuleni.

Niliambiwa shuleni, na mtu mwenye hekima,
Mwenye akili kichwani, na nyingi mno heshima,
Kwamba “haki”duniani, watu wengi huwachoma,
Haki huvunja milima, niliambiwa shuleni.

Najua tangu zamani, wajinga watanisema,
Mwalapoteza kiiru, cha mambo niliyosema,
Kutukana gazetini, mwajivunjia heshima,

Haki huvunja milima, niliambiwa shuleni.

Mjibuo fikirini, mbona mwajibu hasama,
Ninavyotaka yakini, Afrika kusimama,
Mbona meli baharini, mwaiendesha mrama,
Haki huvunja milima, niliambiwa shuleni.

Ndipo nami gazetini, ninazidi kulalama,
Uhuni wenu ombeni, ili mzidi kukuwema,
Haifai barazani, bure mkitusakama,
Haki huvunja milima, niliambiwa shuleni.

4. Siafu Wamekazana

Nyoka amegutuka, ndani ya shimo kutuna,
Tena amekasirika, hasira zenye kununa,
Nyoka anababaika, shimoni kwa kujikuna,
Siafu wamekazana, nyoka amekasirika.

Shimoni ataondoka, hilo nataja kwa jina,
Nyoka anajua fika, siafu wakiungana,
Nguvu zinaongezeka, shimoni watagombana,
Siafu wamekazana, nyoka amekasirika.

Siafu zikijishika, mshiko kushikamana,
Kwamba zinampeleka, Sultani wao bwana,
Shimoni wanapofika, nyoka la kufanya hana,
Siafu wamekazana, nyoka amekasirika.

Siafu wanapofika, na nyoka wakikutana,
Nyoka hawezi kufoka, kuwa ametuliza,
Ndipo nyoka huondoka, na wana wakilizana,
Siafu wamekazana, nyoka amekasirika.

Kupo na kukanyagika, hilo natujue sana,
Nyoka anapoondoka, siafu hulaliana,
Huuma hupumzika, hapo hakutafanana,
Siafu wamekazana, nyoka amekasirika.

Nyoka akisha ondoka, na siafu hujazana,
Shimoni wakipeleka, vyakula kutiliana,
Ndilo walilolitaka, wale kwa kutulizana,

Siafu wamekazana, nyoka amekasirika.

5. Kwetu ni Kwao kwa Nini ?

Mtu huuliza nini, kitu hiki ni cha nani ?
Kitu hiki ni cha nani, na hiki kitu ni cha nini ?
Nacho kinaitwa nini, ni cha nani na kwa nini ?
Kwetu ni kwao kwa nini, na kwao kwetu kwa nini ?

Na kwa nini cha nani, na chake ni kwa njia gani?
Jawabu liwe yakini, lisiwe purukushani?
Kwa nini sababu gani ? kwao ni kwetu kwa nini?
Kwetu ni kwao kwa nini, na kwao kwetu kwa nini ?

Kwa nini kwao kwa nini, kuwe kwetu ni kwa nini?
Na kwetu pia kwa nini, kuitwa kwao kwa nini?
Kwa nini inayakini, kwetu ni kwao kwa nini?
Kwetu ni kwao kwa nini, na kwao kwetu kwa nini ?

Mtu kwao kuthamini, ijapokuwa jiweni,
Pia alale mtini, na baraza liwe chini,
Nile matunda porini, kuitwa kwenu kwa nini?
Kwetu ni kwao kwa nini, na kwao kwetu kwa nini ?

6. Waafrika Njooni

Ninawapeni fununu, Waafrika njooni,
Msiwe penye upenu, wa nyumba zenu njoni,
Njoni niwape tunu, kaja la heba njoni,
Waafrika njoni, njoni muandike TANU.

Njoni katika TANU, na tusimame fuleni,
Cham chetu cha TANU, msikae ujingani,
Kina Suwedi kina Nunu, hima upesi njoni,
Waafrika njoni, njoni muandike TANU.

TANU hii ni ya kwenu, huru kuwa o mbeeni,
Na kazi kubwa ya TANU, ambayo yawatakeni,
Kuunga kabila zenu, liwe taifa thamani,
Waafrika njoni, njoni muandike TANU.

Njoni nyumbani mwenu, nyumba ni TANU njoni,
Muongoze nchi yetu,itukuke duniani,
Mtoe maarifa yenu,yaonwe ulimwenguni,
Waafrika njoni, njoni muandike TANU.

Sasa sikifani chenu, kutawaliwa nchini,
Tazameni hali zenu, mtakubali yakini,
Watazameni wenzenu, watu wa Ghana nchini,
Waafrika njoni, njoni muandike TANU.

Kutawaliwa kwenu, mtu hakui yakini,
Hamjui nchi yenu, muongoze njia gani,
Na vile vinono vyenu, vikiliwa hamuoni,
Waafrika njoni, njoni muandike TANU.

Mpeni nguvu mwenzetu, Bwana Nyerere mpeni,
Mpeni umoja wenu, umoja wenu mpeni,
Mkombozi wangu wenu, atutowe utumwani,
Waafrika njoni, njoni muandike TANU.

Nafunguwa shairi lenu, sisi si masikini,
Beti kumi ziwe kwenu, zitieni akilini,
Ombeni uhuru wenu, hivi karibu ombeni,
Waafrika njoni, njoni muandike TANU.

7. Ondoka Nchini Mwetu

Shairi hili linajieleza, ni juu ya kumkataa mwingereza kututawala.

Raia tumekutana, mbele ya wakubwa wetu,
Raia tumeungana, kuunda taifa letu,
Na sisi tuwe mabwana, kutawala nchi yetu,
Ondoka nchini mwetu, mwishoni wa mwaka huu.

TANU inalia sana, wote wanachama wetu,
Wana kulilia bwana,uondoke hapa kwetu,
Bwana tafadhali sana, ondoka nchini mwetu,
Ondoka nchini mwetu, mwishoni wa mwaka huu.

Nchi tunayo inena, hii Tanganyika yetu,

Nchi yote kuungana, Afrika ni ya kwetu,
Afrika ya kazana, tokeni tokeni mwetu,
Ondoka nchini mwetu, mwishoni wa mwaka huu.

Sheria yajulikana, na kwa viumbe wenzetu,
Uingereza hata China, kwamba hii nchi yetu,
Haipendezi hiyana, chako kukifanya chetu,
Ondoka nchini mwetu, mwishoni wa mwaka huu.

Kumkataza kunena, Kenyatta mzee wetu,
Si tendo la kiungwana, latuchoma mioyo yetu,
Tunawaombeni sana, asema mzee wetu,
Ondoka nchini mwetu, mwishoni wa mwaka huu.

Maombi yetu bayana, hatujamficha mtu,
Wazee hata vijana, twawatangazia watu,
Tuwe huru kama Ghana, nasi tutawale kwetu,
Ondoka nchini mwetu, mwishoni wa mwaka huu.

Ondoka tukilingana, tuje kwenu uje kwetu,
Mikono tukipeana, huru Afrika yetu,
Si vyema kupunjana, mle vyenu tule vyetu,
Ondoka nchini mwetu, mwishoni wa mwaka huu.

8. Kitumike Kiswahili.

Bwana Edita andika, twakuomba tafadhali,
Kilio chetu peleka, wakaone serikali,
Kwamba tunasikitika, wenyeji kutupwa mbali,
Kitumike Kiswahili, Baraza la Tanganyika.

Baraza la Tanganyika, ambalo la serikali,
Ndilo tunalolitaka, litumike Kiswahili,
Tupate Waafrika, kuendesha serikali,
Kitumike Kiswahili, Baraza la Tanganyika.

Sheria zinapotoka, tuzisome bila ghali,
Ndipo tujue hakika, za haramu na halali,
Ili tupate zishika, na kuzitii kwa kweli,
Kitumike Kiswahili, Baraza la Tanganyika.

Tanganyika kwa hakika, ni kabila mbali x2

Zote zimekutanika, kutumia Kiswahili,
Tukipata Tanganyika, kiwe lugha serikali,.
Kitumike Kiswahili, Baraza la Tanganyika.

Tunataka madaraka, ya uchaguzi kamili,
Wajumbe tunaotaka, isichague serikali,
Tuchague tunaotaka, ipokee serikali,
Kitumike Kiswahili, Baraza la Tanganyika.

Viti tunavyovitaka, tupewe na serikali,
Sisi ni wengi hakika, kuliko taifa mbili,
Haki isiyo na shaka, tuzidi hata viwili,
Kitumike Kiswahili, Baraza la Tanganyika.

Wageni kuongezeka, tunasoma mushkeli,
Kwani tusije tabika, kupungukiwa maloli,
Wametosha waliofika, twaomba serikali,
Kitumike Kiswahili, Baraza la Tanganyika.

Hawale Tanganyika, kwa lugha ya Kiswahili,
Tupate kuelimika, ifanyavyo serikali,
Nasi sasa tumechoka, kusemwa tungali mbali,
Kitumike Kiswahili, Baraza la Tanganyika.

Hatuwezi kuokoka, kwa lugha za watu mbali,
Lugha yetu twaitaka, utumike kila hali,
Pasiwe cha kufichika, zikae wazi akili,
Kitumike Kiswahili, Baraza la Tanganyika.

Wasalamu kutamka, si kimaliza kauli,
Watanganyika twataka, kusikose Kiswahili,
Ndipo ututoke shaka, kuishuku serikali,
Kitumike Kiswahili, Baraza la Tanganyika.

9. Tumshukuru Manani

Nalia nafurahiwa, tukumbuke ya zamani,
Tukumbuke majaliwa, kutawaliwa nchini,
Viumbe kutawaliwa, tulikuwa utumwani,
Tumshukuru Manani, uhuru tumejaliwa.

Tabu nyingi tulitiwa, shariaziso imani,
Ubaguzi ukatiwa , hata vyoo safarini,
Sisi tulibaguliwa, hata kule hotelini,
Tumshukuru Manani, uhuru tumejaliwa.

Tulifanywa ni wakiwa, tungemlilia nani,
Tukisema hutishwa, tutatiwa gerezani,
Ndivyo tulivyotumiwa, kama punda mizigoni,
Tumshukuru Manani, uhuru tumejaliwa.

Tulifanywa kama nyiwa, waliotiwa tunduni,
Mtama tukitiliwa,kama ndege kifungoni,
Bure nilidhulumiwa , tulikosa kosa gani,
Tumshukuru Manani, uhuru tumejaliwa.

Pasi na kuaunguliwa, ya kwamba tu masikani,
Kodi inapotakiwa, hufungwa kamba shingoni,
Pamwe na kuadhiriwa, kupitishwa mitaani,
Tumshukuru Manani, uhuru tumejaliwa.

Shuleni hatukutiwa, ili tuwe ujingani,
Fusi hatukupatiwa, kutiwa utajrini,
Kucha kutwa hukomewa, kama majitu haini,
Tumshukuru Manani, uhuru tumejaliwa.

Leo nasi twajaliwa, tuwe huru duniani,
Tuondokwe na ukiwa, tuwe viumbe thamani,
Tupate kuthaminiwa, baraza ya duniani,
Tumshukuru Manani, uhuru tumejaliwa.

Uhuru kuachiliwa, kwamba haiwezekani,
Ndivyo tulivyoambiwa, si sisi wana chuoni,
Vizingiti vilitiwa, tubabaike njiani,
Tumshukuru Manani, uhuru tumejaliwa.

Mafumbo tulifumbiwa, kama watoto shuleni,
Wengine kuathiriwa, na kufukuzwa mijini,
Kesi zilifunguliwa, na kutozwa mafaini,
Tumshukuru Manani, uhuru tumejaliwa.

Si kwamba ninachukiwa, kukumbuia shairini,
Hayo ndiyo majaliwa, ya giza letu zamani,

Leo tunafunguliwa, na Mola wetu manani,
Tumshukuru Manani, uhuru tumejaliwa.

Uhuru tumejaliwa, sasa tufanye nini,
Wananchi twaambiwa, kazi zizidi nchini,
Ardhi kufukuliwa, iwe kazi namba wani,
Tumshukuru Manani, uhuru tumejaliwa.

Vyema kufunguliwa, vya mapato ya chini,
Ndipo tutapojaliwa, kuyafaidi madini,
Uvivu tukiingiwa, wote tutarudi chini,
Tumshukuru Manani, uhuru tumejaliwa.

Maadui waambiwa, ni watatu twabaini,
Ujinga twasimuliwa, ni adui namba wani,
Na maradhi yametiwa, pamoja na uskini,
Tumshukuru Manani, uhuru tumejaliwa.

Tusipate kutatiwa, kushindwa nao katani,
Tukazane watatiwa, kufikiwa ardhini,
Tusije kutawaliwa, na kutiwa hatarini,
Tumshukuru Manani, uhuru tumejaliwa.

Ijapo tukitolewa, fedha kutoka London,
Ya kwamba tuliletewa, na viongozi nchini,
Na iwapo mtalewa, mtarudi utumwani,
Tumshukuru Manani, uhuru tumejaliwa.

10. Kujitawala

Ni mume si mwanamke, aliniambia fahamu,
Mtawaliwa mcheke, cheko la kumlaumu,
Na tena ya pambazuke, kujitawala kugumu,
Kujitawala kugumu, tujikongoje tufike.

Utawala tuushike, una mambo maalumu,
Yafaa tuerevuke, tujinyanyuwe makamu,
Sherehe tuziepuke, vinanda na densi tamu,
Kujitawala kugumu, tujikongoje tufike.

Akili zituchemke, dunia itabasamu,
Plani tuziandike, ziende Buckingham,
Huko nako watamke, ya kwamba tumehitimu,

Kujitawala kugumu, tujikongoje tufike.

Tusipende tuanguke, kama watu kadimu,
Walipenda wanawake, nchi wakazihasimu,
Wakanywa na pombe zake, za mazabibu matamu,
Kujitawala kugumu, tujikongoje tufike.

Mtu yeyote na chake, tumlinde kialimu,
Fakiri na hali yake, lazima tumuhishimu,
Tajiri na mali yake, katu tusimdhulumu,
Kujitawala kugumu, tujikongoje tufike.

Tushikilie tufike, tujitawale tudumu,
Wenye moyo wapinduke, wawe watu makarimu,
Na sisi tuamirike, tule vinono vitamu,
Kujitawala kugumu, tujikongoje tufike.

Mungu kaumba viumbe, wamuabudu Manani,
Pia na washike jembe, wafukuwe ardhini,
Wakitingwa wamuombe, adriki adrikini
Ya Ilahi Manani, tusaidie viumbe.

Tusaidie viumbe, TANU iwe heshimani,
Tukusanyike tuombe, uhuru wetu yakini,
Malibari tujipambe, tujitawale nchini,
Ya Ilahi ya Rahamani, atunyanyue viumbe.

Atunyanyue viumbe, tuwe watu wa thamani,
Tanganyika kila pembe, itukuke duniani,
Umkokote harambe, mwenye husuda moyoni,
Ya Ilahi Rahamani, tusikilize viumbe.

Tusikilize viumbe, na dola za duniani,
Tunapotuma wajumbe, tusiwe kushikakani,
Wanapofika waombe, wapate bila utani,
Ya Ilahi ya Manani, ututulize viumbe.

11. Utenzi Wa L

Bwana Rajabu Salehe,
Hakika umabalehe
Utunzi wako sherehe
Barua imewasili

Nimeshukuru hakika
Kupata wako waraka
Ya kwamba wanikumbuka
Kumbuka ya awali.

Tumetengana zamani
Rafiki mwenye hisani
Vilima havikutani
Tutaonana wawili

Kandoro mie mcheka
Tena ninasikitika
Hasa ninayakumbuka
Hayo yalo kukabili

Kwamba umefirisika
Na duka limeanguka
Na mkeo kukutoka
Huo ndio mshikeli

Nikaapo hutazama
Na akili zikizama
Dunia ina mrama
Kandoro msemakweli

Habari zako mayonzi
Zinanitoa machozi
Kandoro sijiwezi
Zimenivunja mwili

Nilitumaini kwako
Unibebe kwa mbeleko
Unipe na matandiko
Ya kuniinuwa hali

Kwamba ni mabadiliko
Yako kwangu yako kwako
Na sasa sina kishiko
Nimekuwa mdhalili

Masikitiko simema

Na Mungu atayapima
Mwenyewe atatizama
Kuleta ngazi ya pili

Hapo usiwe na hofu
Kumpata ukondefu
Jalilu Mola latifu
Atatujaza akili

Sasa ninakueleza
Pale nilikwenda Mwanza
Nikawa nambembeleza
Kusema na Serikali

Kwamba intuumiza
Ng'ombe zetukupunguza
Nilikuwa naeleza
Nikisema tafadhali
Ng'ombe ushuru kutoza
Pamba bei kupunguza
Ushuru pamba kutoza
Ni mambo ya idhilali

Na kusema bila shaka
Utawala tunataka
Kutawala Tanganyika
Ni nchi yetu balali

Simu tulipeleka
Kwa waziri msifika
Uingereza ikafika
Wajue watu wa mbali

Tulisimama kiume
Kuomba kwa wafalume
Maombi yetu wapime
Mengine hawakubali

Mnyonge kupata haki
Iwapo atakushitaki
Na mwenye nguvu hataki
Hapo huzuka kitali

Kabla kutahadhari
Wakafika askari
Wamevalia hanjani
Za kutuonya ajali

Na wazungu wakafika
Ikazuka hekaheka
Mimi na Bwana Munanka
Twaketi bila kujali

Tulizingwa pete
Na ofisi yetu yote
Hawakusaza chochote
Walitwaa hata mali

Na sisi tukawa huru
Katu hawa kutudhuru
Sasa waombwa uhuru
Popote kila mahali

Hayo hapo nafupiza
Mbele kuyaendeleza
Nataka kusheneneza
Ambayo yamenikabili

Ndipo nikaja Kigoma
Vitu vimebaki nyuma
Mpaka hivi nasema
Nimebaki filihali

Vimebaki kupita
Nyumba ya Bwana Kaluta
Na hivi navipata
Kuagiza sikubali

Hapo ndipo najigamba
Ujiji naenda shamba
Nashika jembe naimba
Tongwe nilipowasili

Nimelifungua shamba

Naliita kumba kumba
Kwa hatua ukitamba
Ekari kumi na mbili

Niliyapanda mahindi
Kuyapanga kwa ufundi
Mahindi yakakaidi
Mgogoro shamba hili

Katu sikupata kitu
Nilipo ufyeka mwitu
Kitu sikupata katu
Nalima nasitahimili

Naendelea Saadani
Ninalima shambani
Kuna nguruwe na nyani
Hata akina tumbili

Kandoro sina bunduki
Kandoro sina mkuki
Wapi nende kushitaki
Nguruwe hana wakili

Maisha ni tafrija
Bado sijapata tija
Ninamlilia haja
Enzie Lam yazali

Bado kupumzika
Na kituoni kufika
Maisha ya viraka
Mtu ya faa kusali

Hii taabu kutufika
Nchi imebadilika
Ni wageni walofika
Wanatushinda maswali

Tusiwe kubabaika
Tutazidi kuanguka
Tusikose pakushika

Sisi walao ugali

Lazima tuwe imara
Itabadilika kura
Yataafiki majira
Tule ngano na samli

Sisi kuwa watumishi
Na mume kuwa mpishi
Huo ujinga wa pishi
Lazima tutaamuli

Kweli kazi ya kulima
Inayo nyingi rehema
Ndio kazi ya uzima
Inayo leta kivuli

Nawe wataka kulima
Bahati yako kupima
Shauri hilo ni jema
Usibadili kauli

Hima trekta pata
Chapu upesi tafuta
Uyapindue matuta
Ulime na pilipili

Ukipata usisahau
Kitumbo sinidharau
Nakulilia ki- nyau
Uje tulime maakuli

Tulime buni nadhifu
Tupanda nazi kwa safu
Pia karafuu ndefu
Ifate misheli sheli

Uje tupande korosho
Huku aridhi si jasho
Hata mihogo ya posho
Nakadhalika na wali

Njoo huku kuna kazi
Kunasitawi migazi
Itaifai utarazi
Tuzivue sumali

Ninayo mambo mapevu
Ningelima kierevu
Washangae wenye ndevu
Nafananisha mithali

Katani bila turufu
Kavata kuzisanifu
Utakuwa kama ndufu
Kisu kisicho kikali

Salam kwa wake zako
Salam watoto wako
Salaam na kaka yako
Huyo alokubadili

Flowarose salaamu
Aleta kwako kwa hamu
Mwakipiti Ibrahimu
Twamtaka si kabili

Wasalam Saadani
Abdu si la utani
Kandoro wangu bini
Nimemaliza

Kiambatisho E: Mashairi ya Amri Abedi

Diwani: *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri* (1954)

1 . Nguo Ziteremsheni Yapungue Maasia

Sitara kubwa kuvaa, vazi refu miguuni,
Msiige bila njia, mabibi kunradhini,
Vazi refu kulivaa, ni sitara muilini.
Nguo ziteremsheni, yapungue maasia.

Muovu aliyevaa, si Yule asiye soni,
Alojiteremshia, si mkudia gotini,
Zuri ni zuri sikia, japo liwe kwa haini,
Nguo ziteremsheni, yapungue maasia.

Kuvaa fupi si njia, na avae muumini,
Baya ni baya tambua, ingawa la Uzunguni,
Hujahoji kwa hatua, bibi rudi kwa Manani,
Nguo ziteremsheni, yapungue maasia.

Moto usipochochea, hufukutia mekoni,
Bali ukiupepea, unazidi muwakoni,
Vivyo nguo kupania, mwazidisha matamani,
Nguo ziteremsheni, yapungue maasia.

Ni wengi wanaovaa, kanzu za kushuka chini,
Wake na waume pia, waendao macho chini,
Wepi zimewapamia, motokaa za njiani?
Nguo ziteremsheni, yapungue maasia.

Ai ! Umesha sikia , yaliyoko Uropani,
Huko chungu waumia, kwa kupondwa majiani,
Tuseme hawajajua, kuvaa za magotini?
Nguo ziteremsheni, yapungue maasia.

Ima tanihesabia, Waganda washusha chini,
Wale zimewapamia, motokaa za mijini,
Hata ukaja tambua, ushone za magotini,
Nguo ziteremsheni, yapungue maasia.

Ima utaniambia, kwa usemi wa yakini,
Kaputula kutumia, ni wasisagwe njiani?
Ai! Hukuyapimia , ole! Hunayo yakini,
Nguo ziteremsheni, yapungue maasia.

Wasubiri kulemaa, ndipo uvae za chini?
Watu wasije kujua, una ulema mwilini?
Kumbe unajikudia, wakujue rasmini!
Nguo ziteremsheni, yapungue maasia.

Tafadhali vumilia, shairi hili kwinini,
Chungu, bali inafaa, kukinga homa mwilini,

Hii ni njema tabia, nguo ziteremsheni,
Nguo ziteremsheni, yapungue maasia.

2. Wakudao Magotini, Hawachelei Khasar

Utungaji wa busara, hutarajia kiini,
Hoja hazendi kwa kura, usijitoe thamani,
Usione nakukera, makosani kubaini,
Wakudao magotini, hawachelei khasara

Hawachelei khasara, wakudao magotini,
Wengi wao si fukara, hili nawe hulikani,
Siige bila fikira, ukajishusha mizani,
Wakudao magotini, hawachelei khasara.

Buibui za sitara, zapandishwa magotini!
Kanga ndefu barabara, hazishushwi miunduni,
Huoni kuwa ibura, khasara, khasara gani?
Wakudao magotini, hawachelei khasara.

Siwafanyii hasira, hutii mambo kichwani,
Nawafunza ya tohara, maovu yapwe nchini,
Huoni hizi khasara, ukware na ushetani?
Wakudao magotini, hawachelei khasara.

Shungi kufunka sura, jambo zuri lenye shani,
Bibi hapauki sura, kwa jua barabarani,
Vipi apate madhara, na aonea tunduni?
Wakudao magotini, hawachelei khasara.

Jambo hili la busara, hupunguza matamani,
Linazuia fikira, mbaya kupenya moyoni,
Wanawake wa sitara waheshimiwa njiani,
Wakudao magotini, hawachelei khasara.

Kina bibi wenye ghera, walioko Uzunguni,
Wanashona za sitara, zinashuka miundini,
Wale si wenye busara, wavaa fupi gauni,
Wakudao magotini, hawachelei khasara.

Kuiga bila fikira, ni ujahili yakini,
Huzivaa kaputura, mabibi wa Uzunguni,

Je hili ni busara, kwa kuwako Uzunguni?
Wakudao magotini, hawachelei khasara.

Kwao sio masikhara, chupi tupu kiunoni,
Zinawatwaa kamera, utupu pasipo soni,
Haya je, ni busara, kwa kuwa ya uzunguni?
Wakudao magotini, hawachelei khasara.

Muumba mwenye kudura, mpe fahamu mwandani,
Mambo haya yenye dhara, asiwe nayo rohoni,
Hajui, mpe busara, ayajue kwa viini,
Wakudao magotini, hawachelei khasara.

3. Njema Haina Mkosi Japo Aivae Koja

Nimeitwaninakuja, haya nipeni nafasi,
Naja tena toa hoja, za mabibi na libasi,
Uvaaji wa viroja, tuusute hata basi,
Njema haina mkosi, japo aivae koja.

Ni ujinga upataje, kuiepuka khilasi,
Mabibi mmekuwaje, kuzikudia libasi,
Wacheni si uvaaje, tumfupize bilisi,
Njema haina mkosi, japo aivae koja.

Nawe binti wa Ujiji, nguo fupi si libasi,
Usijitie ujaji, hujui kukata kesi,
Wacheni ya ufujaji, tumche Mola Quadusi,
Njema haina mkosi, japo aivae koja.

Msizidishe porojo, kujinaki ufarasi,
Komesheni hii fujo, teremsheni libasi,
Msighurike na banjo, na huko kucheza dansi,
Njema haina mkosi, japo aivae koja.

Haya hima kina bunju, mlio na ufanisi,
Wakutanisheni manju, wasute huu mkosi,
Sisemi ya umanjunju, na ikome adharusi,
Njema haina mkosi, japo aivae koja.

Bibi situnge kasida, ya kufundisha maasi,
Nguo zenu kuzikuda, ni kuanzisha nuhusi,

Wafupizwe kina dada maovu yasende kasi,
Njema haina mkosi, japo aivae koja.

Libasi wasizikude, zachusha kadamunasi,
Chonde kina dada chonde, waadhi wangu muhisi,
Hauna haja ushinde, kushindania maasi,
Njema haina mkosi, japo aivae koja.

Tufuate irishadi, wema, tusiufilisi,
Chonde msinikaidi, mtapona ninyi nasi,
Turejee kwa wadudi, tusafike na danasi,
Njema haina mkosi, japo aivae koja.

Beti hizi madoido, hidashara fafanusi,
Tuvifupishe vishindo, tuende nyendo khalisi,
Nyoyo tuzijaze pendo, zisijae ubilisi,
Njema haina mkosi, japo aivae koja.

Bure msinihusudu, tuufupishe utesi,
Kwani mtesi hamudu, ateteapo maasi,
Sianze Alhamdu, ukakhubiri matusi,
Njema haina mkosi, japo aivae koja.

Mjapo mje kwa hoja, msije nayo matusi,
Mtukanaji hufuja, akazikera nafusi,
Msiupige pambaja, ulimwengu una kasi,
Njema haina mkosi, japo aivae koja.

4. Uhuru Jambo Halisi

Tundu liwe la dhahabu, na lulu na alimasi,
Litiliwe abuwabu, kwa mbao za abunusi,
Ndege huona adhabu, kuwekwamo mahabusu,
Uhuru jambo halisi, kuukosa ni taabu.

Uhuru ni mawahibu, katoa Mola Mkwasi,
Pamwe na kuukutubu, uenee kwa unasi,
Uhuru jambo wajibu, kwa ajinanina insi,
Uhuru jambo halisi, kuukosa ni taabu.

Kwa tunu watughilibu, wapate kutufilisi,
Tudumu na ubawabu, nao washike urasi,
Tuzidi kuwatulubu, kwa kazi za piga pasi,

Uhuru jambo halisi, kuukosa ni taabu.

Utumwa haujaghibu, bado waenda kwa kasi,
Mwenye nguvu anasubu, mnyonge hana nafasi,
Ukisema una tabu, wazidishwa tatasi,
Uhuru jambo halisi, kuukosa ni taabu.

Vya bure vyao vitabu, wao haviwatakasi,
Wamevipangia babu, kuupambaza unasi,
Na usawa umeghibu, hata ndani ya kanisi,
Uhuru jambo halisi, kuukosa ni taabu.

Na ufanye la harubu, u mweusi, u mweusi!
Kamwe hulipiwi thawabu, sawa na aso mweusi
Wewe zako ni sulubu, kuwakhudumu wakwasi,
Uhuru jambo halisi, kuukosa ni taabu.

Dharau zinatusibu, kudharawiwa weusi,
Maponjoro hutujibu, kwa maneno ya matusi,
Asili ya hii taabu, ni kwamba ni mahabusi,
Uhuru jambo halisi, kuukosa ni taabu.

Nchi hii mahababu, haki ni nchi ya sisi,
Vile kuwapa karibu, sisi tumekuwa fisi,
Sasa ni kheri kilabu, wapendwa kuliko sisi,
Uhuru jambo halisi, kuukosa ni taabu.

Kutawaliwa labibu, mtu hukui upesi
Yako mema maarubu, hayaachiwi nafasi,
Watapenda uwe bubu, wakunyonye kipapasi,
Uhuru jambo halisi, kuukosa ni taabu.

Mwenyeji kuwa gharibu, huu dhahiri mkosi,
Na jingine la ajabu, ni woga wetu wa fisi,
Jambo latustahabu, tuunganike upesi,
Uhuru jambo halisi, kuukosa ni taabu.

Ninawataka khatibu, na ambao wandarisi,
Wapite wakikhutubu, kuzitoa fafanusi,
Uhuru twautulubu, wakazane mafarisi,
Uhuru jambo halisi, kuukosa ni taabu.

Iko siku kwa wahabu, sisi tutakuwa sisi,
Hapo hatutawasubu, kwa dhiki na wasiwasi,
Japo wanatuharibu, hatutawapa tatasi,
Uhuru jambo halisi, kuukosa ni taabu.

23. Kiwakacho Huzimika

Huzuni imenivaa, moyo unasononeka,
Majonzi yamenikaa, roho inataabika,
Simanzi imenitwaa, nalia naungulika,
Kiwakacho huzimika, na ina mwisho dunia.

Moyo huingia siri, huzuni ikienea,
Tamu ikawa shubiri, kula ukalimatia,
Usiishe kufikiri, kupanga na kupangua,
Kiwakacho huzimika, na ina mwisho dunia.

Hupigwa na bumbuazi, na macho yakashangaa,
Na zikakwama pumzi, kabla ya kupumua,
Ole dhiki ya majonzi, khasa ukidhulumiwa,
Kiwakacho huzimika, na ina mwisho dunia.

Hapo akili huduru, angani ikasambaa,
Kila unapodhukuru, moyo unakuungua,
Enyi waovu mu huru, nasi wema twafungiwa,
Kiwakacho huzimika, na ina mwisho dunia.

Na mtutende uovu, hatutawarudishia,
Tutajishika mashavu, Mola tutamlilia,
Dunia mti mkavu, japo mwauparamia.
Kiwakacho huzimika, na ina mwisho dunia.

Ee Rabbu Rahamani, hata lini nitalia?
Hukupungua Manani, nitendee nitendea,
Iniondoke huzuni, moyo upate pumua,
Kiwakacho huzimika, na ina mwisho dunia.

Daima nimekuomba, Mola nimenyenyekea,
Mungu ivunje miamba,na dhambi nighofiria,
Kwa hayo ambayo kwamba, ninayokushitakia,
Kiwakacho huzimika, na ina mwisho dunia.

Mola umkamilifu, moja halikupungua,
Yote ni malainifu, huna la kukulemea,
Haya yangu yasarifu, kwa wema kupindukia,
Kiwakacho huzimika, na ina mwisho dunia.

Majonzi yalonifikia, pindi nikikumbukia,
Hukonda kwa kusumbuka, hukaa peke nalia,
Lini utaniitika, wema kunizidisha,
Kiwakacho huzimika, na ina mwisho dunia.

Nalia naomboleza, Rabi Muweza sikia,
Nikuambayo timiza, ya Huru msafi nia,
Ambaye atanipoza, na fani zote kujua,
Kiwakacho huzimika, na ina mwisho dunia.

24. Sote Tu wa Nyumba Moja

Japo twakhiilafiana, Dini yetu dini moja,
Si vibaya kuonyana, kwa kutoleana hoja,
Lakini tukigombana, tutakizua kiroja,
Sote tu wa nyumba moja, ikifa tutacharara.

Muhammadi Seyidina, Mtume wetu mmoja,
Sote twampenda sana, kwake twapate faraja,
Na tuache kuzozana, tushike mambo ya haja,
Sote tu wa nyumba moja, ikifa tutacharara.

Kitabu cha Maulana, Kur'ani yetu moja,
Kwayo tunafungamana, kuzitosheleza haja,
Humo tutoe bayana, tukiambizana hoja,
Sote tu wa nyumba moja, ikifa tutacharara.

25. Umoja

Msituni nikakuta, nyuki wamo mzingani,
Kwa juhudi wanakita,mara nje mara ndani,
Husuda wameikata, hata hawasengenyani,
Nyuki ni wadudu duni, wanashinda kwa umoja**.**

Mchwa nao nikaona, wamejenga masikani,
Wafanya bidi sana, uvivu hawatamani,
Wao husaidiana, tena hawadanganyani,
Nyuki ni wadudu duni, wanashinda kwa umoja**.**

Nalo jeshi la siafu, hutandawaaa njiani,
Laenda bila hofu, maana lajiamini,
Silaha zao dhaifu, meno, tena hawaoni,
Nyuki ni wadudu duni, wanashinda kwa umoja.

Nao chungu wacvhukuzi, nyawarima wa njiani,
Masikini wapagazi, mizigo yao kichwani,
Ingawa si wachokozi, wakali ukiwahini,
Nyuki ni wadudu duni, wanashinda kwa umoja.

Sisi ni wana Adamu, mbona hatusikizani?
Tusitietie hamu, ukubwa kuutamani,
Wachache wataalamu, tuwasadi kwa imani,
Hii, “Huyu awezani,” yatuvunjia umoja

KIAMBATISHO A: Kibali cha Utafiti Chuo Kikuu cha Kenyatta

KENYATTA UNIVERSITY
GRADUATE SCHOOL

E-mail: kubps@yahoo.com
dean-graduate@ku.ac.ke
Website: www.ku.ac.ke

P.O. Box 43844, 00100
NAIROBI, KENYA
Tel. 8710901 Ext. 57330

Our Ref: C82/31403/15 Date: 19th August, 2019

The Director General,
National Commission for Science, Technology & Innovation,
P.O. Box 30623-00100,
NAIROBI

Dear Sir/Madam,

RE: RESEARCH AUTHORIZATION FOR MS.NEXSUNA H. WANJIKU- REG. NO. C82/31403/15

I write to introduce Ms. Wanjiku who is a Postgraduate Student of this University. She is registered for a Ph.D. degree programme in the Department of Kiswahili & African Languages in the School of Humanities & Social Sciences.

Ms. Wanjiku intends to conduct research for Ph.D. thesis entitled "Hali Zilizochochea Mabadiliko ya Kimaadhui ya Ushairi Nchini Tanzania Kati ya 1930-1960".

Any assistance given will be highly appreciated.

Yours faithfully,

PROF. ELISHEBA KIMANI
DEAN, GRADUATE SCHOOL

EM/cao

KIAMBATISHO B:Kibali cha Utafiti Taasisi ya Taaluma za Kiswahili

CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM
TAASISI YA TAALUMA ZA KISWAHILI

S.L.P. 35110 Dar es Salaam
Simu Na Mkurugenzi: 2410737
Simu ya Ofisi: 2410308-9 Ext. 2047
Fax: 022 - 2410334

Barua-pepe: taki@ikr.udsm.ac.tz
ilo@bcbm.ac.tz
Tovuti: www.udsm.ac.tz/taki
www.udsm.ac.tz/ilo

Kumb: TATAKI/B 116

Tarehe: 27.04.2017

Bi. Njuguna Hekina Wanjiku

Yah: Kutumia Maktaba ya Taasisi ya Taaluma za Kiswahili

Barua ya Mkuu wa Idara ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Kenyatta ya tarehe 13.04.2017 inarejelewa.

Napenda kukuhakikishia kuwa mnamo tarehe 27.04.2017 Mkurugenzi wa Taasisi ameikubali ombi lako. Ajifha, ruhusa imetolewa kutumia maktaawani/Maktaba kwa muda wa siku tatu za kazi kuanzia tarehe 27.04.2017.

M. Mbinda
Kny: Mkurugenzi, TATAKI

nk: Mkurugenzi, TATAKI
nk: Mkutubi (Maktaawani), TATAKI
nk: Mkutubi (Maktaba), TATAKI

KIAMBATISHO C: Kibali cha Utafiti Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM
TAASISI YA TAALUMA ZA KISWAHILI

S.L.P. 35110 Dar es Salaam
Simu Na Mkurugenzi: 2410717
Simu ya Ofisi: 2410508-8 Ext: 2647
Fax: 022 - 2410334

Barua e-pe: tuki@ud.ac.tz
tuki@udsm.ac.tz
Tovuti: www.udsm.ac.tz/tuki
www.udsm.ac.tz/tuki

Kumbu: TATAKI/D 116

Tarehe: 07.04.2017

UNIVERSITY OF DAR ES SALAAM
27 APR 2017
LIBRARY

Mkurugenzi
Huduma za Maktaba ya Wilbert Chagula
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Yah: Bi. Njuguna Helina Wanjiku

Mbajwa hapo juu ni mwanafunzi wa Uzamivu katika Chuo Kikuu cha Kenyatta. Hivi sasa yupo katika hatua ya utafiti. Mada yake ya utafiti ni 'Sera ya Lugha na Ubunifu wa Istilahi Nchini Kenya na Tanzania'. Imebainika kuwa maktaba na maktazazi za Taasisi ya Taaluma za Kiswahili hazikuweza kukidhi haja zake za utafiti wa Bi. Njuguna.

Kwa kuzingatia hoja hapo juu ninapenda kukuomba umruhusu Bi. Njuguna kufanya maktaba ya Wilbert Chagula ili kufanikisha utafiti wake.

M. Mbenda
Kny: Mkurugenzi, TATAKI

nk: Mkurugenzi, TATAKI

KIAMBATISHO D: Kibali cha Utafiti Chuo Kikuu Huria cha Tanzania

KENYATTA UNIVERSITY
KISWAHILI AND AFRICAN LANGUAGES DEPARTMENT

P.O. BOX 43844
NAIROBI, KENYA
Office Tel: 8710222/8712722/ 8710901-913
EXT: 57546
FAX: (254) (2) 811575
Website: http// www.ku.ac.ke

27th June 2022

The Head Librarian
The Open University of Tanzania
TANZANIA

RE: PERMISSION TO USE LIBRARY

The bearer of this letter, NJUGUNA HELINA WANJIKU – CR2/31405/2015 is a PhD student in this department. She is currently conducting her doctoral research on **"Hali Zilizochochea Mabadiliko Ya Kimaudhui Ya Uhariri Wa Kiswahili Nchini Tanzania Kati Ya 1930 – 1960"**.

Kindly allow her use your library facilities.

Thank you.

PROF. PETER GITHINJI
CHAIRMAN
KISWAHILI AND AFRICAN LANGUAGES DEPARTMENT